

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 28 Julai, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

SPIKA: Kabla sijamwita Naibu Waziri wa Habari, nawakaribisha tena katika juma hili baada ya mapumziko ya mwisho wa wiki natumaini sote tupo salama na kwamba naweza kuwa na matangazo mazuri ya kusoma baada ya kipindi cha maswali. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa habari, Utamaduni na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. HAROUB SAID MASOUD (k.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA):

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI – MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Taarifa ya Msemadi wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 292

Ubovu wa Barabara ya Kongwa – Suguta

MHE. GORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI) aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kongwa – Suguta ni mbaya na haipitiki kwa miaka kadhaa sasa:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu ukarabati na ujenzi wa barabara hiyo muhimu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kongwa – Suguta yenyeye urefu wa kilometra 33 ni sehemu ya barabara ya Mkoa inayoanzia Mbande – Kongwa – Suguta yenyeye urefu wa kilometra 49 inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba sehemu kubwa ya barabara hii kati ya Kijiji cha Ibwaga na Suguta yenyeye urefu wa kilometra 25 ni mbaya ambayo hupitika kwa shida wakati wa kiangazi na wakati wa masika haipitiki. Hali hiyo imetokana na ufinyu wa Bajeti ya kuifanyia matengenezo makubwa barabara hii ambayo haiwezi kutengenezwa kwa Bajeti ya matengenezo ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Seriali ilifanyia matengenezo makubwa sehemu ya barabara kutoka Mbande hadi Kongwa kupitia mradi wa *HIPIC* mwaka 2005/2006. katika mwaka wa fedha 2006/2007, matengenezo ya kawaida kwa jumla ya Sh. 7.2m/. Katika mwaka 2007/2008, maeneo ya Kongwa Mjini, Ibwaga na Sagala katika barabara hii yalifanyiwamatengenezo kwa gharama ya Sh. 106m/.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara hii na itaendelea kuitengeneza kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, ningependa kumwomba Mheshimiwa Mbunge kusaidia kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwani uharibifu wa mazingira katika maeneo husika mbali na madhara mengine, huchangia sana uharibifu wa haraka wa barabara.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Kongwa

inapakana na Jimbo la Mpwapwa na kwa kuwa Barabara hii ni muhimu sana. Barabara ya Kongwa-Suguta-Mlali-Chamkoroma mpaka Mpwapwa, na kuwa Serikali ilikwishaahidi kuifanyia matengenezo makubwa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba fedha imetengwa milioni 100.6 kwa eneo hili la Ibwaga, Sagara mpaka Suguta. Je, sasa Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana iko haja ya kuitengea fedha za kutosha hasa kutengeneza daraja la Ijaka, Sagara pamoja na Ibwaga.

SPIKA: Kabla Waziri hujajibu kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi swali lililoulizwa ni 292 aliyeuliza alisema 291 ni 292.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili wakati najibu swali namba 222 lililoulizwa na Mheshimiwa Ndugai kuhusu barabara hii ya Mbande Kongwa hadi Mpwapwa niliisema kuwa Serikali pamoja na kuutambua umuhimu mkubwa wa Barabara hiyo sasa inaipa kipaumbele na juhudzi zitafanywa ili kuhakikisha kwamba inaitengea pesa za kutosha itengenezwe kwa matengenezo ya uhakika na kamili ili iweze kupitika kwa majira na hivyo ndivyo ambavyo tutafanya katika miaka hii inayofuata.

Na. 293

Vitendea Kazi kwa Kitengo cha Hali ya Hewa Nchini

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI K.N.Y (MHE. PINDI H. CHANA) aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kutambua hali ya hewa nchini ni la muhimu sana hasa wakati wa mvua nyingi au ukame na kwa kuwa kitengo cha hali ya hewa nchini hakina vitendea kazi muhimu kama vile rada na kadhalika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiwezesha kituo hicho kupata vitendea kazi muhimu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kupata taarifa za hali ya hewa hasa nyakati za mvua nyingi au ukame. Aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mamlaka ya Hali ya Hewa inatakiwa kuwa na vifaa vya kisasa na vya kutosha ikiwemo rada.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuongeza vifaa kwa njia mbalimbali zikiwemo za kutenga fedha katika Bajeti za Mamlaka na pia kusaidiwa na wahisani. Katika mwaka uliopita wa fedha 2007/2008 Mamlaka ilitumia Sh. 552m/= kununua Retim nne na *Synergies*, ambayo ni mitambo ya mawasiliano na utabiri na kuiweka katika viwanja vinne vya ndege vya Mwalimu Nyerere, Kilimanjaro, Mwanza na Zanzibar. Hii imeboresha huduma katika viwanja hivyo. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya hali ya Hewa iko katika hatua za mwisho kukamilisha rasimu ya mkatuba wa ununuzi wa Rada moja ya Hali ya Hewa. Kutokana na viwango vya Kimataifa Tanzania inahitaji rada saba ili kuwa na taarifa za hali ya hewa za nchi nzima. Rada moja itagharimu kiasi cha Sh. 2bn/=.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na mitambo ya kisasa ya utabiri wa Hali ya Hewa kufuatana na upatikanaji wa fedha.

MHE. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri sana hata hivyo naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa vile mazingira ya Wilaya Ludewa ina miinuko mikubwa na tambarare mpaka sawa na usawa wa bahari na kwenda juu katibu mita 3000.

Je, Wizara haioni kuna umuhimu kuweka kituo angalau cha hali ya hewa maeneo hayo ili kusaidia utabiri wa hali ya hewa kwa maeneo ambayo yanatoa mahindi na mazao mengine ya chakula.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, ni kweli hali ya Ludewa ingehitaji mitambo zaidi kwa ajili utabiri bora zaidi wa hali ya hewa katika maeneo hayo ili kuwezesha juhudhi za kujenga uchumi katika maeneo hayo ili ziwe za mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la msingi katika Bunge hili kabla nilisema kwamba tuna upungufu mkubwa wa vyombo vya kupimia hali ya hewa na Serikali itaendelea siyo tu kwa eneo la Wilaya ya Ludewa lakini kwa Tanzania nzima ili kuhakikisha kwamba utabiri huu unakuwa kamili na wenye kukidhi haja na mahitaji ya wakulima na wafanyakazi wan chi hii.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kutokana na jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna upungufu mkubwa wa vyombo hivi vya kupimia hali ya hewa na mara nyingi taarifa zimekuwa zikitolewa na utabiri wa hali ya hewa kwamba itanyesha mvua na mvua hainyeshi taarifa zimekuwa siyo za uhakika kutokana na upungufu mkubwa, au jua litawaka au haliwaki kwa hiyo hii inaathiri kabisa hata wakulima amba wanategemea sana mvua kwa ajili ya kilimo;

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta namna ye yeyote kuhakikisha kwamba bila kutegemea Bajeti inapata vifaa hivi ili tuweze kuwa na taarifa za uhakika za utabiri wa

hali ya hewa kama ambavyo nchi zingine wamekuwa wanazitumia kwa ajili ya shughuli za kilimo na shughuli zingine?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, wakati najibu swal la 260 ndani ya Bunge hili nilieleza Bunge lako Tukufu kwamba kwa viwango nya kimataifa tunahitajika tuwe na kituo kikuu cha kupimia hali ya hewa katika kila baada ya kilomita 112 na kwa hivi sasa tumefikia asilimia 35 kukidhi mahitajji hayo. Serikali inaweka umuhimu mkubwa kuhakikisha kwamba tunafikia viwango hivi nya kimataifa ili utabiri uweze kuwa wa kuaminika, nilizungumza pia kwamba katika taaluma ya utabiri wa hali ya hewa, kadri muda wa utabiri unapokuwa mfupi na ndivyo tunapopata usahihi bora zaidi katika huo utabiri, siku zinapokuwa nyingi katika utabiri na kiwango cha kuaminika kinapungua pia. Kwa hivyo, ni mambo mawili muhimu, kwanza ni kuwa na vyombo nya kupimia vingi zaidi lakini namba mbili katika taaluma unatakiwa utoe utabiri muda mfupi mfupi.

Mheshimiwa Spika, bado tuna mapungufu kwa maana hiyo wakati mwingine inatokea mapungufu katika kutoa habari za utabiri na ninaomba tu Bunge lako likubali kwamba Serikali inatambua hilo na itafanya kila juhud kuhakikisha kwamba mamlaka ya hali ya hewa inakuwa na vifaa nya kutosha.

Na. 294

Mfuko wa Pembejeo kwa Wafugaji na Wavuvi

MHE. ANIA S. CHAUREMBO aliuliza:-

Kwa kuwa mfuko wa pembejeo umeanza kwa mfanikio kwa lengo la kuwawezesha wafugaji na wavuvi kupata mikopo:-

- (a) Je, ni matatizo gani yanayoukumba mfuko huo kwa sasa?
- (b) Je, Serikali inawaelekeza nini wafugaji na wavuvi katika kutumia mfuko huo kupata mikopo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalil a Mheshimiwa Ania Saida Chaurembo, Mbunge wa viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2002/2003 hadi 2006/2007 jumla ya watoa hudumaza mifugo 22 wamefaidika na mikopo kuitia Mfuko wa Pembejeo (*The Agricultural Inputs Trust Fund*) ambapo zaidi ya Sh. 425m/= zimetolewa.

Mikopo hiyo ilihu huduma mbalimbali za mifugo zikiwa ni pamoja na utengenezaji wa vyakula nya mifugo, ununzi dawa na chanjo za mifugo, utengenezaji wa vifungashio nya maziwa, uimarishaji wa hduma za kliniki za mifugo, ununuzi wa

matrekta na zana za kukatia na kufunga malisho ya mifugo. Matatizo yanayoukumba Mfuko wa Pembejeo kwa sasa ni pamoja na:-

(i) Uwezo mdogo wa kifedha kuweza kutosheleza mahitaji ya maombi ya mikopo yanayopokelewa kila mwaka kwani fedha inayotolewa katika bajeti yake ninkidogo. Kwa wastani Mfuko wa Pembejeo hupokea maombi yenye thamani ya Sh. 10bn/= kwa mwaka, wakati Mfuko hutoa mikopo ya wastani wa Sh. 5bn/= kwa mwaka.(ii)Marejesho hafifu ya mikopo kutokana na wakopaji kushindwa kurejesha mikopo yao kwa kisingizio cha hali mbaya ya hewa kwani wakulima wengi bado wanategemea sana mvua.

(iii) Baadhi ya wakopaji kushindwa kabisa kurejseha mikopo yao. Kwa mfano, wakopaji 234 wa aina mbalimbali kati ya wakopaji 1,300 wameshidnwa kufanya hivyo kwa mikopo yenye thamani ya Sh. 2.2bn=/. Baadhi yao tayari wamefikishwaMahakamani.

(b)Ili kuhakikisha kwamba mikopo kutokana na Mfuko huo inawafikia walengwa walio vijijini ambao wngi hujishughulisha na shughuli za ufügaji nauvuvi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Hamashauri za Wiaya itaendelea kuwahamasisha wafugaji na wavuvi ili waweze kupata mikopo kuitia Mfuko wa Pembejeo. Tunashauri wananchi waimarishwe viwango vya mikopo wanayoomba, mawakla waogo wadogo wanaojishughulisha na usambazaji wa pembejeo katikangazi za Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji waunde vikundi ili kuongeza nguvu zao na wananchi wanaopata mikopo hiyo wairejeshe na wasibadilishe matumizi ya mikopo hiyo kwa kufanya shughuli nytingine.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, hivi sasa kuna zoezi la kuwakamata wavuvi na nyavu ambazo wanazitumia katika bahari ambazo Serikali haziruhusu na zoezi hilo pengine hufanyika katika maji na wakati mwengine hufanyika nchi kavu, na kwa kuwa katika bahari kuna samaki ambao wameumbwa maumbile yao ni madogo kwa mfano samaki uwenu, tongue kwa tongue dagaa na vibua na bagala samaki hawa huvuliwa maji makuu na nyavu zinazotumika ni zile ambazo hivi sasa ziko katika zoezi la kuchomwa zinapokamatwa.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wavuvi ili wajue ni kitu gani mbadala au nyavu gani mbadala za kuvulia samaki hawa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kuna zoezi ambalo linaendelea katika bahari ya Hindi la kuwakamata wavuvi haramu na zoezi hili hukamatwa na wakati huo huo hutakiwa kulipa faini na faini hutegemea wavuvi wanaokuwa ndani ya boti ile kama wakiwa wavuvi watano ina maana watalipa faini ile kila mmoja na faini ile wanalipishwa kutokana na umri, ukiwa na umri mkubwa zaidi unalipa bei kubwa zaidi.

Je Waziri analifahamu hili na lipo katika sheria?

SPIKA: Naona Waziri amesimama ingawa maswali haya kidogo yamekwenda pemberni, lakini Mheshimiwa Waziri atusaidie.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Kwanza swali la msingi lilivyokuwa limeulizwa na Mheshimiwa Mbunge lilikuwa linahusu masuala ya pembejeo na mkopo. Lakini kwa sasa hivi limeelekezwa kwenye masuala ya uvuvi na wavuvi katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, sheria inayozingatiwa katika masuala ya uvuvi baharini ni sheria namba 22 ya mwaka 2003 pamoja na *regulation* zake za mwaka 2005 na hii ni sheria inayozingatia katika upande wa Tanzania Bara, katika upande wa Tanzania visiwani ni sheria ya mwaka 1988 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1998. (*Makofi*)

Sheria hizi zote zinasisitiza kuzuia uvuvi haramu unaofanyika katika mabahari na katika maziwa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bahari kwa sasa hivi kuna *MANCEP* ambao una zaidi ya bilioni 51 ambazo wavuvi wanaweza wakazitumia katika kukopa na kupata zana ambazo zinaweza zikawasaidia ili kupambana na uvuvi haramu katika maeneo yao na hivyo kuimarisha maisha yao kwa ujumla. (*Makofi*)

Na. 295

Maslahi Duni ya Wastaafu

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa, wastaafu wengi hasa wale waliostaafu kabla ya mwaka 1996 ambapo mishahara ya watumishi wa umma iliboresha wanapata pensheni duni ya Sh. 21,000/= kwa mwezi na kwa kuwa Wabunge wamekuwa wakiisubiri Serikali kuweka kiwango cha pensheni kisichopungua kima cha chini cha mishahara. Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa kurekebisha Sheria ya Pensheni ili izingatie kutumia mshahara wa kima cha chini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji ya wastaafu wake kwa maana hiyo, Serikali imeanza mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Pensheni kwa kupitia vifungu vilivyomo ndani ya Sheria hiyo ambavyo vinaonekana kuwa na mapungufu katika utekelezaji unaoendelea wa malipo ya pensheni. Suala la kuangalia uwezekano wa

kupandisha kima cha chini cha pensheni ni sehemu ya mambo tunayoyaangalia. Madnalzii yatakapokamilika, Serikai itawasilsa Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Penseheni hapa Bungeni. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wastaafu kwa ujumla, wavute subira hasa tukizingaia kwamba Serikai iko katika mikakati ya kuongeza mapato ya ndani.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana umenisaidia kulitanguliza hilo, kama inavyoonekana ni kweli kima hiki kiko chini sana naona hata Naibu Waziri ameona aibu kikitaja ni shilingi elfu 21,000. Kwa hali ya maisha inavyopanda sasa hivi ndiyo kinazidi kwenda chini kwa hiyo nadhani tutakubaliana na Serikali kwamba Bunge lina haja ya kuwekea muda wa kutekeleza hili kwa maana ya *time frame* nilikuwa nadhani napenda kupendekeza kwamba ikifika mwezi mei mwaka ujao kwa kweli iwe imeshatengezwa ili angalau tuwape matumaini kidogo ya kuishi hawa wastaafu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wake nataka nimwahidi kwamba tutalitekeleza kabla ya hapo. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa jibu zuri linalowapa faraja wastaafu wote nchini.

Na. 296

Ripoti ya CAG

MHE. JOYCE M. MASUNGA (K.n.y. MHE. LUHANGA J. MPINA) aliuliza:-

Kwa kuwa usimamizi madhubuti wa rasilimali na fedha za umma unategemea kazi inayofanywa na CAG kwa niaba ya Bunge pamoja na uwezeshaji wa vitendea kazi na sheria zinazokwenda na wakati:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kitendo cha Ofisi ya *CAG* kuwa chini ya Ofisi ya Waziri wa Fedha na Uchumi kinamwondolea uwezo wa kujitegemea?

(b) Je, kuna sababu gani za msingi zinazosababisha ripoti ya *CAG* kupelekwa kwa Waziri wa Fedha na Uchumi amaye kimsingi ndiye mkaguliwa?

(c) Kupitia Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2005/2006 baadhi ya Wizara na Mashriika yaligundulika kuwa naupungufu mkubwa wa utunzaji wa vitavu, kumbukumbu na matumizi mabaya ya fedha. Je, ni Wizara na Mashrika mangapi yamefanyiwa *intensive investigation*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhanga Joelson Mpina, Mbunge wa Jimbo la Kisesa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Ibara ya 143 imeagiza kuwa kutakuwa na Mdhibitina Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikai ya Muungano wa Tanzania.

Katika Muundo wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi si moja kati ya Idara zake. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*National Audit Office*) ni ofisi huru inayojitegemea na ina fungu lake (Fungu Na. 45) na inafanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria yake na Katib aya nchi. Wajibu wa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa Ofisi ya CAG ni kuwasilisha Bajeti ya Ofisi ya CAG Bungeni kutegemeana na uwezo wa Serikali kwa mwaka husika.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu za msingi zinazopeleka ripoti ya CAG kupelekwa kwa Waziri wa Fedha na Uchumi, ambaye kimsingi ndiye mkaguliwa ni kutohana na kwamba Waziri wa Fedha na Uchumi ni msimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, jumla ya Wizara na Idara za Serikali ishirini na saba na Mikoa mitano ilipata Hati zenyenye mashaka na Wizara tatu zilipata hati chafu. Wizara ya Fedha na Uchumi haina utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kina (*intensive investigation*) kwa taasisi ya Serikali iliyopata hati mashaka au chafu.

Hata hivyo, Wizara ikiwa ni msimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali, inafanya uchunguzi wa kina pale inapoonekana kuna ubadirifu wa mali ya umma. Kwa upande wa Hati ya Mashaka au Chafu, Wizara hutoa maelekezo kwa taasisi husika ili waweze kutunza vizuri vitabu, kumbukumbu na kufanya matumizi kwa mujibu wa sheria.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali amekuwa anagundua makosa mengi sana katika utendaji wa Serikali lakini Serikali pia huwa inapata kigugumizi kikubwa katika kutekeleza ushauri ambao unatolewa na CAG ni kwa sababu gani Serikali huwa haitekelezi moja kwa moja ushauri ambao unatolewa na CAG?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):
Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba ripoti za *CAG* zinatoa ushauri kwa Serikali. Lakini nataka nimwambie kama anazifuatilia kwa ukaribu kila baada ya mwaka, mwaka unaofuata na mwaka mwingine utagundua kwamba yale matatizo yanapungua kwa maana hiyo, ushauri unaotolewa na *CAG* Serikali inautekeleza ipasavyo.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Wizara huwa haifanyi kazi ya uchunguzi (*Intensive Investigation*) na kwa kuwa swalii la msingi liliuliza kwamba kuna kumbukumbu na matumizi mabaya kwa ajili ya taarifa za *CAG* na kwa kuwa ukaguzi wa 2005/2006 ambao uliwasilishwa Bungeni na katika taarifa ya Kamati ya *PAC* huwa kuna taarifa zinazotolewa zinazohusu upotevu wa fedha ikiwa ni pamoja na fedha zilizoibowi, fedha ambazo hazikupokelewa na kwa kuwa sasa Wizara haifanyi ukaguzi. Je, ni chombo gani baada ya Bunge kuweka azimio lake na kukubali taarifa ya *PAC* kinachofanya uchunguzi wa fedha nyingi hizo zinazopotea? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):
Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la C nimesema kwamba Wizara ya Fedha haina utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kina. Lakini pale inapobainika narudia pale inapobainika kuna ubadhirifu hapa umetokea ndipo tunapofanya uchunguzi wa kina. Katika maeneo ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa labda ameyaona kwamba umefanyika ubadhirifu wa kina yale ndiyo maeneo ambayo Wizara inayafanya uchunguzi wa kina.

Na. 297

Uchimbaji wa Visima Virefu/Vifupi kwa ajili ya Maji – Masasi

MHE. DUNSTAN D. MKAPA K.n.y. MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanza kuendeleza mradi wa kuzipatia maji sehemu za Masasi Magharibi katika Kata za Namajani na Namatutwe kwa kuchimba visima virefu na vifupi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani huko huko Magharibi wa kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Kata ya Lukuledi hasa Vijiji vya Lukuledi, Nambawala, Mpanyani, Mihima na Nanyindwa?
- (b) Je, kwa nini mpango mkubwa wa kujenga Bwawa – Lukuledi ambao ungefadhiliwa na Serikali ya Japan na ambao ungeondoa kwa kiasi kikubwa tatizo la maji Magharibi uliondolewa bila maelezo mahsus?
- (c) Je, mradi wa maji Mbinji wa kupeleka maji Masasi hauwezi kufikisha maji yake kwenye maeneo hayo, hata ikibidi kuongeza ujazo kwa kutumia vyanzo vya chemchem vilivyopo Lipitu, Mwena, Mwiti na kadhalika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali hili la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) (b) na (c) napenda kwanza nitoe shukrani zetu za dhati kwa Wabunge wote walio tuchangia katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Ninachopenda tu kusema ni kwamba ahadi yetu kwenu ni kuhakikisha kwamba tunafanya juhudzi zaidi kuwapeni maji ya kunywa, maji ya kilimo cha umwagiliaji na mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Masasi ni mionganoni mwa Wilaya za Mkoa wa Mtwara ambapo mradi wa maji Vijiji uliofadhiliwa na Serikali ya Japan ulitekelezwa mwaka 2005.

Katika eneo la Masasi Magharibi mradi huo ulitekelezwa kwa kuchimba visima virefu katika Vijiji vya Namkungwi, Kilosa, Nanyumbu na Namasogo. Wananchi wanapata huduma ya maji.

Mwaka 2006 shirika lisilokuwa la Kiserikali lijulikanalo kama Masasi Masasi *Environmental Conservation and Agricultural Association (MECAA)* liligharimia uchimbaji wa kisima kirefu katika Kijiji cha Mihima ambapo Halmashauri ya Wilaya ilinunua pampu ya mkono.

Pampu hiyo ilifungwa na inafanyakazi. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ilipata jumla ya shilingi 138,190,000 kupitia programu ya Maendeleo ya sekta ya maji. Sehemu ya fedha hizo zilitumika katika kukarabati visima vifupi vinne (4) katika vijiji vya Nasindi 2 na Napata 2 katika Kata ya Lukuledi.

Aidha, visima virefu viwili vilichimbwa katika Kijiji cha Mpanyani, Kata ya Lukuledi. Kisima kimoja kilipata maji na kilifungwa pampu ya mkono. Sehemu nyingine ya fedha hizo zilitumika katika mradi wa maji Lupaso, kukarabati Ofisi ya Idara ya maji Wilaya, ukarabati wa visima katika kata za Lisekese na Chiungutwa na uhamasishaji wa usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya imepanga kufanya usanifu wa kina wa miradi ya maji katika Kijiji cha Nambawala katika kata ya Lukuledi kupitia *program* ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijiji. Ujenzi wa miradi utaanza mwaka wa 2009/2010 baada ya usanifu kukamilika.

(b)Ni kweli kuwa Serikali ilipanga kujenga Bwawa kubwa katika kijiji cha Mbagala, Kata ya Lukuledi Wilayani Masasi, ili kupata ufumbuzi wa tatizo la ukosefu wa maji katika eneo hilo. Mradi huu ultarajijiwa kuvinufaisha Vijiji vya Namalemba, Chingulungulu, Namatutwa na baadhi ya vijiji katika Kata ya Namajani.

Gharama za ujenzi wa Bwawa hilo kwa wakati huo mwaka 1980 ilikadiriwa kuwa shilingi milioni 2. Kutokana na ukosefu wa fedha Serikali ilisitisha utekelezaji wa mpango huo na badala yake ilichimba visima vifupi 2 na visima virefu 8 katika vijiji nya Chingulungulu, Namajani, Chikoweti na Nanyindwa.

(c)Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Mbinji/Masasi/Nachingwea utakaotumia chanzo cha maji cha Mbwinji una lengo la kufikisha maji katika Miji ya Masasi na Nachingwea, pamoja na vijiji vilivyopo kandokando ya njia ya bomba kuu la kupeleka maji katika Miji hiyo. Kwa wilaya ya Masasi, vijiji hivyo ni Mwena, Mkalapa, Chikundi, Chukukwe, Liyola, Namakongwa na Chanika Nguo. Usanifu wa mradi huo ulifanyika kwa kuzingatia uwezo wa chanzo cha maji cha Mbwinji na mahitaji ya maji kwa ajili ya Miji ya Masasi na Nachingwea na vijiji vilivyo jirani na bomba kuu la maji. Vyanzo nya maji vilivyopo nya Mwiti na Mwena vilibuniwa kwa ajili ya vijiji 15. Chemchemi zilizopo Luputa zinatumwi na Vijiji nya Luputa na Nangoo.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Masasi una matatizo makubwa sana ya maji na kwa kuwa kulikuwa na Bwawa moja la Nchema pale Mjini Massasi ambalo lilikuwa linasaidia sana wananchi pale kupata maji, lakini libomoka kutokana mafuriko.

(a) Je, Wizara sasa haioni ni wakati muafaka kulikarabati lile Bwawa ili wananchi wa Masasi waweze kupata maji?

(b)Kwa kuwa matatizo ya Masasi yanashabihiana sana yale ya Mangaka, watu wa Mangaka wanapata tabu sana ya maji na hawana mahali pa kwenda wanaokota tu maji hapa na pale. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watu wa Mangaka kupata maji safi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la Bwawa la Nchema naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mkapa kama tulivyozungumza katika hotuba yetu kwamba ni utaratibu wetu kuhakikisha kwamba mabwawa yote yaliyokuwa yakifanyakazi halafu yakabomoka basi sisi Serikali tunayapa kipaumbele kwa sababu hakuna haja ya kuanzisha mabwawa mapya kama yale ya zamani yameharibika.

Kwa hiyo, namhakikishia kabisa kwamba hilo nalo tumelichukua tutaliweka katika mipango yetu ya kazi.

Kuhusu Mangata utaratibu wa kuwapa maji kwanza sijui ni Wilayani gani nadhani Nanyumbu nataka niseme kwamba tumejitahidi katika muda huu uliopita tumejaribu kupeleka fedha za *quick wins* kila Halmashauri ya Wilaya na Wilaya ya Nanyumbu sasa najua baada ya kuhama kutoka pale ilipokuwa kumekuwa na mkanganyiko mdogo.

Lakini nina taarifa pia kwamba Wilaya ya Nanyumbu nayo ilipata gawio la shilingi milioni 101 katika fedha zetu hizi za *quick wins*. Kwa hiyo, ninachotaka

kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mipango ya kuwapatia maji wananchi wa Nanyumbu hebu ianzie katika Halmashauri ya Wilaya halafu mje mtuambie sisi kwamba sisi tumepanga hivi. Lakini nimfahamishe kwamba Nanyumbu ilipata shilingi milioni 101,012,000 kwa ajili ya mipango ya maji. (*Makofii*)

MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa matatizo ya Masasi na Nanyumbu yanafanana sana na matatizo ya majirani zao Wilaya ya Tunduru, naomba nipate maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri wana mpango gani juu ya kufufua miundombinu ya Wilaya ya Tunduru kwa sababu ina muda mrefu sana kiasi kwamba inashindwa kuhimili ongezeko la idadi ya watu katika Mji wa Tunduru?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tunduru haiko peke yake. Sisi katika Serikali tunao huo mpango wetu wa *Water Sector Development* ambao tumeainisha Halmashauri zote za Wilaya na zile za Miji ili ziweze kuorodhesha matatizo yao na hatimaye ziweze kufaidi kutokana na fedha za Mkopo wa *World Bank*. Kwa hiyo, Halmashauri ya Tunduru mimi ninachowea kuwaomba tu ni kwamba ili muweze kupata msaada kwa haraka hebu sasa tufuatilia Halmashauri yenewe iweze kukidhi vigezo tulivyoviweka ili baadaye tuweze kupata fedha hizi na hatimaye kazi ianze maana mambo yako mikononi mwetu sasa hatuwezi tena kuwasemama *world bank* ni sisi Halmashauri kujua tunachohitaji ni nini. Ninamwomba Mheshimiwa Mtutura awasiliane na Halmashauri yake wamuonyeshe mipango ya maji pale mtakaposhindwa kitalaam sisi kazi yetu ni hiyo. Mtakaposhindwa kwamba hili limetushinda kitalaam basi mje tuweze kuwasaidia kuwapa watalaanam. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Kijiko niliona unasononeka sana basi uliza swali la nyongeza la mwisho.

MHE. FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la Masasi na tatizo la Tunduru lililotolewa halina tofauti na wale wananchi wanaokaa wanaokaa Mjini wa Kibondo wananchi wapatao 17000 ambao wanaishi bila kuwa na uhakika wa maji. Sijui Waziri anasema nini kuhusu hao wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie kwa kuwa mimi mwenyewe nimefanya ziara Wilayani Kibondo, nimetembelea miundombinu ya Wilaya ya Kibondo, nimekuta ni mbaya kama ilivyo katika Wilaya nyingi na katika miji mingi. Nataka tu nimhakikishie kwamba yale niliyoyaona Mheshimiwa Kijiko nimeyachukua tena ukipenda niseme kibin afsi kwa sababu unazozijua kwamba nitahakikisha Wilaya ya Kibondo nayo na hasa Mji wa Kibondo unapaswa maji kwa utaratibu tulioweka. (*Makofii*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Chunyu Wilayani Mpwapwa wana matatizo makubwa sana ya maji na kwa kuwa wananchi hao tayari wamechangia mfuko wa maji zaidi ya shilingi 1,500,000/=.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia huduma ya maji wananchi hao?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa, George Malima Lubeleje, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Chunyu ni mojawapo kati ya vijiji 10 ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, ilichagua kutokana na maombi yake na kuviweka katika mpango wa utekelezaji wa programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji.

Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2002 kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia na Dola za Kimarekani milioni 2.6 na mchango wa Serikali na walengwa wa dola 1.7. Utekelezaji ulianza katika Wilaya tatu za Mpwapwa, Kilosa na Rufiji kama majoribio ya utekelezaji wa sera ya maji ya mwaka 2002. Programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira muda wake umekwisha tarehe 30 Juni, 2008 na miradi yote ambayo haikukamilika chini ya programu hiyo sasa itatekelezwa na programu ya kuendeleza sekta ya maji (WSDP) kuanzia mwaka 2008/2009. Kijiji cha Chunyu ni miiongoni mwa vijiji 10 vitakavyojengewa miundombinu ya maji chini ya program ya kuendeleza sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na utaratibu wa kutoa fedha za *Quick wins* unaolenga kufanya ukarabati wa miradi ya maji na kutoa matokeo ya mafanikio haraka. Katika mwaka 2006/2007 Wilaya ya Mpwapwa haikupata fedha za *Quick wins* kwa sababu haikupata sifa ya kupewa fedha hizo za ruzuku. Mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imepata sifa za kupata ruzuku hiyo ya kujenga miundombinu ya maji na imepewa shilingi 58,218,00/=.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Lubeleje na wananchi wa Kijiji cha Chunyu, kwa kuchangia mfuko wa maji kwa kiasi cha shilingi 1,500,000. Namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Chunyu wawe sasa na subira kidogo kwa kuwa fedha za utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya maji zipo, mipango ya Halmashauri ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji itaendelea kutekelezwa hata kabla ya watalaam washauri hawajapatiwana.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema fedha zipo na wananchi wa Kijiji cha Chunyu waendelee kusubiri.

(a) Je, kama fedha zipo kwa nini mradi huu usiendelee kutekelezwa?

(b) Kwa kuwa hivi sasa kuna mradi mkubwa wa uboreshaji wa maji Mji wa Mpwapwa unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa kwa ghamara ya shilingi bilioni 3 na kwa kuwa mradi huu haujaanza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana maelezo gani kwa wananchi wa Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Lubeleje na swali la pili kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametokea huko nimeshamwomba ajibu swali hilo la pili. Swali la kwanza kabisa kwa kuwa fedha zipo kwa nini sasa tusitekeleze? Tunarudi pale pale kwamba katika kutekeleza tunatumia utaratibu, tumeshakubaliana kabisa kwamba katika utaratibu huu ziko taratibu za kuandaa, kufanya upembuzi, siyo upembuzi yakinifu lakini upembuzi wa makandarasi ambao watazifanyakazi hizi. Sasa tumeshakubaliana kwamba Halmashauri ya Wilaya iweke wazi taratibu na waanze kupekua sasa nani watazifanyakazi hizi. Sasa hakuna sababu yoyote nzito ya kusema kwa nini sasa usianze isipokuwa ni Halmashauri ya Wilaya yenyewe kuanza kutekeleza. Sisi tumefikiri kwamba kati ya sasa na mwezi wa Machi mwaka ujao, basi tungependa Halmashauri zote ziwe zimekwishakamilisha hii Habari ya kutafuta wakandarasi ili utekelezaji halisi uweze kufuatwa. Kwa swali linalofuata kwa ruksa yako naomba Waziri anisaidie.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumjibu Mheshimiwa Lubeleje, kwanza swali lake la kwanza la nyongeza halafu la pili.

La kwanza ilikuwa ni kumthibitishia tu kwamba mimi mwenyewe baada ya kupita kijiji cha Chunyu na kusimamishwa na wananchi wengi walionionyesha maji ambayo wanatumia sasa nimetiwa moyo sana kwamba lazima tufanye kazi ya bidii wananchi Chunyu wapate maji safi. (*Makofi*)

La pili, kuhusu Mpwapwa niseme tu kwamba Mpwapwa na Utete wana bahati kati ya miji ile 14 wao wamechaguliwa kuanza kutekeleza *program* ya kuendeleza maji katika hiyo miji na usanifu umeshafanyika, fedha zipo, mkandarasi anatafutwa atapatikana hivi karibuni na ataanza kazi na tunategemea kwamba hali itakuwa nzuri na hii miji miwili Utete na Mpwapwa itapata maji safi na salama. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi inayotekeliza katika Wilaya ya Mpwapwa kwa Wilaya ya Masasi tayari ilishatekelezwa lakini visima vilivyo chimbwa katika vijiji vya Mpanyani, Napata havijatoa maji hata siku moja. Je, Mheshimiwa Waziri atafanyaje ili wananchi wale kwenda tena kuangalia vile visima ambavyo havitoi maji ili kuwawezesha wale wananchi waweze kupata maji kwa sababu tatizo bado liko pale pale visima vilivyo chimbwa havitoi maji? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo tumekuwa tukipata kutokana na visima, moja kubwa ni hilo la visima kutokuwa na maji au pampu zinafungwa lakini baadaye zinaonekana hazikidhi mahitaji ya visima hivyo. Kuhusu maji kutopatikana katika visima naomba nimhakikishie Mheshimiwa

Kasembe kwamba pale ambapo tumechimba tukakuta maji hayatoki ni wajibu wetu tena kwenda tena kule kutafuta tena maeneo mengine mpaka tuyapate maji. Kama mahali hapo hayawezi kupatikana kabisa basi lazima tututafuta vyanzo mbadala. Kwa hiyo, ninamhakikishia kwamba watalaam watakwenda tena na kuchagua maeneo mapya ya kuchimba visima. (*Makofit*)

Na. 299

Hitaji la Sheria ya Watu wenyewe Ulemavu

MHE. MARGARETH A. MKANGA aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa watu wenyewe ulemavu ilishakamilika tangu mwaka 2004:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria kuhusu masuala ya watu wenyewe ulemavu nchini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa watu wenyewe ulemavu ilipitishwa na Baraza la Mawaziri tangu mwaka 2004. Aidha, kuwepo kwa sheria kutasaidia sana katika usimamizi wa utekelezaji wa sera ya watu wenyewe kwa maana Serikali imeuona umuhimu wa kuwepo kwa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Margareth Mkanga, pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa tayari Wizara imekwishaandaa rasimu ya Muswada wa sheria ya watu wenyewe ulemavu. Aidha, kwa sasa Wizara inaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri. Ni matarajio yetu kuwa Muswada wa Sheria ya watu wenyewe Ulemavu itawasilishwa Bungeni mapema mwaka huu wa fedha 2008/2009.

MHE. MARGRETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Wizara imesema kwamba Muswada huo utaletwa mapema iwezekanavyo katika mwaka huu wa fedha. Lakini mapema zimekuwa nyingi, ningependa kufahamu mapema hii ya sasa *framework* yake ni ipi? Hilo swali la kwanza.

La pili, nashukuru kwamba rasimu imekwishaandaliwa. Nataka kufahamu ndani ya rasimu ya Muswada huo ulioandaliwa. Je, Wizara imezingatia maudhui yaliyopo

kwenye Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu Duniani ambapo sasa hivi Mkataba huo umekwishakuwa ni Sheria ya Kimataifa kwa sababu nchi zingine zimekwisha kuuridhia pamoja na kwamba Tanzania hatujauridhia?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka nimhakikishie kwamba katika mwaka huu wa fedha tutakuwa na Mikutano ya Bunge iliyosalia mitatu ukiacha Mkutano huu wa Bajeti. Kama tutapata fursa mapema zaidi Muswada huo kupitiwa na Baraza la Mawaziri, nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Bunge lijalo au linalofuatia Muswada huo utaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii lake la pili, nataka nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Muswada wa Sheria umezingatia haki za watu wenye ulemavu kama vile ambavyo Umoja wa Mataifa umetuelekeza.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa watu wengi ambaa hawana ulemavu wamekuwa na tabia ya kuwanyanyasa walemaavu.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali kutokuleta Muswada huo mapema na kuzidi kuuchelewesha si ni muendelezo ule ule wa kuwaunga mkono watu wengi ambaa wanawanyanyasa hao walemaavu na kutowatendea haki na kwa nini Serikali haioni umuhimu huo tangu muda mrefu uliopita?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niwaombe Watanzania wote wasiwanyanyase watu wenye ulemavu.

Watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii ni watoto wetu, ni ndugu zetu, ni mama zetu, ni kaka zetu, ni bibi zetu na ni babu zetu. Kwa hiyo, hatuna budi kuishi nao pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kwamba kwa sababu hiyo anayoilezea yeye tunataka tuweke sheria ili hao watu ambaa wanawanyanyasa walemaavu waweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Nataka Mheshimiwa Mbunge avute subira sheria hiyo itakuja mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

Na. 300

Kuwepo kwa Madini Sehemu Mbalimbali Bukombe

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA aliuliza:-

Kwa kuwa, wapo wananchi wengi Wilayani Bukombe ambaa wamebahatika kupata madini katika mashamba yao, lakini walipokwenda kutafuta *Primary Mining*

Licence wameambiwa kuwa, maeneo yote ya Bukombe yameshachukuliwa na watu mbalimbali. Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ambao wameishi ndani ya maeneo hayo kwa miaka minge jinsi ya kupata leseni hizo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati ya Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu Na. 6 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998, mtu au kampuni yoyote hairuhuswi kujihusisha na shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini bila kuwa na leseni husika. Leseni za utafutaji au uchimbaji madini hutolewa kwa waombaji kwa kuzingatia Kifungu Na. 12 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 kinachoelekeza kuwa mwombaji wa leseni aliyetangulia ndiye mwenye stahili ya kupewa leseni (*first come, first served principle*)

Pamoja na wananchi wa Wilaya ya Bukombe kubahatika kuwa na madini katika mashamba yao, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 (Sura 113), inayotoa miliki ya ardhi, madini yaliyopo ardhi si sehemu ya ardhi ambayo mmiliki wa ardhi ana haki nayo, hivyo Sheria ya Madini ya mwaka 1998 haiwaruhusu kuendesha shughuli za uchimbaji madini katika mashamba hayo bila kuwa na leseni zinazowaruhusu kufanya hivyo.

Baada ya mchimbaji au mtafiti wa madini kupata leseni, Sheria ya Madini kifungu Na. 95(1)(b) inamtaka mwenye leseni ya uchimbaji au utafiti wa madini asianze utafiti au uchimbaji bila kwanza kupata kibali cha maandishi toka kwa mmiliki kwa ardhi. Hivyo kuna uwezekano kuwa maeneo mengi ya Bukombe yameshatolewa leseni za utafiti au uchimbaji madini ila wenye leseni hizo bado hawajaanza kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika Wilaya ya Bukombe kuna wananchi 16 ambao wanamiliki leseni 26 za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha kuna ombi moja la leseni ambalo bado linafanyiwa kazi. Sababu iliyosababisha baadhi ya wananchi wa Bukombe waliowasilisha maombi yao kukataliwa kupewa leseni za uchimbaji mdogo wa madini ni kutokana na ukweli kuwa maeneo waliyoyaomba yalikuwa tayari yalishatolewa kwa waombaji walitangulia kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo endapo kumegundulika rasilimali madini mahali fulani, si vizuri mmiliki wa eneo hilo kuwepo pamoja na shughuli zinazoendelea za uchimbaji, kwa madini kwa sababu nyingi, pamoja na sababu za kiusalamu. Kifungu namba 3 cha Sheria ya Utoaji Ardhi namba 47 ya mwaka 67 *Land Acquisition Act* kinamruhusu Mheshimiwa Rais kutwaa ardhi hiyo kwa manufaa ya umma. Tafsiri ya manufaa ya umma katika Sheria hiyo kifungu cha 4 inajumuisha pia uchimbaji wa madini na petroli. Kwa mujibu wa Sheria ya Utoaji Ardhi, *Land Acquisition Act* ya mwaka 1967, ardhi inapotwaliwa kupisha shughuli za madini, utaratibu wa fidia kwa mwenye ardhi unafanyika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1969 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inawashauri wananchi wa Wilaya ya Bukombe na maeneo mengine yenye madini kote nchini, kufuata Sheria na taratibu zilizopo katika upatikanaji wa leseni na uchimbaji wa madini.

Aidha, tunaahidi kwamba tutafanya jitihada za makusudi za kuongeza ufahamu wa Sheria na taratibu katika maeneo hayo, ambayo wananchi wanajishughulisha na uchimbaji wa madini kwa ngazi mbalimbali. Ni matarajio yetu pia kwamba masuala haya yatafanyiwa kazi kwa kina katika Sheria mpya ya Madini inayoandaliwa.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ambayo ni mazuri yanaonekana kama semina kidogo kwa wananchi wangu. Swali kwa kuwa wachimbaji wamesema katika Wilaya ya Bukombe sehemu kubwa ina leseni za wachimbaji wadogo wadogo na watafiti ambao sio wenyeji. Je, Serikali inaweza ikakubaliana na mimi hata kama siyo leo kunipatia orodha ya leseni ziliko ndani ya Wilaya ya Bukombe, wamiliki wake na muda wake wa kwisha ili wana Bukombe watakapoomba wasikwame kwa ajili ya mgongano huo? (*Makofî*)

Swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Bukombe asilimia 60 ni msitu, na asilimia 40 ni eneo linaishi watu pamoja na shughuli zingine, ikiwa ni pamoja na uchimbaji mdogo mdogo. Serikali inaweza ikakubali kulifanya hilo eneo la *open area* liwe la wachimbaji wadogo wadogo na *STAMICO* wafanye utafiti huo ili wananchi waweze kufaidi na uchimbaji huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kama nilivyosema kuna leseni 26 zinazomilikiwa na Watanzania 16. Nadhani nakubaliana naye kwamba ni utaratibu mzuri kwa wale wanaoomba kuweza kupata taarifa ya leseni ambazo tunatarajia kwamba zitakuwa wazi ndani ya muda mfupi. Tunawashauri wananchi wa Bukombe na Watanzania wengine wote kuwa ili waweze kuendesha shughuli za uchimbaji madini kisheria kama tulivyosema ni lazima wafuate hizi taratibu tulizozizingumza za kuomba leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi wa Bukombe endapo watahitaji kufahamu maeneo yaliyo wazi kwa ajili ya kuomba leseni ninawashauri watumie Ofisi za Madini zilizoko katika maeneo hayo. Kwa wale wa Wilaya ya Bukombe Ofisi hizo ziko katika Mji wa Kahama, ili kupata taarifa za maeneo yaliyo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa hili eneo la wazi. Tulilizungumza wakati wa kuhitimisha maelezo ya Bajeti tarehe 9 Julai, 2008 na tulizungumzia suala la maeneo ya wazi na Mheshimiwa Luhahula aliulizia suala la maeneo yanayobaki baada ya wachimbaji kufanya utafiti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu kwamba maeneo hayo yakibaki yanarudishwa kwenye miliki ya Serikali. Tayari Wizara ya Nishati na Madini inafanya taratibu ili maeneo hayo yazingatiwe kupewa wachimbaji wadogo wadogo na naomba pia

niseme kwamba hili wazo la kwamba *STAMICO* wapewe ili wawewe kuyafanya utafiti ni mzuri lakini pia tukubaliane kwamba kama tulivyosema wakati wa Bajeti, kama ilivyo *TANESCO* kwa umeme na *TPDC* kwa gesi. Ni lengo la Serikali na kwa ushauri wa ninyi Waheshimiwa Wabunge kwamba *STAMICO* ifanye kazi hiyo. Lakini *STAMICO* yenye we pia ipo katika utaratibu wa kuwezeshwa zaidi ili kuweza kufanya kazi hii kwa nguvu na kwa uhakika zaidi. (*Makofî*)

SPIKA: Nimewaoneni wengi tu lakini muda hauruhusu. Kwa hiyo, tumalize swalî la mwisho, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundî. Linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ibeshe Hewa, Viti Maalum Mwanza. Aah! kwa niaba yake Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

Na. 301

Elimu ya *Pre-Form One*

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. MARIA I. HEWA) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetamka rasmi kufuta elimu inayojulikana kwa jina la *Pre-Form One* kwa nchi nzima:-

- (a) Je, Serikali ina uhakika gani kuwa elimu hiyo haipo kabisa katika shule ye yote hapa nchini?
- (b) Kama shule zenyé kuendesha elimu hiyo bado zipo. Je, shule hizo zipo Mikoa ipi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalî la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo rasmi wa elimu na mafunzo katika nchi yetu ni miaka miwili ya elimu ya Awali, miaka 7 ya Elimu ya Msingi, miaka 4 ya Elimu ya Sekondari ngazi ya kawaida, (*O level*) miaka 2 ya elimu sekondari ngazi ya juu na kiwango cha miaka isiyopungua 3 ya elimu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kuna wamiliki wa shule wanaoendesha shule kwa kuwa na utaratibu wa *Pre-Form One*, watambue kuwa huo siyo mfumo rasmi wa elimu ya sekondari katika taifa letu na kwamba wanakiuka Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na Marekebisho yake Namba 10 ya mwaka 1995 na baadaye ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali inawataka wazazi kuwa makini pale wanapowasajili watoto wao katika shule za aina hii kama zipo. Kwani mambo hayo yanapaswa kukubaliana kabla ya mwanafunzi kuanza masomo hayo. Wizara inatoa wito kwa wamiliki wa shule kuzingatia Sheria na Kanuni za Elimu na kuwa hatua stahili zitachukuliwa kwa wale watakaokiuka agizo hilo.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Ingawa muda umepita sasa dakika 4 hivi. Naruhusu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nyawazwa ili tumalize.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo tu. Kwa kuwa Serikali inatambua hiyo kwamba kuna shule nyingi zinakiuka sheria mbaya tu. Kwa kuwa Serikali inatambua kuwa kuna shule nyingi zinakiuka sheria ambazo tumetunga sisi wenyewe. Sasa leo Serikali inasemaje kuhusu shule hizi ambazo zimekiuka sheria za kuanzisha hii *Pre-Form One*?

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mwantumu Mahiza. Na karibu tena Bungeni, sijakuona kwa muda mrefu kidogo.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunikaribisha. Serikali au niseme Wizara hatuna taarifa za kuwepo kwa shule zinazotoa *Pre-Form One*. Kama zipo tunaomba tupatiwe taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo suala hili ni gumu kidogo kwa sababu wazazi wanapowapeleka wanafunzi wao kwenye zile shule, tunawaomba na ninawasihi wasome masharti ya kujiunga na zile shule wanapokikuta kipengele hicho si vyema wao kuwaacha watoto wao pale. Kwa sababu mfumo wetu wa sekondari ni miaka minne na siyo mitano. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita kidogo. Matangazo na nitaanza na wageni tulionao kwa siku ya leo. Nitangulie kusema tu kwamba tunapata wageni wengi na kwa hiyo Ofisi yangu imeweka utaratibu wageni wengine wanafuutilia yanayotokea humu ndani ya Ukumbi küpitia kifaa maalum kichopo katika Ukumbi mkubwa kabisa uliyopo chini ya jengo hili.

Kwa hiyo, mara nyingine hamtawaona hapa lakini wanaweza kuja wanafunzi 50, 50, 50, 50 wakawa 200 ni vigumu kuenea wote hapa. Sasa wageni wa Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mbunge na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ni kama ifuatavyo:-

Bibi Ana Ernest Mkuchika, ambaye ni mkewe. Naomba asimame pale alipo. Ahsante sana. Karibu sana Bungeni. Mwanaye ambaye nimearifiwa anawakilisha wenzake wanne, Eveline Mkuchika, yule pale. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pamoja nao waliokuja, wamejumuishwa kwa pamoja tu Watendaji kutoka Wizarani, ambaye nadhani atakuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara, Bibi Kijakazi Mtengwa, naona Katibu Mkuu yule pale. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mara nyininge Wabunge wanawake huwa wanapiga vigelegele lakini leo naona mmeshangaa tu. (*Vigelegele*)

Sasa wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Mkuchika, ni wawakilishi wa Chama cha Wamiliki wa vyombo vyaya Habari kama ifuatavyo Bwana Reginald Mengi, Mwenyekiti *MOAT*. Naona kama hajafika, Bwana Henry Mhanika, Katibu Mtendaji *MOAT*. Nadhani wako njiani. Yupo, aaah ahsante sana, Katibu Mtendaji. (*Makofi*)

Bwana Samwel Nyala, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Bibi Rose Mwakitwange, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Bwana Absolom Kibanda, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Bwana Said Kubenea, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji. (*Makofi*)

Said Kubenea yuko sijui. Bwana Fayazi Bojani, Mjumbe pia wa Kamati ya Utendaji. Nadhani watakuwa njiani. Waheshimiwa wapo pia wageni wa Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wetu wa Maendeleo na Mifugo na Uvubi amba ni ujumbe kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jinja Uganda. Makao Makuu ya *Lake Victoria Fisheries Organization*, Shirika la pamoja la masuala ya uvubi Ziwa Victoria. Yupo Bwana Dick Nyeko, Katibu Mtendaji *Executive Secretary* yule pale. Karibu sana.

Pia yupo Bwana Mathias Wafula, Naibu Katibu Mtendaji, yule pale, karibuni sana, karibuni sana wageni wetu kutoka huko Jinja na Bwana Geoffrey Nanyaro, Mkurugenzi wa Uvubi, yule pale. Ahsante sana sana Bwana Nanyaro. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, ni Ndugu Haji Sunday Manara, Ahsante sana. Wageni wa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, ni *Reverend Mboni Baga, Askofu Mkuu wa Corinth Church of Tanzania*, Ahsante sana. Karibu sana Askofu. William Masoud Kimondo, Mratibu wa Miradi katika Kanisa hilo. Yule pale, ahsante sana, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr. Emmanuel Nchimbi, Mbunge, jumla ya wachezaji na viongozi 30 wa Timu ya Maji Maji ya Songea. Nadhani wanawenza kuwa wako katika ule Umbo mwengine. Nawakaribisha sana wana michezo. Wageni wa Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ni Ndugu Shafi Barunguza, Katibu wa *CUF Wilaya ya Igunga*, Ahsante sana. Akiambatana na wanachama mashuhuri wa *CUF* kutoka Wilaya hiyo ambaye ni Jumbe Kumega, Bi. Fatma Mhina, Bwana Shabaan Said. Bi. Tatu Ramadhani, Mama Jarosi Japhet na Samwel Mwatanoka. Karibuni sana kutoka Igunga. Karibu na nyumbani kwetu pale. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Diana Chilolo ni wanafunzi 70 na walimu watano kutoka shule ya Sekondari ya Ziwa. *Lake Secondary*, angalau walimu wamepata nafasi

naona, kwa sababu wanafunzi 70 siwaoni. Wanafunzi wapo baadhi yao ahsante sana, simameni waweze kuwaona. Ahsante sana. Mimi nilizoea *Lake Secondary* iko Mwanza sasa hii sijui iko wapi. Hata hivyo karibuni.

Wageni wa Mheshimiwa Ania Chaurembo, ni sasa huyu sina hakika, majina haya ya Zanzibar haya huwezi kujua mwanaume au mwanamke. Sumai Hija, sasa sijui Sumai, unaona sasa, kumbe ni mwanamme. Ni mwanamme aah! Mimi natoka Bara jamani hamjui? Mgeni wa Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata Mbelekesi, Ndugu Iddi Masudi. Yule pale, karibu sana. (*Makofi*)

Wanafunzi 40 kutoka Shule ya *Central*, nadhani hii ni ya Dodoma. Shule ya *Central* na walimu, ni wale pale. Karibuni sana. Tunakutakieni mafanikio katika masomo yenu. Ahsante. (*Makofi*)

Kikundi cha watu 30 wanaoishi na virusi vya UKIMWI, kutoka Kanisa la *Meno Night Tanzania, Diocese* ya Kati. Wale wenzetu 30 ambao wanaishi kwa matumaini. Ahsanteni sana, ahsante sana. Karibuni sana hapa Bungeni.

Sisi Wabunge tuko nanyi na tutaendelea kusaidia kwa kila hali ili muweze kutunzwa katika jamii bila kunyanyapaliwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa hawa wameleta mwisho mwisho hawa, Mheshimiwa John Cheyo, anaomba nitambue kuwepo kwa Mheshimiwa Rachel Mkwabi, huyu Mheshimiwa Mkwapi ni Diwani wa *UDP* kule Meatu. Aah yule pale, karibu sana, karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Vita Kawawa, ameniomba nitambulisse kuwepo kwa wageni wake. Kwanza ni kijana anaitwa Kawawa Vita Mfaume ambaye anasoma *Martin Luther Secondary School* Kawawa uko wapi sasa? Pia shemeji yake Mheshimiwa Vita ambaye anaitwa *Engineer* Hamidu Mbeo, anafanya kazi ya kuchimba mgodi kule Lubumbashi, Congo. Huyu nadhani siyo mjasiriamali. Huyu sasa amekwishakubuhu, ni mfanya biashara mzito huyu.

Wageni wa Mheshimiwa Maige, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, na Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, ni Ndugu Paul Magazi, oooh Mheshimiwa Paul Magazi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kahama. Yule pale, karibu sana, karibu sana. Karibu sana jirani zetu. Nyinyi watu wa Kahama huwa mnaponea mahindi kutoka Urambo. Kwa hiyo tunafurahi sana kuwakaribisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Furaha Kagoro, Diwani wa Kahama Mjini. Yule pale, karibu sana. Ndugu Felix Kimario, Afisa Mipango Miji wa Mji wa Kahama. Ahsante sana. Karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa matangazo ya kazi. Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na

Maji, mukutano leo saa 6 adhuhuri, Ukumbi Namba 227 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji saa 6 kamili mchana huu, Ukumbi Namba 227.

Tangazo la Ofisi, aaah ndiyo nimekwilitoa hili linahusu *basement*. Waheshimiwa Wabunge nafurahi kuwaarifu yafuatayo, nilipoingia humu nilisema nitakuwa na matangazo ya kufurahisha. Michezo, Mheshimiwa Mohamed Rajab, Mwalimu Msaidizi wa Timu yetu ya Bunge, amenipa taarifa ifuatayo kwamba siku ya Jumamosi, tulicheza mpira dhidi ya timu ya CRDB na kama kawaida timu ya Bunge ikashinda kwa goli moja kwa bila. Kwa hiyo CRDB wakalala kwa bao moja kwa sifuri. (*Makofi*)

Siku ya Jumapili yaani jana sasa, baada ya mchezo mkali kabisa, wakaenda Mpwapwa timu zetu sasa ya Miguu na Netiboli mpira wa pete, wakaenda huko kucheza na *veteran* wa Mpwapwa.

Nimepata taarifa kwamba kulikuwa na usaliti wa Wabunge wawili, Lubeleje na Simbachawene pamoja na hayo bado wakafungwa goli moja kwa bila. (*Kicheko/Makofi*)

Kwenye mpira wa mikono, timu machachari ya Wabunge Wanawake wa Bunge letu ikaifunga *veteran* Mpwapwa, loh! magoli 35 kwa 6. Sasa nadhani mtakubaliana na Spika kwamba timu hizi sasa zimefikia kiwango ambacho siyo cha kucheza humu ndani.

Kwa hiyo, nilipopata habari hizi nimewasiliana na Spika, Kenneth Marembe wa Kenya, mfanye mazoezi, tunatarajia nitaongoza mimi mwenyewe timu zetu hizi kwenda Nairobi kwenda kucheza na Wabunge wa Kenya. (*Makofi*)

Kwa tangazo hilo, naomba tu Wabunge wa Kenya wasije wakafanya mchezo uliofanywa na Yanga. Oooh Mheshimiwa Simbachawene, mnajua mnapochelewa kuna wageni wa Mheshimiwa Simbachawene amba ni Masista kutoka Mpwapwa, wale Masista kutoka Mpwapwa. Ahsanteni sana, ahsante sana na karibuni sana.

Namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene kutambua kazi yenu ya kujitoa kweli kweli kwa kuwashudumia watu bila malipo (*Makofi*)

Tangazo langu la mwisho kwamba Kamati Ndogo inayoshughulikia Sheria ya CDF tukutane mara baada ya matangazo haya kwenye Ukumbi wa Spika hapa nyuma, kwenye jengo hili. Na kwa maana hiyo basi itanibidi nitoke.

Sasa namwomba Mheshimiwa Mwenyekiti, Zubeir Ali Maulid, aweze kuja kuongoza shughuli, nitarejea mara baada ya kikao hicho kifupi. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika. Subiri kwanza Mheshimiwa.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Kanuni ya 64 Fasili ya 7. Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tumepokea ratiba mpya ya Buge lako.

Lakini Bunge hili linamalizika na shughuli za Miswada ya Sheria ya Serikali ambayo iko minne na hakuna chochote kuhusu Muswada wa *National Assembly Administration Bill*, pamoja na *CDF*. (*Makofî*)

Pia kulikuwa na ombi la kujadili Taarifa ya Mheshimiwa Bomani ya Madini. Yote haijapewa nafasi. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo. Tarehe zilizotamkwa katika ratiba hiyo ambayo imezingatia zaidi Miswada iliyokwishaiva, ni tarehe 25 mwezi wa nane. Bunge hili linaendelea mpaka tarehe 29 Agosti, 2008

Kwa hiyo, hayo yaliyotamkwa kwa mfano Kamati ya Madini, Muswada wa *National Assembly* na hata mengine, nadhani tutaweza kujadiliana na Serikali, ili ziweze kuwepo kwa sababu tunazo siku nne za kufanya kazi ya ziada.

Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi na kwa kuanzisha mchakato huo ndiyo maana natoka ili tukajadiliane na Kamati Ndogo inayoshughulikia Sheria ya *National Assembly Bill*. Ahsante sana.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir A. Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu endelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Fedha za Serikali kwa mwaka 2008/2009 Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na asasi zake kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kuniwezesha kusimama mbele ya

Bunge lako tukufu leo. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani kubwa kwangu na kunitua kuwa Waziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile sina budi kuwashukuru wazazi wangu, marehemu Mzee Augustino Mkuchika na mama yangu Thecla Bernadetta Mkuchika kwa malezi yao mazuri na upendo mkubwa kwangu. Pia nakishukuru Chama changu, Chama cha Mapinduzi, kwa kunitua kuwa mgombea Ubunge wa Jimbo la Newala, na kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Newala kwa kunichagua kwa wingi kuwa Mbunge wao. Ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais, wananchi wa Newala na Watanzania wote ni kuchapa kazi kwa juhudhi, maarifa na uadilifu kwa faida ya Taifa zima kwa ujumla. Napenda pia kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za kipekee kwa familia yangu, na hasa mke wangu mpendwa, Anna Ernestina, na watoto wangu kwa uvumilivu wao wa kukosa kuwa nami wakati mwingi ninapokuwa safarini kutekeleza majukumu ya kitaifa. Nawashukuru kwa kunitia moyo na kwa mapenzi yao kwangu. Mungu azidi kuwabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na hotuba yangu, napenda vile vile kutumia fursa hii kumpungeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti ambayo ameeleza kwa ufasaha na umahiri mkubwa Utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka wa 2007/2008. Aidha, ametoa malengo ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, MKUKUTA na miongozo mingine ya Kitaifa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake iliyotupa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Pia ametupa mwelekeo wa hali ya uchumi na mapato ya Serikali na kuonyesha maeneo yaliyopewa kipaumbele cha Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwa mwezi Februari mwaka huu, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alivunja Baraza la Mawaziri kufuatia kujiuzulu kwa Mheshimiwa Edward Lowassa aliyekuwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wengine wawili, Mheshimiwa Nazir Karamagi Mbunge, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Ibrahim Msabaha aliyekuwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kufuatia hatua hiyo, Mheshimiwa Rais alimteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kuwa Waziri Mkuu.

Katika kipindi hiki kifupi, tumeshuhudia utendaji makini wa uadilifu, unyenyekevu kwa watu wote, na ushupavu wa Waziri wetu Mkuu. Kwa niaba yangu na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, nachukua fursa hii kumpungeza Mheshimiwa Pinda kwa kuteuliwa kushika wadhifa huu mkubwa Serikalini. Nawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika mabadiliko ambayo aliyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kuchukua nafasi hii vile vile kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimia Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho

kwa kujadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara yangu, niruhusu pia niwapongeze Wabunge wapya waliojiunga nasi katika Bunge lako Tukufu katika siku za hivi karibuni. Nao ni Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum (CCM) na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mbunge wa Kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Taifa lilipata msiba wa Marehemu Salome Joseph Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole familia, ndugu na jamaa wa marehemu hao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuchukua fursa hii vile vile kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa kujadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu tarehe 3 Juni, 2008. Kadhalika, tunaishukuru Kamati kwa kutembelea Taasisi na Miradi mbalimbali inayosimamiwa na Wizara yangu. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hii yamezingatiwa katika bajeti hii kadri ilivyowezekana na tutaendelea kuyafanya kazi maelekezo mengine yaliyobakia na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Wizara. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ina majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa Sera za Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kusimamia utekelezaji wa Sera za Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kuandaa Mipango ya ukuaji wa sekta za Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kuhamasisha uanzishwaji wa vyombo vya Habari katika maeneo ambayo hayavutii sekta binafsi;
- Kukuza na kuimarisha fani mbali mbali za sanaa nchini, hususan sanaa za maonyesho, ufundu na muziki kama kielelezo cha utaifa na chanzo cha ajira;
- Kuimarisha na kukuza Kiswahili na matumizi ya lugha za asili ambazo ni vijenzi vya lugha hiyo na kutoa mafunzo ya lugha za kigeni kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa;
- Kuimarisha utawala bora katika michezo nchini;

- Kukuza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika fani za habari;
- Kuandaa na kusimamia viwango na ubora wa kazi za sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo;
- Kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo; na
- Kusimamia Maendeleo ya Watumishi katika sekta za Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya 2007/2008. Mapato, mwaka wa 2007/2008 Wizara yangu ilipanga kukusanya Mapato ya jumla ya shilingi 229,331,000/= kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2008 jumla ya shilingi 341,320,961/= zilikuwa zimekusanya ambazo ni sawa na asilimia 149 ya lengo la makusanyo ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida, Matumizi Mengineyo na Mishahara kwa mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa 2007/2008 Wizara yangu ilitengewa jumla ya shilingi 11,627,046,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizo zilijumuisha:-

- Mishahara ya Wizara shilingi 1,196,109,000/=;
- Mishahara ya asasi shilingi 2,352,976,000/=;
- Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara shilingi 3,492,925,300/=;
- Matumizi Mengineyo (OC) ya asasi shilingi 4,585,035,700/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa Juni 2008 jumla ya shilingi 11,611,993,897/= zilikuwa zimetolewa. Kiasi kilichotumika ni shilingi 11,610,461,332/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa 2007/2008. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilitengewa jumla ya shilingi 5,339,745,680/= kwa ajili ya kutekeleza miradi kumi (10) ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 4,821,000,000/= zilikuwa fedha za ndani na shilingi 518,745,680/= fedha za nje. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2008, jumla ya shilingi 4,721,000,000/= zikiwa ni fedha za ndani na shilingi 348,745,680/= fedha za nje zilikuwa zimetolewa. Shilingi 5,069,738,680/= zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara imeshuhudia utekelezaji wa kuridhisha wa Malengo ya Dira ya Maendeleo 2025, Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ambayo ni kuwa na Taifa lenye raia wenyewe ufahamu, linalothamini utamaduni wake na lenye wananchi mahiri katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viashiria vya mafanikio haya ni pamoja na:-

- Kuanza kutumika kwa Uwanja Mpya wa Michezo wa Kisasa;
- Kupanda kwa kiwango cha mpira wa miguu nchini kutoka nafasi ya 165 duniani mwaka 2006 hadi nafasi ya 115 mwaka huu;
- Kuongezeka na kuimarika kwa miundombinu ya Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo hususan Chuo cha Michezo cha Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo;
- Kukamilika kwa ujenzi wa Ukumbi wa Maonyesho ya Wazi wa Baraza la Sanaa (BASATA);
- Kukamilika na kuanza kutumika kwa Tovuti ya Wananchi; na
- Kukamilika kwa maktaba ya kisasa ya Picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Habari. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, katika Sura ya Nne Kifungu 116, imeweka bayana azma ya Serikali ya kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari, kueneza Redio ya Serikali na Televisheni ya Serikali nchi nzima; kuanzisha gazeti la Kiswahili la Serikali na kuelimisha waandishi. Katika kutekeleza hayo yote, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Sekta ya Habari imeendelea na Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003 ambayo pamoja na mambo mengine ina lengo la kuweka mazingira yatakayowezesha sekta hiyo kukua, kuhamasisha Vyombo vya Habari kutoa huduma kwa kuzingatia maadili ya taaluma, kuweka utaratibu wa kujenga uwezo endelevu wa sekta hiyo na kuwawezesha wananchi kutoa habari na kupata habari kwa uhuru ili zichangie kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ndiyo Msemaji Mkuu wa Serikali kuitia Idara ya Habari (MAELEZO). Idara kama Msemaji wa Serikali hufanya kazi zifuatazo:-

- Kukusanya na kusambaza kwa vyombo vya habari taarifa kuhusu shughuli za Serikali kote nchini;
- Kusimamia Tovuti ya Wananchi ambayo pamoja na mambo mengine inamwezesha mwananchi kuwasiliana moja kwa moja na Serikali yake;
- Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji;
- Kuratibu shughuli za Vyombo vya Habari, hususan wakati wa maadhisho na matukio ya kitaifa;
- Kuratibu maombi ya wanahabari wa nje wanaotaka kuja kufanya kazi Tanzania kwa vipindi mbalimbali; na
- Kusajili magazeti na majarida.

Msheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sera ya Habari na Utangazaji Wizara yangu imeanzisha mpango wa mawasiliano imara kati ya Wananchi na Serikali yao, baada ya kukamilisha ujenzi wa Tovuti ya Wananchi ambayo mkandarasi aliikabidhi rasmi Serikalini mwezi Aprili mwaka huu baada ya muda wa majaribio. Uanzishwaji wa Tovuti hiyo pia umeiwezesha Wizara yangu kufanikisha mpango wake wa kuanzisha mtandao wa mawasiliano kati ya Idara ya Habari (MAELEZO) na Vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano vya Wizara zote katika jitihada za serikali za kuimarisha uwazi na uwajibikaji Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Tovuti hiyo inafanya kazi vizuri katika kujibu hoja mbalimbali za wananchi. Katika kipindi cha majaribio, kati ya mwezi Aprili hadi Juni 2 mwaka huu, hoja za wananchi zilizoletwa Serikalini ni 1,556. Hoja zilizoshughulikiwa na Serikali ni 762. Hoja ambazo zinashughulikiwa ni 794. Wizara yangu imeandaa mpango maalum wa kuitangaza Tovuti hiyo ya Wananchi kupitia vipindi vya televisheni, redio, magazeti na vipeperushi. Uzinduzi rasmi wa Tovuti hiyo unatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa mwezi Septemba mwaka huu. Baada ya uzinduzi wa Tovuti hiyo na juhudi za kuitangaza, wananchi wengi wataweza kuitumia vizuri zaidi. Aidha, wananchi wako huru kuwasilisha maoni, mapendekezo, maswali na kero zao kupitia ujumbe wa simu zao za mkononi, barua pepe au barua za kawaida kupitia Posta. Tovuti hii inaiwezesha Serikali kupata maoni ya wananchi kuhusu huduma wanazopatiwa na watumishi wa umma na kutafuta njia bora za kuziboresha huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari. Wizara yangu imekamilisha mchakato wa kutayarisha mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari baada ya mashauriano marefu na wadau wa Sekta ya Habari nchini, uliofikia tamati kwa kukusanya mapendekezo hayo. Mambo muhimu yanayozingatiwa katika mapendekezo ya Muswada huo wa Sheria ni pamoja na:-

- Kuanzisha Bodi itakayosimamia viwango vya elimu na taaluma ya habari pamoja na maadili ya taaluma hiyo kwa mujibu wa sheria;
- Kuanzisha Mfuko wa Mafunzo ya wanahabari;
- Kuweka utaratibu bora zaidi wa usajili na umiliki wa vyombo vya habari; na
- Kufutwa kwa sheria za vyombo vya habari zilizopitwa na wakati na ambazo zinalalamikiwa na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maktaba ya Picha. Kutohakana na mabadiliko ya kiteknolojia, Wizara yangu ilianzisha Mradi wa kubadilisha mfumo wa uhifadhi wa picha kuwa katika mfumo wa elektroniki. Mradi huo ulioanza mwaka 2006/2007 umekamilika kwa asilimia 85 na zaidi ya picha milioni mbili zimelewewka katika mfumo wa elektroniki hadi mwishoni mwa mwezi Juni mwaka huu na kazi bado inaendelea. Kuna usemi katika duru za wanahabari kuwa “picha moja ina thamani ya maneno elfu moja”. Usemi huu

unadhihirisha umuhimu wa kuhifadhi picha zenyenye umuhimu wa Kitaifa na Kiserikali kama kumbukumbu ya historia na utamaduni wetu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Malengo ya baadaye ya maktaba ya picha ni kuweza kusambaza picha hizo na kuziuza popote duniani kupitia mtandao wa intaneti. Aidha, tutaendelea kukusanya picha nyingi zaidi zenyenye umuhimu wa kitaifa na kiserikali ili ziweze kuhifadhiwa kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya Wizara yangu ni kutangaza kuwepo kwa Maktaba hii ya kisasa ya picha na ninawahimiza wananchi wenyepicha zenyenye umuhimu wa kitaifa na kiserikali kuzileta Serikalini ili zihifadhiwe katika maktaba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 186 la tarehe 1 Julai, 2007 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992. Majukumu ya Shirika ni pamoja na yafuatayo:-

- Kutoa huduma bora na sahihi za utangazaji kwa wananchi;
- Kueneza usikivu wa Redio na uonekanaji wa Televisheni nchi nzima;
- Kuimarisha mitambo ya Redio na Televisheni kwa kuipatia vipuri na matengenezo wakati wote; na
- Kuongeza uwezo wa Shirika wa kufanya biashara na kujiongezea mapato ya kutosha kuijidesha lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania limeboresha vipindi vyapya redio na televisheni pamoja na kuimarisha usikivu wa redio kwa kujenga vituo vyapya FM katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza, Tabora, Musoma, Bukoba, Kigoma, Mbeya, pamoja na kufunga mtambo wa “*FM International*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Shirika halikutengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mradi unaoendelezwa kutoka mwaka wa fedha wa 2006/2007 ni wa ujenzi wa vituo vyapya FM uliotokana na fedha zilizotolewa shilingi 1,175,772,071.95 kama fidia kwa ajili ya Kituo cha Mabibo, kilichochukuliwa na Serikali kwa ajili ya shughuli nyingine za uwekezaji kitaifa. Shirika linafanya kazi nzuri ya kustahili pongezi. Watu wengi zaidi siku hizi wanasiliza vipindi vyake vyapya redio na kuangalia vipindi vyapya televisheni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya Mwaka 2003, Sehemu ya IV, imeanzisha Kamati ya Maudhui ambayo wajumbe wake wanateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Utangazaji baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano. Kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Kamati hiyo ina wajibu ufuatao:-

- Kumshauri Waziri kuhusu Sera ya Utangazaji;
- Kufuatalia na kudhibiti maudhui potofu ya Utangazaji;

- Kufuatilia uzingatiaji wa maadili ya Utangazaji; na
- Kushughulikia malalamiko yatokanayo na Utangazaji na Maudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/2008 Sekta ya Utangazaji imeendelea kukua na wawekezaji wengi wamezidi kuomba leseni za kuanzisha vituo vya Utangazaji. Mpaka sasa kuna vituo 68 vya redio na vituo 26 vya televisheni na vingine 18 vinavyounganisha na kurusha matangazo ya vituo vingine. Baadhi ya vituo hivyo vinamilikiwa na Serikali za Mitaa, watu binafsi na taasisi za dini. Aidha, kuna jumla ya magazeti na majarida 614. Majarida yaliyosajiliwa hadi Juni, 2008 ni 404 na magezeti ni 210. Majarida na magazeti mengi ni ya mashirika ya umma, taasisi, idara za serikali, watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ambayo inaruhusu wawekezaji kutoka nje ya nchi kumiliki asilimia 49 ya hisa katika kituo cha utangazaji, wawekezaji na wadau walio wengi katika sekta hii ni wazalendo. Kwa ajili hiyo, kumekuwepo na vipindi vingi vinavyotangazwa vya elimu kwa jamii na vinavyohamasisha wananchi katika kujiletea maendeleo. Katika mwaka wa 2007/2008 Kamati ya Maudhui ya TCRA imetekeleza yafuatayo:-

- Kufanya mikutano saba na wadau katika mchakato wa kuhama kutoka teknolojia ya utangazaji ya “*analogue*” kwenda “*digital*”. Mikutano hiyo ilihudhuriwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*), Wamiliki wa Vyombo vya Habari (*MOAT*), watengenezaji wa vifaa vya Utangazaji, Wizara ya Miundombinu, viongozi kutoka Baraza la Maaskofu la Kanisa Katoliki Tanzania na Serikali za Mitaa zinazomiliki vituo vya aina hiyo. Uhamaji kutoka teknolojia ya “*analogue*” kwenda “*digital*” unatakiwa uwe umekamilika ifikapo mwaka 2015, kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa Shirika la Mawasiliano Duniani (*ITU*).
- Kusikiliza malalamiko ya wananchi, watangazaji na wadau mbalimbali yanayohusu vipindi vilivyotangazwa na vituo mbalimbali. Malalamiko hayo yalihusu kupotoshwa kwa ukweli, kutozingatia maadili, kukiuka haki miliki ya maudhui ya vituo vingine na kuendesha shughuli za utangazaji bila kuwa na leseni halali. Kamati ya Maudhui ilifanya vikao vinne kusikiliza malalamiko hayo na vituo viwili vilipewa onyo. Hakuna kituo kilichofutiwa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyoko katika Sekta ya Utangazaji ni kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa sasa ambao ni wa “*analogue*” kwenda “*digital*”. Kama nilivyosema, ifikapo mwaka 2015 televisheni na redio tulizo nazo sasa hazitawenza kutumika bila kuunganishwa na chombo maalumu kutokana na mfumo mpya utakaotumika wa “*digital*”. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanya mikutano mingi na wadau ili kuwaelewesha juu ya ulazima wa kubadilisha teknolojia na pia kuwashauri wajiandae kwa gharama zinazohusu uhamaji huo. Mchakato wa kubadili mfumo huo umeendelea vizuri na *TCRA* sasa inachanganua namna bora ya kupata kampuni itakayojihuisha na urushaji matangazo, kwa jina la kitaalamu, “*Multiplex*

Operator”. Vyombo vyatya habari vilivyopo vitaendelea kujihusisha tu na utengenezaji wa vipindi. Mabadiliko haya ni ya lazima, kwa sababu teknolojia ya “*digital*” inatumia masafa kwa ubora zaidi kuliko “*analogue*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Magazeti ya Serikali - (*TSN*). Kampuni ya Magazeti ya Serikali ilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni (*CAP. 212*) ya mwaka 1961. Wamiliki wa Kampuni hii ni Serikali ya Tanzania yenyeye asilimia 99 ya hisa na Mhariri Mtendaji asilimia 1. Madhumuni ya kuwa na Kampuni hii ni kutoa fursa kwa Watanzania kupata habari sahihi zilizotafitiwa bila upotoshaji. Kampuni inatakiwa kujiendesha kibiashara kama yalivyo makampuni binafsi. Mwaka wa fedha wa Kampuni ni kuanzia Januari hadi Desemba, na hivyo malengo yake yanapangwa kwa mwaka unaoanzia Januari mpaka Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka ulioishia Desemba 2007, Kampuni ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- Kupata faida ya shilingi milioni 351;
- Kuanzisha Maktaba ya elektroniki ya magazeti, picha na machapisho mbalimbali ya Kampuni, tangu ilipoanzishwa mwaka 1961; na
- Kubadilisha sura ya magazeti ya Kiingereza ya *Daily News* na *Sunday News*, ili kuongeza mvuto kwa wasomaji na kuongeza uzalishaji wa nakala za gazeti la HabariLeo ambalo mahitaji yake yamekuwa yakiongezeka kwa kasi tangu lilipozinduliwa tarehe 21 Desemba, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2007, Kampuni ilipata faida iliyokaguliwa ya shilingi milioni 268 ikilinganishwa na lengo la mwaka la shilingi milioni 351. Aidha, Maktaba ya elektroniki ya magazeti, inapokea kutoka kwa nkandarasi picha na machapisho mbalimbali ya Kampuni, tangu ilipoanzishwa mwaka 1961. Usanifu upya wa magazeti ya Kiingereza tayari umefanyika na kinachosubiriwa ni kufanya uzinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utamaduni. Ilani ya Uchaguzi ya CCM imesisitiza azma ya Serikali ya kuendeleza, kuenzi na kulinda historia, mila na desturi nzuri za watu wetu, na kuzitokomeza mila na desturi mbaya. Hivyo basi, Wizara yangu, kwa kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Utamaduni, ina wajibu wa kukuza, kuendeleza na kueneza utamaduni. Idara hiyo inayo majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997;
- Kuandaa mipango ya ukuzaji lugha, sanaa, maadili na utafiti wa mila na desturi;
- Kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu muhimu za utamaduni, ili kufanikisha shughuli za utawala, uendeshaji, mipango na biashara;

- Kuratibu maonyesho, mashindano na matamasha ya utamaduni kitaifa na kimataifa;
- Kukuza matumizi ya lugha sanifu, fasaha pamoja na uandishi;
- Kuratibu shughuli za ushirikiano wa utamaduni baina ya Tanzania na nchi nyingine na katika mashirika ya kimataifa kama vile *UNESCO, SADC, EAC* na *EACROTANAL*; na
- Kuratibu utendaji wa Baraza la Kiswahili la Taifa, Baraza la Sanaa la Taifa, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Mfuko wa Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kuhusu vazi la Taifa. Mheshimiwa Spika pamoja na Bunge lako Tukufu, mtakumbuka kuwa hoja ya kuwepo kwa Vazi la Taifa kwa ajili ya utambulisho wa wananchi wa Taifa letu ni jambo lenye umuhimu mkubwa na wa kipekee. Ni kutokana na umuhimu huo Wizara yangu sasa imedhamiria kuufikisha mchakato wa kutafuta Vazi la Taifa kwenye hitimisho lake. Mchakato wa kutafuta Vazi la Taifa ulianza mwaka 2003 kwa kuwashirikisha Wabunifu wazalendo wa mishono ya nguo ngazi ya Mikoa. Mwaka 2004 mashindano yalifikia ngazi ya Taifa na mavazi 10 bora kwa wanaume na 10 bora kwa wanawake yaliteuliwa. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kufanya utafiti juu ya mwelekeo wa Watanzania wa uvaaji wa mavazi yanayolekea kufanana na yale yaliyoshinda ili kupata mavazi yanayopendwa zaidi. Matokeo ya utafiti huo yametumika kuandaa rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri. Kinachosubiriwa sasa ni kuwasilisha rasimu hiyo kwenye Baraza la Mawaziri kwa maamuzi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/2008 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni ilitekeleza yafuatayo:-

- Idara ilisimamia na kuratibu Tamasha la 26 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania ambalo lilizinduliwa tarehe 23 Oktoba, 2007;
- Kuratibu mchakato wa shughuli za ujenzi wa Jumba la Utamaduni la Taifa ambapo hadi sasa upimaji, tathmini na ulipaji fidia kwa wananchi husika umekamilika;
- Kuendesha Mkutano Mkuu wa Tano wa Sekta ya Utamaduni ambapo wadau takribani 250 walishiriki Mjini Dodoma tarehe 11 – 15 Desemba, 2007;
- Kuratibu na kusimamia maadhisho ya Siku ya Utamaduni Ulimwenguni ambapo huadhimishwa tarehe 21 Mei ya kila mwaka. Kaulimbiu ya maadhisho ya mwaka huu ilikuwa Utamaduni ni Utu na jumla ya vikundi 23 vya utamaduni vilishiriki kikamilifu;

- Kuratibu na Kusimamia tamasha la muziki na ngoma za asili kwa shule 5 za Msingi za Buguruni Viziwi, Lumumba, Msimbazi Wavulana, Mwanamakuka (Bagamoyo), Vingunguti, na Miembeni kwa madhumuni ya kuibua vipaji katika sanaa za maonyesho na muziki;
- Kukarabati Jengo la Maonyesho ya Sanaa katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Uzinduzi wa Jengo hilo unatazamiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2008;
- Kutafiti mila na desturi katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma na Shinyanga ili kubaini hekima za asili zinazoweza kuboresha uandaaji wa sheria mbalimbali;
- Kuendesha Warsha ya utafiti mjini Dodoma tarehe 7 – 9 Januari, 2008 kwa Maofisa Utamaduni kutoka wilaya 19 za Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma. Katika warsha hiyo walengwa walipewa mbinu za utafiti ili waweze kumudu kufanya utafiti wa maeneo muhimu na yale ambayo yapo hararini kupotea kwa lengo la kuyahifadhi; na
- Utafiti wa lugha za asili ulifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Tanga kati ya mwezi Septemba na Oktoba 2007, ili kubaini maneno yanayoweza kutumika katika Kiswahili badala ya yale yanayotatanisha. Kazi hii itaendelea katika mikoa mingine mwaka 2008/2009. Mikoa hiyo ni Iringa, Mwanza, Ruvuma na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Baraza la Kiswahili la Taifa lilitekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuandaa na kufanya semina ya matumizi ya Kiswahili sanifu katika biashara na lebo kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mamlaka ya Vyakula na Dawa Tanzania na Chama cha Haki Miliki Tanzania (*COSOTA*);
- Kukusanya istilahi zenye utata 280 na kuzifanyia uchanganuzi, kuzisanifu na kuzisambaza kwa wananchi;
- Kuandaa na kufanya semina ya mafunzo kwa wakalimani na wafasiri 20. Lengo la mafunzo hayo ni kusaidia kuziba pengo la wataalamu na kuwaongezea umahiri wa fani hizo;
- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya “Lugha ya Taifa”, vipindi 52 vya “Kumepambazuka”, katika redio na vipindi 52 vya “Ulimwengu wa Kiswahili” katika televisheni ambavyo vimewasaidia sana wananchi katika kuelewa maana, matumizi na maendeleo ya Kiswahili kwa ujumla;
- Kuandaa na kufanya warsha ya wahariri wa vitabu vya kiada vya kufundishia shulen. Warsha hii imewasaidia wahariri hao kuwa na urari wa matumizi ya maneno, istilahi, vifupisho, vituo na kadhalika katika vitabu vya kiada. Jumla ya wachapishaji 15 walishiriki katika warsha hiyo;

- Kuhariri Mwongozo wa Waandishi wa Kiswahili Sanifu kwa mara ya mwisho na kuongezewa sura kwa lengo la kutumika katika ngazi ya shule za msingi na sekondari;
- Kusanifu istilahi katika uwanja wa diplomasia na uhusiano wa kimataifa, ambapo muswada wa istilahi 2000 wenyewe fafanuzi na visawe umekamilika;
- Kuhariri Muswada wa kitabu cha Kiswahili kwa Wageni hatua ya kwanza. Warsha ya maandalizi ya kitabu hicho ilifanyika na masomo 20 yalitayarishwa na mapendekezo ya picha yalitolewa;
- Kusoma Miswada ya vitabu nya taaluma na kuipa ithibati. Jumla ya miswada 153 ilisomwa na kupewa ithibati ya lugha;
- Kuratibu na kutoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano ya kimataifa na katika shughuli za Serikali, mashirika, kampuni na watu binafsi. Hati na nyaraka mbalimbali zilitafsiriwa zikiwemo Katiba 5 za vyama nya Soka, Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Mwongozo kwa Madereva na Mwongozo wa Matumizi kwa Usajili wa Bidhaa za Chakula zilizunuliwa kutoka Tanzania;
- Kutoa wakalimani na wafasiri na kuratibu upatikanaji wa wataalamu hao kwa ajili ya mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, Accra Ghana, na Addis Ababa – Ethiopia; Mkutano wa Marais wa Jumuia ya Ulaya na Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika na Mikutano ya Bunge la Afrika;
- Kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo nya habari na watumiaji wengine. Jumla ya makosa 450 yalibainishwa na kuorodheshwa pamoja na usahihi wake. Makosa hayo yamekusanya katika mfululizo wa makala za “Zingatia Matumizi Sahihi ya Kiswahili” ambayo hatimaye yatachapishwa katika Kitabu cha Makosa ya Kawaida katika Kiswahili; na
- Kuandaa kongamano la Idhaa za Kiswahili Duniani ambalo limefanyika kwa mara ya kwanza nchini tarehe 12 hadi 15 Novemba, 2007, na kutangazwa moja kwa moja na Televisheni Zanzibar, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), TBC Taifa na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Takribani washiriki 150 walihudhuria, wakiwemo watangazaji mbalimbali kutoka idhaa za radio na televisheni 7 kutoka nje ya nchi na 9 kutoka ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Baraza la Sanaa la Taifa lilianzishwa kwa madhumuni ya kufufua na kuhimiza maendeleo ya sanaa na kuongeza ubora wa utengenezaji wa bidhaa za sanaa. Majukumu makuu ya Baraza kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1984 ni:-

- Kubeba dhamana ya kufufua na kukuza maendeleo na kuongeza uzalishaji wa kazi za sanaa, ikiwa ni pamoja na utengenezaji na utumiaji wa vyombo nya muziki, nyimbo, mashairi na ngoma za kwetu za mapokeo;

- Kufanya utafiti wa maendeleo na uzalishaji wa kazi za sanaa na utafutaji wa masoko ya kazi hizi, ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa viwango na thamani ya kazi za sanaa zinazotengenezwa Tanzania;
- Kutoa huduma za ushauri na misaada ya kiufundi ambayo ni ya lazima au ya nyongeza katika kuendeleza shughuli za sanaa kwa mashirika ya umma na kwa watu mbalimbali wanaojishughulisha na kazi hizi;
- Kuandaa mipango na kuratibu shughuli za sanaa zinazofanywa na watu mbalimbali Tanzania;
- Kuishauri Serikali juu ya mambo yahusuyo maendeleo na uzalishaji wa kazi za sanaa nchini Tanzania; na

- Kutoa na kuimarisha njia na vifaa vya mafunzo kwa ajili ya watu wanaojishughulisha, walioajiriwa au watakaoajiriwa katika vyombo vya uzalishaji wa kazi za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/2008 Baraza lilitekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa mpango wa utafiti na uhifadhi wa makala na nyaraka za sanaa. Walengwa wa mpango huo wakiwa wakufunzi, wajasiriamali, watawala na viongozi wanaojishughulisha na shughuli za sanaa;
- Kuendelea na mchakato wa kuhuisha Sheria Na. 23 ya mwaka 1984 inayoliunda Baraza;
- Kukamilisha kazi ya kuhuisha Muundo wa utumishi wa Baraza. Kibali cha kuanza kutumika kilitolewa tarehe 1 Julai, 2008;
- Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa wazi wa Maonyesho ya Sanaa. Unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwaka huu; na
- Kutoa mafunzo kwa jumla ya wasanii 538: 163 katika Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma; 200 kutoka Wilaya ya Kasulu, Mkoani Kigoma; 80 kutoka Manispaa ya Iringa na Wilaya ya Iringa Vijijini; 35 kutoka Morogoro Vijijini; na 60 kutoka Mkoani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/2008 Baraza lilikadiria kukusanya mapato ya shilingi 40,520,000/= kutoka vyanzo vifuatavyo:-

- Usajili wa vibali kwa uendeshaji wa shughuli za sanaa shilingi 15,660,000/=.
- Upangishaji wa baadhi ya majengo kwa ajili ya matumizi ya ofisi na vibanda vya biashara shilingi, 24,860,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa Juni 2008, Baraza lilikusanya jumla ya shilingi 32,899,800/= sawa na asilimia 81 ya matarajio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Jukwaani. Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani iliundwa kwa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya mwaka 1976. Majukumu ya Bodi ni haya yafuatayo:-

- Kuhakikisha kwamba Filamu na Michezo ya Kuigiza zinawiana na mila, desturi na maadili mema ya jamii ya Watanzania;
- Kuhakikisha kwamba Filamu na Michezo ya Kuigiza zinawapa Watanzania burudani safi na stahili yenye elimu na mafunzo mema;
- Kuhakikisha kwamba Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini zinakuwa zenye viwango stahili vya usanii na ujumi.
- Kuhakikisha kwamba usanii na uhuru wa ubunifu wa sanaa hauzuiliwi na kuwekewa vipingamizi bila sababu za msingi; na
- Kuhakikisha kwamba ukuaji na maendeleo ya fani za Filamu na Michezo ya Kuigiza unawiana na unalingana na mabadiliko halisi ya msimamo na mtazamo wa jamii ya Watanzania kuhusu maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/2008 Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ilitekeleza yafuatayo:-

- Kukagua filamu na kanda za video 500, vikundi vya sanaa za maonyesho 30 na kutoa ushauri wa kuzingatia maadili kwa waandaaji 300 wa vipindi vya maigizo na programu mbalimbali za televisheni;
- Kutoa mafunzo ya maadili ya filamu na utamaduni kwa wadau wa filamu na sanaa za maonyesho kuitia mpango shirikishi wa mikutano, semina, warsha na vipeperushi, kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa; na
- Kukusanya takwimu za fani ya filamu na sanaa za maonyesho hususani vikundi vya wasanii wa filamu, wamiliki wa vituo vya televisheni na wasambazaji wa filamu katika Mikoa ya Morogoro na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa ili kufanya kazi zilizokuwa zinafanywa na Chuo cha Sanaa Bagamoyo. TaSUBa ilianzishwa rasmi tarehe 2 Novemba 2007 kwa tangazo la Serikali Na. 220, kwa mujibu wa Sheria Na.30 ya mwaka 1997 ya kuanzishwa kwa Wakala za Serikali. Dira ya TaSUBa ni kuwa

Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha ubora uliotukuka katika Afrika. Majukumu ya TaSUBa ni pamoja na:-

- Kutoa mafunzo ya kiwango cha hali ya juu ya sanaa na utamaduni katika fani za ngoma, maigizo, muziki, sanaa za ufundi, ufundi Jukwaa, teknolojia ya habari na mawasiliano, utafiti na uongozi wa shughuli za sanaa na utamaduni;
- Kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu wa sanaa na utamaduni; na
- Kuzalisha kazi za sanaa na utamaduni zilizo katika kiwango cha hali ya juu cha ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/2008 Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ilitekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 105 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 150 walio kazini katika sehemu mbalimbali nchini;
- Kuendesha Tamasha la 26 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania lililofanyika mwezi Oktoba 2007 na lilifunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein.
- Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Maonyesho kwa asilimia 90. Ukumbi huo unatarajiwa kuzinduliwa tarehe 13 Oktoba 2008 wakati wa ufunguzi wa Tamasha la 27 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania;
- Kujenga mabweni matatu na nyumba ya Mtendaji Mkuu. Kazi hiyo tayari amekabidhiwa mkandarasi; na
- Kukamilisha mchakato wa kukigeuza Chuo cha Sanaa Bagamoyo kuwa Wakala wa Serikali ifikapo Novemba 2007 ambapo uzinduzi wake ulifanyika tarehe 16 Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuzihamasisha Halmashauri kupeleka watendaji wake, hususani Maofisa Utamaduni wa Wilaya, katika Taasisi hii imefanyika na inaendelea. Katika mwaka wa fedha uliopita walikuwapo Maofisa Utamaduni wanne kutoka Halmashauri za Wilaya ya Mbozi, Mpanda, Kiteto na Ruangwa waliokuwa wakichukua kozi fupi. Aidha, Maofisa Utamaduni wa Wilaya nne kutoka Halmashauri za Wilaya ya Mtware, Nanyumbu, Lindi na Bukoba walimaliza masomo yao ya kozi ndefu mwaka huo huo. Kwa mwaka huu wa fedha wapo Maofisa Utamaduni wanne kutoka Halmashauri za Wilaya ya Singida, Simanjiro, Bukoba na Handeni wanaoendelea na masomo ya kozi ndefu. Wizara inasilitiza umuhimu wa Halmashauri zote nchini kuitumia Taasisi hiyo kwa kuapeleka wataalamu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Mfuko wa Utamaduni Tanzania ni asasi ya kiutamaduni inayoendesa shughuli zinazohusu utamaduni hapa Tanzania. Mfuko ulianzishwa na Serikali mwaka 1998 kwa madhumuni ya kuimarisha na

kuwezesha Sekta ya Utamaduni kuchangia kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya uchumi wa Taifa kwa kuhamasisha jamii kujituma kufanya shughuli za utamaduni zenyet kuchochea ubunifu, kuzingatia ubora wa bidhaa, kuongeza kipato katika kaya na kuhimiza ajira za kujitegemea. Ili kufanikisha majukumu haya Mfuko unatekeleza majukumu maalum yafuatayo:-

- Kufadhili miradi na shughuli za utamaduni.
- Kutoa tuzo kwa kazi bora za utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007/2008 Mfuko wa Utamaduni ulitekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuendesha semina kwa Waheshimiwa Wabunge 177 mjini Dodoma tarehe 11/12/2007 kuhusu wajibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni;
- Kufanya tathmini ya shughuli za Mfuko katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2005 hadi 2007. Katika tathmini hiyo iliamuliwa kuwa Mfuko ufanyiwe marekebisho ili kwenda sambamba na majukumu mapya baada ya baadhi ya wafadhili kusimamisha ufadhili wao;
- Kuendesha mikutano wa wawakilishi wa wadau wa sekta watakaopokea matokeo ya tathmini Agosti 2008 mjini Morogoro ambapo jumla ya wadau 27 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar walishiriki;
- Kufanya mikutano na wafadhili wakuu wa Mfuko. Baadhi ya mikutano muhimu iliyofanyika ni kati ya Mfuko na Serikali ya Norway tarehe 12/11/2007; SIDA, Sweden tarehe 17/12/2007 na Finland tarehe 19/05/2008;
- Kuendesha warsha za kukamilisha mchakato wa kuboresha muundo wa uwajibikaji wa majimbo ya Mfuko kwa Wadau wa Sekta tarehe 12 hadi 16/05/2008 mjini Morogoro. Majimbo ya Mfuko yamegawanywa kulingana na fani kama ifuatavyo: Sanaa za Maonyesho, Sanaa za Ufundu, Filamu za Vielelezo, Urithi wa Utamaduni, Tasnia za Utamaduni na Luga na Fasihi; na
- Kufadhili watu binafsi, taasisi, vikundi na vyama ili kuendeleza fani mbalimbali za utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Michezo. Moja ya mambo ambayo yamesisitizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ni Serikali kujihusisha kwa nguvu zaidi na maendeleo ya michezo nchini, ili kuhakikisha kwamba ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya Kimataifa unalingana na vipaji vilivyopo nchini. Tunaamini kwamba vijana wa Tanzania wana vipaji vya michezo mbalimbali kama walivyonavyo wenzao wa nchi nyingine za Afrika na za Dunia. Hivyo basi, Wizara yangu inalo jukumu la kuendeleza michezo kwa mujibu wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005, pamoja na Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Yafuatayo ndiyo mambo muhimu yaliyotekeliza na Wizara

yangu katika kipindi cha mwaka wa 2007/2008. Kuendelea Kusimamia Ukamilishaji wa Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo la Taifa. Awamu ya kwanza ambayo ilihu ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo wenyewe uwezo wa kuchukua watu 60,000 wakiwa wamekaa, umekamilika kwa asilimia 95. Kazi ya uwekaji wa zulia la kukimbilia (Tartan) katika eneo la michezo ya riadha imekwishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja Mpya wa Kisasa ni mradi mkubwa unaohitaji menejimenti ya kitaalamu. Wizara ilitangaza zabuni kupata Kampuni binafsi yenyenye nia na uwezo wa kufanya kazi kibiashara. Kampuni nne zilijitokeza na baada ya uchambuzi wa zabuni, hakuna Kampuni iliyofaulu kulingana na vigezo vya zabuni hiyo. Wizara imetangaza upya zabuni hiyo ili kutoa nafasi kwa Kampuni nyingine zaidi. Ukarabati wa Uwanja wa Taifa, uwanja wa zamani wa Taifa umekarabatiwa na Serikali na uliwekwa nyasi bandia kwa msaada wa FIFA, hivyo kuuwezesha kutumika kuchezea michezo mingi kwa wiki kuliko ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ipo kwenye mchakato wa awamu ya pili ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo ambalo tunatarajia kutumia mfumo wa Kujenga, Kuendesha na Kukabidhi (*Build, Operate and Transfer – BOT*). Hatua iliyofikiwa ni ya kuandaa Nyaraka za Zabuni ya BOT na kuititia upya mchanganuo wa kibiashara. Ujenzi huo unajumuisha Uwanja wa Maandalizi, Uwanja wa Ndani, Bwawa la Kuogelea lenye viwango vya Olimpiki, Uwanja wa Mazoezi wa Mpira wa Miguu, Uwanja wa Kriketi, Kumbi za Mikutano, Chuo cha Michezo na Hosteli yenyenye vyumba 750 vikiwemo vyumba vya hadhi ya hoteli ya nyota tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya Michezo Tanzania ilifanyika tarehe 21 Septemba, 2007 katika Uwanja wa Mnazi Mmoja Dar es Salaam. Kaulimbiu ya maadhisho haya ilikuwa Michezo kwa Amani na Maendeleo. Serikali ilitumia siku hii kuwashimiza wananchi na bado inaendelea kuwashimiza wananchi wapende kushiriki katika mazoezi ya viungo vya mwili ili kujenga mwili timamu wenyewe nguvu na afya, hivyo kutumia michezo kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Wizara inasisitiza kuwa maandalizi ya michezo hii yamefanyika nchi nzima kuanzia ngazi ya Kijiji, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilishiriki katika michezo ya Mataifa ya Afrika iliyofanyika nchini Algeria kwa kuwakilishwa na wachezaji 21 na viongozi 9 wa michezo ya riadha, ngumi na michezo kwa watu wenyewe ulemavu wa viungo vya mwili (Paralimpiki). Nchi yetu ilipata medali moja ya fedha katika michezo wa Marathon ambapo Mwanariadha Martin Sule alishika nafasi ya pili. Katika michezo hii nchi yetu ilishika nafasi ya 33 kati ya nchi 52 zilizoshiriki. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya utaalamu wa Michezo (ualimu, uamuzi, uongozi na Kinga na Tiba kwa wanamichezo). Jumla ya washiriki 300 walihudhuria mafunzo haya katika vituo vyetu vya Michezo Kanda za Kaskazini (Arusha) na Kusini (Songea). Pia, mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya ufundishaji Michezo yalianza mwezi Januari 2007 katika Chuo cha Michezo Malya na yanatarajiwa kumalizika mwezi Agosti 2008. Jumla ya wanachuo 34 wanashiriki katika mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisajili Vyama na Vilabu vya Michezo kulingana na Sheria na Kanuni za Michezo. Jumla ya vyama na vilabu vya michezo 144 vilisajiliwa na jumla ya Katiba 250 zilidurusiwa. Kadhalika, Wizara ilikutana na uongozi wa Vyama 22 vya Michezo ngazi ya Taifa katika kuboresha Mipango Mkakati ya Vyama hivyo kwa ajili ya Maendeleo ya Vyama vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha na kuongeza miundombinu ya michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, maktaba yenyewe uwezo wa kuchukua watu 70 kwa wakati mmoja na Chumba cha Kompyuta chenye kompyuta 30 vimekamilika na vinatumika. Aidha, jumba la Michezo ya Ndani limekamilika kwa karibu asilimia 80. Natoa mwito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, na Taasisi za Watu binafsi kupeleka wanamichezo wake kusoma katika Chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliiwezesha timu ya '*Special Olympics*' (Michezo kwa Watu wenye Ulemavu wa Akili) yenyewe wachezaji 24 na viongozi 6 kushiriki katika Michezo ya Dunia iliyofanyika Shanghai – China. Timu hii iliyoshiriki katika michezo ya riadha na mpira wa miguu iliiletea nchi yetu sifa kem kem kwa kutwaa jumla ya Medali 33, zikiwemo 19 za Dhahabu, 6 za Fedha na 8 za Shaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilianda mazingira mazuri kwa Timu ya Taifa ya mpira wa miguu iliyoshiriki katika mashindano ya kutafuta nafasi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika 2008 huko Accra - Ghana. Timu yetu ilishiriki na kushika nafasi ya tatu katika michuano ya makundi. Timu hii imepata mafanikio ambapo imepanda katika kiwango cha mpira wa miguu kinachowekwa na Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), kutoka nafasi ya 165 mwaka 2006 hadi nafasi ya 115 duniani hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuinua kiwango cha michezo nchini, mashindano ya Kombe la Taifa kwa mpira wa miguu yalifanyika kwa ufanisi yakishirikisha Mikoa 23. Katika mashindano hayo, Mkoa wa Ilala uliibuka bingwa. Pia mashindano ya mpira wa miguu kwa Vijana wenye umri wa chini ya miaka 17 (*Copa Coca Cola*) yalifanyika mwezi Juni 2008 na kushirikisha Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mkoa wa Ruvuma uliibuka bingwa. Aidha, mashindano ya Kombe la Taifa kwa michezo wa Netiboli yalifanyika yakishirikisha Mikoa minane ambapo Mkoa wa Dar es Salaam ulichukua ubingwa. Natoa mwito kwa Mikoa ambayo haikushiriki mwaka huu kuhakikisha kuwa mwakani inashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mashindano ya *Copa Coca Cola*, timu yenyewe jumla ya vijana 16 ilichaguliwa kwa nia ya kuiwakilisha Tanzania katika mashindano ya kimataifa yaliyofanyika Brazil. Katika mashindano hayo ya Brazil, Timu ya Tanzania ilinyakua ushindi wa kwanza kwenye kundi lake baada ya kucheza na kupata matokeo kama ifuatavyo:-

-	Tanzania Vs Chile	0:0
-	Tanzania Vs Argentina	2:0
-	Tanzania Vs Paraguay	2:1
-	Tanzania Vs Chile (Fainali)	1:0

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulishukuru tena Bunge lako Tukufu kwa kuwapokea, kuwapongeza vijana wetu hapa Bungeni tarehe 17 Julai, 2008 na kuwachangia zawadi ya fedha Shilingi 3,180,000/=. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchezo wa “*Kick Boxing*” mchezaji wa Tanzania, Ndugu Japhet Kaseba alililetea Taifa heshima kwa kushinda ubingwa wa Dunia tarehe 24/11/2007 na kuutetea tarehe 29/6/2008 kwa kumshinda mchezaji toka Ufilipino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya katika michezo yanatokana na mambo yafuatayo:-

- Kuundwa kwa mkakati wa Operesheni Ushindi;
- Serikali kuajiri Makocha kutoka Brazil, Bw. Marcio Maximo (Kocha Mkuu wa Taifa Stars), Bw. Amorin Itamar (mtaalam wa mazoezi ya viungo) na Bw. Marcus Tinoco (kocha wa timu ya vijana chini ya miaka 20);
- Kupata michezo ya kirafiki ya kimataifa ya nje na ndani ya nchi ambayo imewapa uzoefu wachezaji wetu;
- Msukumo uliotolewa na Viongozi wa juu kitaifa akiwemo Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge, Wafadhili, Wadau na Watanzania kwa ujumla katika kuigharamia na kuishangilia kizalendo; na
- Kujitokeza kwa wafadhili wa michezo wakiwemo Mohamed Enterprises, Tanzania Breweries, Serengeti Breweries, Coca-Cola, NMB, GTV, TICS, na wengine wengi huko Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango wa ushirikiano na nchi ya Ujerumani, Serikali imempata mkufunzi wa michezo wa riadha Bw. Peter Hans Thumm. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta makocha kwa ajili ya michezo mingine kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia michezo iliendelea kupambana na tatizo la Maambukizi ya UKIMWI kwa kuendeleza programu ya mongoarika la wanamichezo. Jumla ya wanamichezo 74 kutoka tarafa ishirini za Wilaya ya Kilosa walipata mafunzo kupitia mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu, ilipata heshima ya kuwa nchi pekee barani Afrika kupewa nafasi ya kukimbiza Mwenge wa Olimpiki tarehe 13 Aprili 2008. Mbio za Mwenge huo zilianzishwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, na ulikimbizwa kwa amani na utulivu wa hali ya juu. Madhumuni ya mwenge huu ni kuashiria kuanza kwa michezo ya Olimpiki na pia ni alama ya Amani na Urafiki kupiditia michezo pote duniani. Ujio wa mwenge huu katika Taifa letu umetupa faida nyingi zikiwemo heshima kimataifa, kukuza uchumi kupiditia wageni wengi walioingia nchini wakalala kwenye hoteli na kununua vitu vya Kitanzania, kuwahamasisha wanamichezo wetu kuinua viwango vyao na kukuza urafiki uliopo kati yetu na China. Nawaomba Watanzania wenzangu kuendelea kuilinda amani katika taifa letu maana bila kuwepo amani, hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Baraza la Michezo la Taifa liliundwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na Marekebisho yake katika Sheria Na. 6 ya mwaka 1971. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, majukumu ya Baraza ni pamoja na:-

- Kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo;
- Kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano mionganoni mwa Vyama vya Michezo mbalimbali; na
- Kuidhinisha mashindano ya Kitaifa na Kimataifa katika michezo na matamasha yanayoandaliwa na Vyama vya Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukukumu mengine ni pamoja na:-

- Kuandaa, baada ya kushauriana na vyama vya michezo vinavyohusika, mashindano na Tamasha za Kitaifa na Kimataifa kwa nia ya kubadilishana uzoefu na kukuza mahusiano ya kirafiki na mataifa mengine;
- Kuamsha ari ya kupenda aina zote za michezo kwa ngazi zote; na
- Kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwezesha kuwepo fursa za michezo kwa ngazi zote na kujitahidi kujenga moyo wa uanamichezo na nidhamu ya hali ya juu kwa wanamichezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Baraza la Michezo la Taifa lilitekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuanzisha mchakato wa kufufua michezo kuanzia ngazi ya vijiji kwa kuanza na utoaji mafunzo kwa Walimu wa Michezo katika Wilaya. Jumla ya walimu 320 katika Wilaya za Kondoa, Kasulu, Tabora na Nzega wamepata mafunzo. Lengo ni kutoa

mafunzo katika Wilaya zote Tanzania Bara katika kipindi cha miaka 3 kuanzia mwaka 2007/2008;

- Kuendesha mchakato wa Mjadala wa Maendeleo ya Michezo katika Wilaya zote na Mikoa yote Tanzania Bara kama sehemu ya maandalizi ya Mjadala wa Taifa;
- Kuendesha mafunzo ya Elimu ya UKIMWI kuitia michezo na utunzaji wa mazingira kuitia michezo kwa Waalimu wa michezo katika Wilaya za Kasulu, Tabora, Nzega, Kondoa, Babati, Karatu, Kilindi na Ngara. Pia, kuendesha mafunzo ya mapambano dhidi ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa BMT;
- Kupeleka wafanyakazi wawili masomoni ambapo mmoja amehitimu mafunzo ya Utunzaji Kumbukumbu (ngazi ya cheti) kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma – Magogoni na mwingine anaingia mwaka wa pili kuchukua mafunzo ya Diploma ya Uhasibu. Aidha, wafanyakazi wawili walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Michezo kwa jamii, nchini Nigeria;
- Kutoa jumla ya mipira 180 na Bips 200 katika Wilaya za Tabora, Nzega, Kondoa, Kasulu, Babati, Karatu, Kilindi na Ngara kwa ajili ya kuhamasisha maendeleo ya michezo katika Wilaya hizo;
- Kusimamia chaguzi za Vyama vya SHIMIVUTA, SHIMMUTA na Tanzania SHOTOKAN karate;
- Kusambaza nakala 300 za vitabu vya Sheria ya BMT katika Wilaya na Mikoa yote Tanzania Bara ili kuwezesha wadau kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu marekebisho ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utawala na Utumishi. Katika mwaka 2007/2008, Wizara imeendelea kukamilisha upatikanaji wa wafanyakazi wenye sifa, kwa kuajiri watumishi wapya kujaza nafasi wazi kwa mujibu wa Ikama iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nafasi wazi zilizokuwepo ni 79, kati ya hizo nafasi 64 zimejazwa. Nafasi 15 hazikupata waombaji wenye sifa na mchakato wa kuzijaza unaendelea. Aidha, watumishi kumi na nne walipandishwa vyeo na watumishi 15 walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwajengea uwezo watumishi, Wizara imeendelea kuwagharamia watumishi 14 mafunzo ya muda mfupi na mrefu, mafunzo ya Shahada ya kwanza watumishi wawili, Shahada ya Uzamili watumishi tisa, Shahada ya Uzamifu mtumishi mmoja, Stashahada ya Kawaida mtumishi mmoja, na Cheti mtumishi mmoja. Vile vile, Wizara imepeleka jumla ya watumishi ishirini na nne kwenye mafunzo mbalimbali ya muda mfupi. Katika kipindi hicho Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi 150 juu ya Sheria ya Usalama ya mwaka 1970 pamoja na kuwafanya upekuzi (vetting). Wizara pia imeweza kutoa mafunzo juu ya Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma kwa watumishi 225 na kukabidhiwa vitabu vya Kanuni hizo ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002. Aidha, watumishi watatu wanaendelea kulipiwa gharama za kujiendeleza wenyewe kwa lengo la

kupata elimu ya Sekondari ambayo ndiyo kiwango cha chini kilichowekwa na Serikali kwa ajira ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za Wizara kuhamasisha na kuwaelimisha watumishi juu ya ugonjwa wa UKIMWI na namna ya kupambana nao, Wizara kwa kushirikiana na *TACAIDS* imeendelea kutoa mafunzo na elimu ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa watumishi 244 wa ngazi zote, Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi, na wale wa Kamati za Uadilifu za Wizara na Taasisi zilizo chini yake wapatao 28. Mafunzo hayo yalihusu pia zoezi la kupima Virusi vyta UKIMWI kwa hiyari. Aidha, Wizara iliendesha warsha kwa viongozi 36 wa vyama vyta wasanii na Vijana nje ya shule 74 katika wilaya ya Kilosa kwa lengo la kuwapa uwezo wa kubuni na kuibua hisia zitakazoleta hamasa ya kupima kwa hiyari ili kujierepusha na maambukizi ya UKIMWI. Ni matarajio ya Wizara kuwa wale wote waliopata elimu hiyo wataitumia kuelimisha jamii wanayoishi nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Wizara kuwezesha uundwaji wa tawi la TUGHE na Baraza la Wafanyakazi, kwa lengo la kuwawezesha watumishi kushauri uongozi wa Wizara juu ya mambo mbalimbali yanayoihusu Wizara na maslahi yao, Wizara imeendelea kutumia vyombo hivi katika kutoa ushauri na utekelezaji wa dhana ya ushirikishwaji wa watumishi katika sehemu za kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kupunguza mianya ya rushwa na kuhakikisha inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya fedha ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2001, kutumia Kamati za Uadilifu za Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Maadili na Sheria zinazoongoza Utumishi wa Umma. Vile vile Wizara imeendelea kutumia Kamati ya Ukaguzi ya Wizara kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha zilizotengwa kutekeleza shughuli mbalimbali. Usimamizi huu umeiwezesha Wizara kupata Hati Safi za Ukaguzi wa Hesabu tangu Wizara ilipoanzishwa mwaka 2006/2007. Katika kuwawezesha watumishi kiuchumi, Wizara imeweza kuunda Ushirika wa Kuweka na Kukopa – SACCOS. Jitihada za kuimarisha chama hicho zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Mwaka 2008/2009. Sekta ya Habari, waraka kuhusu Mapendekezo ya Sheria ya Kusimamia Vyombo vyta Habari unatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo ya wadau kuwa mengi, Serikali imeamua kutunga sheria nyingine ya pili ya habari itakayoitwa “Sheria ya Haki ya Kupata Habari”. Mchakato umeanza. Ni matumaini yangu kuwa utaweza kufikishwa katika Bunge lako tukufu mapema mwakani. Mapendekezo ya Sheria hiyo ya pili yana malengo yafuatayo:-

- Kuvipa Vyombo vya Habari uhuru mkubwa zaidi katika kutafuta na kutangaza habari kwa kuzingatia maadili ya taaluma ya habari ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 116 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005;
- Kulinda vyanzo vya habari vya waandishi wa habari; na
- Kuwalinda watoto na vijana dhidi ya taarifa na picha zisizofaa kwa malezi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurekebisha kasoro ya kuchelewesha majibu ya hoja za wananchi katika Tovuti, Wizara yangu katika mwaka ujao wa fedha itaendeleza mafunzo ya watendaji wa Wizara mbalimbali wanaohusika na Tovuti ya Wananchi na kufanya mkutano wa Makatibu Wakuu wa Wizara zote kuzungumzia umuhimu wa Tovuti hiyo ya Wananchi. Kama nilivyoeleza hapo awali, Tovuti ya Wananchi inatarajiwa kuzinduliwa rasmi mapema mwezi Septemba mwaka huu. Ni matarajio yangu kuwa baada ya uzinduzi huo, Watendaji Wakuu Serikalini watazidisha kasi ya kujibu hoja za wananchi, ili Tovuti hiyo kweli ikidhi haja na matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). *TCRA* katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 imejipanga kuwaelimisha wananchi juu ya faida ya mfumo wa utangazaji katika teknolojia ya “*digital*”. Elimu kwa umma itatolewa kwa njia ya redio, televisheni, vipeperushi, warsha pamoja na njia nyingine mbadala ili kuwaweka katika hali ya kuelewa yanayoendelea na pia waweze kuepuka udanganyifu na wafanya biashara wajanja wanaotaka kupata fedha kwa kupotosha umma juu ya televisheni na redio walizonazo nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 mionganoni mwa malengo makubwa ambayo Shirika limejiwekea ni ukarabati wa majengo ya Shirika yaliyoko Mikocheni, Barabara ya Nyerere na kujenga vituo vya TV na Redio katika miji mikuu ya Mikoa kumi ambayo ni Iringa, Morogoro, Ruvuma, Rukwa, Mtwara, Manyara, Kilimanjaro, Pwani, Singida na Shinyanga. Shirika limepanga kuanzisha mkondo wa pili (2nd Channel) wa Televisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato, Shirika linatarajia kukusanya shilingi 4,000,000,000/= kama mapato na limetengewa shilingi 3,000,000,000/= kama fedha za Matumizi Mengineyo (*OC*), na shilingi 2,097,046,000/= fedha za Mishahara. Aidha, Shirika limetengewa shilingi 4,000,000,000/= kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Magazeti la Serikali (*TSN*). Shirika la Magazeti la Serikali katika mwaka wa 2008/2009 limepanga kufanya yafuatayo:-

- Shirika linategemea kupata faida ya shilingi 326,000,000/= kwa mwaka 2008. Mpaka tarehe 31/03/2008 Kampuni imepata faida ya shilingi 92,000,000/=;
- Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni ambapo wadaiwa wengi ni Wizara na Taasisi zake ili kupata mtaji wa uendeshaji;

Kununua Jengo la Uchapaji kutoka NSSF. *NSSF* wamekubali kimsingi kuuza jengo hilo na wako kwenye mchakato wa kulithaminisha;

- Kuanza uchapaji wa kibiashara wa magazeti ya kila siku ya wamiliki wengine;
- Kumalizia kazi ya kuorodhesha (*Indexing*) machapisho ya TSN yaliyonakiliwa; na
- Kufungua Ofisi za Kanda Tanga na Mtwara na kuboresha ofisi za Mbeya na Morogoro zilizofunguliwa mapema mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utamaduni. Katika mwaka 2008/2009 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendesha Maonyesho ya kazi za Mikono katika fani za utamaduni ili kupanua utambulisho wa kazi za mikono na kuwezesha wasanii/wajasiriamali kutafuta soko sahihi;
- Kuibua vipaji vya watoto kupitia sanaa;
- Kuhamasisha matumizi ya sanaa katika ufundishaji shulenii;
- Kupeleka washiriki 25 kwenye Tamasha la Muziki wa Asili na Ngoma za Asili nchini Namibia mwezi Agosti 2008; na
- Kutumia sanaa katika kutafiti, kutambua na kutatua matatizo yanayowazingira wanafunzi wa Shule za Sekondari katika kupata elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara pia itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kusimamia na kuendesha Tamasha la 27 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania mwezi Oktoba 2008;
- Kusimamia na kuendesha Maadhisho ya Siku ya Utamaduni Mei 2009;
- Kuendelea na ujenzi wa Jumba la Utamaduni;
- Kusimamia na kuendesha mashindano ya sanaa na lugha ngazi ya kanda; na
- Kufanya utafiti wa lugha za asili katika Mikoa ya Iringa, Mwanza, Ruvuma na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Idara itatekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kufanya utafiti wa kubaini dhamira ya sheria za mila na desturi kama ziliviyotumika/zinavyotumika katika shughuli za uongozi wa utawala na jinsi

zinavyozingatia hali, usawa, demokrasia kwenye mabaraza ya jadi katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara;

- Kuendelea kuendesha warsha ya utafiti kwa Maofisa Utamaduni wa Wilaya 16 za Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga;
- Kusambaza matokeo ya utafiti wa mikoani na kuchapisha vijarida vya mila na desturi; na
- Kuandaa na kuratibu vipindi 52 vya kuzungumzia maadili na utamaduni wa Mtanzania katika redio na televisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha warsha ya matumizi ya Kiswahili sanifu kwa wahariri wa vyombo vya habari;
- Ununuzi na usambazaji wa vitabu vya Kiswahili kwenye Balozi za Tanzania;
- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni;
- Kusambaza istilahi na orodha ya makosa ya matumizi ya maneno na usahihi wake kwenye Idhaa za Kiswahili za ndani na nje ya nchi katika kutekeleza maazimio ya Kongamano la Kimataifa la Idhaa za Kiswahili Duniani;
- Kusoma miswada ya vitabu vya taaluma na kuipa ithibati;
- Kuratibu na kutoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano ya kimataifa na katika shughuli za mashirika, makampuni na watu binafsi;
- Kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho;
- Kuhariri na kuweka urari wa matumizi ya lugha katika matini za programu za kompyuta kwa ajili ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ushirikiano na Kampuni ya Microsoft.
- Kufanya uhariri wa mwisho wa kitabu cha Kiswahili kwa Wageni Juzu Na. 1 na kuchapisha pamoja na Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu; na
- Kuandaa semina ya wamiliki wa vyombo vya habari kwa lengo la kusisitiza umuhimu wa kuwa na wakuza lugha (wasimamizi wa lugha) katika vyombo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Katika mwaka 2008/2009 Baraza la Sanaa la Taifa litatekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendeleza na kukuza stadi za usanii, uongozi na utawala wa shughuli za sanaa kwa wasanii 500 wa sanaa za ufundi, muziki na sanaa za maonyesho;
- Kutoa mafunzo ya stadi za Uongozi na Utawala kwa viongozi 30 wa vikundi vyaa sanaa;
- Kuendeleza mpango wa kuraghibisha na kuhamasisha wasanii 100 na watumishi 30 wa Baraza kuhusu kujikinga na VVU/UKIMWI;
- Kuandaa Maonyesho ya Sanaa za Ufundi;
- Kuendelea na mchakato wa kuhuisha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya mwaka 1984;
- Kukamilisha Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho ya Sanaa;
- Kufanya utafiti wa sanaa za jadi; na
- Kukuza vipaji vyaa wasanii chipukizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa). Katika mwaka 2008/2009 TaSUBa itatekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 100 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 150 walio kazini;
- Kuanzisha kituo cha utafiti na uhifadhi wa ngoma na muziki wa Kitanzania;
- Kushiriki katika Tamasha la 27 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania litakalofanyika kuanzia tarehe 13 mpaka 18 Oktoba 2008;
- Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Maonyesho;
- Kukamilisha ujenzi wa mabweni matatu ya wanafunzi na nyumba moja ya Mtendaji Mkuu; na
- Kuendelea na awamu ya pili ya Mpango Kamambe wa TaSUBa kwa kujenga mabweni mawili, vyumba viwili vyaa madarasa na kutayarisha michoro ya jengo la utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Mwaka wa 2008/2009 Mfuko utatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha miradi inayoleta ufanisi katika kuendeleza utamaduni wa Taifa kwa kufadhili miradi minne ya kimkakati. Miradi hiyo ni:-

(i) Uanzishaji wa Chuo cha Kufundisha Muziki wa Taarab Asilia unaoendeshwa na ‘*Culture Music Club*’;

(ii) Ukuzaji wa kazi za mikono kwa akina mama waishio Vijiji;

(iii) Ukuzaji wa taaluma asilia ya useketaji wa nguo kwa lengo la kuinua taaluma, kuhimili ushindani na kuongeza ajira; na

(iv) Ukuzaji wa Tasnia ya Filamu.

(b) Kuimarisha muundo wa utendaji wa Mfuko katika kuhudumia Sekta ya Utamaduni;

(c) Kufadhili miradi midogo midogo ya utamaduni ili kuhimiza ubora wa bidhaa pamoja na kutekeleza lengo la Serikali la kuongeza ajira;

(d) Kuandaa na kusimamia maadhisho ya Wiki ya Mfuko wa Utamaduni na kutoa Tuzo ya Zeze kwa watu waliojitekeza kuwa mahiri katika kuendeleza shughuli mbalimbali katika Sekta ya Utamaduni; na

(e) Kuongeza ufahamu wa umuhimu wa utamaduni katika mipango ya maendeleo kwa viongozi na wadau wa sekta kwa kuendesha semina ya Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya na Maafisa Utamaduni wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Michezo. Kuhusu Maendeleo ya Michezo, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia ukamilishaji wa Uwanja Mpya wa Michezo kwa kuwekwa zulia la kukimbilia “tartan” yenyi ithibati ya I.A.A.F. na kukamilisha mchakato wa kupata kampuni itakayosimamia na kuendesha uwanja huu. Mchakato wa kumpata mwendeshaji unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004.

- Kuandaa na kusimamia shughuli za Siku ya Michezo Tanzania itakayoadhimishwa nchi nzima na kilele chake kuwa tarehe 21 Septemba, 2008. Mwaka huu sherehe za kilele zitafanyika Dar es Salaam. Utaratibu wa kufanya sherehe za kilele za Siku ya Michezo Tanzania katika mikoa mbalimbali hapo baadaye unaandalishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Michezo ya Olimpiki itafanyika huko nchini China mwezi Agosti 2008. Timu ya Tanzania itakuwa na jumla ya wachezaji kumi na moja wakiwemo nane wa riadha, wawili wa kuogelea, na mmoja wa paralimpiki. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wafadhili na wadau wa michezo kuendelea kusaidia Timu za Taifa katika maandalizi ya mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji wa Michezo na Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, vituo vya Michezo vya Kanda za Kaskazini (Arusha) na Kusini (Songea) vitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya maendeleo ya michezo kwa Vyama na Vilabu vya Michezo. Wizara inazihimiza Halmashauri, Mashirika, Wizara na waajiri wote kwa jumla wavitumie kikamilifu Chuo na Vituo vya michezo kwa kuwapeleka wafanyakazi wao wenye sifa kuchukua mafunzo husika ili kuboresha vipaji vya michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kudurusu katiba mpya za Vyama na Vilabu vya michezo na kuvisajili, kutoa ushauri utakaowezesha Vyama na Vilabu vya Michezo kuhuisha Katiba zao ili kupunguza migogoro na kuleta amani na utulivu katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu kuboresha Miundombinu ya michezo na kuhimiza ujenzi wa miundombinu mipy kwa maeneo ambayo hayana, ili kuinua viwango pamoja na kuchochea ari ya kukuza ushindani wa michezo, ufundishaji, uamuzi na uchezaji. (*Makofî*)

Aidha, Wizara itaendelea pia kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, kwa kujenga awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000. Hosteli hii itajengwa kwa awamu tatu.

Kuhusu tiba kwa wanamichezo, Wizara itaendelea kutoa huduma za kinga na tiba kwa wanamichezo kwa kufanya upimaji wa afya na kuendesha kliniki za wazi kwa wanamichezo. Aidha, kuwashauri Watanzania kuitumia michezo kwa ajili ya kinga na tiba ya magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine yatakayoteklezwa na Wizara ni:-

- Kuwahamasisha wanawake kujihuisha kwa wingi katika michezo ili kuongeza ushiriki wao pamoja na kugombea nafasi za uongozi katika Vyama na Vilabu vya Michezo;

- Kuendelea kushirikiana na Wizara za Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TAMISEMI katika kuimarisha somo la Elimu kwa Michezo shulen na vyuoni, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua mashindano ya shule za Sekondari Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Kibaha. Wizara yangu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zimeunda kamati kulishughulikia suala hili;

- Kuendelea na Programu za mafunzo ya Muongoarika katika Michezo;

- Kuhimiza na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali za Mitaa kuwa na Mpango wa Maendeleo ya Michezo, kutenga maeneo ya wazi na viwanja vya michezo na kujenga miundombinu ya michezo katika Halmashauri zao. Aidha, kuhimiza Wizara, Mikoa, Halmashauri za Wilaya na Miji kutenga bajeti kwa ajili ya maendeleo ya michezo kama alivyolekeza Mhe. Waziri Mkuu alipokuwa akifungua mashindano ya SHIMIWI mwaka

2007 mjini Tanga, Kombe la Taifa kwa mpira wa miguu tarehe 6 Mei, 2008 na Netiboli tarehe 28 Juni, 2008 Jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisisitiza maagizo yake haya kwa waraka alioandika tarehe 20 Juni, 2008 kwenda kwa Mawaziri na Wakuu wa Mikoa wote; na

- Kutoa ushauri kwa TFF na BMT kuhusiana na masuala ya kuendeleza soka nchini ikiwa ni pamoja na taratibu za uanzishaji wa vituo vyta kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) katika mwaka wa 2008/2009 Baraza la Michezo la Taifa linakusudia kufanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo na kutoa huduma bora kwa wadau wa michezo;

- Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya ufundishaji michezo kwa walimu wa michezo katika Wilaya za Tanzania Bara. Mategemeo ni kuwahusisha jumla ya walimu 1,800 kutoka Wilaya 40;

- Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa Vyama vyta Michezo vyta Taifa kuhusu Mipango ya Maendeleo ya Michezo; na

- Kuandaa na kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi wa BMT na Vyama vyta Michezo kuhusu elimu ya Maambukizi ya VVU na UKIMWI. Aidha, kujenga uwezo wa Wafanyakazi wa Baraza la Michezo la Taifa kwa kuwaongezea elimu na vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Baraza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zingine zitakazofanywa na Baraza la Michezo ni:-

- Kusaidia, kushirikiana na kuratibu programu za wabia na wadau wengine wa michezo wanaotumia michezo kama zana muhimu ya kutekeleza malengo ya Taifa na Kimataifa;

- Kukamilisha ukusanyaji wa mapendekezo na marekebisho ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa na kuendesha Mjadala wa Mustakabali wa Michezo nchini; na

- Kushiriki katika mikutano, matamasha na mashindano yanayoandalili na wadau au wabia wa Baraza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utawala na Utumishi. Katika mwaka 2008/2009, Wizara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kuelimisha watumishi juu ya ugonjwa wa UKIMWI na kuwahamasisha wale ambao hawajapima kujitokeza kupima ili wajue afya zao na

kuwaweka katika nafasi ya kujilinda na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuilinda jamii wanayoishi nayo;

- Kufanya tathmini ya athari za ugonjwa wa UKIMWI kwa Wizara na Taasisi zake ili kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana nao kiwizara. Aidha, tutaendelea kutoa huduma ya msaada kwa watumishi waathirika kwa kadri watakavyojitokeza;
- Kuendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi watakaostahili kulingana na Miundo ya Utumishi ya kada zao na kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma;
- Kukamilisha upatikanaji wa watumishi wenyewe sifa kujaza nafasi wazi kwa mujibu wa ikama iliyoidhinishwa na kwa kuzingatia mwongozo wa masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma;
- Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kugharimia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;
- Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi kwa uwazi na kwa matokeo (*OPEN PERFORMANCE REVIEW AND APPRAISAL SYSTEM – OPRAS*). (*Makofi*)
- Kuendesha mafunzo kuhusu Utawala Bora na kusimamia utendaji kazi wa watumishi hao kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na mapambano dhidi ya rushwa; na
- Kuendesha mikutano ya wafanyakazi wote na ile ya Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shukrani. Utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu umewezekana kutokana na ushirikiano mzuri uliopo mionganoni mwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Ninapenda kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Mashirika na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa jitihada zao za kutekeleza majukumu waliyopewa. Ninapenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib (Mb), kwa uongozi wake mzuri wakati akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kabla ya mabadiliko aliyoyafanya Mheshimiwa Rais. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki aliyekuwa Naibu Waziri katika Wizara yangu ambaye bado Wizara inamkumbuka kwa ushauri na ushirikiano aliuonyesha. Kwa kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera Mbunge wa Korogwe Mjini na Naibu Waziri katika Wizara yangu. Ananisaidia sana kazi za kila siku na hata Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi jinsi anavyojibu maswali kwa unyenyekevu na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Hajjat Kijakazi Rajabu Mtengwa, kwa uongozi wake thabiti, Wakuu wa

Idara na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano mzuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuwashukuru washirika wetu wote ambao wametuunga mkono katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Nawashukuru wahisani wote ambao wametusaidia na nina imani wataendelea kutusaidia. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambao ni Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Sweden, Norway, Denmark, Ujerumani, Japan na Finland; Mashirika ya kimataifa ya UNICEF na UNESCO. (*Makofi*)

Pia ninapenda kuyashukuru makampuni ya Vodacom, Safari Lager, Serengeti Lager, NMB, NBC, Mohamed Enterprises, SBC Ltd, Benki ya Posta na Coca Cola Afrika - Kanda ya Tanzania.

Navishukuru Vyombo vyote vya Habari nchini kwa kufanya kazi nzuri ya kuitangaza vizuri nchi yetu tena kwa uadilifu wa hali ya juu. Hongera sana Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2008/2009. Mapato, mwaka 2008/09 Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 313,451,000/= kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya Mapato ukilinganisha na shilingi 229,311,000/= zilizopangwa kukusanya mwaka 2007/08. Ongezeko hili linatokana na lengo la kukusanya shilingi 120,000,000/= kutoka Uwanja wa Taifa ukilinganisha na shilingi 75,000,000/= mwaka 2007/08. Kadhalika, shilingi 90,000,000/= zitakusanya kutoka vibali vya kupiga picha za video ukilinganisha na shilingi 65,000,000/= mwaka 2007/08 na ada za mafunzo na mitihani katika vyuo shilingi 54,501,000/= kutoka shilingi 20,700,000/= kwa mwaka 2007/2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida. Kwa mwaka 2008/2009 Wizara imetengewa shilingi 11,235,964,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

- Mishahara ya Wizara – shilingi 1,091,100,000/=.
- Mishahara ya Taasisi – shilingi 2,663,473,000/=.
- Matumizi Mengineyo ya Wizara – shilingi 3,001,391,000/=.
- Matumizi Mengineyo ya Taasisi – shilingi 4,480,000,000/=.

Mchanganuo wa makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara upo katika Kiambatisho Na. VII(a) kilichopo ukurasa wa 81 wa kitabu cha hotuba na Kimbatisho Na. VII(b) kilichopo ukurasa wa 82 wa kitabu cha hotuba, kinaonyesha mchaganuo wa Matumizi Mengineyo kwa kila Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maendeleo. Mwaka 2008/2009 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 9,929,221,000/= kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo shilingi 9,279,221,000/= ni fedha za ndani na shilingi 650,000,000/= ni fedha za nje. Mchanganuo wa Mradi kwa Mradi upo katika Kiambatisho Na. VIII kilichopo ukurasa wa 83 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutetekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2008/2009, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 21,165,185,000/= ambapo kati ya hizo fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 11,235,964,000/= na shilingi 9,929,221,000/= ni fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono na pia ninakushukuru kwa uwasilishaji mzuri kabisa na ulio makini.

Sasa ni zamu ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo naona Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud atakuja kuwasilisha kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Karibu!

MHE. HAROUB SAID MASOUD - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, nachukua nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, majukumu ya Kamati hii pamoja na mambo mengine imefanya kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Tarehe 3 Juni, 2008, Mjini Dar - es – Salaam, Kamati ilifanya kikao na ilipata maelezo toka kwa Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, MB, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Katibu Mkuu akisaidiana na Wataalam wa Wizara. Timu hiyo ilieleza kuhusu dira, dhima na majukumu ya Wizara na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008. Aidha, Kamati pia ilipata maelezo ya kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe Wa Kamati. Kabla ya kutoa taarifa ya maoni na ushauri wa Kamati, napenda kwanza kuwatambulisha Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Fatma O. Ally, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji, Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Dr. Gertrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Elietha N. Switi, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Mohamed A. Said. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na Maagizo ya Kamati Kwa mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo yanayohusu:-

- Ujenzi wa ofisi za Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA);
- Fedha za maendeleo kwa *TUT* kwa sasa *TBC* na kuanzisha mazungumzo na *NSSF* kwa lengo la kupata fedha za kukamilisha ujenzi wa majengo ya iliyokuwa *TVT*, Mikocheni na kufanya ukarabati mkubwa wa ofisi iliyokuwa Radio Tanzania Dar- Es Salaam;
- Ujenzi wa Jumba la Utamaduni nchini;
- Tovuti ya Wananchi;
- Mikakati ya kuboresha Bodi ya Ulagazi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini;
- Mikakati ya kuongeza bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo; na
- Mikakati ya kupata fedha za kukamilisha Ujenzi wa Uwanja wa Taifa awamu ya pili na nyingine zitakazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi baadhi ya maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudzi zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji Wa mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2007/2008. Katika Mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara iliidhinishiwa na Bunge Matumizi ya shilingi 16.02 bilioni ili kutekeleza majukumu yake. Waziri alituelezea kwa undani kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2007/2008. Baadhi ya shughuli tulizoleezwa zimetekelawa pamoja na mafanikio yake ni kama ilivyoorodheshwa hapa chini:-

- Mafunzo yalifanyika kwa wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI na kununua vifaa vya kinga dhidi ya UKIMWI;
- Wizara imefanya ukarabati wa Chuo cha Sanaa, Bagamoyo;
- Kuhusu ujenzi wa Ofisi za BAKITA, Kamati ilifahamishwa kwamba mchakato wa kupata kiwanja unaendelea kufanyika;
- Ukumbi wa Wazi wa Maonesho ya Sanaa jengo limeezekwa na kupigwa lipu imeshakamilika;
- Ujenzi wa Jumba la Utamaduni eneo la hekta 100 limepatikana huko Bagamoyo;
- Mfuko wa Utamaduni umefadhili watu binafsi, taasisi, vikundi na vyama kuendeleza fani mbalimbali;
- Chuo cha Malya, jumba la michezo ya ndani limeezekwa na ujenzi wa Maktaba na Kompyuta umekamilika;
- Mradi wa Habari kwa umma kazi ya kuingiza *negatives* kwenye mfumo wa *digital* imefanyika, aidha kazi ya kutengeneza tovuti ya wananchi imekamilika na inatumika;
- Ufungaji wa mitambo ya Kampuni ya TSN umekamilika na inatumika;
- Usikivu wa Radio Tanzania (sasa *TBC Taifa*) na uonekanaji wa televisheni umeendelea kuimarka, pia umeongezeka kwa kuweka mitambo ya Radio ya FM katika Mikoa tisa ya Tanzania Bara na Mikoa mingine iko katika maandalizi;
- Tulielezwa pia kwamba vipindi vya Radio Tanzania (sasa *TBC Taifa*) na Televisheni vimeanza kuwa vya kuvutia zaidi na vinakidhi matarajio ya umma wa Watanzania;
- Kampuni ya Magazeti ya Serikali usanifu upya wa magazeti ya kiingereza tayari umefanyika na kinachosubiriwa ni kufanya uzinduzi;
- Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (*TaSUBa*) iliendesha mafunzo ya Stashahada kwa wanafunzi na imeanza mchakato wa ujenzi wa mabweni;

- Baraza la Kiswahili la Taifa limeandaa na kufanya semina ya matumizi ya Kiswahili sanifu, kukusanya istilahi zenyetata 280 na kuzifanyia uchanganuzi, kuandaa na kufanya semina ya mafunzo kwa wakalimani na wafasiri 20, mwongozo wa waandishi wa Kiswahili sanifu ulihaririwa, kazi ya kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine imefanyika;

- Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza, imekagua na kupanga katika madaraja filamu na kanda za video katika Mkoa wa Dar - Es Salaam. Kazi za kukusanya takwimu zinazohusu majumba ya filamu, maktaba za video, maduka ya kanda za filamu na video, takwimu za watengenezaji na wasambazaji wa filamu na video imefanyika. Aidha kazi ya mchakato wa marekebisho ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 imeanza;

- Baraza la Sanaa la Taifa liliandaa mpango wa mafunzo ya stadi za usanii na sanaa za muziki, ufundu na maonesho na kazi ya ujenzi wa ukumbi wa wazi unaendelea;

- Mfuko wa Utamaduni Tanzania uliwezesha watu binafsi, vikundi, taasisi na vyama 46 kuendeleza fani zao; na

- Baraza la Michezo la Taifa (BMT), limeanzisha mchakato wa kufufua michezo kuanzia ngazi ya vijiji, limeanzisha mafunzo ya elimu ya UKIMWI kuitia michezo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kueleza mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kwa kina changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2007/2008, changamoto hizo ni pamoja na;

- Uhaba wa vifaa/nyenzo za kufanya kazi katika Wizara na taasisi zake. Hii iliathiri sana utendaji kazi na utoaji wa huduma;

- Ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha hasa za maendeleo kutoka katika Wizara ya Fedha na Uchumi hali ambayo imevuruga mipango ya Wizara;

- Katika utendaji kazi wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) kwa sababu ya kutumia kiasi kikubwa cha fedha katika kununua mtambo, Kampuni inakosa mtaji wa uendeshaji;

- Kuhusu utendaji kazi wa BAKITA ruzuku ndogo inayotolewa kwa Baraza upungufu wa wafanyakazi na ufinyu wa ofisi unaathiri utendaji kazi wa Baraza; na

- Wizara imekuwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika Idara zake muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2008/2009, imeomba kiasi cha shilingi 21,165,185,000, hii ikiwa ni shilingi 11,235,964,000 maombi ya matumizi ya kawaida na shilingi 9,929,221,000 matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata taarifa na maelezo ya kina ya malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, Kamati ilijadili kwa undani masuala mbalimbali na kuipitisha. Kamati yangu inaunga mkono maombi ya Wizara hii, hata hivyo Kamati inatoa maoni na ushauri kwamba kwa kuwa tatizo la ufinyu wa Ofisi za BAKITA ni tatizo sugu ambalo linaludisha nyuma ufanisi na utendaji kazi wa BAKITA, tatizo hili linahitaji ufumbuzi wa haraka na kwa kuwa BAKITA tayari wanaendelea na mazungumzo ya kupata jengo kubwa ambalo liko katika hatua nzuri ya kukamilika na linagharimu shilingi bilioni moja na kwa kuwa jengo hilo likinunuliwa na Serikali linaweza kutumika pia na Wizara, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- (a) Wizara iendelee na mazungumzo katika kulinunua jengo hilo;
- (b) Serikali itenge fedha kwa mpango mahususi ili Wizara iweze kupata fedha za kununua jengo hilo katika mwaka huu wa fedha 2008/2009; na
- (c) Baada ya jengo hilo kununuliwa na kumalizika ujenzi wake, Wizara ihamie katika jengo hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutenga fedha za maendeleo kwa *TBC*. Kwa kuwa *Tanzania Broadcasting Corporation* (*TBC*), ni muhimu sana katika nchi yetu kwani nchi yoyote haiwezi kutegemea vyombo vya habari vya watu binafsi peke yake na kwa miaka mingi *TBC* imetoa mchango mkubwa katika nchi yetu, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali iendelee kutoa fedha za maendeleo kwa *TBC* ili kuimarisha vitenda kazi muhimu kama vile kununua mitambo ya kisasa kwa lengo la kuboresha usikivu wa radio na televisheni kwa nchi nzima;
- (b) Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo iwaalike viongozi wakuu (Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Spika wa Bunge), kutembelea *TBC* kujiona hali halisi;
- (c) Serikali izingatie maoni ya Kamati yaliyotolewa katika kikao cha pamoja kilichofanyika tarehe 22 Julai, 2008, Mjini Dodoma kilichohusisha Mawaziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Shirika la Hifadhi ya Jamii ya Taifa (*NSSF*) kilipojadili mikakati ya kupata fedha za ukarabati wa majengo ya *TBC* Taifa na *TBC1*, Mikocheni; na
- (d) Serikali iweke mikakati ya kuiwezesha *TBC* kujidoresha kibiashara na kutafuta vyanzo vingine vya mapato kuliko kuendelea kutegemea Serikali pekee yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Jumba la Utamaduni Bagamoyo. Kwa kuwa utamaduni ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na kwa kuwa Serikali imekuwa na mikakati ya kutafuta kiwanja cha kujenga jumba la utamaduni, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Kiwanja kimepatikana katika eneo la Bagamoyo, Serikali ianze sasa kutenga fedha za kutosha kujenga jumba la utamaduni na kijiji cha Utamaduni huko Kiromo Bagamoyo;

(b) Kabla ya ujenzi, Serikali ihakikishe inapata hatimiliki ya kiwanja hicho ili kuondokana na migogoro ya ardhi inayojitokeza mara kwa mara hapa nchini; na

(c) Kwa kuwa Mji wa Bagamoyo, ni mji wenye vivutio vingi vya utamaduni, Serikali iweke mikakati ya dhati katika ujenzi wa kijiji cha utamaduni ili kijiji hicho kiweze kuvutia zaidi mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi na Makampuni chini ya Wizara kujiendesha kibiashara. Kwa kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, inazo taasisi na makampuni mengi (Shirika la Utangazaji (*TBC*), Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Baraza la Kiswahili la Taifa), Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza na Baraza la Sanaa la Taifa, Mamlaka ya Mawasiliano - *TCRA* (Kamati ya Maudhui), kama yangejiendesha kibiashara ingeipunguzia Serikali gharama kubwa. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ifanye juhudzi za kuziwezesha taasisi na makampuni ambayo yapo chini ya Wizara kuongeza mapato na kudhibiti matumizi ili taasisi hizo ziweze kujiendesha kibiashara; na

(b) Kampuni ya Magazeti ya Serikali iendeleteleze juhudzi zake kujiendesha kibiashara na kutoa gawio kwa Serikali, Makampuni na taasisi zingine ziige mfano wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuboresha utendaji kazi wa Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza. Kwa kuwa Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza imeundwa kwa Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 ambayo ni ya siku nydingi sana na imepitwa na wakati kwa mambo mbalimbali na kwa kuwa Bodi hii ni muhimu sana katika kudhibiti maadili ya vijana wetu, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iweke mikakati ya kuiwezesha Bodi kukusanya takwimu muhimu zinazohusu majumba ya filamu, maktaba za video, maduka ya kanda za filamu na video, watengenezaji na wasambazaji wa filamu na video, kuboresha takwimu hizo kwa lengo la kujenga maadili mema; na

(b) Serikali ikamilishe rasimu ya Waraka wa Marekebisho ya Sheria Na.4 ya 1976 na kuwasilishwa katika ngazi zinazohusika na hatimaye kuleta Muswada huo Bungeni kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuongeza Bajeti ya Wizara. Kwa kuwa Wizara hii ni mpya, kwa miaka mingi, ilikuwa ni Idara tu katika Wizara mbalimbali, hadi sasa Bajeti ya Wizara hii ni ndogo na haina watumishi wa kutosha katika baadhi ya idara zake muhimu. Aidha Kamati imegundua kuwa Wizara hii haipewi fedha za kutosha kulingana na majukumu yake, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali itoe kipaumbele katika kuipatia Wizara hii watumishi wenye sifa zinazostahili ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu;

(b) Serikali ione umuhimu wa Wizara hii kuongeza bajeti hasa fedha za michezo, kuendeleza Kiswahili na masuala yanayohusu habari; na

(c) Serikali ihakikishe agizo la Waziri Mkuu alilotoa tarehe 18/7/2008 nyumbani kwake akiwa na wajumbe wa Kamati kwamba vijana hao walelewe kielimu na kimichezo hadi kufikia kiwango cha kucheza timu ya Taifa linatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Taifa awamu ya pili. Kwa kuwa Ujenzi wa Uwanja wa Taifa mpya (changamani), ni muhimu sana kwa maendeleo ya michezo hapa nchini, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ione umuhimu wa ujenzi wa Uwanja huu kwa utaratibu wa Kujenga, Kuendesha na Kurudisha (BOT) zikamiliike haraka iwezekanavyo na Kamati ijulishwe maendeleo yake; na

(b) Pamoja na kwamba Ujenzi huo utajengwa kwa utaratibu wa *BOT*, Serikali lazima iweke mikakati ya kutoa fedha za Maendeleo kwa ajili ya Ujenzi wa Uwanja wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kucheleweshwa kupata fedha kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi. Wizara nyingi zinacheleweshwa sana kupata fedha kutoka HAZINA hasa fedha za Maendeleo kwa visingizio mbalimbali hali ambayo inavuruga mipango mingi ya maendeleo inayokusudiwa kutekelezwa na Wizara hizo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iweke mikakati ya kutoa fedha za maendeleo mapema iwezekanavyo ili kuziwezesha Wizara kutekeleza mipango iliyowekwa; na

(b) Wizara ziweke utaratibu wa kutoa taarifa za fedha ambazo hazijafika katika Wizara zao mara baada ya mwisho wa mwaka wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za UKIMWI katika Wizara. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa kila Wizara na Idara zinayojitegemea kwa ajili ya ugonjwa

wa UKIMWI na kwa kuwa UKIMWI ni janga la kitaifa, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa miaka mingi kumekuwa na semina za kuelimisha watumishi kuhusu UKIMWI, watumishi wengi sehemu za kazi sasa wamelielewa tatizo hili, Serikali ielekeze fedha za UKIMWI kwa waathirika, kwa kutoa chakula, madawa na virutubisho vingine muhimu kwa walengwa; na

(b) Serikali iongeze fedha hizi kwa waathirika/walengwa na iweke mikakati ya kudhibiti fedha hizo, zisitumike vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mikataba ya Huduma Bora kwa Wateja. Kwa kuwa Serikali inasisitiza utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja amba ni muhimu sana katika kuboresha utendaji kazi, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Wizara iweke mikakati ya kutekeleza mkataba huo hasa kwa kutoa mafunzo na elimu kwa wahusika; na

(b) Ili kutoa mafunzo kwa ufanisi Wizara itoe machapisho ya kutosha na kusambazwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na pia kukushukuru wewe, Naibu Spika na Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti wangu, narejea tena, kwa namna ya pekee, naomba nimeshukuru Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Kapt. George Huruma Mkuchika, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwataki mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Brown Mwangoka, kwa kazi nzito katika kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa hii kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Haroub Masoud.

Sasa kabla hajaja msemaji anayefuatia ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, napenda sasa nimuombe Mheshimiwa Spika aje achukue hiki Kiti ili sasa yeze ndio aweze kumuita Mheshimiwa Mheshimiwa Mwanawetu ili tuweze kuendelea.

Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea. Hatua ya sasa ni kusikiliza maoni ya Kambi ya Upinzani kwa sekta hii ya habari. Kwa hiyo, namwita sasa Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye ni Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, karibu!

MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwanza na kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa Rehema na Amani, kwa kutuwezesha sote kufika hapa tukiwa wazima wa afya, tukiwa tayari kuwajibika kama tulivoagizwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Kambi ya Upinzani Bungeni, chini ya Uongozi thabiti wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kuniamini na kunichagua tena kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara hii. Nami naendelea kuwaahidi kuwa, nitaendelea kuitumikia Kambi, pia nawahakikisha wananchi wote kuwa nitaendelea kutetea haki ya Watanzania kila itakapostahiki.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitakishukuru chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*), chama kinachojikita katika kusimamia na kutetea haki na usawa kwa Watanzania bila kujali itikadi, dini wala rangi. Pamoja na hao, napenda pia kuwashukuru viongozi na wanachama wote wa *CUF* Wilaya ya Kilwa. Kwa pamoja, napenda kutambua ushirikiano wanaonipa ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda nichukue fursa hii pia kuipongeza timu ya vijana chini ya miaka 17 ya Mkoa wa Ruvuma, kwa kuibuka kidedea katika michuano ya *Copa Cocacola*. Ushindi wao huo umetudhihirishia kuwa vipaji haviko tu katika Jiji la Dar-es-Salaam bali hata katika Mikoa iliyopo pembezoni mwa nchi hii. Naipongeza pia timu ya mpira wa pete ya Dar es Salaam katika mashindano hayo ya Taifa. Wakati huo huo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naipongeza timu ya mpira wa miguu Ilala kwa kufanikiwa kutwaa kombe la Taifa Cup. Pia sijaisahau timu yetu ya *Copa Cocacola* ambayo imetuletea fahari baada ya kutupatia ushindi katika mashindano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa pole kwa Mheshimiwa Savelina Mwijage pamoa na familia yake, kwa msiba mwingine wa mjukuu wake aliyepata ajali na kwa kipindi chote alikuwa hospitalini. Mwenyezi Mungu ampe roho ya ustahimilivu, Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, sasa naomba nianze moja kwa moja kutoa hoja ya Kambi ya Upinzani katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi za Wizara katika mwaka wa fedha 2007/2008. Ni jukumu la msingi la Kambi ya Upinzani, kuikosoa na kuikumbusha Serikali, juu ya wajibu wake wa kuwatumikia wananchi. Napenda kuikumbusha Serikali juu ya ahadi ambazo Wizara hii iliahidi kukamilisha ndani ya mwaka wa fedha uliopita 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwanza, upanuzi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Moja kati ya haki za msingi za mwananchi wa Tanzania kama inavyotambuliwa Kikatiba katika ibara ya 18(b) ni kuwa:-

“Kila mtu anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi”.

Hii inadhihirisha kuwa kupata habari ni moja ya haki za msingi za raia. Serikali ina jukumu la kusimamia haki na kutetea haki za wananchi wake. Hivyo kusambaza habari ni jukumu la Serikali, ingawa hata vyombo binafsi vinayo majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza hili kwanza kwa nia ya kuweka bayana jukumu la Serikali kuitia Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Ahadi hizo zilitolewa na Wizara wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2007/2008. Hata hivyo, ili Shirika liweze kufanya kazi yake na kutekeleza matakwa ya Katiba, linatakiwa kusambaa nchi nzima na kuwa na ubora wa hivyo kuwafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, wakati nasoma maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008, nilitilia msisitizo kuhusu suala la majengo kwa iliyokuwa Shirika la Utangazaji la Taifa. Mheshimiwa Waziri alitanabaisha kuwa Wizara tayari ilikuwa kwenye mazungumzo yanayoendelea na wafadhili na wadau mbalimbali na kuwa walikuwa wamefika hatua nzuri. NSSF walielezwa kuwa tayari kuyakarabati majengo yaliyoko Pugu Road na Mikocheni.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwenye taarifa za Kamati yetu, zinaonyesha kuwa marekebisho ya majengo haya bado yanabakia kuwa ni malengo ambayo Wizara hii inapanga kuyatimiza ndani ya mwaka huu. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni lini hatua zitachukuliwa ili majengo ya shirika hili yakarabatiwe na kuboreshwa kwa lengo la kuwapa watumishi wa shirika hili nafasi na mazingira bora ya kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu vazi la Taifa. Suala la vazi la Taifa sasa limekuwa donda ndugu au gonjwa lisilo na dawa. Kila mwaka watu kutokea kada tofauti wanaihoji Serikali juu ya vazi la Taifa. Mungu ameibariki sana Tanzania kwa kuipamba kwa makabila mengi na tamaduni nyingi, wanyama wa kila aina na rasilimali zinazotofautiana. Vyote tunavyo lakini vazi la Taifa hatuna. Inashangaza tumeshindwaje kuchukua hatua ya kupata vazi la Taifa ambalo ni kielelezo muhimu cha Uzalendo na Utaifa wetu?

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kutafuta vazi la Taifa ulijitokeza toka wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu na Serikali ya Awamu ya Nne sasa imebakiza miaka miwili hivi kumaliza muda wake. Mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara iliahidi kuwa mchakato unaendelea vizuri na Wizara ilikiri kuwa imeshabainisha mavazi matatu ambayo wanafikiri ni rasmi, pia walikwishaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuwawezesha Mawaziri waweze kufanya uamuzi wa pamoja kama Serikali kwa kusema sasa hili ndilo vazi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi uamuzi kutoka katika Baraza la Mawaziri huchukua muda gani? Kama kweli Waraka huo ulikuwa umekwishatayarishwa takriban mwaka mmoja uliopita, hivi nini hasa nia ya Wizara kutoa ahadi ambayo wala haitajwi tena mwaka huu? Hapa ni dhahiri kuna fumbo. Fumbo hili namwachia Mtanzania alifumbue.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu umuhimu wa vazi la Taifa. Nchi nyingi Afrika ikiwemo Nigeria na Ghana zimeweka bayana vazi lao ambalo husaidia kujitambulisha duniani. Kambi ya Upinzani, inataka ufanuzi wa kina juu ya sababu ya msingi inyosababisha kucheleweshwa kuwepo kwa vazi la Taifa. Hivi ni kweli mpaka wananchi wapige kura za maoni kupata vazi la Taifa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa ni pamoja na mavazi ya makabila mbalimbali. Hivyo basi, ni vyema Wizara ikaja na mkakati wa kuhamasisha na kuhakikisha kuwa mavazi ya makabila mbalimbali yanaenziwa kwani hii nayo ni sehemu ya utamaduni wa Taifa. Serikali lazima iweke sera na mikakati ya kuhamasisha mavazi ya makabila mbalimbali ama sivyo yatapotea. Sasa hivi Watanzania wengi wanafahamu tu vazi la Wamasai wakati ambapo makabila karibu yote nchini yana mavazi yao ya asili.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Baraza hili liliundwa kwa Sheria Na.27 ya mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1983. Sasa ni takribani miaka 25 yaani robo karne tangu kuundwa kwa Baraza hilo. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Baraza ni wazi yana manufaa sana kwa maendeleo ya jamii yetu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini moja kati ya kero kubwa katika Baraza hili ni ukosefu wa majengo kwa ajili ya Baraza hili. Pamoja na ukweli kuwa Baraza la Kiswahili ni moja kati ya mabaraza ambayo yameundwa kwa muda mrefu sana uliopita lakini ujenzi wa ofisi zake unaendelea kusuasua.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliyoko madarakani imechukua takribani miaka 41 kuweza kugundua tatizo hili. Lakini hiyo si hoja sana, suala tunalolihoji ni ukweli kuwa katika bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu iliidhinisha jumla ya shilingi milioni mia nne na katika bajeti ya mwaka jana tulipitisha jumla ya Shilingi milioni mia moja, hiyo ni jumla ya shilingi milioni mia tano, jasho la walipa kodi wanaotabika wakichangia nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni miaka mitatu sasa, lakini la kustaajabisha Wizara hata kiwanja bado haijapata. Mchakato bado unaendelea, mpaka lini? Wizara inajinadi kuwa ipo kwenye hatua ya kuandaa michoro ya kiusanifu ya majengo na kukadiria gharama za jengo ilhali kiwanja bado. Kambi ya Upinzani inauliza kama kupatikana kwa kiwanja kunachukua muda mrefu kiasi hiki je kujenga itachukua muda gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nne ni Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza. Bodi hii iliundwa kwa Sheria Na. 4 ya Mwaka 1976. Hii ni takriban miaka 32 iliyopita. Mazingira ya dunia yamebadilika miaka ya sabini haifanani na wakati tulionao sasa. Serikali ambayo inajisifu kwa kusoma alama za nyakati iliahidi ndani ya mwaka kufanya marekebisho kutokana na ukweli kuwa Sheria hiyo ilikuwa imepitwa na wakati. Wizara ilitanabaisha kuwa mchakato wa kuiangalia upya Sheria ile ulianza kwa sababu kweli walitambua kuwa haifanani na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka tayari, Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo uko wapi? Kwa nini Wizara inakuwa nzito kuwasilisha ahadi zake? Tatizo ni nini? Kambi ya Upinzani inahitaji majibu ya kina kuhusiana na hili na si vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujio wa timu ya *Real Madrid*. Miongoni mwa mafanikio ambayo yalismwa kuwa ni kutokana na ziara za Mheshimiwa Rais nje ya nchi ni pamoja na ujio wa timu ya mpira wa miguu ya *Real Madrid* ya Hispania. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilitoa tamko la kuthibitisha kuwa timu ya *Real Madrid*, ingefika Tanzania rasmi kwa michezo ya kirafiki Julai mwaka 2007 ikiwa na msafara wa watu wapatao themanini. Hili ni tamko rasmi la Serikali ndani ya Bunge. Kambi ya Upinzani inauliza ujio wa timu hii ni lini? Je, Rais alipotoshwa? Kuna jambo gani hapo? Kama imeshindikana ni kwa nini Serikali inakosa ujasiri wa kulieleza Taifa kilichojiri kama ilivyotamka rasmi na kwa mbwembwe wakati wa kutangaza uwepo wa utaratibu huo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani, inahitaji kupata uhakika kama kweli timu hii itakuja na kama itakuja, ni lini? Pia inaitaka Wizara husika kutoa takwimu sahihi ya, je, kama timu hii itakuja Serikali itatumia shilingi ngapi kwa safari nzima? Sambamba na hilo, inataka kufahamu mpaka sasa Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwenye maandalizi ya ujio wa timu hiyo, hasa ukizingatia kuwa Kamati

ilikwishaundwa na shughuli za uaandaaji na kazi zilikwishaanza kama iliviyotangazwa ndani ya Bunge hili Tukufu!

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikiweka malengo katika kukuza vipaji ili kujenga wanamichezo bora na katika kuwekeza huko viongozi ambao wana jukumu la kuaanda vijana wetu wako katika ngazi ya Wilaya. Pamoja na mapungufu mengi, viongozi hawa ambao huitwa Maafisa Michezo katika Wilaya zetu, ni wachache sana na katika Wilaya nyingi, Maafisa Utamaduni hufanya kazi za Maafisa Michezo na Maafisa Vijana.

Mheshimiwa Spika, hii inawazidishia mzigo wa kazi na hawana marupurupu yoyote, wao wanabakia kufanya kazi tatu kwa pamoja. Kweli huku ndio kuwekeza ili kuibua vipaji? Pamoja na hilo, kutokana na ukubwa wa Wilaya zetu, bado tumekuwa tukiona matatizo makubwa wanayoyapata katika kutimiza majukumu yao. Sote tunajua ukubwa wa Wilaya zetu, matatizo ya miundombinu yetu tunayafahamu, lakini tunamsaidia viyi mtumishi huyu?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Wizara husika kutoa takwimu zinazoonyesha, je, nchi yetu ina Maafisa Michezo wangapi katika Wilaya zetu, Maafisa Utamaduni na Maafisa Vijana?

Mheshimiwa Spika, sanjari na hilo, maafisa hawa bado wanapatwa na matatizo makubwa katika utekelezaji wa kazi zao. Katika uandaaji wa mpango kazi, maafisa hawa huandaa bajeti inayoonyesha ni kiasi gani wanahitaji katika kutimiza majukumu yao ya mwaka mzima lakini maaafisa hawa hutegemea pesa kutoka katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu si mbaya iwapo utawezeshwa na ukafanya kazi lakini matatizo wanayoyapata ni kwamba, pamoja na mpango kazi mzuri wanaopanga, Halmashauri haiwapatii pesa kama mahitaji yanavyosema kwa vile Halmashauri hazina vianzio vya kutosha na hivyo michezo au utamaduni kuwa si kipaumbele kwao.

Mheshimiwa Spika, pale wanapopatiwa fedha na nyenzo na kukatokea tatizo kwenye masuala mengine wao ndio hupunguziwa na kuambiwa kuwa hayo ni masula nyeti na yanahitajika zaidi kuliko wao. Kwa utaratibu huu, utamaduni utajengeka viyi na au michezo itakuzwa viyi? Daima Tanzania kwa mtindo huu itabaki kuwa wasindikizaji katika michezo ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inapenda kutoa rai kwa Wizara husika kuwa, iwapangie mafungu kutoka Wizarani ili kupunguza kero zinazowapata maafisa wetu katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, lakini hilo halitoshi, maafisa hawa wamekuwa wanarushwa rushwa kama mpira wa kona. Kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Afisa Michezo ameondolewa na kwenda kufanya kazi za elimu wakati tupo katika harakati za kukuza vipaji! Hii inaaonyesha dharaui ya wazi kwa maafisa hawa. Kambi ya Upinzani

inaitaka Wizara husika kuchukua jukumu la kuangalia na kusimamia maafisa hawa moja kwa moja na kuwa na mipango madhubuti ya kuwaendeleza na kuwamotisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ngoma za Asili. Moja kati ya kazi za msingi za maafisa hawa ni pamoja na kuendeleza vikundi mbalimbali vyta sanaa. Katika miaka ya 1990, hata katika Wilaya Mijini kama Temeke tulikuwa tukiona vikundi vyta ngoma vikitumbuiza katika viwanja vyta wazi kwa muda wa wiki moja. Hizi ngoma zilikuwa zikijulikana kama ngoma za kabisa na kadhalika. Kutunza tamaduni zetu ni jambo la msingi sana na katika kuzitunza pia tuna jukumu la kuzirithisha kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona katika Tanzania ya leo, kama mkazi wa Jiji la Dar es salaam anataka kuona ngoma za asili anatakiwa asubiri mgeni atoke nje na yeze awahi kiwanja cha ndege. Kwa sababu ni pale ndio zinaonekana, au asubiri siku za sherehe za Kitaifa na awahi uwanja wa Taifa. Hii ni fedheha, kwani lile lengo letu la kuutunza na kuuenzi Utamaduni wetu limeishia wapi? Kambi ya Upinzani inatoa rai kuwa Wizara iandae mkakati ambao wiki ya utamaduni iadhishwe katika ngazi za mikoa na Wilaya zote na sio kwenye ngazi ya Taifa kama ilivyo sasa. Hii itasaidia kuenzi na kudumisha mila zetu kwetu wenyewe kabla ya kuzionyesha kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubadhifuru katika Vyama vyta Michezo. Majukumu ya Wizara ni pamoja na kuimarisha utawala bora katika michezo nchini, kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na hapo ndipo Vyama vyta Michezo vinapopata uangalizi. Hapa nchini kwetu Vyama vyta Michezo ni vingi sana na mojawapo ya kero kubwa katika Vyama hivi ni ubadhifuru wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio yenye jukumu la kufuutilia uwajibikaji na maadili katika Vyama hivi kuititia kwa Msajili wa Vyama vyta Michezo. Pamoja na ukweli wa kuwepo kwa mikingano mingi ya kikatiba inayolinda kuingiliwa kwa Vyama hivi na taasisi au Wizara yoyote kutoka nje. Lakini Wizara kuititia ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Michezo inaweza kumwita Mkaguzi wa kutoka nje ya Chama na hivyo kutambua kama kuna ubadhifuru wowote. Pia msajili ana uwezo wa kuhakikisha kuwa vyama hivi vyote vinakuwa na vikao vyta mwaka na kutaarifiana juu ya mapato na matumizi kwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ambazo Wizara inaweza kuzuia matatizo mengi ambayo yana malalamiko mengi katika Vyama hivi ni kwa kupeana taarifa. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa rai katika Wizara husika kumwezesha Msajili wa Vyama ili aweze kufanya kazi zake kwa umakini na hivyo kusaidia kupunguza kero nyingi ambazo zinawapata wanachama wa vyama hivi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vituo vyta Michezo. Katika nchi yetu tumebahatika kuwa na vituo vyta Michezo viwili, cha Arusha pamoja na Ruvuma. Hivi ni vituo ambavyo vinalengo la kukuza vipaji vyta wanamichezo wetu. Wizara husika hupanga mafungu kwa ajili ya maendeleo ya vituo hivi. Pamoja na ukweli kuwa kila mwaka katika vituo hivi hupanga mpango kazi wake wa mwaka na hivyo huwasilisha kiasi cha

fedha ambazo wanahitaji kwa mwaka mzima na kupitia Bunge lako Tukufu, Bunge huidhinisha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kinachowanyong'onyesha watumishi wa vituo hivi ni ukweli kuwa Wizara inakuwa ngumu sana kutoa pesa hizo, ambazo ni halali kwa matumizi ya vituo hivyo. Kwa nini Wizara inakuwa ngumu katika kutoa fedha ambazo imeviombea vituo hivi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, vituo hivi huandaa mafunzo ya muda mfupi kwa Maafisa Michezo ya Wilaya na katika mafunzo hayo maafisa huja kutoka Halmashauri mbalimbali. Hii ni mipango madhubuti na endelevu katika kuimarishe michezo katika Wilaya zetu na Tanzania nzima kwa ujumla. Lakini kero kubwa inakuja kutokana na ukweli kuwa vituo hivi haviwezeshwi na Wizara kwa njia yoyote katika kuandaa mafunzo hayo. Hili si zuri hata kidogo kwa Serikali kama kweli imedhamiria kuwa na lengo la kuibua vipaji katika michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hii hupelekea vituo hivi kuwatoza fedha maafisa hawa ili kuandaa mafunzo hayo. Hivi kweli unatoa mafunzo kwa ajili ya kuboresha kazi za Maafisa Michezo halafu hao hao pia unawatoza fedha? Jambo hili haliingii akilini hata kidogo! Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara kutoa majibu ya kina ni kwa nini vituo hivi havipati kasma yoyote katika kuandaa mafunzo hayo ya Maafisa wa Michezo wa Wilaya?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua kuwa suala la michezo mashulen i lipochini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, ila Wizara hii haina budi kuhakikisha kuwa wanaweka mkakati maalum kwa ajili ya kukuza michezo mashulen na vyuoni. Kambi ya Upinzani, inapendekeza kuwa pawepo na shule maalum kwa ajili ya michezo angalau shule moja kila Wilaya na Serikali itoe fungu maalum kwa ajili ya kuzisaidia shule hizi kupata vifaa vya michezo pamoja na wataalam ili kuinua sekta ya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi za wenzetu ambao wanathamini michezo huwa wanakuwa na mkakati maalum wa kuvisaidia vilabu kuanzisha timu za watoto ambao hupelekwa kwenye *Academies* za vilabu. Huko watoto hao wanasoma elimu ya kiada pamoja na elimu ya michezo. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuiga mfano huu na kuanza kuvisadia vilabu ambavyo vitaanzisha *Academy* hizo kwa kuvipatia ruzuku na hilo lianze sasa kwani bila kuwa na mkakati wa muda mrefu wa kulea vipaji haitasaidia kukuza michezo kwa kuleta makocha wa kigeni pekee. Sambamba na hilo Serikali iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku kwa shule na vyuo binafsi ambavyo vimejihusisha na kukuza vipaji vya michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo ya jadi. Sote tunafahamu kuwa hata kabla ya ukoloni, Tanzania tulikuwa na michezo mingi ya kijadi, hii ni pamoja na mieleka, bao na mingineyo. Moja kati ya mambo yaliyoainishwa wazi kwenye Sera yetu ya Michezo ni kukuza michezo ya jadi. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu, je Wizara ina mikakati gani ya kukuza Michezo hii? Katika suala hili zingatio liwe katika michezo yote ya

kijadi. Michezo hii ikiimarishwa itakuwa ni sehemu muhimu ya kuvutia watalii na hivyo kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza. Pamoja na hilo, moja kati ya majukumu muhimu ya bodi hii ni kuhakikisha kuwa filamu na kanda za video zinazotengenezwa ndani na nje ya nchi hii zinakaguliwa na kupewa madaraja husika kabla ya kuonyeshwa kwa watumiaji au kuonyeshwa mbele ya hadhara ya watu wengi. Huu ni mpango mzuri kwani taasisi inakuwa na jukumu la kulinda maadili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji kufahamu kama ni taasisi hii ndio yenyeye mamlaka ya kukagua filamu zinazoingizwa nchini na kama hivyo ndivyo, ni kwa nini filamu ambazo maudhui yake hayaendani na utamaduni wa Kitanzania zinaingizwa nchini bila ya angalizo lolote? Je, maadili ya Mtanzania kupitia filamu yanalindwa na nani na kama bodi hii inafanya kazi yake kwa makini, mpaka sasa ni filamu ngapi za nje zimekwisha kaguliwa na kukataliwa kuingia nchini kutokana na utofauti wa maadili tulionao na nchi za wenzetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo, bodi hii ambayo ilianzishwa miaka ya 70, mpaka leo haina Wakurugenzi wa Bodi na wala haina Mtendaji Mkuu. Imekuwa hivi kwa muda mrefu sana sasa, toka hata nchi yetu haijaingia katika mpango wa Vyama Vingi. Hii ni ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu hili tatizo litaisha lini? Au hakuna wananchi yenyeye uwezo wa kuweza kushika nafasi hizi? Tunaitaka Wizara kuwa wazi kwa hili na kama hawana uwezo wa kufanya hili tupeni Kambi ya Upinzani jukumu hilo tuwatafutie watu yenyeye sifa za kushika nafasi hizo ambazo zimekaa wazi kwa takribani zaidi ya miaka ishirini sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuendeleza usawa kwa jinsia ni jambo la muhimu kwa maendeleo ya maisha ya wananchi wote kwa pamoja. Kwa kuzingatia hilo, napenda kuipongeza Serikali kwa kutambua kuwa michezo si tu mahitaji ya wanaume pekee bali na wanawake pia na hivyo kutoa fursa sawa kwa watu wote. Hili liko dhahiri katika Sera ya Michezo ya Taifa ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, lakini mizizi ambayo inaendeleza utofauti wa kijinsia, haupo tu katika ushiriki wa watu wa jinsia tofauti katika michezo bali upo pia katika aina za michezo. Kwa hili, naomba nieleweke vizuri. Napenda kutoa pongezi kwa Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania, kwani kwa nafasi ya kipekee imeweza kupiga hatua katika masuala ya jinsia. Hili ni kwa sababu sasa, imefanikiwa kuwa na marefa wanawake, pia sasa hivi Tanzania tunayo timu ya mpira ya wanawake katika ngazi ya Kitaifa (*Twiga Stars*).

Mheshimiwa Spika, sanjari na hilo, nguvu zinazoelekezwu katika kuboresha usawa wa kijinsia kinadharia zinatakiwa zitoke katika pande zote mbili. Kwa kuzingatia hili, naomba kwa nafasi ya kipekee kabisa nigosie michezo wa mpira wa pete nchini

maarufu kama netiboli. Kabla sijaendelea zaidi, naomba kuwapongeza timu ya wanaume ya mpira wa Pete ya Polisi, kutoka Zanzibar kwa kuendelea kutetea ubingwa wao katika mchezo huu, Afrika Mashariki na Kati. Wenzetu wa Visiwani, kwa hili wametuzidi na wanastahili pongezi kwani wanadhihirisha wazi kuwa wao elimu ya jinsia wameielewa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuweka hayo bayana, nirudi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tunatambua kuwa, Bunge ndio kioo cha jamii, ndio taswira ya jamii, pamoja na hilo Bunge linatakiwa kuwa chachu ya mabadiliko ya jumuiya yote. Bunge limeweka wazi kuwa usawa wa kijinsia ni moja ya vitu muhimu kwa maendeleo ya Wabunge wote na ushiriki wa Wabunge kwenye Michezo haujatofautiana kwa minajiri ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wanawake wanashiriki katika michezo ya mpira wa miguu vizuri kabisa. Lakini mpira wa pete ni tofauti. Timu ya mpira wa pete ya Bunge ni ya wanawake tu. Hapa kuna tatizo. Kwa nini Wabunge wanaume hawashiriki katika michezo huu? Hili linaweza kuonekana kuwa si tatizo lakini kwa wanaojali na wanaotaka mabadiliko ya kweli wanalionna hili kama tatizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tovuti ya Wananchi, katika mwaka wa 2007/2008, Wizara hii ilikamilisha uanzishwaji wa Tovuti ya wananchi na mkandarasi alikabidhi mradi Serikalini mwezi wa Aprili 2008, baada ya muda wa majaribio wa mwaka mzima. Wizara husika kwa unyoofu wake inakiri kuwa Tovuti inafanya kazi vizuri kwa ushirikiano kati ya Idara ya Habari (MAELEZO), Wizara zote za Serikali pamoja na Mikoa katika kujibu hoja za wananchi.

Mheshimiwa Spika, hii inatia fedheha, kwani Tovuti hii ya wananchi imegharimu fedha nyingi sana ambazo ni kodi za wananchi ambaa ni maskini na wanazitoa kwa uchungu mkubwa kwa kuzingatia ugumu wa hali ya maisha uliopo nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani inaomba kuchukua nafasi hii kufikisha mezani malalamiko ya wananchi juu ya Tovuti hii. Wananchi wanalamika kuwa, ufanisi wa Tovuti hiyo ni sawa na hakuna. Hii inatokana na ukweli kuwa pamoja na kuwa wananchi wanatumia mwanya huo kutaka majibu kutoka kwa Wizara au taasisi zote za Serikali lakini majibu hawapati. Hivi ni ya nini kama haifanyi kazi yake? Kuna umuhimu gani wa kuwa nayo ilhali haisaidi chochote. Hii ni Tovuti tu bado hatujaangalia simu wala barua. Kambi ya Upinzani inahitaji majibu ya kina kuhusiana na sakata hili, ni kwa nini Tovuti hii haitoi majibu ya hoja za wananchi? Je, kazi yake ni nini? Je, ni watu gani ambaa wako chini ya Wizara ambaa wamepewa mamlaka ya kufuatilia maswali ya wananchi na kufuatilia majibu?

Mheshimiwa Spika, tatizo la tovuti hii linafanana sana na ile ya Ikulu ambayo kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa haifanyi kazi pamoja na ukweli kuwa hivi sasa kuna Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa Ikulu ambaye analipwa fedha za walipa kodi kwa ajili ya kuwapatia wananchi habari mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kutambua kuwa Tovuti hii ipo chini ya Ofisi ya Rais, inatambua pia kuwa jukumu la kuhabarisha umma lipo chini ya Wizara ya Habari. Hatuoni umuhimu wa kuwepo na Mkurugenzi wa Habari kama utendaji kazi wake ndio huu, tunashauri kuwa badala ya kuanzisha vyeo ambavyo havina ufanisi katika utendaji, basi sasa ni wakati wa kurudisha utamaduni wa hapo awali wa kuwa na Mwandishi wa Habari wa Rais na huku majukumu mengine yakiwekwa chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uhuru wa vyombo vyahabari. Suala la habari ni suala linalowagusa Watanzania wote kwa ujumla na hata wakazi wasio raia wa Tanzania. Haki ya kupata habari kwa wananchi ni haki ya msingi tena inayotambulika kikatiba. Katika nchi yetu ya Tanzania pamoja na ukweli kuwa *radio* ndio chanzo kikubwa cha kusambasa habari Mikoani, asilimia 56%, runinga na magazeti pia ni vyanzo vikubwa vyahabari katika miji, amba ni asilimia 44% na zaidi ya asilimia 20% (Chanzo: Taarifa ya hali ya umaskini na maendeleo ya watu - 2007).

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vyahabari ni jambo la msingi hasa kwa kuzingatia kuwa ndio njia pekee inayoweza kuwapasha wananchi habari zile za uhakika kwa maendeleo ya jamii yote na nchi yenye kuheshimu uhuru wa vyombo vyahabari ni nchi ambayo inatambua nini maana ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyahabari ndio vyenye uwezo wa kuweka wazi maovu yanayofanywa na watu au viongozi wanaotumia nafasi zao vibaya. Hivyo uhuru wa kufanya kazi yao bila kuingiliwa na nguvu za dola unatuhakikishia uwajibikaji na pia kuchochaea utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapongeza kazi na majukumu ambayo yamekuwa yakifanywa na waandishi wa habari hapa nchini na jinsi ambavyo wameweza kufanya kazi zao kwa ufanisi pamoja na mazingira ya kazi zao kuwa ni magumu. Tunapenda kupongeza kazi ambayo imefanywa na mwandishi wa habari wa BBC, Vicky Mtetema, kuhusiana na mauaji ya albino hapa nchini mwetu pamoja na wale wote waliofanya vizuri kama Richard Mgamba kwa kushinda Tuzo mbalimbali za Kimataifa katika uwanja wa uandishi wa habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mauaji ya albino kama alivyofanya Vicky Mtetema ni habari iliyokuwa ngumu kuifua tilia na kuchunguza na hata ya kuhatarisha maisha yake kwani aliweza kwenda na kuwahoji waganga wa jadi amba wamekuwa wakijihuisha na mauaji ya albino hapa nchini. Taarifa ile inapaswa kuchukuliwa na Serikali na kufanyiwa kazi kwa kina kwani sasa Serikali imeweza kupata taarifa kuhusiana na ni nani hasa hao wanaojihuisha na mauaji hayo. Pia tunataka kujua ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali ili kumlinda mwandishi huyu kwani kutokana na taarifa yake pamekuwepo na taarifa kuwa waganga wale pamoja na watu wengine wasiojulikana wanamtishia maisha yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika siku za karibuni tumeona viongozi wengi wakishutumu gazeti la Mwanahalisi, ambalo linaongozwa na Mkurugenzi wake Ndugu

Saed Kubenea. Mara ya kwanza alivamiwa ofisini kwake na kumwagiwa kimiminika kinachosemekana kuwa ni tindikali, lakini hilo halikutosha hivi majuzi Serikali kupitia vyombo vyake vya dola na hapa tunamaanisha Polisi walienda katika ofisi za gazeti hilo na nyumbani kwa mhariri huyo na kukagua bila ya kuweka wazi nia yao ni nini? Wanakagua bila kusema sababu na ni dhahiri polisi haikufuata utaratibu uliowekwa na sheria katika ukaguzi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, je, polisi wako juu ya sheria hata kama walikuwa na hati ya Mahakama? Isitoshe, ni vipi polisi badala ya kufuatilia ukweli au la wa taarifa inapoteza muda na fedha za walipa kodi katika kufuatilia chanzo cha habari? Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe ufanuzi wa kina katika hali hii ambayo kwa dhahiri inalenga kuua kazi na uhuru wa vyombo vya habari. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inadhani waandishi wa habari wenye kutoa taarifa za ubadhirifu kama hizo wanatakiwa kupewa tuze badala ya kunyanyaswa na kutishwa kwani kwa siku za hivi karibuni ni dhahiri vyombo vya habari vimekuwa mhimili muhimu wa demokrasia na wa mali na rasilimali za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji Serikali kutoa tamko juu ya sababu ya msingi ya polisi kuvamia ofisi za magazeti haya na kupekua na kuchukua vitendea kazi kama *computer* bila ya kutoa sababu. Je, huku sio kuingilia haki ya uhuru wa vyombo vya habari? Lakini pamoja na hilo Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara husika kuleta haraka Muswada wa Sheria ya Habari ndani ya Bunge hili ili mambo kama haya yaweze kudhibitiwa kisheria, na si kufuata matakwa ya mtu au kundi la watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inalaani na kukemea kitendo hiki kwa nguvu zote na tunapenda kuchukua nafasi hii kuwashakikishia waandishi wa habari wote kuwa tu pamoja nao kwa hali zote, na katu hatutakaa kimya kuona haki zao zinanyang'anywa kwa njia yoyote. Tutadumisha ushirikiano wetu na kama wana lolote wasisite kututaarifu nasi tutalifanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa kumalizia Kambi ya Upinzani inataka Waziri atoe majibu ya ni kwa nini hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, haikuonyeshwa moja kwa moja na Shirika la Utangazaji la Taifa siku akiwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu, Bajeti ya mwaka 2008/2009 na badala yake kituo hicho kikawa kinarudia kurusha hotuba ya Waziri Mkuu kinyume na ilivyozoleka kuwa hotuba za Wabunge wote zinakuwa zikionyeshwa moja kwa moja yaani *live*. (*Makofi*)

Tatizo hili limejirudia pia siku ya Alhamisi iliyopita, wakati wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo maswali takriban yote ya Wabunge wa Upinzani kuanzia na Kiongozi wa Upinzani Bungeni hayakuonyeshwa, na mara baada ya hapo *Television* ya *TBC* ikaendelea na kipindi cha maswali kama kawaida.

Suala hili linapaswa kutolewa majibu kwani pamekuwepo na malalamiko na manung'uniko kutoka kwa wananchi juu ya tukio hilo. Hili ni Shirika la Utangazaji la Taifa na siku za karibuni imejizolea sifa kwa kuwa na vipindi vizuri. Ni kitu gani kinaanza kujitokeza tena? Dalili hii ya ubaguzi isipokomeshwa na kuchukuliwa hatua basi tunaanza kuporomoka na kuelekea kubaya tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ningependa kujua juu ya Kijiji cha Michezo, je kimeishia wapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nitoe angalizo kuwa Kambi ya Upinzani inahitaji majibu ya kina kuhusiana na masuala yote yaliyoulizwa na ni matarajio yetu kuwa majibu yatakayotolewa na Wizara yataendana na maswali yaliyoulizwa na si vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na wananchi wote ambao wanansikiliza, pia ninawashukuru Mheshimiwa Waziri wa Wizara, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuiendeleza Wizara hii ambayo ni ngumu na ina majukumu makubwa na ipo kama Wizara tatu zilizo ndani ya Wizara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ahsante na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi ahsante sana kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji 13. Muda uliopo hata nikiongeza nusu saa jioni kwa mujibu wa Kanuni nitaweza kuwawezesha wachangiaji wanane tu kuweza kuchangia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mtiririko utakuwa kama ifuatavyo, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Richard Ndassa, nadhani tutamalizia na Mheshimiwa Martha Miata. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla sijaendelea kuwaita wachangiaji, nilikuwa nimemtaka hapa kwamba Chama cha Wamiliki wa Vyombo vyta Habari kilikuwa na uwakilishi, hapa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo aliwaalika kidogo kulikuwa na matatizo wamekuja kwa ndege, lakini sasa ninawaona wapo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba nitambue kuwepo kwao Mwenyekiti wa *MOAT* Ndugu Reginald Mengi, yule pale. Karibu sana. Katibu Mtendaji wa *MOAT* Ndugu Henry Muhanika yule pale, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Ndugu Samuel Nyala yule pale

karibuni sana, Bibi Rose Mwakitwange, Mjumbe mwingine nadhani yeye bahati mbaya hayupo. Ndugu Absalom Kibanda Mjumbe mwingine wa Kamati, ndugu Saed Kubenea, Mjumbe mwingine wa Kamati hiyo na Ndugu Fayazi Bojani. Basi karibuni sana ndugu zetu wa *MOAT*, sisi tunafurahi sana kuwaona na ni vizuri msikie maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu sekta hiyo muhimu sana ya upashanaji habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Raphael Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Mudhihir Mohamaed Mudhihir na wakati huo Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar ajiande. (*Makofi*)

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, napenda na mimi kuanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuwasilisha hotuba ya Bajeti yake. Napenda kwa kuanza kusema kwamba naunga mkono hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, habari ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote lile na habari ikitumika vyema ina mchango wa msingi sana kuleta tija katika ustawi wa jamii inayohusika. Kwa sasa hivi maendeleo ya wanahabari hapa nchini yamezungukwa na changamoto mbalimbali ambazo ni lazima jamii tuzielewe na lazima Serikali izielewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia na Bunge lako Tukufu sasa hivi kila mwananchi anaewela kwamba Bunge linafanya nini. Sasa wananchi popote walipo wanasiliza na kufuatilia kwa makini sana habari za Bunge ni kwa sababu ya mfumo wa uvezeshaji wa habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza sana wanahabari kupitia vyombo vyao vya habari. Kwa sababu wameleta mapinduzi makubwa sana ya habari hapa nchini. Sasa hivi unaweza ukaangalia televisheni ukiwa kijijini, ukasikiliza redio kwa usikivu mzuri sana, na vilevile ukafuatilia maandiko mbalimbali kwenye magazeti yanayohusu mchakato na mustakabali wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni fursa ya kujivunia kwa Watanzania. Napenda kupitia Bajeti ya Wizara hii nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kweli aimarishe vyombo vya habari, aimarishe uhuru wa vyombo vya habari na aviwezeshe viweze kutoa mchango muhimu kwa tija na mustabakali wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukianza na *TBC*, kabla ya *TBC* tulikuwa na *TVT* ilikuwa inatoa taarifa vizuri zaidi, *Star TV* ilikuwa inatoa vizuri zaidi pamoja na redio zake, *Radio One* na *Radio Free Africa*. Sasa hivi vyombo hivi vimeimarika, lakini kuimarika huko iwe ni sehemu ya changamoto kwa Watanzania. Sasa hivi Serikali inatoa fedha kuimarisha *TBC*, ninaomba kweli itoe fedha za dhati ili kusudi *TBC* iimarike vizuri zaidi na iweze kutoa mchango mkubwa kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unajua katika habari ni kama hadithi ya kuku na yai. Mara nyingi nyama ya kuku ikiwa nzuri mlaji anafurahi, lakini kuku hawezu kupatikana bila ya kuwa na yai. Mimi nafikiri vyombo vya habari hapa nchini sasa hivi vinahitaji visaidiwe kwa maana ya kwamba Serikali isianze kuviona kwa mtazamo hasi lazima Serikali ivitazame kwa mtazamo chanya badala ya mtazamo wa hasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninasikitika kusema kwamba sijui Serikali kuna wakati inaenda likizo, sijui namna gani sielewi. Mheshimiwa Rais alitoa agizo kwamba Wizara ziwe zinatoa habari kwa wananchi, lakini ni Wizara ngapi zimeweza kutoa habari kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliagiza. Sasa kama Mheshimiwa Rais anaagiza na bado watendaji hawatekelezi ni nani aliye juu ya Rais, mwanamume hapa Tanzania ni mmoja tu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye mwenye kutoa agizo ambalo lazima litekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetumia lugha kidogo ya kusema mwanamume, lakini nasema kwamba kiongozi mkuu hapa nchini Rais. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli inasikitisha kuona kwamba pamoja na agizo la Mheshimiwa Rais, lakini bado Serikali na baadhi ya watendaji wa Serikali wameshindwa kutoa taarifa zinavyotakiwa kutolewa. Matokeo yake watasema kwamba kuna tangazo kwenye gazeti juu ya taarifa fulani, hatuhitaji matangazo, tunachotakiwa ni taarifa zifafanuliwe kwa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, linapokuja suala la upotoshaji wa habari kumekuwa na mambo mengi sana ambayo tunadhani kwamba kuna upotoshaji wa habari. Lakini kwa nini habari zinapotoshwa? Kwa sababu pengine wanahabari wanatafuta habari bado mtoa habari hataki kutoa habari. Ninaomba hizo taarifa zitolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa hata masuala ya *Richmond*, ya *IPTL*, ya *EPA* yalianza kama habari rojo rojo, lakini tukaishia hapa ndani ya Bunge kuthibitisha kwamba yalikuwa na sehemu ya ukweli ndani yake. Hivi Serikali ilikuwa wapi kutoa taarifa kama hizo na kuna wakati Serikali ilikanusha ikasema ni uzushi ni nini na kila kitu, na kuita waandishi wa habari ni waongo. Sasa uongo uko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli Serikali sasa ibadilishe mfumo wake wa utendaji kazi, ijaribu kuona sasa kwamba kila changamoto inayokuja iitazame kwa mtazamo chanya siyo mtazamo hasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa mara nyingi tunaangalia kwamba uhuru wa vyombo vya habari umekuwa sasa ni tatizo. Mimi sielewi kama kweli ndiyo misingi ya utawala bora. Hivi mwanahabari anapokuwa na habari akaandika na baada ya kuandika Serikali haikukanusha. Baadaye tunaanza kusema kwamba ni tuhuma tuhuma. Mimi ninafikiri hatutendei haki hii sekta ya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hebu jaribu kukaa vizuri na wamiliki wa vyombo vya habari muweze kuwa na

mustabakali wa wenyewe mtazamo sahihi kwa nchi hii. Kwa sababu habari ikipotoshwa tunaowapata hasara ni Watanzania wote. Habari ikiwa njema ni kwa faida Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii suala la ufisadi limepamba moto kila mahali. Mtazamo wa nje unakuwa kwamba Watanzania ni mafisadi, Serikali ni fisadi kumbe siyo hivyo. Sasa kwa sababu gani, ni kwa sababu hatujaweza kuweka mustakabali mzuri kati ya vyombo vyaa habari na Serikali juu ya mfumo wa kutoa habari. Kwa sababu habari ni nzuri kama imetolewa sahihi, habari ni mbaya kama imepotoshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana hata wamiliki wa vyombo vyaa habari wachangie kutoa habari ambazo zinajenga nchi yetu, sote ni wadau wa nchi hii. Nchi hii ikiharibikiwa hakuna cha mwanahabari na hakuna cha nani wala si suala la Serikali peke yake ni suala la Watanzania wote. Waandike habari wakiwa na uzalendo ndani ya miyo yao kwamba wanajenga nchi yao, lakini wasisitize kufichua maovo, wafichue maovo lakini wawe na uzalendo ndani ya miyo yao. Nawaomba sana hii wanahabari wajaribu kuizingatia. Hawaandiki habari kwa ajili ya kukomoa mtu fulani na habari ya aina hiyo haitasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara nyingi waandishi wa habari wanapashwa kutumia weledi zao pamoja na miiko ya kazi yao kuandika habari ambayo kweli inastahili kuingia katika jamii. Watanzania siku zote sasa hivi kukicha asubuhi wanakimbilia kusikiliza magazeti yanasema nini, redio inasema nini na wapinzani wanasema nini? Hoja yoyote hapa ni ya Watanzania wote. Kama kuna habari ambayo kweli tunastahili kuifahamu Watanzania tusikilize na itolewe taarifa zilizo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi inaniwia vizuri sana kuona kwamba mara nyingi kunakuwa na msakamano sana katika ya Serikali na vyombo vyaa habari. Tumesema kwamba sheria ile ije imechukua muda mrefu na sijui kwa nini imechukua muda mrefu. Kwa nini tusifike mahali tukubaliane basi Muswada uje Bungeni ili tuweze kutoa mwongozo sahihi kuhusu sekta ya habari. Kwa sababu sekta ya habari inakwenda na wakati, wakati ukipita inakuwa tena haina mantiki yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vyema zaidi nilikuwa naomba Wizara husika ijaribu kuharakisha mchakato wa kuleta Muswada Bungeni hapa ambaa utaboresha suala la sekta ya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo ukisikiliza kila siku hata wananchi sasa waanza kusema kila siku ni habari, habari, lakini tunayosema sasa ni kwamba Watanzania tubadilike. Mimi kitendo cha juzi hapa cha mwanahabari kwenda kupekuliwa kwa sababu ametoa taarifa fulani, mimi sidhani kama tumemtendea haki. (*Makofi*)

Ningeomba pengine Serikali ijaribu kuangalia kwa sababu *approach* ya namna hiyo ni ya kutisha waandishi wa habari wasiandike habari na hii inajaribu kukinzana na dhana nzima ya uwazi. Hizi ni zama za uwazi na ukweli. Kama kuna taarifa wacha

itolewe, hakuna mtu aliyejua kwamba kuna ufisadi, kuna fedha zinaingia kwenye mabenki mbalimbali, isipokuwa waandishi wa habari walitoa taarifa hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba jamani Serikali hebu ijaribu kuangalia, nadhani Serikali ijibu hoja badala kukurupuka. Ningombwa sana sana Serikali ijielekeze katika kujibu hoja ambazo ni za msingi badala ya kukurupuka. Ukiangalia katika suala hili la kumpekua mwandishi wa habari sawa kama kulikuwa na misingi hiyo, lakini inaleta picha mbaya kwamba tunaingilia uhuru wa habari. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuangalia namna gani tunaweza kufanyakazi kwa kujenga nchi yetu zaidi badala ya kujaribu kuanza kushindana, kuanza kuwindana na mwanahabari gani anafanya hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wanahabari wenyewe kuna wengine ambao kweli wanakiuka miiko ya kazi yao. Naomba na wenyewe waache kukiuka miiko ya kazi yao, watumie taaluma na weledi zao kuhakikisha habari wanayoitoa inajenga nchi. Habari wanayoitoa wanaitoa inasaidia kuimarisha nchi. Siku hizi bila kuathiri mambo mengine habari imekuwa ni sawa na uchumi. Kwa hiyo, naomba tutumie habari kujenga uchumi wa nchi yetu.

Napenda kumpongeza sana dada yangu Vicky Mtetema, juzi alikwenda kufuatilia suala la mauaji ya albino, amekwenda mpaka Jimboni kwangu, amekwenda mpaka kwenye kijiji maarufu cha wachawi kule Gamboshi kule Bariadi, amekwenda kula na ukiangalia sasa kwenye BBC imo ndani imeshakuwa *posted* juu ya mauaji ya albino Tanzania. Hivi mpaka haya mambo yatoke kote kule nje sisi Watanzania tunafanya nini? Naomba kwa kweli suala hili tujaribu kuliangalia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine kwa haraka hebu jamani Mzee Mkapa tumsifu jamani katika yote huyu Rais Mstaafu anastahili sifa kwa Watanzania. Kama ni binadamu kuna mazuri mengi sana ameyafanya, lakini kama binadamu pengine amekuwa na mapungufu machache. Lakini katika sekta ya michezo ameacha historia kwa Watanzania. Tunapaswa kumsifu sana Mzee Mkapa. (*Makofi*)

Kwa kweli baadhi ya Watanzania wengine wanaonyesha kidole kwa Mzee Mkapa ohoo, Mzee Mkapa sijui kitu gani, mimi nasema jamani eeh ni binadamu hakufanya kazi Serikalini peke yake alikuwa na wasaidizi wake, mambo mengine huyu mzee kajitahidi kutujengea misingi imara ya uchumi wetu alikuwa makini na alikuwa mkali. Alikuwa mkali Mzee Mkapa. Sasa hayo yote tunayaona mengi ni kwa sababu mzee alifanyakazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka kingine michezo ni uchumi. Huu uwanja sasa hivi ni kitega uchumi hiki. Nasikitika sana Yanga kuingia mitini jana, nimesikitika sana. Kitendo hicho ni cha fedheha kabisa na lazima tukilaani kabisa. Kama kuna viongozi wa Yanga waliofanya vile naomba wachukuliwe hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Namuita sasa Mheshimiwa Mudhihir ambaye ni mdau katika Yanga, kwa hiyo, sijui itakuwaje sasa. (*Kicheko*)

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Spika, sina maneno mazuri sana ya kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimehangaiaka sana kuomba kuchangia leo nakushukuru sana itoshe kwa maneno hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi bado ni muumini wa ile dhana kwamba Wizara ya Habari, popote duniani ndio kinywa cha Serikali. Nimesema bado ninayo dhana hii kwa sababu nilishawahi kuzungumzia huko nyuma ikataka kunipa matatizo kidogo. Lakini nashukuru baadaye wamenifahamu kwamba mimi sikuwa *misguided missile* lakini nilikuwa nazungumza lile ambalo nalihisi kwamba ndiyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vina sura mbili duniani kote, kuna sura ya ndani ya nchi na kuna sura ya nje ya nchi. Nitatoa mifano michache. Ukikaa nchini Marekani *channel* ya CNN ambayo tunaiona huku Afrika hutaona hata kitu kimoja ndani ya Marekani. CNN iko Marekani lakini wanachoonyesha ni kitu kingine kabisa na haya tunayoyaona sisi hapa Tanzania na kwingineko kwa sababu wanajua kwamba habari inayotangazwa na CNN ipo inayowahusu Wamarekani, ipo inayohusu maslahi ya Marekani na ipo ile inayohusu sera za nje za Marekani. Iraq ukiangalia CNN hakuna shutuma dhidi ya nchi za Magharibi hata siku moja. Lakini tulitarajia wanaoifahamu historia ya Iraq ugomvi wa Shia na Suni siyo ugomvi wa jana, ni ugomvi ulioachwa kwa ubia wa *Ottoman Empire* na ukoloni wa Kingereza ndani ya Iraq. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Ottoman Empire* na ukoloni wa Kingereza ndiyo ambao uliwakabidhi Suni wachache kuongoza Shia walio wengi. Lakini leo kinachozungumzwa ni ukorofsi wa jamii ya Waislam wa Kisuni na Washia na wengine tunalazimika kuamini hivyo tu, bila kuangalia kwamba ukweli wa machafuko yanayotokea Iraq ni uchochezi wa kutoka nje ya wana Iraq wenyewe. Hiyo ni kazi moja ya chombo cha habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *Sky News* inavyoizungumzia Zimbabwe inazungumzia matokeo siyo kiini cha mgogoro wa Zimbabwe. Wazimbabwe walipigana vita kugombea ardhi yao ambayo *Hain Smith* aliamua kuikalia, kitendo ambacho Tanzania tulilazimika kujitoa kwenye *commonwealth* kwa miaka kadhaa. Lakini wakati Zimbabwe inapata uhuru Uingereza iliahidi Serikali ya Zimbabwe kwamba ingechangia kulipa fidia kwa wazungu wale ili ardhi na waafrika nao waipate. Fidia ile haikutoka jana na haikutoka leo wala haitatoka kesho. Tulitegemea *Sky News* pengine ingezungumzia chanzo cha mgogoro wa Zimbabwe. Lakini leo kinachozungumzwa na vyombo hivi vya habari vya nje ni unyama alionao Rais wa Zimbabwe, ni waafrika kung'ang'ania madaraka, ndiyo utaratibu wa vyombo hivi vya habari vina mambo yao ya kutetea ndani ya nchi zao, lakini vina mambo yao ya kuharibu nje ya nchi zao. Hili lazima tulifahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanasema pengine ningelizungumzia hili kwenye Wizara ya Nchi za Nje, nazungumzia humu kwa sababu nazungumzia habari. Lakini nakubaliana na kila mmoja wetu hapa kwamba wanahabari ni watu muhimu sana, ni watu

muhimu katika maendeleo ya nchi ni watu muhimu katika mageuzi ya kisiasa, wanahabari ni watu muhimu katika kutengeneza amani na utulivu ndani ya nchi na wanahabari ni watu muhimu katika kujenga uchumi wa nchi na ni muhimu sana katika kufichua maovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi wala sikasiriki wanahabari wanaposema kwamba sisi ni mhimili wa nne wa nchi hata kama hawamo kwenye Katiba kwa kazi wanayoifanya kwa kweli wanastahili kufanana fanana na mhimili wa nne wa nchi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninawaunga mkono sina nongwa na mwanahabari yejote na kwa kweli ukiamua kuwachukia wanahabari unajichukia mwenyewe. Kwa msemo wa Waarabu ukijipiga kofi mwenyewe usilie huna haki ya kulia (*mandhara banafsihi la yabk*).

Mheshimiwa Spika, najua kiarabu unakifahamu kidogo kwa hiyo huna taabu ya kutafsiri hili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwanahabari ambaye kwa mapenzi yake akiamua kwenda kinyume na maadili yake hatari yake inakuwa kama moto unaoweza kuunguza mbuga na nyika. Katika hili mimi nisingependa kuweka *blanket statement* kwamba wanahabari wote wana matatizo, hapana jamani mwanahabari huyu ni mwanadamu na mwanadamu ana mambo yake anayoyapenda, ana mambo yake anayoyachukia hata ukifanyaje huwezi ukambadilisha. Sasa si vizuri anapotekea mwanahabari mmoja kafanya tatizo tukafikiria huo ndiyo udhaifu wa wanahabari wote. Hili nalielekeza kwa Serikali kwamba wanapozungumza mabaya kuhusu Serikali tusiwaone kwamba wale wamekuwa ni wanga kwa Serikali. Lakini kama anafanya vile kwa makosa vile vile tusiwichanganye wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, akitokea Padri akafanya zinaa siyo Ukristo siyo Biblia, ni yeye. Akitokea maalim, Ustadhi, Shehe akaua siyo Uislam, siyo *Quran* ni yeye, hali kadhalika akitokea Kiongozi wa CCM, akafanya ufisadi siyo CCM ni yeye. Kwa hiyo, akitokea mwanahabari mmoja akafanya anayofanya kwa mapenzi yake kwa raha zake tu, si vizuri kuona kwamba hiyo ndiyo *tendency* ya wanahabari au wamiliki wa vyombo vya habari hilo ni tatizo lake yeye mmoja na kwa kweli inafaa kushughulikiwa yeye peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo tulitegemea nini katika wingi huu wa vyombo vya habari, vipo vyombo ambavyo wala havihitaji kujitangaza nitanunua magazeti yake, nitafungua *station* yake, iwe *television* au redio. Lakini kuna vyombo ndiyo vimezuka vimeibuka vyenyewe vinatafuta kujijenga vitatengeneza tu habari kwa namna yoyote watu wanunue wanasoma *heading* kitu kingine, habari ya chini kitu kingine. Ndiyo matatizo ya kuwa na vijogoo wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu msemo mmoja hapa rahisi sana. Huu ni wa *Mabedui* wa Kiarabu; “*katharat-duyyuk safadu laili.*” Vijogoo vikiwa vingi vinaharibu usiku vingine vitawika saa nne usiku, vingine saa sita, vingine saa nane ndiyo vijogoo. Lakini hatimaye majogoo imara *wata-survive* wale wabovu wabovu watajiondokea hali

itakuwa nzuri. Kwa hiyo, haya ni mambo ya kupita ningeomba Serikali mjaribu kuvivumilia sana vyombo hivi vya habari ambavyo wakati mwingine vinalazimika kusema hayo wanayoyasema au kuandika wanayoyaandika kwa sababu ya kutafuta *ku-exist*. Muda ukifika au vitajirekebisha au vitapotea vyenyewe tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo basi naomba kupendekeza mambo yafuatayo, la kwanza Serikali iendelee kutoa umuhimu kwa vyombo vya habari vya Serikali kwa kuviongezea uwezo. Uwezo wa vifaa na uwezo wa wataalam viweze kupambana na vyombo vingine na ningeomba vyombo vingine vile vile pendekezo langu la pili wajenge utamaduni wa kustahimiliana. Ukiona mwenzako amekwenda juu wewe pambana uende juu yake zaidi badala ya kuanza kujenga kutuhumiana, kuanza kupikiana majungu, kuanza kupelekana Mahakamani ni vitu havipendezi kidogo. (*Makofi*)

La pili, BAKITA Serikali yetu imetuhimiza hapa kwamba tukuze Kiswahili tusiwaruhusu majirani zetu kuwa Waswahili kwa sababu Kiswahili kilizaliwa Tanzania, kilikufa hapo kwa jirani zetu na kitazikwa kwa jirani zetu wengine. Tunajitahidi sisi Waswahili wa Kitanzania kukikuza Kiswahili, lakini Serikali hiyo hiyo inatuvuruga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili nina *interest* nalo na naomba ku-*declare*. Mimi baada ya kusikia Serikali inapiga kelele sana juu ya Kiswahili kukuzwa, nikatunga kitabu changu kinaitwa Mwele Bin Taabani ni mgogoro wa wananchi na Serikali yao kupitia Mbunge wao Mheshimiwa Chemka. Baraza la Kiswahili limetoa ithibati ya kitabu hiki muda mrefu, Wizara ya Elimu Idara yake inaitwa *EMAC* ikapendekeza kitabu hiki kisomwe fasihi *Form III* na *Form IV* lakini kuna kitu kinaitwa Idara ya Mitaala sijui Taasisi ya Mitaala wanasema kimechelewa kisubiri miaka mitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunayo habari kwamba na wenyewe nao wanatunga vitabu kwa hiyo anapokuja mwandishi mwingine wanaona kama vile anakwenda kuwafunika. Katika mazingira haya ya Wizara ya Elimu kusema kingine, BAKITA kupitia Wizara ya Habari kusema kingine hamtownapata Waswahili wa kutunga vitabu na kuvileta nchini kwetu tutavipeleka kwa *publishers* wa Kenya. Hatuna njia nyingine maana mnakuwa kama yule anayebembeleza cheo akishapata anasahau. Na hii nimnukuu Bruto kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika. William Shakespear katika kitabu Julius Ceasar onyesho la kwanza sehemu ya nne alisema hivi “Lakini ni wazi kwamba unyenyekevu ni ngazi ya kila mtaka cheo ambaye anayepanda huitazama kwa juu bali akishakanyaga kile kipago cha mwisho mara huipa kisogo ngazi aliyoipandia akatazama mawingu na kudharau vya chini.” Mmetubembeleza tutunge vitabu hivi na tumeweka katika Ilani yetu tunafanya hivyo kwa sababu mllichokitaka kimeshapatikana hamuoni tena umuhimu wa jambo hili. Hili jambo linaumiza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa Yanga, alinitaja kwamba ni mdau, ni kweli. Kilichofanyika jana kama nisingekuwa muungwana ningesema siamini kilichotokea, lakini kwa sababu ni muungwana unatakiwa uamini kilichotokea kilikuwa ni kitendo cha aibu na cha fedheha kubwa. Lakini *Sir Arthur Connan Doyle* katika kitabu chake cha

Sharlock Holmes anasema; “*It is a capital mistake to twist facts in order to form a decision.*”

Tunasikia habari eti *CECAFA, TFF*, Yanga na Simba walikutana kujadiliana shilingi milioni 50 ilioingia uwanjani. Kama hawa kweli walikutana watu wote hawa wamefanya kitendo cha kihuni. Kanuni za *CECAFA* zinafahamika na zinatakiwa zizungumzwe mwanzo zikishirikisha timu zote lakini unapofikia baadaye unaamua kuwaita Yanga na Simba kwa sababu wao ndio wanaingiza pesa nyingi uwanjani, huu ni uhuni wanaopaswa kulaumiwa wote waliohusika na kikao hicho. (*Makofi*)

Kwa hivi sasa naogopa kusema aliyojasema ndugu yangu Mheshimiwa Raphael Chegeni kwamba nalaani kitendo cha Yanga kwa sababu naogopa *ku-twist facts in order to make a decision*. Lakini utakapotambulika ukweli kwamba *CECAFA, TFF*, Yanga na Simba walishiriki kufanya kikao hiki haya ni mambo ya kihuni na sio uongozi wa mpira na kwa kweli ndio wanatuharibia mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba tena nikushukuru kwa kutambua udao wangu katika Yanga na mimi nikushukuru kwa kutambua udao wako katika Simba ninaamini kadri tunavyokwenda mambo yetu yatakuwa mazuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mudhihir, namwita sasa Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar atafuatiwa na nadhani ndio atakayekuwa wa mwisho, Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makofi*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa pungezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuchika kwa kazi yake nzuri ya ushirikiano katika kuiendeleza Wizara hii. Pia napenda kumpongeza na kumshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Bendera pia kwa ushirikiano mzuri kwa kuiongoza Wizara hii pamoja na Katibu wake Mkuu Mama Hajrat Kijakazi Rajab Mtengwa, vile vile na watendaji wote wa Wizara hii napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika nchi yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuunga mkono hoja napenda kusema na wenzangu waelewe hivyo kwamba Wizara hii imetengewa pesa kidogo. Pesa kidogo sana Wizara hii ni nyeti na ni kubwa sana katika kuendeleza Taifa hili lakini kila siku tukija hapa Wizara hii inatengewa fedha kidogo. Naomba isitokee tena hili kutengewa fedha kidogo hii Wizara na baada ya hapo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye nyanja ya habari. Napenda kuwapongeza wanahabari wote wa nchi hii ya Tanzania kwa kazi yao nzuri na nzito wanayoifanya. Mbali na matatizo mengi ambayo wanayapata hapa na pale, lakini wanahabari wanafanya kazi nzuri sana. Sera ya habari inatamka kwamba Serikali ndiyo yenye dhamana ya kutoa habari au ya kupasha habari jamii ya nchi nzima.

Lakini kutokana na Bajeti kila mwaka inakuja finyu nafikiri ndio maana Wizara hii haitekelezi labda ikafikia kiwango kikubwa sana. Kwa sababu inasemekana kwamba na inaonekana kwamba habari haziwafikii jamii kubwa iliyoko vijijini kama *TV* au redio. Kama utakuwa huna fedha za kutosha huteweza kufikia kule, tusiilaumu hii Wizara tulaumu kwamba fedha ni kidogo lakini tunapenda sana Serikali sasa ione kwamba Wizara hii ifikishe habari yaani vyombo vya habari vifike hadi vijijini huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema hivyo kwa sababu redio hii ya Taifa ndiyo redio ambayo inategemewa na Watanzania. Watanzania si kweli kama watategemea redio za binafsi ama *TV* za binafsi. Kitu ambacho cha Kitaifa cha Serikali ambacho kinataka kutolewa habari lazima taarifa itoke kwenye chombo cha Taifa, lakini sasa utakuta vyombo vingine viko mbele zaidi kuliko vyombo vya Kiserikali. (*Makofi*)

Naomba sana swalii hili lirkebishwe ili *TV* na redio za Taifa ziweze kufika Tanzania nzima. *TBC One* tunaipongeza sana kwa kuboreka, huyu Bwana Tido Mhando kwa kweli hapa anafanya kazi nzuri pamoja na watendaji wake. Ameboresha sana hii katika mfumo huu wa utangazaji na utoaji habari katika vyombo vyetu hivi. Vile vile wanahabari, watangazaji wote wataalam wote maafisa wote pia wa *TBC* napenda kuwapongeza kwa kazi zao nzuri za kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutenda hayo katika kutoa habari katika nchi yetu waandishi wa habari wana jukumu kubwa sana katika kutoa habari lakini wana mambo mengi ambayo yanawakwaza yakiwemo waandishi wa habari kwanza wawe na utaalamu mzuri ama wawe na elimu nzuri, lakini inaonekana wengine elimu inakuwa ndogo kidogo, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwapatie mafunzo hawa waandishi wa habari kwa kila kipindi. Vile vile mitambo ya kisasa, vile vile vifaa vya kisasa, majengo ya kisasa, kwa sababu huwezi kufanya kazi jengo linavuja wewe mwandishi una elimu yako nzuri lakini jengo linavuja, huwezi kujisikia, kwa hiyo, vitu vyote hivyo Serikali iboreshe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye mambo ya utamaduni. Katika utamaduni hapa nataka nizungumzie matumizi ya lugha ya Taifa ya Kiswahili. Napenda kusema kwamba sioni kwamba BAKITA kama inatilia sana maanani hii lugha ya Kiswahili kila siku inaleta *dictionary* mpya mpya hapa lakini kwa kweli lugha ya Kiswahili inadharaulika sana hatia hapa kwetu achilia mbali kwa wenzetu. Lugha ya Kiswahili kwa kweli bado. Mimi nasema hivyo kwa sababu hatujaitangaza vizuri, kwa sababu sisi wenyewe hapa Bungeni tukiongea kitu kidogo unasema-*Swahili English* hapa. Halafu vile kwenye semina mbalimbali utakuta lugha ya Kiswahili hatuwezi kuisema *frequent* yaani unaona narudia sasa moja kwa moja. Lakini ukienda kwenye bodi mbalimbali unaweza kumwona mzungu mmoja tu katika bodi ile lakini eti bodi inaendeshwa kwa kiingereza. Vile vile mambo ya mikutano mbalimbali lazima tuseme ukweli sisi wenyewe hatujawa tayari katika kuikuza lugha yetu ya Kiswahili. Naomba Serikali iendeleze msukumo mzuri wa lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wasanii ni watu muhimu sana kwa sababu wasanii ndio kioo cha jamii. Wasanii mbalimbali wa nyimbo, utenzi, maigizo na kadhalika hawa ni watu muhimu sana katika jamii yetu lakini wanaonekana kama watu tu eti wanawenza kustarehesha tu. Mtu haoni kama wasanii ni watu muhimu sana. Wasanii wa Tanzania wanafanya kazi katika hali ngumu, lazima Serikali ione hiyo wasione tu kama wasanii. Mfano *Ze Comedy* wale wanaona labda wachekeshaji tu mambo wanayoyafanya *Ze Comedy* ni mambo muhimu sana, wanaelimisha sana jamii kwa yule mtu anayeelewa. Lakini kama mtu haelewi atasema wale labda watu tu wasanii wanachekeshachekesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wasanii ni watu muhimu sana. Wasanii wanafanyakazi kwa hali ngumu katika kazi zao kwa kukosa fedha. Hawana mtaji wasanii hawa, hawapewi hata vifaa, Serikali haiwasaidii pengine kuwapatia elimu ya kisanii sehemu za mazoezi zimekuwa chache vile kumbi za mazoezi zimekuwa chache na vile mambo ya mikopo, mikopo inakwenda kwa wajasiriamali wote kwani hawa sio wajasiriamali? Kwa sababu usanii vile ni kuondoa umaskini, ni ajira ni uchumi. Kwa hiyo, napendekeza Serikali iwapatie na wao mikopo, misaada mbalimbali wasanii ili waweze kuendelea kuelimisha jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nazungumzia mambo ya *COSOTA* hivi hii *COSOTA* kila siku *COSOTA*, *COSOTA*. Mimi nasema hapa leo kwamba *COSOTA* sijaona kwamba inawasaidia wasanii. Hatimiliki zao wasanii zinapotea hawana raha mimi naamini *COSOTA* wanashirikiana na hawa ma-promoter, nina wasi wasi. Lakini kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri yupo pale atafuatilia na naomba Wizara hii ifuatilie kwa sababu mimi huwa nawasikia kila siku wasanii wanalamika kwenye TV na redio wanasema hatimiliki zao hazitunzwi, hawatunzwi hatimiliki na hii *COSOTA* ndiyo inayoshughulikia hawa wasanii sasa inakuwaje na naamini hii *COSOTA* itakuwa na watu fulani wabaya, ichunguzwe sana hii *COSOTA*. Kwa sababu wasanii wachanga mtu anatoka kijijini huko akija hapa sijui amuone nani hawasaidii kwa kweli. Watu wanaorekodi nyimbo zao ni wale wasanii wenye hela zao lakini msanii akitoka kijijini akija hapa atapotea. Naomba sana wasanii wasaidiwe vile vole wapatiwe ziara za ndani na nje ili kupata elimu zaidi katika sanaa zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba au naiomba Serikali hii hukumu ambayo inawakabili hawa *Ze Comedy* naomba ifuatiliwe kwa haraka iweze kumalizika wananchi wapate kuelimika. Watu wanawapenda sana *Ze Comedy*. Tunawapenda na sisi Wabunge tunawapenda *Ze Comedy*. Kwa hiyo, tunaomba hii hukumu imalizike haraka haraka ili *Ze Comedy* warudi hasa yule Joti. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia maadili ya wasanii najua kwamba Serikali inahimiza na kufuatilia maadili ya wasanii lakini mimi napenda kusema kwamba wasanii wanenguaji ama hawa wanaitwa *Miss Tanzania* mimi kwa kweli nawaona jamani wanakwenda nusu uchi, wanacheza nusu uchi. Kama *Miss Tanzania* au mbona *Mr. Tanzania* wakifanya maonyesho yao hawavai nusu uchi. Lakini wanawake kwa nini wawe wanawake iwe nusu uchi, sisi wazazi hatupendi. Ukiangalia TV huwezi kutazama

mbele ya mwanao. Si vizuri kwani hivyo sisi maadili yetu ni yale kweli? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kila siku tukiuliza tunaambiwa aah, tunakwenda na wakati jamani hakuna wakati na kwenda uchi, mtoto anavaa nguo zile za jangwani wanaita *beach wear* (za ufukweni), mtoto ana kichupi na sidiria kweli jamani hivyo kweli yale ni maadili ya Mtanzania? Hivyo tunafanya nini sisi viongozi. Kwa kweli hapa Mheshimiwa Mkuchika, naomba uje unijibu kwa kweli mimi sipendi na nawaomba wazazi wenzangu wote hii wasiipende. Mambo ya maendeleo na kwenda utupu haiwezekani. Dini zetu zinazelezea kwamba tuwe tunajihifadhi lakini leo mtu uchi jamani aah, hii haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, wale wanenguaji tena wamezidi kwa nini wanenguaji wanaume wanavaa suruali ndefu mpaka chini na mashati na wanapendeza au kama hujakaa uchi ndio hupendezi? Wasanii nakuombeni sana mjirekebishe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, michezo ni ajira pia ni uchumi. Pongezi kwa vyama vya michezo, timu za michezo hususan timu ya Yanga, mimi timu yangu Yanga. Haya yaliyotokea jana yatarekebishwa, lakini nakwambia timu yangu Yanga. Mheshimiwa Mudhihir dole!!! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda sana kupongeza michezo katika Wizara hii kwa kweli imepiga hatua kubwa sana Serikali yetu katika michezo. Lakini napenda kuuliza kwa upande mwingine hivyo michezo ni *football* tu, *netball* iko wapi, riadha iko wapi, kuogelea kuko wapi kwa nini hii michezo mingine haipewi kipaumbele. Mheshimiwa Waziri nakuombwa sana michezo isiwe ni mpira wa miguu tu vile vile na wanawake wanataka wafurahi na wanawake wanacheza mpira wa miguu lakini na *netball* pia iwepo. Michezo itiliwe mkazo, kuwepo shulen'i vile kama ilivyo, taasisi mbalimbali ziweko michezo kwa sababu michezo ni furaha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, uwanja wa michezo napenda sana kuipongeza sana Serikali yetu kwa kujenga uwanja wa Kimataifa wa Michezo kama pale Temeke, Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunapenda sana vile viwanja hivi visiwe mwisho pale Dar es Salaam viweko na vijijini, mashulen'i, shule zote ziwe na viwanja vya michezo kwa sababu kambale au mtoto mkunje angali mdogo. Mtoto akishajifunza michezo akiwa mdogo, akiwa mkubwa anakuwa kama tulivyojionea wenyewe watoto hapa wamekuja chini ya miaka 17 tumejionea wenyewe ile ni faraja kubwa kwa Watanzania, ni faraja kubwa kwa Serikali, ni faraja kubwa kwa wazazi, kwa hiyo, viwanja visiwepo Jiji tu la Dar es Salaam au na majiji tu viweko vijijini vile viwanja viweko mashulen'i na katika Taasisi mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda sana kutoa pongezi kwa ndugu yetu Japhet Kaseba, huyu ambaye amechukua ukanda dunia juzi alikuwepo hapa. Vile vile napenda kuipongeza timu ya Simba ingawa mimi sio Simba lakini timu ya Simba kuingia nafasi ya tatu ya michuano ya Kagame, vile vile napenda kuipongeza timu yetu ya Vijana chini ya miaka 17 kwa hapo Serikali naiona kama inafanya kazi yake vizuri, naipongeza sana

Wizara hii na iendelee na sisi tuko pamoja na wewe Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Serikali yetu kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, ni zamu sasa ya Mheshimiwa Kabwe Zitto na nadhani yeye ndiye atakuwa kni msemaji wangu wa mwisho kwa mchana huu. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza kabisa kwa mara nyine tena ningependa kuwapongeza vijana ambao walituletea heshima Taifa katika timu ile ya *Kopa Cocacola* na napenda kurudia kusema kwamba katika vijana 16 wale vijana watano walikuwa wanatoka Kigoma na hata Japhet Kaseba ambaye leo Mheshimiwa Waziri amemwelezea hapa kutuletea heshima anatoka Kigoma tena anatoka Kigoma Kaskazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hili ni suala la kawaida kwa sababu inafahamika nchi hii kwamba vipaji vyta soka ni Kigoma, Morogoro, Mwanza na Tanga katika hali ya kawaida. Kwa hiyo, sio ajabu kwa sababu tunafahamu akina Lunyamila, akina Mavumbi, akina Abedi Muziba wote hawa wanatoka Kigoma akina Sande Manara na kadhalika. Kwa hiyo, ni kiasi cha *TFF* kuhakikisha kwamba inakwenda Kigoma kuangalia vipaji ili kuweza kuhakikisha kwamba Taifa letu linakwenda vizuri. (*Makofi*)

Pili, ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kabisa na kumpongeza mwandishi Vicky Mtetema kwa kazi ambayo ameifanya kuhusiana na mauaji ya albino, amefanya kazi nzuri sana na kwa kweli ni jukumu la Serikali sasa kuweza kutumia taarifa ile ambayo ameifanyia uchunguzi Vicky Mtetema kuweza kuwachukulia hatua wale waganga ambao wanatumia viungo vyta albino kwa ajili ya shughuli zao za uganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kesho Wizara ya Mambo ya Ndani inatoa hotuba yao hapa, tungependa watufahamishe ni hatua gani ambazo wamezichukua kwanza kumlinda dada yetu Vicky Mtetema kwa sababu anapata vitisho sana lakini pili kufanya kazi taarifa ambayo ameitoa na ambayo imeweza kutufumbua macho watu wengi sana kuhusiana na mauaji ya albino. (*Makofi*)

Napenda kuungana na Wabunge wenzangu wote ambao wanalaani hatua za polisi kuvamia gazeti la Mwanahalisi na kwenda kufanya *search* katika nyumba ya Mkurugenzi wa Mwanahalisi Saed Kubenea. Nguvu na uharaka ambao polisi wameutumia kama ungetumika kuchukua hatua za kusaka mafisadi katika Taifa hili tusingekuwa na mafisadi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Mambo ya Ndani ilione hilo na hilo pia tutahitaji majibu na Naibu Waziri yuko hapa atamfahamisha Waziri wake. (*Makofi*)

La pili, napenda na mimi niungane na Wabunge wenzangu kupongeza sana vyombo vyta habari vinafanya kazi kubwa sana. Yote ambayo tunayaongea hapa Bungeni bila ya vyombo vyta habari wananchi hawawezi kuyafahamu, yote ambayo yanatokea katika masuala mbalimbali *investigative journalism* ambayo inafanywa na waandishi

mbalimbali imeisaidia sana Taifa hili. Kuna mfano mmoja wa gazeti la *This Day* ambalo lilifanya uchunguzi kuhusiana na mkataba wa kuuza jengo la Serikali ambalo liliuzwa chini ya thamani, lakini kufuatia habari iliyotolewa na gazeti lile Serikali iliweza kuandika mkataba mpya na kiwanja kile kilikuwepo katikati ya mji wa Dar es Salaam kikawa kimeuzwa na thamani ambayo inatakiwa. Hii ni kazi ya vyombo vya habari na wanatusaidia sana kutupasha habari na ni lazima tuwapongeze. (*Makofi*)

Lakini kuna matatizo mbalimbali ambayo inabidi wamiliki wa vyombo vya habari waweze kuyaangalia ikiwemo maslahi ya waandishi wa habari na hasa hasa waandishi wa habari za mikoani ni mionganoni mwa waandishi ambao wanapata taabu sana, wanalipwa kutokana na habari zao zinavyotoka, wanalamika kwamba wahariri wanawaomba fedha kabla ya kutoa habari zao, wanawaomba vocha za simu kabla ya kutoa habari zao, kwa hiyo, ni muhimu sasa wakati vyombo vya habari vinafanya kazi hii nzuri ambayo wanaifanya pia tuweze kuangalia waandishi wa habari wa mikoani kule vijijini ambazo kuna habari nyingi sana wanapewa motisha ya jinsi ya kufanya kazi yao na ni jukumu la wamiliki na wahariri wa vyombo vya habari kuweza kuangalia jinsi gani ya kuweza kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo ambalo ningependa niikumbushe kwa Wizara hii. Wizara hii inasimamia sera ya habari, inasimamia sheria mbalimbali ambazo tunazitunga kwa ajili ya kusimamia vyombo vya habari, hii Wizara sio Wizara ya *TSN* peke yake, sio Wizara ya *HabariLeo*, sio Wizara ya *Daily News*, Wizara hii sio Wizara ya *TBC One* au Wizara ya *TBC Taifa*, sio Wizara ya *TBC FM* wala ya *TBC International*, vyombo vyote vya habari katika nchi hii vinalelewa na Wizara hii. Umezuka utamaduni *tendency* Waziri wa Habari anakuja anasema naielekeza *TBC* ifanye moja, mbili, tatu, nne. Umezuka utamaduni wa Wabunge kumtaka Waziri wa Habari atoe *commitment* kuhusiana na *TBC* inafanya *coverage* wapi nasema hapana. *TBC* ni taasisi huru na inapaswa kuwa taasisi huru. Haipaswi kuingiliwa na Serikali.

Kwa vyovyyote vile kwa sababu unapotoa upendeleo fulani kwenye chombo cha habari cha umma una-*stiffle competition* katika uwanja mzima wa habari. Mambo haya niliyazungumza mwaka jana na Serikali ikasema kwamba itafanya mazungumzo na wamiliki wa vyombo vya habari binafsi, itafanya mazungumzo na vyombo vya habari vya umma ili kuweza kuangalia njia bora ya kufanya *financing* ya *public broadcasting*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana hakuna ambacho kimefanyika. Mpaka leo hii bado vyombo vya habari vya umma na vyombo vya habari vya binafsi vinashindania watangazaji. Hii ni *made in Tanzania* peke yake. Ni lazima tuweke utaratibu ambapo asilimia mia moja ya *TBC* kwa mfano inafadhiliwa na Serikali bila upungufu wa aina yoyote kwa sababu kazi yao wale ni chombo cha habari cha umma.

Mheshimiwa Spika, ni kweli *TBC* bahati nzuri wanaripoti kwenye Kamati yetu ya Mashirika ya Umma wana shida sana. Wana shida mno, ukienda kwenye studio zao zinavuja kwa wale wachache ambao wamepata bahati ya kwenda lakini wanafanya kazi nzuri sana. Kuna *improvement* kubwa sana. Tulikuwa tunalamika hasa hasa sisi wa

Vyama nya Upinzani kwamba *TBC* inapendelea watu wa upande wa Chama Tawala, hali hiyo imebadilika sana hivi sasa. *TBC* wanatutafuta wana *balance story*, ni hatua nzuri sana ya kupongezwa. Lakini ni lazima tuangalie utaratibu wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na *fair competition* katika soko zima la habari. Ni lazima tuamue mambo mawili, moja ama *TBC* inajientesha kibashara au *TBC* inapata *hundred percent financing* ya Serikali na isiingie kabisa kwenye *competition* na vyombo vingine nya binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo hii tunavyozungumza *TBC* wanafanya mazungumzo na *NSSF* kwa ajili ya kusaidia kujenga majengo yao. Michango ya *NSSF* ni ya wafanyakazi, mionganoni mwa wafanyakazi wanaofanya kazi wanapeleka *NSSF* ni wafanyakazi wa vyombo nya habari nya binafsi. Kwa hiyo, kinachotokea ni nini watu binafsi wanatoa michango yao kupeleka *NSSF*, *NSSF* inatumia pesa hizo kwenda kujenga taasisi moja, *this is very unfair*. Ni *made in Tanzania* peke yake ni lazima ibadilike. Kwa hiyo, ni lazima tukubaliane lazima tuimarishe *TBC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *front bench* ya Serikali inanijibu na nadhani ni utovu wa nidhamu kwa sababu Mbunge ana haki ya kuzungumza na nazungumza *in facts*. Kwa hiyo, nadhani waingie kwenye hiyo, naongea na Spika namfahamisha Spika kwamba mnanipigia kelele. (*Makofi*)

SPIKA: Ni kweli hawana haki ya kuzomea na ku... Nadhani tuendelee kwa utulivu hoja zitajibiwa kwa hoja. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa hiyo, ninachoshauri na tumezungumza hii toka mwaka jana kwenye Bajeti ya Wizara hii na mwaka huu nimeona *TBC* katika *vote 96* inapewa shilingi bilioni 4. Bilioni 4 za umma, bilioni za walipa kodi, walipa kodi ambao ni wote wakiwemo watu wanaofanya kazi kwenye vyombo nya binafsi, wakiwemo wamiliki wa vyombo nya habari nya binafsi ni lazima tubadili *attitude* hatupo kwenye mfumo wa *communism* tena, tuko kwenye *free market*. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunachagua njia ya *ku-finance public broadcasting* ili hii sekta binafsi ambayo tunaitaka tuijenge, iimarike iweze kuendelea kuwepo na iweze kutoza kodi. Lakini ni lazima asilimia 100 ya kazi ya *TBC* iweze kulipiwa na Serikali na ni lazima kwa kweli kionekane chombo cha mfano tusiende pale tukakuta kwamba studio zao zinavuja na kadhalika ni lazima wapate msaada, lakini sio kwa kuingia kwenye *competition*. Kama wanaingia kwenye biashara waingie kwenye biashara, kama wanaingia wanakuwa ni *public, finance hundred percent* wasiingie kabisa kwenye *competition*. Ni msimamo wangu ambao nilitoa mwaka jana na naendelea kuutoa na ni muhimu ni lazima uweze kuangalia. (*Makofi*)

La pili, ni kodi Wizara hii inahitajika sana kusaidia vyombo nya habari katika masuala ya kodi na bahati nzuri bado kuna *finance bill* haijaja, kwa hiyo kuna mabadiliko yanaweza yakafanyika. Nadhani kuna umuhimu mkubwa sana kwa vifaa ambavyo vinasaidia kupashana habari, kwa vifaa ambavyo vinasaidia watu kupata taarifa pasiwepo na kodi kabisa, nchi nyingi sana zinafanya hivyo. Makaratasi ya kuchapisha magazeti, makaratasi ya kuchapisha vitabu na kadhalika lazima suala hili liangaliwe na wanaopasa

kusaidia ni Wizara ya Habari kwa sababu wao ndio wanaangalia vyombo vyote vya habari. Wao sio Wizara ya *TBC* peke yake, sio Wizara ya *TSN* peke yake kama juzi nilivyosema ni Wizara ya vyombo vyote vya habari kwa hiyo ni lazima waangaliwe waweze kuwasaidia watu wa vyombo vya habari waweze kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nimepeleka mchango huu kwa maandishi kwa sababu ni mrefu sana niliona kwamba sitaweza kuumaliza, ni kuhusu wasanii wa Tanzania. Dada yangu Faida Mohamed Bakar amezungumza wanapata taabu sana, kazi zao hazithaminiki hata kidogo na *COSOTA* inaonekana kwamba haijawa na nguvu ya kuweza kuwalinda wasanii wetu hawa *Bongo flavour* na kadhalika. Kwa hiyo, nimepeleka mchango huu kwa maandishi na ninaamini kabisa kwamba Wizara itawenza kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa na naomba hili wamiliki wa vyombo vya habari waweze kuangalia. Tuepuke sana kitu kinachoitwa *media imperialism*. Kuna mwelekeo wa kujengwa kwa vikundi ndani ya wamiliki wa vyombo vya habari kuweza kuhakikisha kwamba wanalinda yale maslahi. Hapa sizungumzii *MOAT*, kwa sababu *MOAT* ni taasisi ya wote, nazungumzia wamiliki wa vyombo vya habari *individual*. Ni lazima kuweza kuangalia jinsi gani ya kulinda waandishi wa vyombo vya habari. Maana yake ni rahisi sana mmiliki wa vyombo vya habari kumsimamisha kazi mwandishi. Ni rahisi mmiliki wa chombo cha habari kumfukuza kazi mwandishi kwa sababu anafanya kazi kwenye chombo chake na ana uhuru wa kufanya hivyo. Lakini ni lazima unapomsimamisha, unapomfukuza uweze kuangalia kama ni kweli kuna misingi ya kazi ambayo hajaweza kuisimamia na hili Waziri lazima iliangularie. Lazima kuwe na njia fulani ya kuweza kulinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kabisa kama nilivyosema wewe ni Waziri wa vyombo vyote sio Waziri wa vyombo vya umma peke yake. Hapa Bungeni kimeanzishwa Chama cha Waandishi wa Habari za Bunge. Nimeangalia hotuba yako sijaona kitu kama hicho na ni sehemu ya *reforms* ambazo tumezifanya ndani ya Bunge ambazo ni lazima ziwe *owned* na Watanzania wote ikiwemo Serikali. Tuone ni jinsi gani ambavyo Bunge linasaidia chombo hiki lakini Wizara inasaidiaje chombo hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda wangu umekwisha ahsante sana nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa muda wa shughuli kwa asubuhi hii. Naomba nitoe sahihisho moja la matangazo kutokana na namna barua ilivyoandikwa niliwatangaza vijana wa Menonite wanafunzi 30 kama ni waathirika wa UKIMWI. Kumbe vijana hawa ni wanaharakati katika shughuli zao, wanapambana katika kueneza elimu ya UKIMWI. Naomba radhi sana kwa hilo lakini ndivyo ilivyoandikwa. Kwa hiyo wao wenyewe wote 30 ni wazima kabisa hawakuathirika na UKIMWI ila ni wanaharakati ambao kwa nyimbo na kadhalika wanaeneza ujumbe wa kupinga UKIMWI, kwa hiyo, naomba lieleweke hivyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jioni nitalazimika kutumia Kanuni ya 28, fasili ya 5 kuongeza muda wa nusu saa ili kuwezesha angalau Wabunge wanne waweze kuchangia

kabla ya kumwita mtoa hoja. Kwa hiyo, wafuatao watapata nafasi Mheshimiwa Ole-Sendeka, atatangulia atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na nitafunga mjadala kwa Mheshimiwa Martha Mlata hao wanne. Baada ya hapo ndio nitamwita mtoa hoja kama kawaida kwa dakika 75 yeye pamoja na Naibu wake dakika 75 wanazo halafu tutaingia katika Kamati. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaarifu pale kabla ya kusitisha shughuli mchana inawezekana kwa wachangiaji wanne wakapata nafasi. Nao ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Martha Mlata. (*Makofi*)

Baada ya hapo nadhani itakuwa imefika saa kumi na mbili tutaanza kuingia katika hatua nyingine. Kwa hiyo, sasa namwita mchangiaji, samahani nimevamia namwita Katibu atueleze shughuli inayofuata. (*Makofi/Kicheko*)

HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo

(*Majadiliano Yanaendelea*)

SPIKA: Wachangiaji tunaanza na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo nikiungana na wenzangu ambao wamenitangulia kuongea. Kwa hiyo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba yake nzuri ambayo imeweka mwelekeo sahihi katika suala zima la utekelezaji wa Ilani ya Chama na hasa pale alipogusia juu ya mkakati uliopo wa sasa wa kuleta sheria ambayo kwa maelezo yake inaongeza uhuru zaidi wa vyombo vyahabari nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka kwamba mara baada ya kuchaguliwa kwa Bunge lako hili na hasa katika Kikao chake cha Pili au cha Tatu tulipokuwa tukichangia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila Mbunge aliyejata nafasi ya kuchangia kwa kweli baada ya kumpongeza Rais kwa ushindi wa kura nyingi alizozipata alichukua nafasi hiyo hiyo ya mwanzo kuvipongeza vyombo vyahabari vyote vyahabari vyetumia na vyahabari vya binafsi kwa kazi nzuri walioifanya ya kulisaidia Taifa na wapiga kura

Watanzania kuelewa juu ya sera zilizokuwa zikinadiwa na vyama vya siasa vilivyokuwa vinaomba uongozi wa kuliongoza Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuliwapongeza wenzetu wa vyombo wa habari si kwa sababu ya unafiki bali walifanya kazi nzuri na ni imani yangu kwamba bado tunavitambua na tunatambua mchango wao kama tulivyokuwa tunatambua wakati tukiomba kura na wakati huu pia ambapo tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi. Pamoja na michango yetu yote lakini nakumbuka maneno ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyojasema na naomba kunukuu; "Wananchi wengi wameelimika na kufuatilia mchakato wote wa Uchaguzi Mkuu kutokana na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na vyombo vya habari. Vyombo vya habari vimetekeleza vizuri wajibu wao kwa Watanzania wakati mwengine katika mazingira magumu, nao nawashukuru na kuwapongeza," haya ni maneno ya Rais wetu akitambua mchango wa vyombo vya habari wakati huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona niseme hivi kwa sababu ni imani yangu kwamba sheria hii inayotarajiwa kuletwa ndani ya Bunge lako lazima iwave matumaini waandishi wa habari na wadau wote wa habari nchini kwamba kutakuwa na uhuru kamili katika utoaji wa habari na kwamba haitakuwa sheria itakayotishia au kuwatia hofu wanahabari. Ni imani yangu kwamba Serikali italeta sheria ambayo itawapa matumaini na faraja watu wote na wadau wote wa habari na pengine itafuta ile ambayo wenzetu waliotangulia kusema kabla yangu wakirejea yaliyotokea siku za karibuni za kujenga hofu kwa waandishi wa habari au kwa vyombo vya habari kutokana na upekuzi uliofanyika karibuni na hasa kati ya moja ya magazeti makini ambayo yamekuwa yakiongozwa na uzalendo wa kufichua maovu nchini na mimi nataka kusema kwamba kazi yote tunayoifanya uwe Mbunge au mwandishi wa habairi au mtendaji wa Serikali kama hulengi katika kulinda maslahi ya nchi kwa kweli kazi unayoifanya ni kazi bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Gazeti la Mwanahalisi ni miongoni mwa magezeti ambayo yamefanya kazi nzuri ya kufichua maovu, kufichua vyanzo vya ubadhifuru na ufisadi unaoanza kujikita na kuweka mizizi katika nchi yetu. Nilifikiri kwa kazi nzuri iliyofanywa na waandishi kama akina Saed Kubenea wangestahili kuzawadiwa na sio kutiwa hofu. Huko nyuma nakumbuka Jeshi la Polisi lilikuwa linafanya kazi nzuri ya kuwazawadia wale ambao wanawafichua waovu na majambazi wanaotumia silaha na walikuwa wanazawadiwa. Nafikiri umefika wakati sasa kwa waandishi makini, mahili na wanaosukumwa na uzalendo wa kuipenda nchi yao kwa kufichua maovu yanayotendeka dhidi ya maslahi ya nchi, wazawadiwe, watambuliwe na waenziwe kama ambavyo tunafanya kwa wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kushindwa kufanya hivyo kutatia mashaka kwamba tunaanza kujenga ubia na watu ambao wanaathiri maslahi ya nchi na hatuwezi kueleweka kwa namna yoyote ile. Napenda kuchukua nafasi hii kuvipongeza vyombo vya habari kwa kazi nzuri inayofanya. Najua waandishi wa habari ni binadamu wakati mwengine wanaweza kukiuka maadili ya uandishi wao wa habari lakini mapungufu haya yapo katika taaluma zote, wao ni binadamu hawawezi kuwa wakamilifu. Tuliwahi kusikia hata Daktari ambaye alimpasua mgonjwa goti wakati alitakiwa kupasuliwa kichwa na hiyo ni taaluma nyingine. Tuliwahi pia kusikia pia watu wengine ambao wakifanya mambo

ambayo ni bahati mbaya au wamezembea. Lakini nataka kusema mwandishi wa habari pia anapokiuka maadili ya kazi basi huyo mmoja tumzungumze kama ye ye na tusishughulike na vyombo vyote na kufikiri kwamba vyote vimekosea. Mapungufu haya yapo kote hata sisi tulioko ndani ya nyumba hii si wakamilifu na ndiyo maana wakati mwingine lazima pia tukubali kwamba hata sisi lazima tunaweza tukakosea mahali fulani. (*Makofi*)

Mheshimia Spika, ninawapongeza waandishi wa habari kwa uzalendo huo na mimi hawa ni rafiki zangu wanaofichua hayo. Haya mengine madogo madogo ya kusemana hapa na pale, wakiteleza na kununuliwa; na wakununuliwa wapo wengi hata Madaktari ambao wakati mwingine mgonjwa yupo pale anasubiri kufanyiwa oparesheni. Lakini wapo pia Madaktari wanaosubiri rushwa, ma-*traffic* wanatuzua njiani wakisubiri rushwa. Kwa hiyo, kuwepo kwa rushwa au kukosea maadili kwa mtu mmoja kusiharibu taaluma nzima na kuanza kunyooshewa vidole. Nimeona niliseme hili ikiwa ni pamoja na suala zima la kuimarisha uhuru wa vyombo vyta habari nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Ilani yetu ya Uchaguzi tumejielekeza na kuahidi kwamba tutaimarisha uhuru wa vyombo vyta habari na kuvi boresha kwa kuwasaidia wanataaluma wenye we na kuimarisha taaluma ya habari kwa kushirikiana na wadau au wamiliki wa vyombo vyta habari. Ni imani yangu kwamba nia hiyo njema iliyotangazwa au tulioisema kwenye Ilani ya Uchaguzi tutaitimiza kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya na uzalendo ukituongoza zaidi kuliko maslahi binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna Shirika letu la Habari la *TBC*; napenda kuungana na wenzangu kwa kweli kuipongeza *TBC* kwa kazi nzuri wanayoifanya. *TBC* wanapaswa kupongezwa, tulianzisha *TBC* kwa nia kama chombo cha habari cha umma kwa maslahi ya umma na nifikiri chombo cha umma ambacho kipo kwa maslahi ya umma kinapaswa kusaidiwa na umma na kugharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa. Chombo cha habari cha umma kinatarajiwa kutofautiana na vyombo vyta habari vyta watu binafsi kwa sababu yenye we ina ajenda mahususi ya kusaidia umma uelewe baadhi ya mambo ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba *TBC* ikiwezesha kwa asilimia 100 suala la kufanya biashara au kuwania vitangazo vyta biashara itakuwa imejiondoa. *TBC* wasaidiwe na wagharamiwe kwa asilimia 100 ili waweze kueleza masuala ya kilimo bora, waonyeshe mashamba na waweze kutangaza mashamba darasa kama ya mpunga kule Kyela, waonyeshe na kutangaza ufugaji bora na wenye tija kwa Watanzania. (*Makofi*)

Lakini ukishaweka *commeical aspect* kwenye *TBC* kwa nia njema tu ya kutaka *TBC* iweze kupata uwezo wa kujiendesha una haribu mantiki au maudhui mazima ya kuwepo kwa chombo hiki cha umma kwa sababu chenyewe lazima nacho kibadilishe vionjo vyake kukidhi mahitaji yake ya soko.

Kwa hiyo, badala ya kueleza suala la ufugaji bora wenye tija itabidi na yenye we ianze kuimba nyimbo za *R&B*, *Ndombolo* na manini mimi sio mtaalam sana. Lakini

ukweli ni kwamba itajiondoa ili kukidhi mahitaji ya soko. *TBC* wawezeshwe kwa asilimia mia moja, vyombo vingine binafsi viachwe vishindane. Tukiifadhili *TBC* kwa kuwapa ruzuku wakati vyombo vingine vya habari binafsi havipati ruzuku katika *competition* unayoitengeneza uwanja huo hautakuwa sahihi, hautakuwa wa haki kwa sababu kuna mwingine una mwezesha, watu wawili wanashindana wanapigana mmoja unamfunga jiwe kwenye mkono huu unambakiza kwenye mkono mmoja wakati mwingine ana mikono miwili halafu unasema hapa kuna *fair competition*. Kufanya hivyo kwa kuiwezesha *TBC* wakati inaingia kwenye ushindani ni kutowatendea haki vile vyombo vingine vya habari. Nalizungumza hili kwa sababu sina chombo cha habari lakini naliona kwamba ipo hatari, ukiritimba ni ukiritimba ufanywe na taasisi ya umma, ufanywe na mtu binafsi ukiritimba unabaki kuwa ni ukiritimba. Mimi nafikiri tuwaondoe wao huku, tuwaache hawa wengine washindane na kuogelea katika uwanja wao. Sisi tuwagharamie kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *TBC* isiendolee kuwa kitega uchumi, tuna vitega uchumi vingi. Tuna madini nchini Serikali haihitaji vihela vya *TBC*; tuwagharamie kama huduma nyingine ya hospitali na huduma zingine. Tuwasaidie *TBC* wasimame kwa miguu yao wao wenyewe, kama wanataka kuingia kwenye ushindani na kama mnafikiri ni bora basi wasaidiwe kwa kuhakikishiwa kwamba wanapewa mtaji wakashindane. Kwa sababu mkifanya hivyo mtakuwa mnadhoofisha uhuru au uwezekano wa vyombo vingine vya habari *ku-compite* na kwa maana hiyo tutakuwa hatutendeki au hatuvitendei haki vyombo hivyo vingine. Mimi nashauri kwamba hebu tuitizame na tuangalie malengo ya kuanzishwa kwa *TBC* na tuyasaidie kwa asilimia mia moja yaweze kufanikiwa na tuondokane na kuifanya *TBC* iendelee kuwa kama kakitega uchumi hivi na kuanza kuingia kwenye kugombania matangazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kushauri tu waandishi wa habari pia wazingatie maadili ya kazi zao. Najua yapo mambo kidogo ya ukiukwaji wa uandishi habari na hili hata sisi wanasiasa hatuwezi kukwepa lawama na hasa kwa kuwa siku za karibuni tumeshuhudia baadhi ya wanasiasa wengi wakiingia kuwekeza katika sekta ya habari kwa kuanzisha vyombo vingi vya habari, najua kwa maslahi ya kisiasa zaidi lakini ukishaweka chombo chenye mwelekeo wa kuandaa ama safu ya uongozi au kujilinda wewe mwenyewe au kukufagilia wewe mwenyewe kwa vyovyote vile mhariri yule wa habari atakiuka maadili kwa sababu wewe mwenyewe unampa mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, najua wapo wanasiasa ambao kama rafiki yangu Mheshimiwa Anthony Diallo, yeche ni mtu wa habari tangu siku nyingi, wako ambao walikwisha wekeza huko. Lakini siku hizi naona kila mtu anaji-*attach* tu kwenye chombo cha habari kama si kuanzisha. Tukifanya hivi kuna hatari nafikiri hata katika fomu za maadili ya uongozi au zile za mali ni vizuri tukatangaza tangaza tuka-*declare interest* ya vitu hivi vinginevyo tunaweza kuwa-*brain wash* Watanzania wakakusifia Ole-Sendeka mzuri kumbe ni mionganoni mwa mafisadi wazuri na baadae unaweza ukarudia na ukachaguliwa kwenye uongozi mkubwa wa nchi na kumbe sifa zingine huna ila vyombo vya habari vimekutakasa na kukufagilia njia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kuwa haya ni mambo ya msingi ambayo yanapaswa kuangaliwa kwa nia ya kujenga misingi ya utawala bora na niseme tu

kwamba nchi yoyote ambayo inayoheshimu utawala wa sheria na utawala bora ni lazima ihakikishe kwamba kuna uhuru wa vyombo vyahabari. Tutunge sheria itakayowahakikishia usalama waandishi wa habari, tutunge sheria ambayo itaondoa ubakaji wa taarifa, labda nisitumie lugha hiyo haifai sana. Lakini niseme kitendo chochote cha kupiga kabari uhuru wa vyombo vyahabari ni sawa sawa na kuvinyonga vyombo hivyo. Alichokifanya Saed Kubenea kwa kuandikia akaunti zile na kama sheria inalinda akaunti zile zisitajwe nafikiri kuna haja ya kuondoa kinga hiyo na hasa katika akaunti zile za fedha chafu. Kama sheria inalinda hata akaunti za fedha chafu basi marekebishesho yake na sheria hiyo yaletwe katika hati ya dharura ndani ya Bunge hili ili tuweke bayana kabisa kwamba kinga ile au faragha inakuwepo tu katika akaunti za fedha safi, akaunti za fedha chafu zisipewe kinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mimi naungana na wenzangu Jeshi la Polisi litumie nguvu zaidi kufuatilia akaunti hizo za hizo fedha chafu badala ya kuhangaika na watu wale na kuwakatisha tamaa na mimi msimamo wangu katika hili upo *clear*. Shughulikeni na watu amba ni wahalifu. Fuatilieni fedha hizo, sisi ng'ombe wetu wakiibiwa wakiingia kwenye zizi lako wala hakuna haja ya kugonga hodii, unaingia kwenye zizi unachagua ng'ombe wako unawaacha wa mwenzako, unafuata nyayo tu. Sasa nyayo za wizi zinapotajwa halafu unasema unaweka faragha, unaweka kinga mimi nafikiri kwa kufanya hivyo tutakuwa tunakiuka haki za msingi ambazo Watanzania wanatarajia tulinde mali ya nchi hii. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba hiyo sheria kama inawalinda kweli hata hao basi leteni marekebishesho haraka sana tuyashughulikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, ahsante sana na nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Awali ya yote niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote kwa kutuletea hoja hii kwa sababu kwa kweli hoja ya habari ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa kutoa masikitiko yangu kwa jambo lilitokea jana kwa timu ya Yanga kushindwa kwenda uwanjani. Kwa sababu yoyote ile hata kama ilikuwa kwa maslahi yao lakini ni jambo la aibu kwa sababu mechii ile ilikuwa ni ya Kimataifa na kwa hivyo Yanga kujitoa ilikuwa ni jambo la aibu sana na limetufedhehesha wote kama Taifa na kama nchi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa unaonekana wewe ni mpenzi wa timu bora sio ile timu kubwa. (*Kicheko*)

MHE. SUSAN J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nianze kuchangia kwenye suala zima la vyombo vyahabari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, habari ni jambo la msingi sana na wote tupo hapa kwa ajili hiyo na bila vyombo vyahabari habari zetu zisingekwenda huko Majimboni na sehemu

nyingine zozote za nchi. Lakini kazi za vyombo vya habari ni ama kuelimisha, kuburudisha na kutoa habari mbali na hilo inakuwa sio habari. Lakini utakubaliana nami kwamba vyombo vya habari sasa au wanahabari wengi sekta hii kwa kweli imevamiwa sana na watu ambao hawana malengo mazuri. Unakuta wakati mwininge taarifa zinatolewa ambazo ukiangalia unakuta hazina uhakika na watu wamekuwa wakichafuliwa majina yao kwa sababu ya vyombo vya habari. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri ataliangalia hili kwa kina ili wale waandishi wa habari ambao si wanahabari waweze kuondolewa katika nyanja hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni kwamba siku za nyuma hasa kwa *ITV* wakati imeanza kulikuwa na wale wataalam hasa wa kusaidia wale watu ambao hawasikii au viziwi, lakini siku hizi hakuna. Kinachoshangaza zaidi kwenye *TBC* ambayo hii inatakiwa ionekane nchi nzima bado hawana wataalam wa kusaidia wale wenzetu. Takwimu za Kimataifa zinaonyesha kwamba Tanzania ina watu wasiosikia yaani viziwi zaidi ya milioni moja na laki nane. Kwa hiyo, ina maana ni zaidi ya idadi ya Mkoa mzima wa Morogoro. Kwa hiyo, kwa kuwa habari ni haki ya msingi ya binadamu ni vema basi vyombo hivi vya habari au Waziri aone ni kwa jinsi gani anaweza kuhakikisha kwamba tunapata wataalam wa wa alama ili kuwasaidia wenzetu wale wasiosikia au viziwi waweze na wao kupata habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa sana na watu wengi ni suala zima la kuvamiwa kwa ndugu yetu Saed Kubenea ambaye ni mwanahabari na alivamiwa kwa kutoa habari, lakini sijaona hata katika hotuba ya Waziri kama jambo hili limezungumzwa. Lakini pamoja na kuvamiwa na kuumizwa vibaya namna ile bado mwandishi huyu huyu juzi ameweza kuvamiwa na polisi kwenda kumkagua. Nadhani kwa kweli wote tunakubaliana kwamba gazeti la Mwanahalisi ni gazeti ambalo limekuwa likifichua maovu mengi sana hapa nchini na hatuelewi ni sababu gani askari hao au makachero hao wameenda kumkagua? Nadhani Waziri wakati anafanya majumuisho atalieleza Bunge lako Tukufu ni kwa sababu gani mwandishi huyu wa habari ameweza kuvamiwa bila sababu yoyote ile, hata kama zipo basi inabidi tuelezwe sisi kama wawakilishi wa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumza ni suala zima la maslahi ya waandishi wa habari. Kwa kweli kama nilivyosema waandishi wa habari ni muhimili wa nne lakini pamoja na hilo tumegundua kwamba waandishi wa habari maslahi yao ni madogo lakini licha ya maslahi waandishi wa habari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kama wanavyofanya polisi. Mahali popote pale penye vita, moto au kwenye hatari zozote zile waandishi wa habari ndiyo wanakuwa wa kwanza kufika pale. Lakini waandishi wa habari hawa hawana vifaa vyovyote vile vya kuweza kujihifadhi. Lakini pamoja na hilo unakuta wanapata maslahi madogo sana. Wanaitwa saa nane za usiku saa tisa lakini bado hawapati maslahi ya kutosha. Ndiyo sababu unakuta kwamba wale waandishi wa habari wengi ambao wamesoma vizuri wanakimbilia fani yao. Unakuta wengi wamekwendwa kwenye mashirika au Wizara mbalimbali kwenda kuwa maafisa uhusiano na hao tunawajua ni wengi tu. Kwa hiyo, unakuta kwamba waandishi wa habari wengi wanaobaki unakuta ni wale ambao labda wana elimu ya kati au elimu ndogo. Kwa hiyo, nadhani Wizara kuna haja kabisa ikawapatia elimu waandishi

wa habari lakini zaidi ya elimu iwapatie maslahi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba kama hawana maslahi utakuta ni rahisi sana kurubuniwa na wale wenye vyombo vya habari. Kwa sababu sasa hivi kuna vyombo vya habari vingi vya binafsi lakini hata vya Serikali. Kwa mfano, magazeti unakuta kwa kuwa wanapewa maslahi madogo yule anayehodhi gazeti anaweza akawarubuni kwa pesa kidogo ili waandike habari ambazo si za kweli au wasiandike habari kabisa.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani kuna haja ya Serikali kuhakikisha kwamba wanawaboreshea maslahi yao ili waweze kuandika habari nzuri. Lakini pamoja na hayo kuna suala zima la maadili. Sisemi kwamba waandishi wote wa habari hawana maadili, lakini utakubaliana nami kwamba kuna haya magazeti yanayoitwa magazeti ya udaku. Magazeti haya yanatoa habari za ajabu, yanatoa picha za ajabu na hiyo sio *style* ya Tanzania, Watanzania ni wastaarabu sana. Lakini unapoona magazeti tena kwenye *front page* hata kama huyu mtu amefanya kosa, ni kosa lake binafsi inabidi atolewe picha yake ya kawaida. Lakini wanapotoa picha za utupu sio tu kwamba lina muadhibu yule mtu lakini anaadhibu jamii nzima inayomzunguka pamoja na watoto wao. Kwa sababu unakuta mtoto anakwenda shule kwa kuwa baba yake au mama yake ametolewa kwenye gazeti basi kule shulen i hakukaliki. Mtoto yule atazomewa. Kisaikolojia mtoto huyu atapata shida sana. Nadhani kama kuna msajili wa magazeti na Waziri au Wizara inaona mambo haya yanatokea lakini imekuwa inaacha na kila siku magazeti mapya yanakuwa yanazaliwa na magazeti hayo yanakuwa yanatoa picha mbaya sana kwa jamii. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atalionna hilo na aone ni jinsi gani Wizara inaweza kukaa na kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa na maadili na inaendela kuwa nchi ya kistaarabu kama ambavyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ni suala zima la habari vijijini. Utakubaliana nami kwamba habari haziko mijini peke yake, habari ziko vijijini. Lakini habari zinazotolewa kila siku kwenye *front page* utakuta ni habari za viongozi wa Kitaifa. Lakini habari za Mikoani za vijijini, miradi mingi inazinduliwa vijijini, unaweza kukuta kule Tambuka Reli, Urambo, Moshi Vijijini sehemu zote nchini kuna miradi inaendelea. Lakini magazeti yote utakuta yanaongelea habari za miji mikubwa, habari za mijini na habari za viongozi. Hazizungumzwi habari za viongozi wa vijiji na hii inakatisha tamaa sana wananchi wetu kule vijijini. Kwa hiyo, nadhani labda inawezekana ni kutokana na vifaa duni lakini ninavyojua mimi sasa hivi kuna waandishi habari Mikoani, kuna waandishi wa habari Wilayani. Kwa hiyo, nadhani ni vyema habari za mikoani na za vijijini pia ziweze kupewa kipaumbele kwenye magazeti yetu au katika taarifa zetu za televisheni. (*Makofi*)

Lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala zima la Kiswahili Tanzania. Kiswahili kimezaliwa Tanzania, kimeanzia Tanzania. lakini ukienda nchi za nje Marekani, Uingereza hata *far East* utakuta wale wanaotafsiri lugha zao kwenda Kiswahili unakuta wengi ni raia kutoka Kenya na hapa Tanzania tuna wataalam wengi sana. Pamoja na kwamba Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali alisema kwamba bado hatuna vyuo

vya kutosha kutoa wataalam wa Kiswahili lakini kwa kweli wataalam wa Kiswahili wapo wengi na wanaweza kabisa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, nadhani kwamba Wizara hii ni changamoto kwaao ihakikishe kwamba inawapatia wale wataalam wa Kiswahili uwezo wa kwenda nje ili wawezwe kuliingizia Pato Taifa letu. Lakini pia kwa njia hiyo wanaweza pia kukieneza Kiswahili chetu vizuri kwa sababu Kiswahili cha Kenya huwezi kulinganisha na Kiswahili cha Tanzania hata kidogo. Kwa hiyo, ni ombi langu kwamba Wizara itashughulikia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala *TBC*. Suala la *TBC* limeongelewa sitaki kurudia tena. Lakini ukiangalia kwenye kitabu cha Waziri ukurasa wa 14 ameellezea malengo ya *TBC* lakini nadhani kwamba ilitakiwa kuwa na lengo la kutenda haki kwa wananchi wote. Nalizungumzia hili kutohana na siku ambayo Kiongozi wetu wa Upinzani Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alipokuwa anazungumzia hotuba yake, siku ile hotuba ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa haikusikika kabisa wala haikuonekana na juzi nilimsikia Ndugu Tido Mhando akitoa sababu, lakini nilikuwa nadhani kwa kweli hatukutendewa haki, wananchi hawakutendewa haki kwa sababu walikuwa wanasubiri kwa hamu sana kusikiliza ile hotuba.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kama alilolisema Ndugu Tido Mhando kwamba kulikuwa na uharibifu katika vyombo au hitilafu katika vyombo basi lingezungumzwa siku ile au kesho yake na baadae labda angetangaza kwamba kile kipindi kwamba kingerudiwa ili wananchi waweze kusikia. Lakini mpaka leo hakikufanyika hivyo nadhani labda ameongea juzi kwa sababu alijua kwamba leo tunakuwa na hotuba hii. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba pamoja na sasa hivi *TBC* inatoa habari za Upinzani lakini kwa siku ile kwa kweli hatukutendewa haki na nilidhani ilikuwa ni wakati muafaka kwa Ndugu Tido Mhando kueleza ni kwa nini kimetokea na kama kweli ilikuwa ni hitilafu basi angeweza kutumia siku nyingine kile kipindi kiwe *recorded* ili Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa aweze kusikilizwa na wananchi kama ambavyo wengine waliskilizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia kuhusu *TBC* ni suala zima la mpira. Ni kweli tunajua *TBC* ilipata *tender* ya kuonyesha mpira lakini kwa kweli kumekuwa na tatizo kubwa sana. Mimi nasema ni sawa wamepewa *tender* ile lakini unaweza ukakaa unasubiri mechii *live* labda Manchester na Arsenal, *whatever* unaambiwa mpira utakujia punde. Mpira unaanza saa nne unaambiwa punde, unasubiri saa nne na nusu unaambiwa punde mpaka baadae mpira ule unakuwa *recorded*. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa nilikuwa naomba kama wamepata hiyo *tender* basi wawatendee wananchi haki wawaonyeshe kwa wakati ule kwa sababu kwa kweli inakuwa ni tatizo tunajua Watanzania wengi wanapenda sana mpira na kwa hiyo, kama wamepata hiyo *tender* kwa mamilioni ya pesa basi wawaonyeshe wananchi na wawatendee haki waonyeshe kwa wakati kama ambavyo tulivyokuwa tunaona katika TV nyingine. Kwa mfano, *Star Tv* ikionyesha inaonyesha kweli muda ule, *ITV* au *Channel Ten* wanaonyesha tena wenyewe wanasema wanaonyesha bila mizengwe kwa maana kwamba huku *TBC* kuna zengwe. Kwa hiyo, naomba *TBC* ijirekebishe na ionyeshe mechii kwa wakati ule muafaka lakini sio tuone ambazo ni *recorded* zinakuwa hazina maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala zima la mpira wa miguu hapa nchini. Ni kweli mpira wa miguu unapendwa Kimataifa na Kitaifa. Lakini jambo lolote unapolipa kipaumbele lazima linakuwa na ufanisi mkubwa. Ni kweli kwamba soka hapa nchini limekuwa na ufanisi mkubwa. Ni kweli kwamba soka hapa nchini limepewa kipaumbele na ndiyo maana tumeona wale vijana wa chini miaka 17 wamekuja hapa wameshinda na hata timu ya Taifa ilipofikia. Lakini michezo mingine yote haijapewa kipaumbele cha aina yoyote.

Kwa hiyo, naomba Serikali au Wizara ione ni jinsi gani inaweza kuvipa vipaumbele michezo mingine na inasikitisha sana kuona kwamba pamoja na kwamba huyu Japhet Kaseba ameshinda *kick boxing* Kimataifa nasikia amepata shilingi 500,000 tu na sijui kama zimetoka Serikalini au ni wafadhili mbalimbali.

Kwa hiyo, nadhani kwa kweli Serikali inawajibu na kuwasaidia kupandisha vipaji vyta wachezaji wetu ili waweze kufanya kwa ufanisi zaidi. Tukielemea kwenye upande mmoja upande mwingine nao unaenda chini. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kusaidia sana vipaji vyta wachezaji wetu na sio tuelekee tu kwenye soka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuendana na michezo kuna suala zima la Kocha aliyepeleka timu ya *boxing* kule Mauritius sijui kama Wizara ina taarifa kwamba wale wote waliokwenda kule walikamatwa kwa sababu inasemekana walikuwa na dawa za kulevya lakini wengine hawakuwa nazo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kujua hatma yao nini? Mpaka sasa hivi wako gerezani kule Mauritius walienda mwezi wa sita.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua, kwa sababu hii timu ilikwenda kuwakilisha Taifa na wamefungwa kule Mauritius, kama Wizara ina Taarifa na ni kwa jinsi gani wanawenza kusaidia au kutupa taarifa kama kweli walikuwa na dawa za kulevya au la; na kama kuna baadhi walikuwa nazo ni vipi walienda nazo na wale ambao hawakuwa nazo ni kwa nini bado wapo gerezani?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala zima la Vazi la Taifa. Suala la Vazi la Taifa ni jambo la msingi sana na ndio linaloonyesha utaifa wa nchi fulani. Wenzetu wa South Africa wana vazi lao, Wanyarwanda wana vazi lao, Waganda na hata wale wa West Africa. Suala la mchakato wa Vazi la Taifa, lilizungumzwa kwa muda mrefu na wakawa wamesha-*tender*, watu wengi wameonyesha na zile *fashion show*, lakini mpaka leo bado hatujawa na Vazi la Taifa. Ninaomba kuuliza; Serikali hivi wana mpango gani wa kuhakikisha kwamba, Tanzania kama nchi tunakuwa na utaifa wetu kwa kuwa na Vazi la Taifa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kama ilivyo kawaida, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Wataalam wote, kwa kutuletea hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nimshauri Mheshimiwa Waziri; nimejaribu kuangalia picha ambazo ameweka kwenye hotuba yake, kuna picha nne; mbili zipo kwenye majalada na nyingine zipo ndani. Kwa uzuri wa Uwanja wetu wa Mpira, nilitegemea moja ya picha angeiweka katika jalada lake kama inavyoonekana nyuma hapo. Ingekuwa nzuri zaidi, lakini pia nia pamoja na kuutangaza Uwanja wetu wa mpira. Naomba siku nyingine basi afanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza waandishi wa habari, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya; kwa kweli ni kazi ngumu, wanajituma na yataka moyo na wanafanya kazi katika mazingira magumu. Mimi naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri wanayofanya, pamoja na madongo wanayorushiwa, lakini naomba muwe imara, mchape kazi zenu kama ambavyo maadili yanawataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya uandishi wa habari siyo sawa sawa na mtu kwenda kuchunga ng'ombe kukaa pale, uandishi wa habari ni taaluma, utangazaji ni taaluma. Watu hawa wamesomea taaluma hii, mwaka mmoja, miaka miwili au mitatu. Kwa hiyo, ni taaluma inayotambulika. Naomba sana ndugu zangu waandishi wa habari, msimamie maadili ya kazi yenu. Pia niwaombe waandishi wa habari, kwa sababu hamna chombo chenu cha kuwatetea hasa mnapofukuzwa au mnaposimamishwa, nawaomba ikiwezekana mara sheria itakapokuja au kabla, mkae muunde chombo chenu cha kuwatetea, kwa sababu bila ya kuwa na chombo chenu, mnaweza mkawa mnapoteza yale maslahi yenu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niwaombe sana wamiliki wa vyombo vya habari, kuna utaratibu ambao si mzuri sana wa kuwatimua timua waandishi wa habari bila utaratibu. Naomba sana wamiliki wa vyombo vya habari, tuiheshimu taaluma hii na ndio maana mojawapo ya nguzo nne ni waandishi wa habari. Naomba sana ndugu zangu wamiliki wa vyombo hivi tuwaheshimu. Kama lipo tatizo, naomba tukae tuzungumze vizuri ili tusiharibu taaluma yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, lazima waandishi kwa sasa kwa kweli ni vizuri waende wakasome. Tukifanya hivyo, wakasomee uandishi wa habari ili maadili na taaluma ya uandishi iweze kuonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama wewe ni mtangazaji uliyefundishwa, unajua hata namna ya kukamata kipaza sauti (*microphone*). Kama wewe ni mwaandishi, ukiandika taarifa yako ni lazima uipeleke katika ngazi inayohusika, unaipeleka kwa Mhariri kwa maana ya *Sub-Editor*, ikitoka kwa *Sub-Editor*, inakwenda kwa Mhariri mwenyewe na baadaye inakwenda kutangazwa au kuwa gazetini. Kwa mtindo wa sasa, inawezekana si hivyo na ndio maana utakuta kichwa cha habari kingine na yaliyomo ndani ni mengine.

Nawaomba hii taaluma inaheshimika, viongozi, *editors* na wamiliki wa vyombo vya habari ni vizuri zaidi kichwa cha habari na yale yanayoandikwa ndani yafanane, hapo mtakuwa mnajijengea umaarufu. Kutokufanya hivyo, wakishaanza kusema hili gazeti

lipo hivyo hivyo, halina maana mtajiua ninyi wenyewe na mnapoteza ile sifa yenu nzuri mliyonayo waandishi wa habari. Nawashauri tufuate maadili ya uandishi wa habari kama mlivyofundishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie michezo. Mwaka jana Mheshimiwa Rais, alilitembelea Jimbo la Sumve, akaja pale kwenye Chuo cha Michezo na Utamaduni Malya. Tulimwomba atusaidie kukiimarisha, bahati nzuri alikubali, Chuo hicho sasa kinaimarika vizuri zaidi. Yapo majengo kama yalivyoandikwa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, naomba kupitia kikao chako Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali kwa kukubali Malya kuwe na Chuo cha Michezo.

Mheshimiwa Spika, Chuo kile ni sawa na kiwanda cha kutengeneza wataalamu wa kwenda kufundisha kwenye shule zetu za msingi hasa michezo mbalimbali. Kile ni kiwanda, Mheshimiwa Bendera anakifahamu, kwa sababu ye ye alishawahidi kuwa Mkufunzi pale.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali, kwa sababu jengo hilo lipo tayari, nakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa heshima kubwa umwombe Mheshimiwa Rais aje alifungue jengo lile, nitashukuru sana. Naomba wenzangu wa Wizara wanisaidie, tunaye Kaimu Mkuu wa Chuo pale, leo mwaka wa pili anakaimu. Kama ana matatizo tuelezeni, lakini kama hana matatizo, kukaimu kwa miaka miwili, nina uhakika hata yale maamuzi ya kutaka kuendeleza Chuo kwa sababu ya kusema mimi nakaimu. Naomba ikiwezekana, basi utaratibu ufanyike wa kumkamilisha ili awe Mkuu wa Chuo Kamili kama hana upungufu. Mimi najua hana upungufu, kwa sababu amesimamia vizuri Chuo kile mpaka kufikia hapo kilipo. Naomba na kushauri, ikiwezekana basi taratibu zifanywe ili huyu athibitishwe kuwa Mkuu wa Chuo kamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, naiomba sana Serikali kuanzia Wizarani, BMT, TFF, kama kweli tunataka kuendeleza michezo katika nchi hii, tujue Kigoma kuna wachezaji gani, Mara kuna wachezaji gani, Urambo kuna wachezaji gani, Mvomero kuna wachezaji gani na kadhalika. Lazima Wizara hii iache u-simba na u-yanga! Tukiendeleza u-simba na u-yanga kwenye BMT, Wizarani, TFF na ndiyo maana yanatokea kama yanavyotokea. Kwa hiyo, ile dhana ya kuendeleza michezo nchini haitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, katika moja ya hotuba yake alisema kwamba, mimi sikuja kusikiliza au kutatua migogoro ya Simba na Yanga, lakini bado. Jana tumeona kwa macho yetu na tumesikia kwa masikio yetu, michezo ule ulikuwa wa kimataifa; cha kushangaza hata kama una akili yako nzuri au akili mbaya, kiwango cha mshindi wa kwanza anayechukua Kombe la Kagame anapewa dola 30,000, ambayo ni sawa sawa na shilingi milioni 36. Hawa Waswahili wanasema wanataka shilingi milioni 50, inakuja kweli; milioni 36 mshindi wa kwanza kwa maana ya dola 30,000, wao wanataka milioni 50, lakini kwa faida ya nani na mnamkomoa nani?

Mheshimiwa Spika, tumepeata aibu jana, CECAFA imepata aibu, TFF imepata aibu na nchi imepata aibu. Kama tutakitumia vizuri Chuo cha Michezo cha Malya, narudia kama tutakitumia vizuri Chuo cha Michezo cha Malya; kwa sababu pale wataalam ndipo wanapozalishwa, viongozi wa michezo ndipo wanapotoka na niombe

Mheshimiwa Waziri, siku zijazo ikiwezekana mwakani, *tuki-up-grade* kile Chuo kiweze kutoa Diploma na kiweze kutoa digri za michezo. Nitashukuru sana Mheshimiwa Waziri kama utalizingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishukuru sana Serikali, lakini nikuombe tena kama nilivyokuomba kwamba, Mheshimiwa Rais aje afungue Chuo chetu cha Michezo cha Malya, kwa sababu yeye aliyejeka na akasema Chuo hiki lazima tukiimarishe.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofit*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri ambayo kama itafanyiwa kazi sawa sawa, pamoja na ufinyu wa pesa, inaweza ikaleta matumaini na matunda mazuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ninavyoolewa ni kwamba, Wizara hii ni Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na jukumu lake kubwa ni kusimamia sekta zote hizi. Labda mimi nizungumzie utamaduni; Wizara hii, utamaduni inakuwa kama imeupa kisogo zaidi na kutoa kipaumbele katika habari na michezo kama vile mchezo wa mpira, kama tunavyoona kiwanja cha mpira kilivyowekwa pale mbele lakini hatujaona ngoma za utamaduni wetu wa asili zikiwa pale. Kwa hiyo, hiyo bado inaonyesha ni jinsi gani utamaduni wa Tanzania, Wizara hii haijupa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kazi yake kubwa ambayo mimi nadhani ingekuwa ni kusimamia na kuhakikisha kwamba, fani mbalimbali za sanaa kama za maonyesho, fani za ufundi, pamoja na muziki zinasonga mbele. Nazungumza hivyo kwa sababu mimi pia ni mdau katika fani hii ya sanaa za maonyesho na sanaa za muziki. Kwa hiyo, ndio maana nataka nizungumzie suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia kuhusu nyumba ya sanaa. Baba wa Taifa alitoa kiwanja cha Ikulu pale Dar es Salaam ili kiweze kujengwa Nyumba ya Sanaa na matarajio yake na matazamio yake yeye aliwatazama wasanii wa Tanzania, akaona kwamba itakuwa ni kituo ambacho kitawezaka kuwasaidia wasanii wote ili wawewe kujikwamua kutoka katika hali duni ya maisha na sanaa yao iweze kuwaweka katika hali bora ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kituo hiki kilijengwa kwa ushirikiano wa Tanzania, pamoja na Serikali ya Norway. Kilikuwa kikitoa mafunzo mbalimbali ya kazi za mikono, ufundi na muziki. Kama mtakumbuka, kuna bendi zetu zilikuwa zikienda mpaka nje ya nchi kutangaza vizuri utamaduni wetu na kazi za mikono pia. Hata akina mama ambao walikuwa wanajishughulisha na shughuli za mikono, walikuwa wakipata masoko hasa ya nje walikuwa wakipatia pale. Walemvu walikuwa wanajifunza pale, lakini ilipofika miaka ya 1990 mpaka 2004, kukatokea mgogoro ambao ulipelekeea Bodi ya Nyumba ya Sanaa ile kuvunjwa. Sasa sielewi Mheshimiwa Waziri, ataniambia nini kuhusu Jengo hili

la Nyumba ya Sanaa, maana mpaka sasa hivi limekaa tu limekuwa kama ni kituo cha biashara cha watu wachache na kama ni kituo cha utalii, lakini si kwa ajili ya msanii kama Baba wa Taifa alivyokuwa amekusudia. Sasa nataka kujua, je, anayemiliki pale sasa hivi ni nani, maana naona imeandikwa *Nyumba ya Sanaa Limited*. Tunataka kujua ni sababu gani zilizopelekea kuvunjwa kwa Bodi ile? Wizara inasemaje na nani anafaidika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niachie hapo kwa sababu naamini Waziri atatoa maelezo kwa kirefu. Mimi nizungumzie pia kuhusu mikataba na haki za wasanii. Ninazungumza hivyo kwa sababu mimi mwenyewe imenigusa; mimi ni msanii ni mwimbaji, nimepata tabu sana, nimesumbuliwa sana pamoja na hawa *promoters* sijui wasambazaji, wametusumbua sana kwa kweli inasikitisha. Nilipanga kulia ndani ya Ukumbi huu, lakini naomba niyazuie machozi yangu yasiweze kutoka kwa sababu...

SPIKA: Huruhusiwi! (*Kicheko*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Sitalia kwa sababu siruhusiwi, lakini nitalia ndani ya moyo wangu na machozi yangu naamini yatafika mbele ya Kiti chako Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mikataba ambayo inafanywa na *promoters*, pamoja na wasanii imekuwa ni mikataba mimi naweza kusema ni ya dhuluma kubwa sana; ni ya unyanyasaji na ni ya unyonyaji. Mkataba huu unakuwa umetayarishwa na yule anayesema kwamba ye ye ni *promoter*, analeta mkataba anakwambia saini hapa, imeandikwa kiingereza, wasanii wanaoibuka wengi wao kama tunavyojua, hatujui kiingereza. Unaletewa mkataba huelewi umeandikwa nini ndani yake, njaa yangu mimi imenipeleka pale, nataka kuona na mimi angalau napata chochote, basi nasema *anyway* Mungu nakushukuru hata kwa hiki nilichokipata unasaini. Matokeo yake, unajikuta umejiingiza kwenye mkataba wa kumtajirisha mtu mwengine, wewe ukabakia kuwa ni mtu wa jua kali, kufuta jasho bila lesu, kutembea kwa miguu, wao wanatembea kwenye magari ya viyoyozi, maofisi yao yana viyoyozi na ni kazi ya msanii inayowatajirisha watu wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze, hawa wasanii wako wapi; wako Wizara yako wewe au wako Wizara gani? Je, tuwaundie wasanii hao Wizara nyingine ili iweze kuwasimamia na kuwatetea? Umeweka chombo cha *COSOTA*; *COSOTA* hii iko wapi; iko kwenye viwanda; michezo; saa ngapi; wapi; na mnashirikiana vipi? *COSOTA* hii tunayoizungumza sasa hivi ni *COSOTA* ambayo wakati mwengine inawarudi wasanii, haiwatetei wasanii. Sasa sielewi, kwa nini ndani ya Wizara yako kisiundwe chombo ambacho kitawea kuwasaidia wasanii?

Hivi ni kwa nini kama kweli tuna nia ya kukuza utamaduni wetu na kusaidia wasanii wetu, kwa sababu ni ajira, watu wangapi wameajiriwa wanauzwa kanda huko, wameajiriwa wanauzwa kaseti zetu na kila kitu; wanasomesha watoto wao, sisi tubaki tunapekua ni ajira bado; kwa nini kisiwepo chombo maalumu kwa ajili ya kutetea

wasanii hawa; wanabaki tu juu kali kuomba omba, mimi msanii wa wapi? Msanii wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba chombo kama *COSOTA*, utueleze kinafanya nini kwenye viwanda na biashara kule, kwa nini kisije kwako? Bado labda niseme chombo hicho sasa kitakachokuwa kama *COSOTA* kiwe na Mwanasheria ambaye kwanza hao wanaojiita *promoters* wawe na leseni, walipe kodi kama kawaida, wawe na cheti kinachotambulika kwenye hicho chombo kitakachoundwa kwenye Wizara yako na kuwe na Mwanasheria. Huyu *promoter* asiruhusiwe kuingia mkataba wowote na msanii yejote, awe amemtoa kule kijijini kama akina Saida Kaloli, awe amemtoa Bungeni kama Martha Mlata, asiingie naye mkataba mpaka amekuja kwa Mwanasheria aliyeo kwenye Wizara yako, kwenye hicho chombo ili msanii huyu aweze kutetewa. Tumechoka kubabaishwa na kudhulumiwa, huu ni unyanyasaji mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia kuhusu studio zetu ambazo zinarekodi nyimbo zetu. Hizi studio zimekuwa nyingi; ni sawa hakuna matatizo kabisa lakini ziwe zinatambulika kwenye hicho chombo ninachokizungumza utakachokiunda. Msanii yejote atakayeingia kwenda kurekodi kama amepelekwa na huyo *promoter* ni lazima aonyeshe kwamba amepitia kwenye chombo hicho na lazima hiyo studio iwe imepitia kwenye chombo hicho ili kuweza kulinda haki za wasanii.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuzungumzia suala la wasambazaji; wanatuibia kwa sababu hatujawakamata, hatuwezi kusema wezi, lakini ni wezi wakubwa. Unaingia naye mkataba sasa hivi, wanatuibia. Mimi nasema hivyo kwa sababu, nilipokuwa naimba, nilirekodi nyimbo zangu, kabla sijaingia mkataba, nilikuwa nauza mwenyewe, natembeza kanda hizo kama mmachinga. Faida niliyoipata, *RAV4* iko nje pale nimeinunua kwa hela hiyo, lakini baada ya kuingia mkataba, mpaka sasa hivi ni laki tano tu ambazo nimeambulia. Kanda zangu ukizunguka ukifika Mbeya, ukienda wapi, unazikuta na *signature* unaikuta ni ya kwangu, ukiuliza unaambiwa hazitoki, ukienda majumbani unakuta zipo. Hivi jamani huo si wizi?

Kwa hiyo, ninaiomba Wizara yako ichunguze hao wasambazaji wanatuibia kanda zetu, wanafoji *signature* zetu, wanaendelea kugonga mihuri yetu, wanaauza kanda. Kwa hiyo, mimi ninaomba hilo pia, Mheshimiwa Waziri naomba sana wasanii wasaidiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini bado pia mimi nataka nizungumzie, kuna hili suala la wasanii kunyanyasika. Mimi ndio mjuzi, kwa mfano, nikimzungumzia Mr. Bean sote tunamjua; ni milionea na ameitangaza nchi yake na amesaidia watu wengi ambao wameajiriwa kutoka kwenye ule usanii wake, uchekeshaji na nini, lakini bado leo wasanii hao hao wanakaa. Mimi nimeingia mkataba na wewe, mkataba umevunjika *fine*, sasa kwa nini unanifuata unanizuia nisiende kufanya sanaa yangu, ujuzi na kipaji ambacho Mungu amenipa, nisikitumie sehemu nyininge? Kwa nini tunafanya hivyo? Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tusinyanyasane na fani zetu. Hizi fani ni zetu Mungu ametupa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hawa *Ze Comedy* hawa, wamekuja juzi hapa; nilimuuliza Masanja wewe mbona unajaza chakula sana, akasema siku nyingi nitakiona wapi, ngoja leo niponee hapa Bungeni kwa sababu sina hela siku hizi nanyanyasiaka, nimezuiliwa kufanya kazi yangu, nitapata wapi pesa! Ni kweli wanapata tabu, tunaomba tuwasaidie hawa wasanii. Watu tunataka kukuza vipaji vyetu, wanatokea watu kwa sababu zao binafsi; sababu binafsi ziwekwe pembeni, wasanii wetu tuwaache wafanye kazi, kama ni jina la *Ze Comedy* waliache basi, watafute lingine lita-win tu. Waachwe hawa watu wafanye kazi zao jamani. Watoto wanapata shida! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka nizungumzie pia suala la mrabaha. Suala hili kuna vyombo vingine kweli vinalipa, maana msanii wewe ukitumia wimbo wangu kwenye televisheni yako au kwenye redio ni lazima unilipe. *COSOTA* kweli imekusanya, kuna wasanii wengine wamepata pesa, lakini kuna vyombo vingine havilipi hela. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na *TRA*, hawa wenye vyombo vyao vya habari vya utangazaji ambao wanatumia sanaa zetu, kama hawalipi mrabaha, basi wakifika kule *TRA*, waonyeshe yeti, risiti au kitu chochote kitakachoonyesha kwamba wamelipa mrabaha. Kama hawajalipa, wasikubaliwe ku-renew hizo leseni zao ili mtusaidie.

Nchi zingine zilizoendelea, ukitumia wimbo wa msanii unamlipa; *fine* wewe endelea kuna kutumika kwenye matangazo, kuna kutumika kwenye burudani, lakini kila sehemu unapotumika kuna gharama zake, basi nilipwe. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, asiipe kisogo hii sanaa yetu ya muziki, sanaa za maonyesho, sanaa za kuchonga na kazi nyingine za mikono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, basi kwa kumalizia nizungumze tu kwamba, kuna wakati nilipochangia Hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumzia suala la Waandishi wa Habari kwamba, pamoja tunasema wasome, wasome wapi; Chuo kipo hapa wengine hawana hata uwezo?

Mtu anaweza akasoma digrii yake ya kwanza, digrii ya pili hawezi kupata kwa sababu hakuna chuo kinachotoa *masters* hapa. Nikasema Serikali iangalie uwezekano wa kuwapeleka nje ya nchi, hata mkiwapeleka kumi kwa mwaka kuna ubaya gani mbona wengine wanaenda? Wapelekeni waandishi wa habari waende wakasome nje na wakitoka huko watakuja kutusaidia zaidi. Sikujibiwa wakati ule. Mheshimiwa Waziri, sasa mimi nakuomba tuwasaidieni waandishi wa habari, tuache tu kusema elimu ya wapi! Wekeni mafungu ya kuwasomesha hawa waandishi wa habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, basi kwa kumalizia kama bado nitakuwa na dakika chache, kwa kuititia Bunge lako Tukufu, ninaomba nitoe shukrani zangu za pekee na za dhati kabisa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida. Nilienda kwa ajili ya kukimbiza Mwenge Kimkoa, wananchi wale walijitokeza kwa wingi na shughuli za maendeleo zilioneekana. Kwa hiyo, mimi napenda niwapongeze kuanzia Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Makatibu Tarafa, Wenyevitii wa Halmashauri, Madiwani na Wananchi wote kwa kushirikiana. Akina mama wote waliweza kujitokeza, hasa vile vikundi vya sanaa. Vikundi vilikuwa ni vya hamasa, kwa kweli vilikuwa vinafanikisha sana.

Nawapongeza hata vijana wale ambao ni wakimbiza mwenge, waliweza kutoa ujumbe kwa ujasiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ujumbe wa mwenge ulikuwa unahuwa kupiga vita rushwa, UKIMWI na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mlata, ahsante sana. Ingawa hukulia humu ndani ya Ukumbi, lakini uliyoyasema yanagusa sana mioyo ya watu. Natumaini Mheshimiwa Waziri, hana moyo mgumu sana. Kwa hiyo, atasaidia.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa uongozi wa Wizara kuanzia Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Bendera, Katibu Mkuu, wakurugenzi wa Wizara, wakurugenzi wa vyombo vyta habari vyta Serikali na zile za binafsi kwa kazi nzuri ya kuhabarisha wananchi katika sekta mbalimbali nchini.

Naipongeza Wizara kwa kupata hati safi, hii ikidhihirisha umakini na uadilifu wa watendaji wote wa Wizara. Naishukuru Wizara kwa kugharamia kikamilifu timu ya watoto wenye ulemavu ya *Special Olymopics* kwani maandalizi yake yanakuwa ni ya gharama sana kwa vile watu wenye ulemavu wana mahitaji mengi ya ziada ikilinganishwa na watu wasio na ulemavu.

Hata hivyo nashauri kuwa yafaa kuunda mfuko maalum wa michezo kwa watu wenye ulemavu ili michango iwe ni ya kudumu na kusaidia Serikali kugharamia shughuli hizi. Mfuko huo ni wajibu uchangiwe na wadau mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TBC* kwa kujitahidi kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuongeza usikuvi na kuweza *TV* yake kuonekana maeneo mengi kama si nchi nzima. Hata hivyo kwa upande wa *TBC One(TV)* ni kwa nini taasisi imeondoa kile kiashiria cha mwanzo wa kipindi cha taarifa za habari ambacho “Babu alikuwa akipiga pembe ya mnyama juu ya Mlima Kilimanjaro? Kwa upande wangu kiashiria kile mimi nilikiona kuwa kinaonyesha utamaduni wa Mtanzania. Kwa msingi huo nitaomba ufanuzi wa suala hili wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kuwa kila wanapoandaa matamasha ya utamaduni na kazi za mikono asili ishirikiane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, vyama vyta watu wenye ulemavu kupitia SHIVYAWATA ili kuweza kubaini vikundi vyta sanaa vyta watu wenye ulemavu ili navyo vile vitakavyokidhi vigezo vyta kushiriki vifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuhakikisha kuwa Kiwanja cha Michezo kipyä imezingatia mahitaji muhimu ya watu wenyé ulemavu, ambao nao sasa wanawenza kuingia uwanjani, kwenye maliwato bila matatizo sana. Naomba hili liendelee kuzingatiwa katika majengo mengine yote ya starehe ambayo Wizara itayasimamia na kuhimiza hata watu binafsi nao wafanye hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, wimbo wa Taifa unapaswa kubadilishwa wimbo uliopo umeigwa kutoka Afrika Kusini na ni lazima tuwe na wimbo wa asili.

Napendekeza wimbo wa “Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote....” Kuwa wimbo wetu mpya wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya kuwa na vazi la Taifa kimaslahi na kitija. Sera iwekwe kuwalinda Marais wastaa fu dhidi ya watu wenyé chuki binafsi ambao wanatumia nyadhifa ama nafasi zao kuwapaka matope. Hii inatia aibu Taifa. Naomba Wizara itoe tamko juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuipongeza kwa dhati hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa hotuba nzuri sana iliyozingatia vizuri maeneo yote muhimu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, leo nina jambo moja tu muhimu nalo ni kuishukuru *Star Television* kwa kuwezesha wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kupata matangazo bila kutegemea ungo. Wananchi wa Songea Mjini wanaushukuru sana uongozi wa *Star TV* na hasa Mheshimiwa Anthony Diallo kwa jinsi alivyolishugulikia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iendelee kuwasaidia wananchi wa Songea kwa kuwaombea kwa televisheni zingine nazo ziige kilichofanywa na *Star TV*, *TV* hizo ni pamoa na *Channel Ten*, *TBC*, *ITV* na *East Africa TV* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niipongeze timu ya soka ya mkoa wa Ruvuma chini ya miaka 17 kwa kutwaa ubigwa wa soka nchini. Pia naipongeza timu ya Majimaji kwa hatua iliyofikia katika ligi ya soka daraja la kwanza *Inshaallah* Mungu ataisaidia siku moja kurudi ligi kuu.

Mwisho nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao mzuri. Naunga mkono hoja.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ambayo kama itasimamiwa vizuri itaweza kuondoa tatizo kubwa tulilonalo la ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutoa mchango wangu napenda kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa kuweza kuandaa hotuba hii nzuri na kumwezesha waziri kuwasilisha ndani ya Bunge leo.

Mheshimiwa Spika, naanza na mchezo wa mpira wa miguu, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza timu yetu ya Taifa kwa kazi nzuri na kiwango walichokionyesha hivi karibuni katika mechis zake, pamoja na kutokufanikiwa kushiriki katika mashindano hayo wasikate tamaa kwa sababu uwezo wanao wakiweza kufikia malengo yao, pia nimpongeza kocha wao na msaidizi wake kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuwafundisha vijana wetu. Niwaombe Watanzania wawe wavumilivu mabadiliko hayaji haraka kama ambavyo wanategemea tuwape moyo vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, *netball* hivi karibuni kulikuwa na mashindano ya Kombe la Taifa kwa mchezo huu lakini mashindano haya yalikosa ushiriki mzuri na msisimko kwa sababu timu nyingi zilishindwa kushiriki kutokana na uwezo mdogo wa fedha. Je, Wizara ina mpango gani wa kusaidia mchezo huu ili uweze kuendelea vizuri kama mpira wa miguu au tunataka mchezo huu ufe? Tunaomba Wizara ishirikiane na viongozi wa mchezo huu ili tuweze kunusuru mchezo huu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri amempongeza mchezaji wa mchezo wa *kick boxing* nami napenda kuungana na Wizara kumpongeza kijana huyu Joseph Kaseba kwa kuweza kuiletea Taifa heshima kubwa kwa kuweza kuleta mikanda miwili ya ubingwa wa dunia amepigana kufa na kupona ili kulinda heshima ya Taifa lake.

Mheshimiwa Spika, kijana huyu amekuwa akishiriki mashindano haya kwa hali ngumu sana na kama asingekuwa anajituma ye ye binafsi asingeweza kushiriki katika mashindano hayo. Mwezi ujao kijana huyu anatakiwa kwenda Japan katika pambano lingine. Je, Wizara hii itamsaidiaje kijana huyu ambaye katika mapambano mengine hakupata msaada wowote? Tunaomba Wizara ilitazame suala hili kwa jicho la huruma ili tuweze kumtia moyo kijana huyu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niwatakie kila la kheri Wizara hii katika kutekeleza yale yote waliyoyaandika katika hotuba yao.

MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Spika, afadhali kuwa na kichache na kugawana kidogo kidogo, kwanza nampongeza Waziri wa Habari, Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera kwa kazi nzuri na kwenda na wakati kwa Serikali ya Awamu ya Nne ya ari, nguvu na kasi mpya. Naamini wataboresha Wizara.

Mheshimiwa Spika, elimu ya habari naiomba Serikali kujali sana wataalam na watendaji wengi wa Wizara kupata elimu vizuri na kwa sekta zote pia kwa kupitia *TV* na redio pamoja na magazeti na kusimamia ukiukwaji wa taratibu zote kwa faida ya nchi yetu, na wananchi kuzingatia maadili ya nchi na utamaduni mzuri tulionao.

Mheshimiwa Spika, michezo idumishwe na Serikali itoe nguzo. *ZFA* ya Zanzibar na *TFF* kwa Tanzania Bara tunatumaini ndio wawakilishi ndani ya michezo nchini kwa kutuwakilisha pia kwa ushirikiano mzuri lakini bado haitoshi na kuwa manung'uniko upande wa Zanzibar. Je, tunadhani utafutwe utaratibu mzuri unaofaa zaidi ya uliopo ni upi? Na kwa nini kusiwe na Chama cha Muungano kimichezo badala ya hii Zanzibar pekee na Tanzania Bara pekee. Naomba kuwa na mhimili wa tatu wa Muungano ili kuondoa yote mabaya.

Mheshimiwa Spika, maadili ya mavazi kwa nchi yetu, baadhi ya maadili si mazuri kwa vijana, watoto pamoja na watu wazima kwa wake na waume, ikichangiwa na wageni wa nje na utalii. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuliona na sheria inayotaka kuandaliwa inacheleweshwa na maadili yanazidi kuharibika ifanywe haraka.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bajeti hii hasa kwa Waziri, Mheshimiwa George Mkuchika na Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, natumai Bajeti ikipitishwa wataisimamia vizuri na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Magogoni naunga mkono hoja.

MHE. GAUDENTIA M. KABAKA: Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mheshimiwa George Mkuchika, kwa hotuba fupi na nzuri. Pongezi kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera kwa umahiri katika kazi zake. Nawapongeza pia Katibu Mkuu, wakurugenzi na watendaji wote Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara. Nachangia katika maeneo mawili kama ifuatavyo:

Kwanza kujenga uhusiano na Chuo cha Ualimu Butimba. Chuo hiki ni chuo pekee cha ualimu nchini kinachotoa *Diploma* ya elimu kwa michezo, sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi na muziki. Hawa ni walimu lakini wamegundua kuwa hawa vijana wetu wana vipaji vikubwa sana katika fani zao na wahitimu wengine huamua hata kwenda kufanya kazi kwenye taasisi za utangazaji wa kujijiri wenyewe.

Nashauri kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo licha ya kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii katika kuhimiza ufundishaji wa michezo shulenii lakini pia Wizara iwe na mahusiano ya karibu na chuo hiki cha Ualimu Butimba ili kutambua wataalam kuwaendeleza zaidi hadi nje ya nchi ili wawe wa manufaa zaidi katika Taifa letu. Lakini pia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo wawe ni kiungo kati ya Chuo cha Ualimu Butimba na Vyuo vya Sanaa Bagamoyo na Chuo cha Michezo

Malya kwa kuendesha matamasha ya pamoja na kubadilishana uzoefu wa fani zao. Kwa namna hii tutakuwa tuna-*promote* sanaa, michezo, utamaduni wa muziki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, matangazo ya *TV (TBC and TCRA)*. Naomba kusema kuwa sasa hivi kuangalia *TV* wakati ukiwa na watu unaowaonea aibu kama wakwe ni jambo la *risk* kubwa sana kwenu watamazaji. Hii ni kutokana na matangazo yanayowekwa *in between* taarifa hasa yanayodaiwa kuelimisha kuhusu suala la UKIMWI. Hivi tangazo la vijana wale wanaozungumza kuweka kufuli katika nguo za ndani kama ujumbe wa kuzuia UKIMWI kweli ni haki kwa kazi hiyo au linatia aibu hasa kama upo na wakwe zako sebuleni?

Ushauri wangu ni kuwa matangazo ya aina hiyo yaondolewe, kama vile ilivyofanyika kwa hili la Usione soo lilivyoondolewa. Wahusika watumie matangazo yaliyonadhifu ili tuangalie *TV* zetu bila wasi wasi wa kuona tusiyoyataka.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema naunga mkono hoja hii asilimia mia moja na hongereni sana kwa kazi nzuri.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda kumpungeza Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika, Waziri wa Habari na Utangazaji na kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu wake pamoja na timu yote ya Wizara hii.

Inanifurahisha na kujivumia jinsi ambavyo *TBC*, ambavyo zamani ilikuwa *TVT* pamoja na vyombo ndugu ilivyopiga hatua katika mawasiliano na habari za uhakika.

Mheshimiwa Spika, heshima yangu kuu iviendee vyombo vile ambavyo vinafanya kazi kwa kufuata *integrity* ya uandishi yenyе dhana ya kuwafundisha na kuwatetea wananchi kwa kuwapa habari zilizo sahihi. Enyi waandishi wa habari, nawaonya kazi yenu ni ya utume na inabidi mpendane na kuoneana huruma. Pia muwapende wananchi kwa kufikisha taarifa zao zilizo sahihi kwa Serikali, Bunge na Mahakama. Sasa ili kufanikisha uwezo wa chombo hiki, mwandishi wa habari anapaswa kuwa ni *well knowledgeable person*.

Mheshimiwa Spika, tafadhalii anzisheni mfuko wa kusaidia elimu kwa waandishi wa habari ili waweze kuchimbua mambo inavyostahili. Chonde chonde, tunajivunia na tunawapenda. Tunayo nia ya kuanzisha kipindi cha Wabunge wanawake ili kuhamasisha wenzetu katika mambo yanayotugusa na kazi zetu na pia kutoa elimu katika mambo tunayoyaelewa, kama *role model* na pia kupokea mawazo kutoka kwa wanawake wenzetu.

Tunaomba mpokee wazo letu ili mtusaidie sisi kama *Tanzania Women Parliamentarians Groups (TWAPC)* kama ambavyo tuliazimia kwenye *business plan* yetu.

Mwisho, natoa shukrani kwa yote tunayoshirikiana hasa katika mazingira magumu yanayojitokeza katika shughuli zetu. Tafahadli wasaidieni wale watoto wa *Ze Comedy* tusikwaze vipaji, ongeeni nje ya mahakama, mmalize yaishe.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na uzima wa afya.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa ushirikiano mwema walioyanayo kwa kutayarisha hotuba hii nzuri yenyewe kueleweka na kujitosheliza.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba yake leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nianzie kuchangia sekta ya michezo na hasa mpira wa miguu. Katika mambo muhimu yaliyositisizwa katika Ilani ya CCM ni kujihusisha kwa nguvu katika michezo, katika kutekeleza hayo uwanja mpya wa michezo umejengwa pia makocha wa Taifa wameletwa nchini kwa kuimarisha mchezo huo.

Mheshimiwa Spika, juu ya juhudhi hiyo kubwa iliyochukuliwa na Serikali lakini bado hali ya nidhamu katika vilabu vyatuhusu na wachezaji ni ndogo sana na hali hii inaletewa na chama cha mpira nchini *TFF*.

TFF inashindwa kuchukua hatua kwa vilabu vinavyokaidi maagizo halali wanayoyatoa na badala yake huongeza muda mara mara hali ambayo inazifanya baadhi ya timu kuzidisha jeuri na kuona ni timu kubwa na hakuna litakalo tokea, pia hali hiyo iko kwa wachezaji wanaochezea vilabu vikubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuiunga mkono Serikali katika kukuza mchezo huu umefika wakati sasa *TFF* kutekeleza kwa vitendo adhabu zinazostahili kutolewa kwa timu na wachezaji bila kujali ni timu gani na mchezaji anatoka timu ipi ili kuondosha dhana kuwa baadhi ya timu kubwa na wachezaji wanaochezea timu kubwa hawawezi kuguswa hata kama kuna hatia na makosa yaliyotendwa.

Mheshimiwa Spika, *TFF* inapaswa kuhakikisha maagizo yake yote yanaanza kutekelezwa sasa kwa sababu kufanya hivyo soka la Tanzania litaendelezw na kufikia kiwango cha Kimataifa ambalo ndio lengo kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nidhamu ndiyo itakayotufikisha tunakotaka kwenda kama ilivyoonyeshwa na vijana wetu chini ya miaka 17 hivi karibuni wametuletea sifa kubwa bila nidhamu sifa hiyo isingepatikana.

Mheshimiwa Spika, mwisho niipongeze sana *TFF* kwa kazi ya kusimamia soka nchini na wasivunjike moyo kwani baada ya marekebisho niliyoyatoa tutafikia lengo na nia tulivoikusudia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani nyingi kwa uongozi wa Wizara hii, nampongeza Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu jinsi walivyojipanga katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba nzuri yenyе kuonyesha matumaini katika sekta hii. Wizara ya Habari ina mzigo mkubwa, ni Wizara kubwa kinyume na mitazamo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatakiwa kuweka maanani mambo ya msingi iwe ishara kwa mwananchi. Kuna matatizo mengi hasa utamaduni umebakи kwenye vitabu si vitendo. Utamaduni umekufa. Wizara inashindwa kudhibiti mavazi yasiendana na Mtanzania, kwenye maonyesho, mavazi wanamuziki na machangudoa. Wizara inashindwa kuliona hili? Na kama zinashonwa hapa nchini kwa nini msidhibiti? Kama mavazi yanatoka nje kwa nini muingizaji asionwe?

Mheshimiwa Spika, habari imekuwa chombo bei mbaya. Wilayani na vijijini hakuna mwakilishi wa habari, utawaona mkoani na wanasafiri au wanaenda kuchukua habari za Mkuu wa Mkoa, Mawaziri na Rais, sasa je, nyie peke yenu mnatakiwa kutoa habari?

Mheshimiwa Spika, tunaomba waandishi wa habari pamoja na kuwapa posho za kujikimu, wanasafiri na kutoa habari za wakubwa kwa sababu mnawapa posho.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vy ya habari sasa imekuwa kero magazeti yamezidi kuandika vilivyo nje ya maadili, wapi kwenye gazeti lililoandika kuwa gazeti hili ni kwa wakubwa tu? Magazeti yanafundisha yanaeneza mambo mabaya kwa watoto wetu na jamii hivi hamna dawa ya kudhibiti uchafu huu na hatari, magazeti yatatugawa tunaomba tamko imeyafungia lini na neno uhuru wa vyombo vy ya habari halina maana.

Mheshimiwa Spika, pelekeeni maofisa utamaduni na michezo kwenye kata. Kuhusu michezo mnajitahidi ila sasa kuondoa migogoro kwenye vyama vy ya michezo na vilabu kwa mfano pia mwongozo wa kuendeleza vipaji muongeze bidii, kwani sasa wakati umefika kuongeze vipaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naipongeza Serikali na Wizara kwa kuamua kuutumia uwanja wa mpira mpya kwa baadhi ya mechi, cha msingi tutafute wakala wa kusimamia na kuendesha uwanja kwa sababu sasa hivi ni kero tupu hasa kutofautisha ukaaji majukwani, kutumia polisi kumepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, sekta ya habari ni sekta nyeti na muhimu sio tu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, sekta hii pia ni muhimu kwa ustawi na amani wa nchi yoyote duniani. Kwa misingi hii kiwango cha Bajeti kilichotengwa kwa Wizara hii ni kidogo sana ukilinganisha na umuhimu wake kwa

ustawi wa nchi yetu. Pamoja na kuwa na sera nzuri za habari watumishi wanataaluma wazalendo kwa kiwango kikubwa ufinyu wa Bajeti ya Wizara hii kila mwaka umesababisha Wizara hususani sekta ya habari kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kucheleta kufikishwa Bungeni Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari ni jambo la kusikitisha. Ningepeda kujua tatizo hapa ni kwa nini mchakato wa sheria hii umechukua muda mrefu? Kwa vile Muswada huu ni muhimu kwa ustawi wa nchi yetu ni muhimu kujua ni lini Muswada huu utaletwa hapa Bungeni, neno mapema mwakani inawezekana ikawa Februari, Aprili au Juni, 2009. Naomba kufafanuliwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuna mkanganyiko wa mgawanyo wa kazi baina ya Idara ya Habari (Maelezo) na Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu. Pamoja na kwamba katika hotuba yake Waziri ukurasa wa 10 Waziri amesema kuwa moja ya majukumu ya Wizara yake ni kuwa Msemaji wa Serikali. Maelezo haya siamini kama ni ya kweli kwani taarifa nyingi za Serikali sasa zinatolewa na Ikulu. Hapa napenda kupata ufanuzi wa suala hili.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari, kwa kuwa sekta ya habari ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu na kwa kuwa wananchi hupata habari/taarifa mbalimbali kuititia vyombo vya habari, hata hivyo waandishi wa habari wa umma/Serikali wanafanyakazi katika mazingira magumu ya kukosa vifaa/vitendea kazi muhimu vya kuboresha utendaji kazi zao na pia maslahi yao ni duni kuliko vyombo vya habari binafsi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vitendea kazi vya kutosha na kuboresha maslahi yao kwa waandishi wa habari wa Serikali ili kuboresha utendaji wao wa kazi? Je, Serikali ina mpango kupeleka afisa habari kila Wilaya ili waweze kuandika habari za maendeleo badala ya waandishi hao kuwa makao makuu ya mikoa tu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*), kwa kuwa *TBC radio* na *TBC One* inafanya kazi nzuri sana ya kuwatangazia wananchi habari za maendeleo na kwa kuwa waandishi wa habari na watangazaji wa *TBC Radio* na *TBC One* wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kukosa vitendea kazi muhimu, uchakavu wa mitambo na maslahi duni na pia kukosa makazi maalum (nyumba za kuishi). Usikivu wa radio kwa nchi nzima wa *TBC One* ionekane nchi nzima.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha *TBC Radio* Kanda zote ikiwemo Kanda ya Kati, Dodoma kwa kuwapatia vitendea kazi vya kutosha, magari ya kukusanya taarifa za habari kutoka vijijiini na pia kuwajengea nyumba za kuishi na pia kuongeza Bajeti. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi yao ili wasihamie vyombo binafsi vya habari.

Kwa kuwa kila fani ina maadili yake na kwa kuwa uandishi wa habari ni taaluma ya kusomea. Je, waandishi wa habari wanaokiuka maadili ya uandishi wa habari na kupotosha ukweli wa habari na pia kuhatarisha usalama wa Taifa letu. Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti hali hiyo?

Kuhusu sekta ya michezo, kwa kuwa sekta ya michezo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu, kwa kuwa kunakuwa na migogoro mingi na hasa mpira wa miguu viongozi kugombea madaraka, matumizi mabaya ya fedha hakuna udhibiti mzuri, je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti hali hiyo? Je, Serikali haioni kwamba migogoro hiyo ndiyo chanzo cha kuzorotesha hali ya michezo katika nchi yetu? Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua michezo yote, *netball, volleyball, handball*, riadha na kadhalika na kuwapatia ruzuku ili kuendeleza michezo hiyo, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vyuo vingi vya michezo hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. HEMED MOHAMED HEMED: Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nuru ya kuona jua kwa tarehe ya leo nasema *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake kwa hotuba yao yenye mwanga wa maendeleo katika Wizara husika japokuwa baadhi ya timu zetu kukimbia mechi muhimu kama za *Kagame Cup*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nielekee katika kutoa mchango wangu katika Wizara husika. Kwa kuanza nianzie hapa wasanii wetu. Kwa kuzingatia kazi zinazofanywa na wasanii wetu nchini ilipaswa Serikali iwaenzi wasanii hawa. Inaonekana wasanii wetu wanafanya kazi zao kwa kipaji na sio kielimu. Hii iko wazi kwani wasanii wetu mara nyingi kazi zao zinabaki kuwa mikononi mwa *promoters* wao na ndio anayefaidika zaidi kuliko huyu msanii aliyekosa mapumziko kwa kutunga au kuchonga inatokana na ukosefu wa elimu. Je, ni njia gani Serikali itatumia ili kuwapatia elimu wasanii wetu pia kuboresha kazi zao?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imebahatika na kuwa na taasisi zake pia na makampuni kama vile, Shirika la Utangazaji (*TBC*), magazeti ya Serikali, taasisi ya sanaa na utamaduni na kadhalika. Bila ya shaka Serikali kama itaweze kuziwezesha taasisi na kampuni hizi zilizo chini ya Wizara itawezekana kuipatia fedha Wizara na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi duniani, vyombo vyao vya habari kama *TV*, zikitoa taarifa zao kuonekana mkalimani wa watu wasiosema (mabubu) kuwapa taarifa kwa ishara zinapotolewa. Kutokana na idadi ya watu wasiosema hapa nchini, ni vyema Wizara ilione hili, ili kuwapa haki wenzetu hao ili nao wawewe kuzijua taarifa za nchi yao. Hili linahitaji ushirikiano na Wizara ya Elimu kwani ni uhakika walimu wa taaluma hii iko chini ya Wizara ya Elimu. Kwa Wizara husika ya Habari, Utamaduni na

Michezo, ni vyema kutoa taarifa na wenzetu hawa waweze kujua kile, kwani nao wana haki kama Watanzania wenzao.

Mheshimiwa Spika, mwisho niwatakie kheri Waziri na Naibu wake. Ahsante.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Spika, tatizo sugu ni kutimiza mafunzo ya maendeleo ya michezo kwa kuanzia ngazi ya umri mdogo miaka 6, 8, 10, 12, 14, 16, 18, 20, 22, 24 kuwa na mashindano ya ngazi za umri huo Kitaifa kuanzia ngazi ya kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Spika, upo usemi usemao samaki mkunje akangali mdogo. Michezo ifundishwe mashulenii. Viwanja vya vijijini viwe na kocha wa michezo, shule mpya ziwe na viwanja, vilabu vya michezo vichague viongozi wenye upeo wa kuendeleza michezo, vyuo vya michezo na makocha na walimu wa michezo kuendeleza, matengenezo ya *TBC* Redio kuboreshwa na majengo ya *TBC One* yaboreshwe.

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, michezo nchini inapendwa sana tatizo kwanza, ni vifaa vya michezo mfano mipira ya miguu na mikono.

Pili, sehemu za michezo kwa viwango vinavyotakiwa kama vile viwanja vya mipira. Wananchi wa Ukerewe wamejenga kwa kujitolea uwanja ujulikanao kwa jina la ‘Getrude Mongela’. Uwanja huu umezungukwa na maduka. Mara kwa mara nimeomba kusaidiwa ukamilishwaji wa uwanja huu, je, ni lini kilio cha wananchi wa Ukerewe kitajibiwa?

Tatu, mazingira ya Wilaya ya Ukerewe yanafaa kwa michezo ya maji kama vile *sailing, boat, roaring* na *swimming*. Ombi, Wizara itusaidie kupata vifaa na kuleta Walimu kwa michezo hii kama inavyofanya kwa michezo mingine.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika kutokana na majukumu na tataribu uliojiwekea, bajeti ya Wizara hii haikidhi haja kwa maana bajeti ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana kwa timu ya vijana ya umri wa miaka 17 walioshinda Kombe la *Copa Coca cola* kwa kuviangusha vigogo wa nchi ambazo kwa *ranking*, Tanzania ndiyo ilikuwa ni ya mwisho lakini kutokana na umahiri wa vijana wetu wakaibuka washindi. Kwa maana hiyo, Tanzania imepata heshima kubwa katika ulingo wa soko la duniani. Vijana hao wanastahili waendelezwe kimichezo na kielimu kama walivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, tendo la timu ya Yanga walilolifanya jana, limeitia doa Tanzania. Tendo hili ni vema likalaaniwa kwa nguvu zote. Hata hivyo *TFF* kwa upande mwengine nayo inastahili kupewa lawama kwa kulea hasa timu hizi mbili za Simba na Yanga kwa kuwasikiliza kila jambo wanadolitaka na kama ni makubaliano basi *TFF* hawana budi kuyatekeleza makubaliano hayo ili kuepusha migogoro ambayo yanaitia aibua Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bado kuna haja ya kutoa elimu kwa wasanii wetu kuhusiana na haki zao kwani wasanii wengi bado hawanufadiki na sanaa zoa kwani wajanja wachache hasa wafanyabiashara ndio wanaonufaika sana. *COSATA* wako wapi? Nawaomba wajipange upya ili kuhakikisha kuwa majukumu waliyopewa wahakikishe wanayasimamia karibu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina utamaduni wa asili tangu enzi. Utamaduni ambao unazingatia maadili ya Kitanzania, lakini maadili hayo yameanza kupungua kwa kasi. Hii inatokana na kuingia kwa utamaduni wa kigeni nchini. Mfano muziki wa dansi, miaka ya nyuma muziki wa dansi hasa ule wa rumba haukuwa na wanenguaji lakini kutokana na mabadiliko ya ukuaji wa teknolojia duniani, wanamuziki wetu wamekuwa wakiiga bila kujali maadili yetu kwa kuchenza rumba/kuwa na wanenguaji wa kike ambao huva mavazi yasiyostahili na mila na desturi za Kitanzania. Pamoja na kuwa muziki wa siku hizi ni wa kibiashara, hata hivyo ni vyema wanenguaji wetu hasa wa kike wakawekewa masharti ya mavazi ambayo yataendana na mila na desturi za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, naipongeza kwa dhati Serikali yetu kwa ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo ulioko jijini Dar es Salaam. Halikadhalika napongeza pia Serikali kwa kuviboresha viwanja vya Mnazi Mmoja (*Karume Memorium Stadium*) na ule uwanja wa Taifa wa zamani kwa kuvipanda nyasi za bandia. Kwa hakika, Tanzania imepata hadhi kubwa katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee na mikakati yake ya kuviboresha viwanja nchini kwa kila Mkoa ili viwe na hadhi angalau ya kulingana na viwanja vya Mnazi Mmoja na ule wa Taifa (uwanja wa zamani).

Mheshimiwa Spika, mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika 2010 Afrika ya Kusini yamekaribia na kwa kuwa timu nyingi zitashiriki katika mashindano haya na kwa kuwa Tanzania haiko mbali sana na nchi hii yatakapofanyika mashindano hayo, je, Serikali imepata maombi mangapi kutoka kwa nchi zitakazoshiriki kwenye mashindano hayo ambazo zitahitaji kufanya mazoezi yao kwenye viwanja vyetu vitatu (Mnazi Mmoja, Uwanja mpya na ule wa zamani wa Taifa)? Kama hakuna nchi iliyojitezea, naishauri Serikali kuititia Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ichukue hatua za dhati kuvitangaza viwanja hivyo sambamba na utalii ili kupata timu ambazo zitakuwa zikifanya mazoezi yake kwa kukodi ili kuinua pato la nchi na kuitangaza Tanzania duniani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mungu ibariki Tanzania.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Habari na Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Joel Nkya Bendera (Mb), Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo mawili tu ninayoona yanastahili kuzingatiwa na Wizara.

Kwanza naipongeza Serikali kwa hatua kadhaa ilizozichukua tangu uhuru kwa lengo la kupanua uhuru na amani hususan uhuru wa vyombo vyahabari nchini. Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, yaliyofanyika mwaka 1984, yaliingiza sura mpya ya Katiba iliyotambua, kwa mara ya kwanza tangu uhuru, haki mbalimbali za msingi za binadamu na wajibu wa kila mtu. Ibara mpya ya 18 ya Katiba ilitamka bayana kuwa:-

“Bila kuathiri sheria za nchi kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta, kupokea na kutoa habari ...na ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati”.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2005, Katiba ya Jamhuri ya Muungano ilifanyiwa marekebisho ya 14 ambayo yalifuta maneno “bila ya kuathiri sheria za nchi” hivyo kupanua zaidi uhuru wa vyombo vyahabari nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, tatizo kubwa tulilonalo Tanzania kwa sasa si la uhuru wa vyombo vyahabari bali ni tatizo la maadili ya uandishi wa habari. Matatizo yanayokwamisha upatikanaji wa uhuru kamili wa vyombo vyahabari ni machache, yanajulikana na yanatatulika lakini suala la maadili bado tete.

Mheshimiwa Spika, njia ya uhakika ya kuimarisha maadili katika fani ya Uandishi, ni elimu. Serikali haina budi kusaidia kwa hali na mali katika suala hili kwa kufadhili kozi za muda mfupi na mrefu za Uandishi wa Habari ndani na nje ya nchi na *study tours*. Bila hatua hizo za makusudi, tatizo la uandishi wa habari usiozingatia maadili, litaendelea kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, aidha, tatizo la uandishi wa habari usiofuata maadili, linachochewa na tabia mpya inayoenea kwa kasi chini ya Viongozi Waandamizi nchini, Wabunge na Mawaziri, kumiliki vyombo vyahabari hususan magazeti na redio. Vyombo hivi vyahabari chini ya umiliki wa wanasiwa, huishia kuwa na majarida ya propaganda yasiyofuata maadili ya uandishi wa habari kwa kuwashambulia na kuwazushia kashfa wanasiwa wengine na kuwamiminia sifa za reja reja wamiliki wao. Michezo huu uliachiwa kwa muda mrefu, tutaua heshima na mchangano mzuri wa vyombo vyahabari kwa maendeleo ya nchi. Badala ya vyombo vyahabari kuwa kioo na kurunzi ya jamii, inageuka kuwa silaha za kumalizana za wanasiwa.

Mheshimiwa Spika, ninatoa mfano mmoja mdogo. Mwezi Machi mwaka huu, *DAWASCO* ilinitangaza kuwa mmoja wa watu wanaojiunganishia maji visivyo halali jijini Dar es Salaam. Taarifa hiyo ilikuwa na dalili mbaya za kisiasa, kunionyesha kuwa pamoja na kuwa Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge iliyopelekea Waziri Mkuu na Mawaziri wawili kujuzulu, nilikuwa mwizi, mchafu! Vyombo vyaa habari, kinyume cha maadili ya uandishi, vikaandika taarifa hiyo kwa hamasa kubwa hata bila kuniuliza.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ilikuwa ya uongo, iliyochochewa na baadhi ya wanasiisa waliochukiwa na kazi ya Kamati Teule ya Bunge niliyoiongoza. Nilipoonyesha dhamira ya kuipeleka *DAWASCO* Mahakamani, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwangiliaji, ilitoa tamko Bungeni tarehe 25 Julai, 2008 kuniomba radhi kwa taarifa ya uongo ya *DAWASCO*.

Pamoja na Mbunge wa Kilindi Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kuiasa *DAWASCO* kuacha kutumiwa na wanasiisa, hakuna chombo chochote cha habari kilichoandika taarifa hii. Huu ni ushahidi tosha wa ukosefu wa maadili upande wa vyombo vyetu vyaa habari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kushiriki kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa michezo ni afya na kwa kuwa kuna vijana wengi Mkoani, Wilayani hadi vijiji wenyi vipaji katika michezo mbalimbali, je, Serikali ina mikakati gani ya kuendeleza vipaji hivyo hadi kupata timu za Taifa zenyet uwezo katika michezo mbalimbali na hivyo kuliwakilisha Taifa letu katika michezo ya Kimataifa pamoja na kulitangaza taifa letu duniani?

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vyaa habari unapaswa kuzingatiwa katika kuimarishe demokrasia hapa nchini hasi ikizingatiwa kwamba vyombo hivyo vinaelimisha jamii kuhusu mambo mbalimbali likiwemo suala la ufisadi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Mhariri wa gazeti la Mwanahalisi, bwana Kubenea alivamiwa ofisini kwake na nyumbani na kupekuliwa na Jeshi la Polisi, je, hii ni sahihi? Kama si sahihi, Serikali inasema nini juu ya kadhia hii?

Mheshimiwa Spika, mpira wa miguu umekuwa mchezo wa dunia. Hapa nchini vijana, wakubwa na wadogo wanashiriki katika mchezo huu kwa hamasa kubwa. Mfano mzuri umeoneshwa na vijana wetu katika mashindano ya *COPA COCA COLA* ambao kwa ujasiri mkubwa wameipatia nchi yetu sifa na heshima kubwa kwa kushinda kombe hilo la *Copa Coca Cola*. Je, Serikali inasema nini kuhusu mfano huu mzuri ulioonyeshwa na vijana wetu?

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu ni mzuri na hivyo unapaswa kukuzwa, kuendelezwa na kufunzwa kwa vijana wetu. Vijana wanapaswa kuelimishwa juu ya

umuhimu wa utamaduni wetu badala ya kuiga tamaduni za kigeni ambazo ni kinyume na mila na desturi za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi liangaliwe kwa vijana wetu hasa kwa wasanii ambao huonyesha sanaa zao katika radio na televisheni (runinga) kama vile michezo ya kuigiza na filamu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kazi za mikono zihamasishwe kwani zinasaidia kupatikana kwa ajira na kuitangaza nchi yetu katika maonyesho kama vile sabasaba na nane nane.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Spika, habari ni chanzo kingine ambacho mwanadamu hupenda kukipata na zimfikie zikiwa hai na kwa wepesi.

Mheshimiwa Spika, katika idara hii ya watoa habari, inaonekana kuna upungufu mkubwa kwa Waandishi wa Habari hivyo kushindikana kwa baadhi ya sehemu kupata habari kwa mantiki hiyo ni lazima kuongeza idadi ya watoa habari katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyta habari kwa baadhi ya sehemu nchini haviwafikii wananchi hivyo kushindwa kupata habari kama redio na TV.

Mheshimiwa Spika, *TBS* kiwe ni chombo huru na kitoe habari zake bila hata kuingiliwa na Serikali, kwani ndio chombo pekee kinawafikia wananchi wengi na kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, vile vile chombo hicho kiimarishe kwa vitendea kazi na vyombo vilivyo bora zaidi ili hata pale ambapo hakiwafikii wananchi kiwafikie kwa urahisi pamoja na *TV* yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuvipongeza vyombo vyta habari vyta watu binafsi kwani navyo vinachangia kwa asilimia kubwa kupatikana kwa habari. Hivyo navyo viwe huru na visiingiliwe na dola kama ilivyotokea hivi karibuni kwa kupekuliwa ofisi ya chombo kimoja cha habari hapa nchini, hii ni aibu na fedheha kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya lakini vijana wadogo wakiendelezwa vema katika mchezo wa mpira wa miguu watatuletea sifa nchi yetu, hivyo napenda kuishauri Serikali ijikite zaidi kwa vijana wadogo, kama wale wa *Copa Coca Cola*, waliotuletea sifa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, timu zetu bado hazijafanya vizuri katika mashindano makubwa, zimekuwa zinashiriki tu, hivyo mkazo na msisitizo zaidi unahitajika ili tuweze kufanya vizuri hapo baadaye na hata mashindano yanayofanyika hapa kwetu tukiwa

tumeshirikisha timu nyingi lakini bado hatujafanya vizuri. Hapa tunajiona kama tumeonewa na hatukutendewa haki na timu zetu kama wapenzi na wazalendo wa nchi.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, kama ilivyodhihirika, fedha inayo toka *FIFA* kwa nchi wanachama haiwezi kugaiwa kwa chama cha *ZFA* kutoka *TFF*.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri *ZFA* imefikia wakati iwe mwanachama wa *FIFA* ili nayo iweze kufaidika na gawio hilo. Je, Wizara hii itasaidia vipi ili *ZFA* nayo iwe mwanachama wa *FIFA* ukitilia maanani uanachama huo hautaiathiri *TFF*?

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri, ukuruasa wa 30, imesema jukumu moja la Bodi ya Uchaguzi wa Filamu na Michezo ya jukwaani, ni kuhakikisha kwamba filamu na michezo ya kuigiza, zinawiana na mila na desturi na maadili mema ya jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, filamu na michezo zinazoneshwa kwenye runinga kupitia *TBC* zinaonesha wachezaji ambapo uvaaji wao ni nusu uchi. Je, hiyo ndio mila, desturi na maadili mema ya jamii ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke mkazo mkubwa sana kwenye michezo kama riadha ili Tanzania iweze kufanya vizuri na kutupatia sifa nchi za nje, tusitegemee peke yake kupata sifa katika mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, kuna manung'uniko kuwa Wizara haifanya vizuri katika kushughulikia maombi ya wataalam wa Kiswahili wanaotakiwa kwenda kufundisha Kiswahili nchi za nje. Hali hiyo inaweza kusababisha Watanzania kukosa ajira wakati Kiswahili hapa Tanzania ndio chimbuko lake.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kunijalia kuchangia hotuba hii.

Nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara na wote walioshiriki kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari ni chombo muhimu sana kwa nchi yoyote duniani katika kupata habari za Kitaifa na Kimataifa mijini na vijijini katika kuelimisha umma.

Mheshimiwa Spika, utamaduni na michezo, ndio dira ya kumweka binadamu katika nchi ya furaha na afya njema, katika maisha ya kila siku na vilevile ni ajira kwa vijana wetu. Ndio maana Rais wetu akatilia mkazo juu ya michezo na utamaduni ili apate taifa lenye watu walio na furaha na afya ndani ya nchi yake na kutoa kipaumbele juu ya habari.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopangiwa Wizara hii bado ni ndogo mno hata kama imeongezwa, ni tofauti na mwaka uliopita lakini bado inahitaji iongezewe fedha kwa ajili ya kununulia jengo la ofisi ya BAKITA ambapo mazungumzo ya kupata jengo hilo kwa Shilingi bilioni moja yanaendelea na likinunuliwa na Serikali jengo hilo pia litawenza kutumiwa na Wizara. Mwaka 2009/2010, tunaomba bajeti hii iongezwe kutokana na shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, habari ni muhimu katika uhai wa binadamu popote alipo habari inahitajika imfikie lakini bado habari haijafikia kiwango kinachotakiwa kwa sababu vyombo vya habari vijiji havijafikia kama vinavyotarajiwa. Redio nyingi hazisikiki, magazeti hayafiki vijiji, *television* haionekani mpaka uwe na ungo, kwa hiyo, utaona kuwa elimu kwa njia ya vyombo vya habari haiwafikii wananchi walio wengi, kama vile elimu kuhusu Ukimwi au elimu ya watoto wetu kwa njia ya redio au TV hawapati, hii ni hasara kwa maisha ya leo. Kwa hiyo, Serikali ifanye mikakati ya makusudi ili kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali kwa kupitia Wizara hii itoe elimu kwa wasanii wetu wa kike kuhusu mavazi wanayovaa wakati wakitoa burudani. Ni mavazi ya uchi kabisa kuliko wasanii wa kiume ambao wanajihifadhi. Huu sio utamaduni wa Kitanzania, unatoa picha mbaya kwa kizazi chetu pale wanapoona kwa kupitia kwenye *TV* zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii lazima iwe na wafanyakazi walio na uwezo na elimu ya kutosha ili kuzuia kuwa na Waandishi wa Habari Makanjanja, wanaoandika habari za hovsky au kutangaza habari pasi uchunguzi au ufanisi na kile wanachokitangaza na kuleta migongano na wananchi au taasisi. Vile vile tunaomba waboreshe vitendea kazi vyao ili kuondokana na kukatika matangazo mara kwa mara au *TV* kuwa na matatizo, mara nyingine wanasema lakini picha haionekani na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, nawaombea kila la kheri Waziri na Naibu wake, kwa kazi zao nzuri na Mungu awape afya njema waweze kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANIA SAID CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi kuhusu hoja ya bajeti mwaka 2008/2009 ya Wizara ya Habari na Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wake, kwa kazi nzuri ya kuweka mikakati endelevu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za wasanii, ni wakati muafaka sasa Sheria ya Kulinda Haki za Wasanii itekelezwe na kuandaliwa, ili wapate manufaa kwa kazi zao za

usanii na kuinua maisha yao badala ya utaratibu wa sasa ambapo wanaonufaika ni wachache, wajanja kwa kuwatumia tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ngoma za utamaduni za makabila yote hapa nchini. Ni vema Serikali sasa ikaimarisha utamaduni wa Mtanzania kwa kila Mkoa kwa kuanzisha Siku ya Utamaduni na kushirikisha Wilaya kuimarisha ngoma zote za jadi na kizazi cha sasa ili kupunguza kuamini kuwa utamaduni wa nchi za nje ndio mzuri, utaratibu huu ukizingatiwa utazidi kuinua utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhaba wa viwanja vya michezo, hivi sasa kuna tatizo hilo hasa katika jiji la Dar es Salaam, watoto wanahangaika sana kucheza mipira na michezo mingine katikati ya barabara na ni hatari kwa watoto hao. Ni vema watoto wapatiwe sehemu ya michezo ya bembeya na bustani nzuri za kupumzikia.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa lugha ya Kiswahili inatumika sana duniani na tumeambiwa hapa Bungeni kuwa kuna baadhi ya nchi zinataka Walimu wa Kiswahili kutoka hapa nchini kwetu. Hii ni ajira nzuri kwa wananchi wa Tanzania. Suala hili lazima Serikali itilie mkazo na kuhakikisha Walimu wengi wanapatikana wenye taaluma ya kutosha ili kuchukua nafasi hizi hasa tukizingatia Kiswahili mizizi yake iko Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SIGIFRID S. NG'ITU: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pili, Ruangwa ni Wilaya ngumu kimiundombinu ya michezo. Kwanza, hakuna viwanja vya michezo *football, netball, basket ball* na kadhalika na pili, Ruangwa hakuna misaada ya aina yoyote ile kwa tatizo hilo hapo juu pamoja na vifaa kama vile mpira.

Mheshimiwa Spika, je, kuhusu suala hili tutasaidiwa vipi na Mheshimiwa Waziri? Kumbuka sana jinsi hali yetu ilivyo kiuchumi na kama tutasaidiwa, itatusaidia pia kutatua matatizo mengine kama vile Ukimwi kwa vile vijana wakiwa *busy* viwanjani, Ukimwi utakimbia lakini pia watajenga afya zao.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri na kuiwasilisha vizuri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kutosikika kwa matangazo ya *TBC – Taifa Wilayani Mbozi*. Pamoja na kituo cha *TBC – Taifa* kilichopo Iwambi – Mbeya kufungwa vifaa vipyta, lakini bado kuna tatizo kubwa la kutosikika vizuri kwa matangazo ya radio katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mbozi. Naomba Wizara kuititia *TBC - Taifa* ifanye jitihada za kutosha ili tatizo hili lirekebishwe mapema, hasa ukizingatia kwamba *TBC – Taifa*, ndio tegemeo kubwa kwa wananchi wetu wengi wa Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Kiswahili. Pamoja na ukweli kwamba lugha ya Kiswahili ilishazinduliwa rasmi kuwa moja ya lugha zitakazotumika katika Umoja wa Nchi za Afrika (AU) lakini bado matumizi yake hayaridhishi. Hata katika vikao vya nchi za Afrika Mashariki na hususan Bunge la Afrika Mashariki bado lugha ya Kiswahili haitumiki ipasavyo. Wakati mwingine hata semina na makongamano yanayofanyika humu nchini huendeshwa kwa lugha ya Kiingereza. Mimi nataka kujua tatizo ni nini? Ukisoma Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005m, Ibara ya 118(d), ukurasa wa 146, inaeleza bayana juu ya kukiimaraisha Kiswahili. Hivi mipango hiyo mizuri imefikia wapi? Je, ni kweli Wizara imedhamiria kweli kuona Kiswahili kinapewa msukumo unaohitajika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Michezo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ukurasa wa 147, Ibara ya 118(i), imeagiza kwamba Vyuo vya Michezo vianzishwe ili kuendeleza michezo nchini. Napenda kujua, je, hadi sasa ni vyuo vingapi vimejengwa katika azma yetu ya kuendeleza michezo nchini?

Mheshimiwa Spika, michezo (mpira wa miguu kwa wanawake). Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Ibara ya 118(i), ukurasa wa 148, pamoja na mambo mengine, kifungu hicho kinaeleza kwamba utawekwa msisitizo kwenye michezo wa mpira wa miguu kwa wanawake. Sina hakika hili limetekelizwa kwa kiwango gain! Nasema hivyo kwa sababu nikizunguka huko Mikoani sioni kama kuna jitihada zozote za kuimarisha michezo huo kwa wanawake. Hakuna timu za mpira wa miguu kwa wanawake katika ngazi ya vijiji, Kata, Wilayani katika ngazi ya Mikoa timu hizo zipo katika Mikoa michache hususani Dar es Salaam. Nashauri, Wizara ihakikishe kwamba ahadi ya kuimarisha michezo kwa wanawake na hasa mpira wa miguu, inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuahirishwa kwa michezo kati ya Yanga na Simba, tarehe 27 Julai, 2008. Jana tarehe 27 Julai, 2008, ilikuwa ni siku ya kuhitimisha mashindano ya Kombe la Kagame kwa nchi za Afrika Masharika. Katika hitimisho hilo, timu zetu za Yanga na Simba zilikuwa zicheze katika kutafuta mshindi wa tatu. Hata hivyo, michezo huo haukufanyika, kwa sababu ambazo watazamaji wengi wameshindwa kuzielewa.

Baadhi ya watu wamekuwa wakiilaumu timu ya Yanga kujitoa katika michezo huo na kuona kama timu na viongozi imekosa uzalendo. Aidha, watu wengine wamelamu Chama cha Mpira, Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) na TFF kwa kutotimiza wajibu wao na kusababisha timu ya Yanga kujitoa dakika za mwisho. Naomba Waziri atueleze usahihi wa sababu za Yanga kujitoa na kuzuia hali hiyo isijitoneze siku za usoni, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza serikali kwa kujenga uwanja mzuri wa kisasa na wa kimataifa, ambao umeipa hadhi nchi yetu kimichezo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia timu ya vijana chini ya umri wa miaka kumi na saba na Taifa Stars ambao wametuletea ushindi unaotupa heshima kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa hizo, nimekuwa nikifuatilia timu kongwe za Simba na Yanga, zinavyojitahidi kujiimarisha. Naomba sasa niiombe serikali ione uwezekano wa kuhamasisha Watanzania wengine kuendelea kujiunga na michezo kwa rika mbalimbali na jinsia zote ili michezo izidi kupewa uzito zaidi. Hata hivyo, serikali ipeleke macho kwenye shule za watu binafsi, hawana kipindi cha michezo (walio wengi), kwa hiyo, naomba watoto wote wapewe nafasi ya kushiriki kwenye michezo wakiwemo walemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali pia ianze kufikiria namna ya kupata wafadhili wa timu nyingine mpya, licha ya Simba na Yanga ili kuondoa ukiritimba na majivuno ya timu hizi zinavyobaki pekee. Naamini kukiwa na timu nyingine, michezo itapata changamoto kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, serikali iendelee kutoa elimu ya habari, utoaji wa habari, uandishi wa usomaji mzuri wa habari ikiwa ni pamoja na kuzingatia kiswahili sanifu, kwani wasikilizaji pia wanahitaji kupata sentensi nzuri/safi na zilizosanifiwa vizuri. Wapo waandishi wengine au wasomaji wengine ambao hawajali kiswahili sanifu katika kuzungumza au kusoma habari.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii na uwasilishaji mzuri wa hoja hii. Nawapongeza pia kwa mara nyingine, kwa jitihada zinazofanywa na Wizara hii katika kuendeleza michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo au ufanuzi juu ya Sheria iliyounda Baraza la Michezo, ambayo mionganoni mwa majukumu yake ni kusimamia na kuendeleza aina zote za michezo ya ridhaa. Hivi Wizara haioni kipengele hicho hakitendi haki kwa michezo mingine ya kulipwa?

Tunafahamu fika, hivi sasa michezo ni ajira ambayo inampatia kipato mchezaji husika na ndio maana vilabu vingi nya michezo vinawalipa mishahara wachezaji wake na pia wachezaji wanunuliwa ili wacheze kwenye vilabu. Hii inaonyesha kuwa, ipo baadhi ya michezo si ya ridhaa tena. Hivi Wizara haioni kuwa kuna haja ya kuifanya marekebisho Sheria hiyo ili na vyama au vilabu nya kulipwa navyo viwemo kwenye Sheria?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa mujibu wa katiba yao, hawafuati Kanuni za BMT; kwa mfano, Kanuni zinaelekeza utaratibu wa kufuata wakati wa kukata rufaa, lakini TFF hawazifuati Kanuni hizo? Hii inaleta mkanganyiko mkubwa sana kisheria.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ninaleta kwako maelezo ambayo ninayachukua kutoka kwa wasanii kuhusu matatizo yao. Ninaomba kupata maelezo juu ya matatizo hayo katika majibu ya Waziri Kwa nini serikali haifanyi majadiliano na COSOTA na vijana hawa (wasanii), ili kujua matatizo yao na jinsi ya kuyatatu?

MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji, kwa kazi nzuri. Ninao mchango ufuatao:-

Sekta ya Habari na waandishi wa habari: Bado tunao waandishi ambao hawaafuati maadili ya kazi zao. Wapo wanaonunuliwa (baadhi), ili kuchafua wengine baada ya kupewa chochote kitu. Baadhi ya magazeti yana ubaguzi katika kuandika habari. Wako baadhi ya wahariri ambao si waadilifu. Wapo pia waandishi na wahariri wazuri na wawajibikaji tunawapongeza. Vilevile wapo ambao hawaandiki habari bila kupewa chochote.

Umuhimu wa kuweka uzalendo mbele katika kila tunachofanya nchini. Hivyo, inapendeza sana wanahabari kuandika mambo *positive* ya nchi pale yanapofanywa na kufichua maovu yanayofanywa nchini.

Sekta ya uandishi wa habari ni vyema ipewe msukumo kwa kuwasaidia waandishi kujiendezea na kuwa na mpango wa kuwakumbusha maadili ya kazi zao.

Usikivu wa radio nchini: Maeneo ya mipakani wengi wanasiakia redio za nchi jirani badala ya redio za nchi yao. Kuna usikivu duni wa redio katika maeneo ya Rombo, Kigoma, Rukwa, Sumbawanga na kadhalika.

Hongereni sana sana katika kufufua michezo. Tunaona mafanikio katika *football, basket ball* na kadhalika. Hongereni, endeleeni kuwasaidia timu zote ziendelee kufanikiwa. Baada ya ujenzi wa uwanja mzuri wa michezo, Wizara itoe hamasa kwa watu kuwekeza katika shule maalum ya kusomesha *footballers, netballers* na *athletes*.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetunyima raha sana wapenzi wa *Ze Comedy* kwa mizozo isiyo ya lazima, japo Wizara haihusiki moja kwa moja, basi wasanii hao wapeni mwongozo. Wanaelimisha sana jamii na *message* zinawafikia wananchi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ifanye mpango wa kuunda Mfuko wa Wasanii ili eneo hili nalo lipate uzito unaofaa. Vilevile iunde Baraza la Washauri la Watumiaji wa Habari ili watumiaji wapate pahali pa kupeleka maoni yao juu ya utendaji wa sekta mbalimbali za Wizara hii. Pia nashauri wasanii wafuate maadili ya nchi yetu.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Habari, Michezo na Utamaduni, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii.

Baada ya pongezi, naomba nitoe maoni yangu kama ifuatavyo:-

Serikali iongeze nguvu kuviimarisha vyombo vyake vya habari na vitendea kazi kama maslahi, usafiri, taaluma na kupeleka habari vijijini.

Mheshimiwa Spika, kila kata iwe na Afisa Michezo ambaye atashughulika na vijana ambao ndio wengi katika maeneo ya ngazi ya chini. Wasanii waundiwe chombo ambacho kitaweza kuwasimamia kikamilifu kwa kulinda maslahi yao na kiwe na uongozi wenye uzalendo wa hali ya juu na kuweza kuimarisha ajira kwa vijana kuititia sanaa. Vile vile nashauri kuwe na tamasha la utamaduni kila mwaka kwa kushirikisha makabila yote kwa kila mkoa. Hii itasaidia kuamsha hali ya kujitegemea.

Serikali itoe kipaumbele kwa michezo ya aina yote kama kuogelea, riadha, *netball* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Hoja yangu ni kuchangia suala la michezo upande wa jinsia kwa kucheza *football*. Tanzania tumekuwa na timu moja tu ya kitaifa ya wanawake ya *football* lakini huko mikoani, wilayani, tarafani, katani, hakuna michezo ya wanawake ya *football*, wala hakuna viongozi wa ngazi hizo wa TFF, yaani viongozi wa *football*. Ushauri ni kwamba, kwa kuwa sasa mchezo wa *football* ya wanawake umeshamiri, basi kuwe na uongozi katika ngazi za chini ili kupata mazoezi, waunde timu za wilaya na mikoa kwani watu wengi wanaupenda.

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote, kwa hotuba yao nzuri ya bajeti ya 2008/2009 ambayo imefafanua kila kitu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ningeomba kuishauri Wizara yafuatayo:-

Mikakati yote pamoja na mipango iliyowekwa mwaka 2008/2009 itekelezwe na Muswada wa Sheria wa Vyombo vya Habari uletwe haraka Bungeni ili kuondoa mgogoro wa vyombo vya habari, kwani wanazidi mno, maji yamezidi chumvi na uhuru waliopewa umepita mpaka. Habari nyingine wanazoiandika zinakereketa na huwa hazina maana yoyote, wanataka umaarufu na kuichonganisha serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, navipongeza vyombo vya habari ambavyo vinaelimisha na kutoa habari zenyenye ukweli na zaidi *TBC*, ambayo tunaomba wapatiwe wataalamu na nyenzo ili kukiboresha chombo hiki muhimu cha taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lugha yetu ya kiswahili iboreshwe kupitia BAKITA, kwani sasa imekuwa inazungumzwa ndivyo sivyo.

Wanamichezo mbalimbali walioipatia sifa na ushindi nchi yetu, watukuzwe na waorodheshwe waliokufa na waliostaafu, ikiwezekana kuwekwe siku maalumu ya kukumbukwa kupitia Idara ya Michezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, masuala ya utamaduni wetu, mila na desturi, yatiliwe mkazo na ikiwezekana liwepo somo la utamaduni wetu kupitia redio, televisheni na vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia kila la kheri Wizara.

MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia siku ya leo kufika hapa Bungeni hali nikiwa mzima.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu haya, sasa naomba nitoe mchango wangu juu ya hotuba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza, nielekee kwa wanahabari. Wanahabari ni kiungo kati ya serikali na raia katika nchi yao. Kwa kuwa serikali mara nyingi hutolewa taarifa zake na chombo hicho cha habari, raia huhitaji taarifa za nchi yao; serikali yetu ni muhimu sana kutoa msukumo ndani ya Wizara hii kwa kuiwezesha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watanzania ambao wamejiweka katika maeneo ya usanii, serikali haiwatendei haki hata mara moja na niseme haiwathamini. Wasanii wetu mara nyingi hufanya kazi zao kwa kipaji tu na sio elimu. Kwa nini serikali haiwawezeshi wasanii kielimu na kifedha? Ukiangalia toka nchi yetu ikumbwe na Ugonjwa wa UKIMWI, walioielimisha jamii ni wasanii. Kwa kuzingatia kazi zao, mara nyingi anayefaidika ni yule *promoter*; aliyekaa na kalamu, kisu na kadhalika hafaidiki. Kwa nini serikali haimtendei haki msanii?

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo bado serikali hajataka kuzingatia kuwepo kwa viwanja. Viwanja ndio chachu ya kuwapata wanamichezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nasema ahsante.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, Mheshimiwa George Mkuchika; Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera; Katibu Mkuu wa Wizara, Hajjat Kijakazi

Rajab Mtengwa na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi yao nzuri ya kuandaa Bajeti hii ya 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maandalizi mazuri na mipango mizuri ya Wizara hii kwa Mwaka 2008/2009, ningependa nichukue fursa hii kutoa mchango wangu katika kuboresha bajeti hii kama ifuatavyo:-

Sekta ya Habari ni muhimu sana hasa katika hali ya sasa ya utandawazi, vyombo vya habari ni mhimili wa nne mbali na Dola, Bunge na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia hilo, nasisitiza umakini katika sekta hii kama ifuatavyo: Waandishi wazingatie Weledi (maadili ya kazi) yao, ili kuhakikisha wanatenda haki. Ipo tabia ya matumizi mabaya ya sekta hii, mara nyingi tunaona jinsi kalamu za waandishi zinavyotumika vibaya kulenga zaidi *personalities* hasa kutokana na visasi au pengine kupewa rushwa katika kumaliza baadhi ya watu (*Character Assassination*).

Namwomba Waziri, aidhibiti hali hii na kuzingatia taaluma kwa waandishi ili tuondokane na makananja wanaoweza kuiharibu sekta hii. Kadhalika, lazima tuone uendeshaji wa vyombo hivi kwa kuzingatia wafanyakazi wake (taaluma yao); mishahara yake; na mahali vinapofanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, bado Sekta ya Utamaduni haina usimamizi wa kutosha katika Wizara, ili kusimamia masuala muhimu ya utamaduni wa nchi yetu. Tumeona hali ya utamaduni wa nchi yetu inavyozidi kupotea siku hadi siku bila usimamizi wowote. Namwomba Waziri ahakikishe Wizara inakuwa na Afisa Utamaduni kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara isizingatie sekta ya mpira wa miguu pekee na michezo mingine ipewe changamoto. Michezo kama riadha, ngumi, mpira wa meza, kikapu na michezo mingine mingi, nayo iendelezwe. Kadhalika, nitumie nafasi hii kusisitiza Wizara iratibu mchezo wa mpira wa miguu kuanzia ngazi za vijiji hadi taifa.

Mheshimiwa Spika, *COSOTA* iwe na hali ya kufanya kazi kwa haki, kwa kuwasimamia wasanii hasa hawa wadogo, juu ya haki zao badala ya kufanya upendeleo wa wazi kwa wamiliki.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi; kwa nini Afisa Utamaduni Wilaya ya Iramba amekaimu nafasi hiyo takriban miaka 15 sasa; kwa nini Wizara isimuidhinishe au kama inaona uwezo wake mdogo bora iletu Afisa Utamaduni mwingine?

Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze serikali inavyo viwanja vya mpira wa miguu vingapi vinavyotambulika na je; ni viwanja vingapi vinavyomilikiwa na taasisi mbalimbali hapa nchini?

Wizara ishirikiane na taasisi kama vile Chama cha Mapinduzi, katika kuhakikisha viwanja ambavyo bado havijakamilika, viendelezwe kama vile Uwanja wa Namfua,

Singida, Uwanja wa Lulumba, Iramba na kadhalika. Kukamilika kwa viwanja hivi kutafanya sekta ya michezo kung'ara zaidi.

Vilevile naomba Mheshimiwa Waziri, atupe ufanuzi wa ngazi mbalimbali katika Baraza la Michezo; wajumbe wake wanapatikana vipi kwenye ngazi ya wilaya na mkoa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Sir George, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii nyeti. Sisi tunaomfahamu kwa muda mrefu, hatushangai kwa uteuzi wake kwani binafsi nikilinganisha uwezo wake na uteuzi wa Uwaziri, naona umekuja kwa kuchelewa sana. Hongera.

Aidha, nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, kwa kazi nzuri anayofanya hasa upande wa michezo. Sifa zake katika eneo hili ni za kutukuka. Nawapongeza pia Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kweli kuwa ni vyema kuvisaidia vyombo vya habari vya serikali kwa maana ya redio, televisheni na magazeti. Hapa natoa tahadhari katika ulimwengu wa ushindani kama tulionao, isifike mahali wakabweteka na kutegemea mgongo wa serikali. Napongeza *reform* za *TBCI*, huu ni mwanzo mzuri, lakini ifike mahali wajitegemee na kuthubutu kuingia kwenye ushindani na vyombo binafsi na hasa kwenye maslahi ya watumishi.

Pili, masafa ya TBC (kwa maana ya Redio), yanapatikana kwa tabu sana katika maeneo mengi ya Wilaya ya Kilindi. Ninaomba kupitia Wizara, mamlaka husika ijaribu kuangalia tatizo na kuleta ufumbuzi, kwani kulingana na hotuba ukurasa wa 14, hili ni moja ya jukumu lao.

Nayapongeza yale yote yanayofanyika katika Idara ya Michezo, yanaonekana wazi. Ushindi wa vijana wetu na timu zetu katika michezo mbalimbali ni hali ya kupongezwa. Illa tu ni lini Wilaya ya Kilindi itapatiwa msaada angalau wa kuanzisha Baraza la Michezo?

Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, aliwahi kuniahidi kuleta wataalamu Kilindi mara baada ya kutoka Kondo; ni lini ahadi hiyo itatekelezwa? Ni vyema pia tukaanzisha *FAT* Wilaya, tuwe na uongozi kama wilaya nyingine. Msione kama mtakuwa mnapoteza muda, wachezji wapo tena wazuri, ambao wakiendelezwa wanawenza hata kutoa timu kubwa za ushindani kimataifa. Naomba majibu ili nia yangu ya kushika shilingi ife.

Mheshimiwa Spika, nasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo:-

Napenda kujua Waandishi wa Habari wanawake wanaoandika habari za kivita au chaguzi za nchi jirani (nje); wanalindwaje kuhusiana na matatizo yanayojitekeza vitani? Je, wangapi wamefariki kutokana na mazingira ya kivita na wangapi wamejeruhiwa; na je, wanawekewa bima gani ya ajali au maisha? Na ni nchi gani walizokwenda kuandikia habari? Kati ya hao wanawake wangapi wamewahi kwenda kuandika habari za kivita au uchaguzi katika nchi nyingine?

Mheshimiwa Spika, uandishi ni kazi ngumu sana, kwa kuwawezesha waandishi kuwa na maisha bora ni vyema serikali iwapatie maslahi mazuri (mishahara, posho na kadhalika). Serikali ikiwapatia maslahi mazuri, basi waandishi watafanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashauri serikali iwashirikishe watu wenyewe ulemavu wa aina zote kwenye michezo tofauti katika nchi yetu. Serikali ikifanya hivyo, itakuwa imewashirikisha vizuri na wao watahisi kuwa wanashirikishwa na serikali yao na hawabaguliwi.

Mheshimiwa Spika, matangazo katika TV au Redio, lakini hasa katika TV ni elimu kama yatatangazwa vizuri, lakini hugeuka kuwa balaa kama yatatangazwa vibaya. Kuna baadhi ya matangazo ya TV hayaelimishi jamii, bali yanapotosha jamii hasa ya vijana. Kwa hiyo, kutangazwa na kuonyeshwa katika TV yafanyiwe *Editing* vizuri (kuhaririwa kwanza).

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kumshukuru Mungu, kwa kutupa sisi sote afya njema. Niwapongeze Mawaziri wetu; Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo; na Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera; Katibu Mkuu, pamoja na Wataalamu wote kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo; kwanza kabisa tunapongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuipa kipaumbele michezo. Kwa muda mfupi mwaka 2006 – 2009, tumeweza kushika nafasi ya 115 kati ya nafasi 165 katika timu za dunia. Kipekee, niwapongeze *Taifa Stars* kwa juhudi zao. Niwapongeze pia timu ya watoto chini ya umri wa miaka 17, kwa ushindi mkubwa waliotuletea. Ni jambo la kujivunia sana, watoto hawa hawajawahi hata kushindana na nchi jirani, lakini walipothubutu kwenda kucheza na timu ambazo zinaogopewa duniani, walirudi na ushindi wa kishindo. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana BMT kwa kuanzisha mchakato wa kufufua michezo kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa. Hii itasaidia sana kuendelea kufufua vipaji vyta watoto wetu na baadaye Tanzania tutaogopwa kwa kuwa na timu bora duniani. Tunahitaji kupata walimu wa michezo katika kila wilaya. Kwa mfano, Wilaya ya Simanjiro, haina mwalimu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kumpongeza Vicky Mtetema kwa ujasiri mkubwa aliuonyesha. Kweli aliuza roho yake hata kwenda kuonana na wale waganga na kupata simu zao. Huu ni ujasiri wa ajabu. Serikali ni vyema ione jinsi gani ya kuweza kumpatia ulinzi kwa kuwa sasa hivi anatishiwa amani. Je, serikali imechukua hatua gani mpaka sasa hivi kuhakikisha ulinzi wake? Je, kwa nini waandishi wetu hawataki kwenda vijijini; na imekuwaje mpaka Vicky Mtetema atoke London na waandishi wetu tunao hapa? Je, waandishi wetu ni wa mjini tu?

Mheshimiwa Spika, tunavipongeza vyombo vyote vya habari, lakini pongezi zangu zaidi zimwendee Tiddo Mhando. Tiddo ni mzalendo, ameweza kuacha kula kuku kwa mrija kule London alikokuwa akifanya kazi na kuona umuhimu wa kuja kuifufua Redio Tanzania ambayo sasa ni TBC. Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, TBC inamfurahisha kila mtu; ni redio ya wananchi wote na hajali itikadi kila mwananchi anaitumia lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu. Sasa. Lile jengo linavuja; hata hivyo tunamshukuru Mungu kwamba NSSF wataanza kuliboresha. Tunaomba NSSF wafanye haraka iwezekanavyo ili kuleta sura nzuri ya nchi yetu. Tunaomba serikali itoe fedha za maendeleo kwa TBC ili kuimarisha vitendea kazi muhimu kama vile kununua mitambo muhimu ya kisasa, kwa lengo la kuboresha usikivu zaidi na *television*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kiwanja kimekwishapatikana eneo la Bagamoyo ni vyema serikali itenye fedha kwa ajili ya ujenzi wa Jumba la Utamaduni na Kijiji cha Utamaduni huko Bagamoyo. Vilevile ni vyema serikali ihakikishe kuwa, hatimiliki ya kiwanja husika inapatikana ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii kwa kuwa ni ndogo sana. Hakuna wafanyakazi wa kutosha. Huenda watumishi wanakwepa kwa kuwa hakuna fedha za kutosha kuwalipa. Serikali ione umuhimu wa kuipatia wizara hii watumishi muhimu katika kutekeleza majukumu muhimu.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote wanaofanya kazi kwenye Wizara hii ya Habari na Michezo, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba Mikoa ya Singida, Manyara, sehemu za Mikoa ya Shinyanga na Arusha ambayo inapakana na Mikoa wetu wa Singida radio yetu ya Taifa haisikiki vizuri na pia TV ya Taifa haionekani

kabisa. Naomba kwa niaba ya wananchi wa maeneo haya, Serikali ifanye mpango wa haraka wa kuwawezesha waweze kusikiliza na kuona vipindi vizuri vinavyotayarishwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa mkazo haujatiliwa kuinua mambo ya utamaduni wetu kwenye Wilaya zetu. Naomba sana Serikali iweke nguvu kukuza utamaduni wa asili zikiwepo ngoma, nyimbo, michezo na kadhalika. Ikiwezekana Maafisa Utamaduni Wilaya zote wapewe vitendea kazi na wawezeshwe kwa fedha za kutosha ili waanze kuandaa mashindano mbalimbali, na pia Wizara ianzishe mashindano ya kitaifa ya ngoma, nyimbo na michezo mbalimbali ya asili.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada wanazofanya kuinua michezo mbalimbali kwa faida ya wananchi wetu na nchi yetu pia. Pia nawapongeza sana kuanzisha vyuo na vituo vya kutafuta vipaji hasa kwa mpira kutoka maeneo mengi hapa nchini. Tunaomba kazi ya kutafuta vipaji na kuinua mchezo wa mpira ianzie ngazi ya vijiji na hatimaye Taifa.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba michezo yote ni muhimu sana ikiwepo *netball*, bao riadha, mieleka, kulenga shabaha. Naomba michezo yote ifufuliwe hapa nchini. Bila kuzingatia ushabiki, timu ya Yanga imetutia aibu sana sisi wananchi kwa kitendo cha kutofika kiwanjani kucheza na Simba kutafuta mshindi wa tatu. Kwenye mashindano ya Kagame. Nchi imepata dosari kubwa sana Ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika na Dunia yote. Naomba kitendo hiki kikemewe na kuhakikisha hakirudiwi tena. Pia ili kukomesha ni lazima Yanga wapewe adhabu kali. Kitendo cha kuiogopa Simba si kitendo cha maendeleo kabisa. Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Bunge tunaomba michezo ndani ianzishwe hapa Bungeni imepita miaka sita tunaahidiwa michezo ya viungo na michezo mingine mpaka leo bado sasa, tunaomba utekelezaji ufanyike kwa faida za Afya kwa Wabunge.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara kwa hotuba nzuri sana. Nina angalizo, ushauri na maombi katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 22 Uk. 13 – 14 kuhusu *TBC* Televisheni kutoonekana kwa wananchi wa Lushoto isipokuwa tu wale wachache wenye uwezo wa kuweka *dish*. Je, njia rahisi ya *Aerial* haiwezekani ili huduma hii iwafikie wananchi wengi?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63 Uk. 46. Lushoto ni Wilaya ya milima ambako uandaaji wa viwanja vya michezo hasa mpira zinahitajika zana nzito za *Bulldozer* na *Grader*. Je, Wizara iko tayari kuisaidia Wilaya kwa kuchimba angalu viwanja nane Makao Makuu ya Tarafa ili kuinua kiwango cha michezo Wilayani Lushoto?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Hoja ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Tovuti ya wananchi Katika hotuba yake *paragraph* ya 17 Mheshimiwa Waziri amezungumzia tovuti ya wananchi, lakini hakuitaja tovuti hiyo anuani yake ni ipi ili Wabunge waweze kuifahamu. Je, anaweza kuitaja anuani kamili ili Wabunge waweze kuwajulisha wananchi katika maeneo yao? *Paragraph* ya 18 inazungumzia wananchi kuwa na fursa ya kuwasilisha kero zao kwa njia ya simu za mikononi. Je, Simu hiyo ni namba gani? Maofisa wanaojibu hoja hizo kwa njia ya simu ni wa ngazi gani ili kutoa majibu ya kuridhisha?

Katika *paragraph* ya 22 Mheshimiwa Waziri anazungumzia kama jukumu mojawapo la *TBC* kuwa ni kuongeza uwezo wa Shirika wa kufanya biashara na kujiongeza mapato ya kutosha kujiedhesa lenyewe kwa kuwa kuna mashirika au Taasisi binafsi pia zinafanya biashara hiyo ili kuomba dhana ya chombo cha umma kuua vyombo binafsi na kuruhusu *fair competition* dhana ambayo inaweza kuathirika kwa *TBC* kupewa ruzuku kwa fedha za umma zikiwemo za vyombo hivyo binafsi, jambo linalomaanisha kuwa kodi zao wenyewe zinatumika kuwaua au kuvuia vyombo hivyo na hivyo kutokuwa na uwanja sawa wa biashara. Je, Serikali ipo tayari kutoa *seed money*, yaani fedha za kutosheleza zitakazotolewa kwa *TBC* ili zifanye kazi zake kibiashara na kutoka hapo isipewe tena Ruzuku kwa fedha za Umma? Kama ipo tayari, ni fedha kiasi gani zinatosheleza *TBC* kufanya kazi zake kibiashara na zitaanza kutolewa lini?

Je, *TBC* imekwishatengeneza *Business Plan* yake angalau kwa miaka mitano ya kwanza ili *TBC* iweze kufanya kazi zake kitaalamu na kujijengea jina kama yalivyo mashirika kama *BBC*, *Deutche Welle* na *VOA*? Utekelezaji wa *Business Plan* hiyo utagharimu kiasi gani na lini fedha hizo zitatolewa ili ziwe kama *seed money* badala ya kuwa ruzuku ya mwaka hadi mwaka kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Spika, kwa vile *TCRA* ilitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutoka Bagamoyo hadi Mkatta kwa taarifa zilizopo, jambo ambalo halipo katika majukumu ya msingi ya *TCRA* kama alivyoeleza Waziri katika *paragraph* ya 24 ya hotuba yake: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulithibitishia Bunge hili ukweli wa jambo hili? Yaani kama ni kweli fedha zilitolewa *TCRA* kwa shughuli isiyo ndani ya majukumu ya *TCRA* na ni fedha kiasi gani? Je, mamlaka gani ilitoa fedha hizo tofauti na utaratibu wa kawaida ya matumizi ya fedha za Serikali? Je, iwapo utaratibu uliotumika ni kinyume na utaratibu wa fedha za Serikali na fedha zimetumika kwa kazi isiyo katika majukumu ya *TCRA* mamlaka au mtu, ni lini fedha hizo zitarejeshwa *TCRA* na wahusika waliokwenda kinyume na utaratibu wa fedha za Serikali amechukuliwa au atachukuliwa hatua gani ya kisheria au ya kinidhamu?

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kuwa ni utaratibu huu wa matumizi ya fedha za umma yasiyofuata kanuni za matumizi ya fedha za umma ndiyo yaliyoua mashirika yetu na kuwa suala hili lisipodhibitiwa mara moja litafisha jitihada za *TCRA* na hatimaye kuliua kabisa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi zinazofanikiwa katika michezo ya aina yote ni zile zinazowekeza katika kuandaa vijana tangu wakiwa wadogo na hasa katika Shule za Msingi na Sekondari: Je, Serikali ipo tayari kuanzisha na kuwekeza katika mashindano

ya kitaifa katika shule kuanzia ngazi ya shule kwa shule, Kata, Wilaya, Mikoa na hadi Taifa, kwa muundo wa UMISETA na kadhalika? Je, Wizara iko tayari kuwasiliana na Wizara ya Elimu na TAMISEMI kwa lengo la kuchagua shule moja ya sekondari katika kila Wilaya itakayotoa wanafunzi watakaokuwa na vipaji maalum vya michezo katika Wilaya na waandaliwe mtaalam maalum kwa lengo la kukuza vipaji hivyo vya michezo ili hatimaye nchi yetu iache kuwa kichwa cha mwenda wazimu na/au wasindikizaji katika michezo ya kimataifa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majengo ya *TBC* yaliyoko Mikocheni yametelekezwa kwa muda mrefu sasa: Je, ni tatizo gani hasa limesibu na hata Serikali kutelekeza kabisa majengo haya kiasi cha Mheshimiwa Waziri kutokuyataja kabisa katika hotuba zake kwa mwaka wa pili mfululizo, wakati watumishi wa *TBC* wanakosa pa kufanya kazi na hata studio ya *TBC1* kukosa kabisa hadhi?

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua gani kupata vifaa ambavyo havikuwasilishwa na Mkandarasi miaka zaidi ya nane sasa?

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoa na Watendaji kwa kazi nzuri ambayo wanafanya ya kukuza michezo hapa nchini.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweka umuhimu katika Serikali hii ya Awamu ya Nne suala la kukuza michezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 – 2010 kuhusu kuleta maendeleo ya michezo nchini bila shaka inahusu pande zote mbili za Muungano na kwa kuwa Serikali imekuwa inafanya ukarabati wa uwanja wa zamani wa Taifa na kuwekwa nyasi bandia kwa msaada wa *FIFA*, madhumuni ya ukarabati huu ni kuuwezesha uwanja huo kutumika kuchezewa michezo mingi kwa wiki kuliko ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya michezo ya Amani, Gamboni na Mao tze Dung vilivyoko Zanzibar viro katika hali mbaya na vinahitaji ukarabari wa haraka ili viweze kutumika kwa kuchezewa michezo mingi zaidi.

Kwa kuwa Serikali inapokea msaada *FIFA* wa kukarabati viwanja vya michezo nchini, ni kwa nini basi Serikali isitumie msaada huo wa *FIFA* kuvifanya ukarabati na kuvitandika nyasi za bandia viwanja hivyo ili viweze kubeba michezo mingi kwa wiki?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni *TFF* iliendesha mashindano ya mipira ya miguu uliohusisha Mikoa ya Tanzania Bara. Lakini jina la mashindano hayo yaliitwa “Kombe la Taifa” kwa maana ya kwamba Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza ni pale ambapo mashindano haya yalihuisha timu za Tanzania Bara pekee bila ya kuzishirikisha timu za Mikoa mitano ya Zanzibar. Ningombaa Mheshimiwa Waziri anieleze ni kwa nini timu za Zanzibar hazikushirikishwa

katika mashindano haya na kwamba sasa Wizara iko tayari mwakani kuzishirikisha timu za Mikoa mitano ya Zanzibar? Kama hilo linawezekana, basi ningeomba Serikali/Wizara iwasiliane na Wizara inayoshughulikia michezo ya Zanzibar mapema iwezekanavyo ili kuweka mazingira mazuri ya kuzishirikisha timu za Zanzibar katika mashindano hayo na mashindano mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, katika ile hali ya kukuza na kuzienzi ngoma za asili, ni vyema sasa Serikali ikaweka msukumo mkubwa juu ya suala hilo. Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia nguvu kubwa imewekwa katika kukuza miziki ya *Bongo Flavor*, Mashindano ya Ulimbwende na Muziki wa Dansi wa kizazi cha leo. Imekuwa ni jambo la kusikitisha kuona kwamba mashindano ya ngoma za asili ya Tanzania, Muziki wa asili imekuwa haipewi msukumo wa kutosha katika ile ile azma na kukuza ngoma na miziki yetu ya asili kwa ajili ya matumizi yetu na kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuiomba Wizara iweke mkakati maalum wa kuzienzi na kukuza ngoma zetu za asili pamoja na muziki wetu wa asili. Mkakati huu uwe ni pamoja na kuvitaka vyombo vya habari vya magazeti, TV na Radio ili kila inapowezekana wawe wanatangaza kwa kuzicheza ngoma zetu za asili, muziki na kadhalika. Hili litakapofanyika tutaweza kuzienzi na kuzitokuza ngoma na muziki wetu wa asili.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii napenda nizungumzie Waandishi wa Habari. Nawapongeza kwa nguvu zangu zote Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika tatizo kubwa linaloikumba nchi yetu sasa hivi la mfumo wa viongozi wachache kuwa wabadhirifu bila ya kulionea huruma Taifa na wananchi waliotuchagua. Vyombo vya Habari vimeduwa kichocheo kikuu cha Serikali kufanya utafiti wa ubadhirifu na kufanikiwa kuwagundua Viongozi na Watendaji wabadhirifu. Maovu mengi yaliyokuwa yanatendeka kwa kificho, kuliangamiza Taifa hili nikiri kwamba magazeti yamekuwa ndiyo chanzo cha kuibua.

Mheshimiwa Spika, niwasihî Waandishi wa Habari wanapotoa habari wahakikishe wanatoa habari zenye uhakika na wajitahidi wapate vielelezo vya uhakika na mimi kwa mtazamo wangu siungi mkono kuhoji wanazipata wapi nyaraka na vielelezo haswa zinazohusu ubadhirifu. Waandishi wetu watumie kila njia kupata vielelezo ili wawe wamejihakikishia uhalali wa habari wanazozitoa kwa jamii. Naomba nirudie kuwapongeza Waandishi wa Habari kwa jinsi walivyojiteti sana kutusaidia katika mapambano yanayoendelea, mapambano ya ujisadi wasirudi nyuma na wala wasihofu misukosuko kwani ni lazima watakutana nayo haswa watakawagusa watu pabaya pale penye maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza Waandishi wa Habari waliosaidia sana kazi ya kuibua ujisadi, naomba niwasihi Waandishi wa Habari ambao wanadhalilisha taaluma yao waache tabia hii mbaya ya kununuliwa na kufanya kazi ya kuchafua majina ya Wabunge wote wanaotetea Taifa kwa kuwanyooshea vidole wale viongozi wote wanaowadhulumu Watanzania na mali zao. Ni kitendo cha aibu na fedheha kwa Mwandishi wa Habari kuandika habari za kumlinda mwovu au kutetea maovu na hii linaonyesha mapungufu makubwa kwa mwananchi huyo na Waandishi wote wenye tabia hii mbaya ya kununuliwa na kuandika habari zisizojenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya magazeti ni kutoa elimu kwa jamii. Elimu hiyo ni vyema ikawa ya kweli na elekezi isiyo na uchochezi, uongo na isiyopotosha jamii nzima. Niwasihi sana wanahabari waijue kazi yao kwamba ni muhimu sana kwa jamii. Kwa hiyo, kununuliwa na watu waovu wakaandika habari za kuchafua watu, kusafisha wachafu, kumaliza watu kwani kazi ya kummaliza mtu ni Mwenyezi Mungu, sio yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naendelea kuwapongeza Waandishi wanaotoa elimu ya uhakika, isiyo na uchochezi na uongo.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya CCM kwa maamuzi mazuri ya kutumia majengo yaliyoachwa na utawala wa Wajerumani na kufanya sasa Chuo cha Michezo ya Afrika kilichopo katika Kijiji cha Malya. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuona umuhimu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kukitembelea Chuo hiki kwa niaba ya wananchi wa Kijiji cha Malya, Kata ya Malya, Jimbo la Sumve. Walishukuru sana kwa ziara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Chuo karibu kinakamilika kwa majengo muhimu ya michezo, naomba mambo yafuatayo yaanze kufanyiwa kazi.

- Chuo hiki kianze kutangazwa Afrika Mashariki, Afrika na sehemu zote ulimwenguni ili kijulikane kiko tayari na hapa Tanzania;
- Chuo hiki kisaidie kutoa mafunzo kwa shule za msingi na sekondari zilizopo karibu na chuo hiki li tupate wanafunzi wenye vipaji toka vijijini;
- Chuo hiki kitenge nafasi maalumu kwa walemavu ili tuwe na wakufunzi wa michezo kwa walemavu;
- Umeme upelekwe haraka katika chuo hicho, *generator* haitoshi;
- Barabara itengenezwe ya lami ili tukipe hadhi chuo hicho. Barabara toka Mabuhi – Ngudu hadi Malya; na

- Chuo hiki itengewe fedha za kutosha ili kiweze kutoa wakufunzi bora wa michezo ukizingatia michezo ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nawapongeza Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ambayo michezo, ndiyo inaanza kupanda kwa nafasi nzuri zaidi. Napenda kuwa muwazi, Yanga walitudhalilisha sana jana, kidunia, kinchi na kitaifa. Ni aibu sana kwa vilabu vya michezo kama Yanga kuwa na viongozi wasio na Utanzania. Naomba Kauli ya Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari hutoa habari kwa wananchi na vinasaidia kutuelimisha mambo mengi sana. Pamoja na hayo, Serikali ina vyombo vyake na viro vyombo vya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, Sheria ya haki na uhuru wa kupata habari, kulingana na muda unavyokwenda utandawazi unazidi kupanuka katika sekta ya habari, Serikali imefikia hatua gani kuleta hapa Bungeni sheria hizi ambazo zitakuwa ni muhimu sana? Naomba majibu ya kina kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu hivi Serikali ina Mfuko Maalumu wa elimu kwa waandishi wetu ili kupata elimu ndani na nje ya nchi hii kwa undani au kwa ujuzi zaidi?

MHE. SALIM ABDALLAH KHALFANI: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari na Michezo inayo jukumu kubwa la uhai na ustawi wa Taifa letu na watu wake. Ili kufikia ufanisi wa jukumu hilo Wizara ni lazima iwezeshwe kwa kupata fungu kubwa katika mgao wa bajeti ya Serikali.

Fedha inayopata Wizara, hivi sasa haitoshelezi kukamilisha yale majukumu yake ya kuiwezesha kuihabarisha jamii, kukuza na kuendeleza tamaduni zetu na kuimarisha shughuli za michezo.

Habari ni nyenzo muhimu katika ustawi na maendeleo ya nchi. Ili habari ziweze kufikia jamii ni lazima viwepo vyombo huru vya habari vya kuwahabarisha wananchi juu ya hali halisi ya harakati mbalimbali zikiwemo za kiuchumi katika nchi yao na nchi nyingine jirani na za mbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jambo hili kutamkwa ndani ya Ilani ya Uchaguzi kifungu 116, zipo dalili za kukandamizwa kwa Uhuru wa vyombo vya habari. Upmekuza

na vitishio kwa Ofisi na wanahabari wa Mwanahalisi ni kiashiria cha uvunjwaji wa Uhuru wa vyombo nya habari.

Aidha, vyombo nya habari vinapokwepa kuandika na kuonyesha habari zinazohusu mijadala mbalimbali ya kitaifa kama mijadala wa Bunge ni dalili ya kutokuwepo kwa uhuru wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la wafanyakazi wa Vyombo nya Habari hasa nya Serikali kulipwa mishahara midogo isiyoshawishi katika ufanisi wa kazi hivyo kusababisha wengi wao kuzihama Taasisi hizo za Serikali na kujiunga na vyombo nya binafsi nchini au kukimbia nchi za nje. Hivyo basi, stahiki na mishahara ya wafanyakazi viboreshwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la michezo, uwepo utaratibu wa kuwaendeleza wanamichezo wenye vipaji ili kupata wachezaji bora wa baadaye wa Taifa. Kwa mfano, wachezaji vijana na timu ya Taifa ya vijana Tanzania walioshinda Kombe la *Copa Coca cola* nchini Brazilili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na michezo ya kuigiza, bado lipo tatizo kubwa ambalo linaathiri ustawi na uendelezwaji wa utamaduni wa Taifa letu. Filamu nyingi kutoka nje haziendani na hali halisi ya utamaduni wa Watanzania. Aidha, baadhi ya michezo ya kuingiza kutoka nje na hata baadhi ya ile inayoigizwa hapa nchini haiwakilishi maadili sahihi kwa Mtanzania, hivyo Bodi lazima ijipange upya kutekeleza jukumu lake.

Mheshimiwa Spika, naomba nijumuise kwa kusema, Kamati za Ufundu katika timu zetu zimepitwa na wakati, *TBC* iwezeshe kufikia wananchi wote hapa nchini na kuwepo kwa uhuru wa kweli kwa *TBC* na vyombo vyingine nya habari, utamaduni wa Kitanzania upewe Kipaumbele na wasanii wetu waandalawe mazingira mazuri ya kufaidika na kazi zao. Ila mashindano ya ma-miss yazingatiwe upya faida na hasara zake katika kudumisha utamaduni wa asili wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tunazo dakika 75 za mtoa hoja na Naibu Waziri. Utaratibu tumekubaliana hapa; Mheshimiwa Naibu Waziri, atatangulia kwa dakika zisizozidi 30 na Mheshimiwa Waziri atamalizia kwa dakika 45. Karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari kujibu hoja.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii, nami nichangie hoja ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema, nguvu na uwezo wa kutekeleza na kuhudumia wananchi katika nchi hii ya Tanzania.

Napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa

Afrika. Aidha, nampongeza kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu mnamo Februari, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wangu, Mheshimiwa George Mkuchika, Mbunge wa Newala, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Aidha, nampongeza kwa uchapakazi wake na ushirikiano wake mzuri na mkubwa anaouonyesha tangu ameingia kwenye Wizara yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sana, nachukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kunibakiza katika Wizara hii kama Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Ninathamini sana heshima aliyonipa na ninaahidi nitafanya kazi kwa nidhamu, uadilifu na nguvu zangu zote. Namwomba Mwenyezi Mungu, aniongoze vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wako, kwa kazi nzuri mnayoifanya ndani ya Bunge hili kwa viwango. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushirikiano walionipa toka nimeanza shughuli hii ya Unaibu Waziri hadi leo. Naomba mzidi kunipa ushirikiano katika kutimiza majukumu niliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Hajjat Kijakazi Mtengwa, Katibu Mkuu. Aidha, kipekee napenda niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini, kwa imani yao kwangu kwa kunichagua kwa vipindi vitatu toka mwaka 1995 hadi leo.

Nataka niwahakikishie kwamba, nipo pamoja nao, nitajitahidi kufanya kazi kwa juhudhi zangu zote ili kutatua matatizo ambayo yapo ndani ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu, kwa kunipa moyo, kuniongoza na kuniombea dua mbalimbali hasa mke wangu Mwalimu Flora Bendera na wanangu Yassin, Herbert na Gloria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nichukue nafasi hii baada ya kumaliza utangulizi huo, kuchambua hoja za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambazo zimejitokeza katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, Wizara hii ina sekta tatu ambazo tumepewa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba, habari zinaenea nchini, utamaduni unaendelezwa na michezo inaendelezwa. Hizi ni Sekta nyeti ambazo zinahitaji umakini wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, kazi nitakayoifanya hapa, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote. Wapo Wabunge wengi sana ambao wameelezea hoja hii kwa maandishi na kwa kusema. Yale ambayo yamesemwa, baadhi nitamwachia Mheshimiwa Waziri wangu aweze kuyaelezea, lakini yale ambayo yameelezwa kwa maandishi hapa, naomba nianze kuchambua moja baada ya jingine. Nitaanza na Sekta ya Michezo.

Mheshimiwa Spika, katika michezo yapo mambo mengi ambayo yamejitokeza, lakini ya msingi ambayo yamejitokeza ni kama 18. Suala ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni la viwanja vya michezo, ujenzi wa viwanja vya michezo, viwanja kuporwa katika maeneo mbalimbali na kukosa viwanja kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la msingi sana, unapozungumzia mchezo wowote duniani, Sheria Namba Moja ya mchezo wowote ni kiwanja; kama huna kiwanja huwezi kucheza mchezo wowote ule. Ninaanza kuzungumza hili, kwa sababu Wabunge wengi wamelizungumza. Nataka nikubaliane nao kwamba, imejitokeza hapa na ukitazama idadi ya Wabunge wanaozungumzia, kwa mfano, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Kambi ya Upinzani pia wamezungumzia hilo na wengine wengi; Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Salim Abdallah, Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir wamezungumza pia.

Mheshimiwa Spika, tunachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, ninaomba na ninatoa wito Halmashauri zetu zihakikishe kwamba, zina jukumu la kutenga maeneo ya viwanja kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa na katika Taasisi.

Ninaomba nikumbushe, shule zote zinazojengwa sasa hizi za sekondari na msingi ni muhimu kutenga maeneo ya viwanja, tena si vya mpira wa miguu ni michezo yote. Ninaomba nilisisitize hilo kwa sababu bila ya kuwa na viwanja, hatuvezi kufika mahali popote.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni suala linalohusiana na vifaa vya michezo kwamba, kwanza ni aghali na kupatikana kwake ni kwa tabu. Ninaomba niseme hapa kwamba, sisi kama Serikali, tunajaribu kuhamasisha wafanyabiashara wengi waweze kuagiza vifaa vya michezo nchini ili iwe rahisi kununulika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni viwanda mbalimbali vya michezo hapa nchini ili iwe rahisi kuvipata hapa hapa nchini, hilo Serikali inalitilia mkazo; tumeshazungumza na Waziri wa Viwanda na Biashara ili angalau wawekezaji wengi wajitokeze kwenye masuala yanayohusiana na masuala ya vifaa vya michezo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa sana hapa ni wataalamu wa michezo nchini, kuanzia ngazi ya Kata unakuja mpaka kwenye Wilaya na kuendelea, kwenye utawala wa michezo, makocha, waamuzi na michezo mbalimbali. Nataka nisitisize hapa kimsingi kwamba, suala hili ni nyeti, sisi kama Serikali tuna vyuo vinavyojulikana sasa hivi viro vitatu; tunacho chuo cha Malya ambacho ni chuo cha maana sana kwa wale Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nilisafiri nao mimi

mwenyewe kwenda Malya. Chuo kile ndiyo kinategemewa kuwa cha kwanza katika Afrika nzima, kwa hiyo, tunataka tukiendeleze. Sasa hivi pale tunajenga ukumbi wa ndani ambao ni wa kimataifa kwa michezo yote, tutaendelea kuboresha chuo kile ili wataalamu mbalimbali wa michezo waweze kufyatuliwa kutoka eneo lile la Malya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna Chuo kingine muhimu sana, ambacho tunashirikiana na Wizara ya Elimu nacho ni Chuo cha Butimba Mwanza. Chuo hiki ndiyo kinatoa walimu wanaofundisha Walimu wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari, tutaweka mkazo pale, tutapeleka wataalamu zaidi ili nacho kiendelee.

Mheshimiwa Spika, si hicho tu, tuna vyuo viwili na vituo viwili vya michezo, kwa kutegemea na nchi yetu ilivyokuwa kubwa tumeweka kanda mbili, kuna Kanda ya Kaskazini tuna kituo Arusha na Kanda ya Kusini tuna kituo Songea. Tumeviweka makusudi kabisa kwa ajili ya Halmashauri zetu na michezo mbalimbali, waweze kupata nafasi ya kupeleka wataalamu kwa kozi fupi fupi ili waweze kupata mafunzo pale na kwenda kuhudumia Halmashauri zetu, hiyo ni sekta ya kuendeleza.

Mheshimiwa Spika, bado tuna uhusiano wa utamaduni na nchi mbalimbali, ambao tunafanya utaratibu wa kupeleka vijana wetu nje ili waweze kupata stashahada na Shahada za Uzamili.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tunayo shahada ya *Physical Education* kwa wale ambao pia wanapata elimu ya juu pale wanaweza kupata shahada ya *physical education*, ndiyo wataalamu wetu wa kutuhudumia katika sekondari na vyuo pamoja na maafisa michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza ni kuendeleza michezo kuanzia ngazi ya utoto. Napenda nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wote kwenye wazo hili, kuna usemi unaosema; samaki m kunje angali mbichi. Hii ndiyo njia pekee ya kuendeleza michezo katika nchi, duniani kote michezo inaendelea kama utaanza katika umri mdogo, sisi hili tunalitilia mkazo sana na ndiyo maana nataka nichukue nafasi hii, kuwapongeza wale watu binafsi ambao wanaanzisha *sports academies*, napenda niwapongeza sana kwa sababu huko ndiyo kwenye msingi.

Mheshimiwa Spika, ukienda nchi kama Cameroon, Ghana, Nigeria; *sports academy* katika nchi zipo zaidi ya mia moja, matokeo yake ni kwamba, watu wanaanza kupata mafunzo kwenye msingi na ndiyo maana naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa kurudisha michezo katika mashule. Kwa sababu huwezi ukamwendeleza mtoto kama hawezi kucheza kutoka chini na huwezi ukatofautisha michezo na elimu, unataka hutaki utamwona mtoto anacheza barabarani. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na utaratibu na bahati nzuri Wizara ya Elimu na Wizara yetu tumejjipanga, mwezi wa Septemba tunategemea tuanze michezo ya shule za msingi na mwezi wa Disemba tunaanzisha michezo ya shule za sekondari .

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza hapa ni Maafisa Michezo katika maeneo kwamba hawapo. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamika ni kweli,

lakini huu ni utaratibu ambao ningeomba Wabunge tusaidiane. Nazungumza kwa uwazi kabisa kwamba, tatizo ambalo tunalo Maafisa Michezo katika maeneo ambako wapo, hawana kazi kwa sababu hakuna hata shilingi ambayo inatengwa kwenye bajeti za Halmashauri na ndiyo maana nataka nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwakumbusha Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwamba ni lazima watenge fedha kwenye Halmashauri zetu ili sekta hii nayo iweze kuendelea kwa sababu hawana shughuli yoyote.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokwenda kufungua mashindano ya netiboli aliliona, alipofungua mashindano ya Taifa Cup aliliona, akaona kuna umuhimu wa kukumbusha na mimi naomba nimuunge mkono na kusisitiza kwamba, kama hamtatenga fedha hawa watafanya kazi ya kukusanya kodi badala ya kuendeleza kazi ya michezo na utamaduni. Kwa hiyo, tuwape kazi kwa kutenga fedha ili sekta hii nayo iweze kuendelea kwa sababu ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa hapa ni suala la watu binafsi kuwekeza kwenye shule maalumu za michezo. Nataka niafikiane nalo na ninaomba wajitokeze kwa sababu sekta ya michezo na utamaduni duniani kote, watu binafsi wengi ndiyo ambao wanajikita huko. Kwa hiyo, hili ni suala la msingi sana, naomba sana tujielekeze katika kufanya haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa kwamba, Serikali iltilie mkazo ni mashindano ya michezo mbalimbali kwa umri mbalimbali; hili ni la msingi, ili mchezaji aweze kuonyesha kipaji chake ni lazima ashindane, kama hakuna mashindano huwezi kuona kipaji cha mtu. Ndiyo maana napenda kuvipongeza baadhi ya vyama na tunataka vyote viige mfano kama *TFF* wanavyofanya, wanajitahidi kwa sababu wao wana mashindano ya *under 17*, wana mashindano ya Taifa Cup, wana mashindano ya ligi na vivyo hivyo inatakiwa vyama vyote vifanye hivyo; *basketball, volleyball*, riadha na michezo mingine yote, ili mtu aanze kujenga kitu ambacho ni cha mashindano ndani ya mwili wake akiwa na umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii kwa kina sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limejitokeza ni uongozi wenye upeo katika michezo; suala hili limetuletea matatizo, kuna baadhi ya viongozi ambao wanachukua uongozi wa michezo lakini uwezo wa kuongoza hawana. Wanaingia mle labda kwa tamaa ili angalau waonekane tu kwamba wao ni viongozi wa michezo wa aina fulani, lakini anachokifanya hakioneekani. Sasa si vizuri, wewe unachukua uongozi kwenye chama fulani na michezo ule unadorora unaitupia lawama Serikali au watu wengine ni vizuri kama unaamua kuchukua uongozi uwe ni mwenyekiti wa chama fulani cha michezo ama kilabu fulani. Uwe na uwezo wa kuweza kuuendeleza michezo ule badala ya kutoa lawama. Napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia.

Mheshimiwa Spika, lipo suala lingine limezungumzwa kwamba, Serikali ijitahidi kufufua michezo yote nchini, kuanzia ngazi ya kijiji mpaka juu. Mimi nakubaliana nalo

hili, ipo baadhi ya michezo ambayo tunaiwekea msisitizo zaidi; ni vizuri tukawa na usawa wa michezo yote isiwe tunapenda labda *football* peke yake ama *netball* peke yake. Michezo yote tuifufue, ni sawa kwamba michezo wa mpira unapendwa lakini suala la michezo wa mpira kupendwa inawezekana michezo wa mpira kama ambavyo tungeiendeleva riadha ama *boxing*, kama hivi Kasheba ametuletea heshima kubwa sana. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuendeleza kufufua michezo yote na ndiyo maana hapa unaona faida ya kuwa na afisa utamaduni au afisa michezo ambaye amepewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni taratibu za michezo ambazo zimewekwa. Sheria ya Michezo imezungumzwa kwamba, imekaa muda mrefu haijahuishwa; naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, mchakato unaendelea, tumeshapata maoni toka kwenye ngazi ya Kijiji, Kata Tarafa, Wilaya na Mikoa, sasa tunamalizia kupata maoni ya Kitaifa ili baadaye sheria ile sasa iweze kuletwala na kukamilisha utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa suala la migogoro katika michezo, hili nakubaliana nalo, tunahuisha Katiba. Tumeona upo umuhimu wa Katiba zetu za michezo mbalimbali, ziwe zinatengenezwa na Wizara ama na wataalamu ziweze kusaidia kuondoa baadhi ya migogoro. Zipo Katiba nyingine kwa kweli ni chanzo cha migogoro, kwa hiyo, tunajitahidi tuwe na *uniform* na tuwe na Katiba ambazo zinalingana lingana na zinapunguza migogoro.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza ni hili la hivi karibuni; suala la Timu ya Yanga kuingia mitini, sisi hilo tumelipata, bahati nzuri tumeshapata majibu kutoka CECAFA tulipokuwa kwenye kikao chetu cha kujumuisha hapa. CECAFA imekaa kwa kufuata taratibu zao za sheria za mashindano ya CECAFA, Timu ya Yanga imefungiwa kutokushiriki mashindano ya CECAFA kwa miaka mitatu mfululizo na imepigwa faini ya dola 35,000. Kwa hiyo, ni taratibu ambazo zipo, wao wenyewe ndiyo wamejidumbukiza kwenye matatizo haya na sheria za mashindano ndiyo zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali, nataka niwe muwazi kabisa, tunalaani kitendo hicho kwa sababu siyo cha kiuanamichezo.

Mheshimiwa Spika, katika sekta hii yapo mengi lakini la mwisho ambalo naomba nilizungumze ni pongezi mbalimbali za vijana ambao wamefanya vizuri kwenye mashindano ya Copa Coca Cola na sisi pia kama Serikali, tunawapongeza. Kutokana na uhusiano kati ya ZFA na TFF, nashukuru kwamba wamekaa jana na wamekubaliana kwamba, wawe na vikao vya mara kwa mara ili kuweza kujenga *harmony* katika uongozi wao.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni Sekta ya Michezo, naomba sasa niingie kwenye Sekta ya Utamaduni. Katika Sekta ya Utamaduni nikianzia na wafuatao; Mheshimiwa Ania Chaurembo, pamoja Mheshimiwa Kabwe Zitto, walizungumzia haki za Wasanii kwa uchungu sana. Kwanza, napenda nikubaliane na wote waliozungumza kwamba, wasanii wetu nchini kwa kweli wanaonewa sana, hata Mheshimiwa Mlata, alilizungumzia hilo.

Nataka nikubaliane na ye ye kabisa, kwa sababu wao ndiyo wanaobuni kitu, lakini hawapati kinachostahili na usanii ndiyo maisha yao. Serikali inafuatilia kwa makini juu ya haki za Wasanii nchini, tangu Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ilipopitishwa Bungeni; hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

Mheshimiwa Spika, kutoa elimu ya haki miliki kwa wasanii 3000 kwa mikoa 15, tangu mwaka 2006 Juni; mwaka 2008 wasanii wamelipwa jumla ya shilingi milioni 98 kama mirabaha kwa kazi zao; wasanii 1300 walinufaika, tunawashauri wajisajili na kazi zao *Copyright Society of Tanzania (COSOTA)*. Hata hivyo ni jukumu la kila msanii, kufuatilia kazi zake zilizoibowi na kutoa taarifa *COSOTA* ili hatua za kisheria zichukuliwe. Kubwa ambalo Serikali wamelifanya ni juhudzi za kuweka stika maalumu, zitakazogharimu shilingi milioni 300 katika kazi zilizorekodiwa, zitaanza mara moja na Serikali inajitahidi kufanya hili kwa sababu hii ndio njia nzuri na stempu maalumu ya kujua kwamba hii ni kazi ya Zitto, hii ni kazi ya Bendera, hiyo kidogo ingeweza kutoa utata ambao upo. Kitu hiki ni kigumu lakini Serikali itajitahidi na hiyo itasaidia hata vyombo kama Polisi na wengine, kuweza kushika kama mtu amechapisha kazi ya mwenzake au ameiba kazi ya mwenzake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, amezungumzia mavazi yasiyo ya heshima kwa wasanii wa kike. Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wasanii na wamiliki wa vikundi vya sanaa nchini ili angalau wavae nguo za heshima. Hakuna anayelipenda hili na sisi Serikali tunalikemea na tunaendelea kulikemea na tumewapa nguvu zote BASATA, wachukue hatua kwa vikundi vinavyowavalisha wale wasanii vichupi ambavyo havina heshima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, amezungumza kwamba, *film* nyingi kutoka nje haziendani na hali halisi za utamaduni wetu; ni kweli na bodi inajipanga upya kutekeleza jukumu lake. Moja ya hatua iliyochukuliwa ni kuteua Wajumbe wa Bodi ambao hawakuwepo kwa muda mrefu, pia Wizara imeongeza Watendaji Wakuu wawili na juhudzi zinafanyika kuongeza watendaji wengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ali Khamis Seif amesema maadili yanamomonyoka; Mheshimiwa Msolwa amezungumzia hilo, Mheshimiwa Vuai Abdallah amesema hilo hilo na Mheshimiwa Lucy Owenya amesema hilo hilo kuhusu maadili ya Watanzania yanavyoharibika. Kilio cha Mtanzania, mmomonyoko wa maadili tuliyoyarithi kutoka kwa wazazi baada ya uhuru, maadili ni suala mtambuka nyote mnafahamu. Kwa hiyo, kila mwanajamii anatakiwa kushiriki kama ilivyo katika ujenzi wa Mtanzania, kwa upande wa Wizara hatua zinazoendelea ni mchakato wa kuhuishwa Sheria ya Utamaduni na Sheria Namba Nne ya mwaka 1976 inaandaliwa upya ili ipelekwe kwa wadau tuone ni namna gani tunaweza kuiboresha sheria hii iweze kuwa na meno zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ania Chaurembo anasema siku ya utamaduni ifanyike katika kila mikoa, pamoja na Mheshimiwa Mwanawetu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwenye suala hili. Tunakubalina nalo, siyo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani

bali ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani, tunakubaliana naye kwamba, siku ya utamaduni tutakuwa tunaifanya si kwa Dar es Salaam, tutakuwa na utaratibu sasa wa kufanya kwa nchi nzima kwa kufanya mzunguko, inaweza kuwa labda mkoaa fulani na mwaka fulani mkoaa mwingine na katika Wilaya nako tutatoa maandishi ili angalau iwe inafanyika kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kwamba, siku hii ya kukumbushana mila, desturi zetu, ngoma zetu na mambo yetu ya asili ni muhimu. Mheshimiwa Stella Manyanya amezungumzia *Ze Comedy* kusaidiwa na Wizara; suala hilo tunalishughulikia. Suala la kikundi cha *Ze Comedy* liko mahakamani, siwezi kulizungumzia hapa, wameshakwenda mahakamani nadhani haki kule itatendeka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanawetu pia amezungumzia marekebisho ya Sheria ya Bodi ya *Film*; hilo tatizo lipo kwenye ufumbuzi linaendelea kushughulikiwa. Mheshimiwa Ali Khamis Seif, amezungumzia maombi ya Wataalamu wa kufundisha Kiswahili nchi za nje. Hili ni suala ambalo nililijibu juzi, tumeendelea kulifanyia mchakato na ukweli wenyewe ni kwamba tunajipanga. Tumeshapata maombi 300, kwa hiyo, tunaendelea kuyashughulikia ili sehemu nyingine zote tuweze kuwapeleka nchi ambazo wanahitajika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi amezungumzia matumizi ya Kiswahili; ni kweli sasa hivi Kiswahili kinatumika katika *AU* na kinatumika katika Afrika Mashariki. Bahati nzuri katika Afrika Mashariki, Tanzania kwa maana ya Zanzibar, ndio itakuwa Makao Makuu ya ile Kamati ya Kiswahili; kwa hiyo ni kwamba tunaendelea kukitumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Mlingwa amekumbusha kwamba, tuache kiswanglish na ninarudia, juzi nililijibu lakini nasisitiza kwamba, kuzungumza kiswanglish ni sisi tubadilike, tunajua Kiswahili tuache kuzungumza kiswanglish kwa sababu robo tatu humu ndani tunazungumza kiswanglish.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Sekta nyingine ya Habari; Sekta ya Habari kuna mambo mengine atayazungumza Waziri wangu, mimi nitazungumzia masuala machache, naomba mnivumilie naona makaratasii yapo mengi hapa, ni masuala yanayohusiana na *TBC*, pamoja na mambo ya redio kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje, amezungumzia vitendea kazi hafifu; Serikali inajitahidi kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba, suala la *TBC* linashughulikiwa. Bahati nzuri napenda niishukuru Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuishawishi Serikali kutupatia shilingi bilioni nne ili tuweze kuendeleza usikivu katika nchi yetu na Mheshimiwa Waziri atatamka baadhi ya Mikoa ambayo mwaka huu hata ukitazama katika kitabu chetu cha bajeti, kuna fedha nyingi tu zimetengwa ili kuweza kuweka FM katika mikoa mbalimbali. Nadhani tukiweka mwaka huu, itabakia mikoa michache sana, mkituongezea fedha nyingine

mwaka ujao tunaweza tukamaliza kabisa mikoa mingine iliyobaki, cha msingi ni kutuongezea fedha ili tuweze kuweka maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Slaa amezungumzia ruzuku ya *TBC*; katika mabadiliko yanayoendelea ya *TBC* lengo la Serikali ni kusaidia ili ijiendeshe yenyewe bila kuitegemea Serikali. Hadi sasa tayari kumefanyika majadiliano ya awali katika mwelekeo huo na Uongozi wa *TBC* umejipanga katika kuhakikisha azma hiyo inafikiwa.

Mheshimiwa Spika, lengo letu ni *TBC* kuweza kujitegemea, hatutaki *TBC* iwe inapata fedha kutoka Serikalini; tunakwenda hivyo kutokana na Bajeti ya Serikali, mwaka huu tumepata shilingi bilioni nne, mwaka ujao tukipata mwisho tutaiachia ijitegemee yenyewe. Inaingia kwenye ushindani, lakini kwa hali ilivyo sasa hatuma njia ni lazima tuisaidie ili iweze kufika mahali inapostahili.

Suala lingine Mheshimiwa Zuleikha anasema *TBC* iimarishe kwa kupatiwa nyenzo; hilo tumelifanya. Mheshimiwa Mgana Msindai amesema, usikivu Singida hakuna, Mheshimiwa Mgana Msindai ukisoma Kitabu cha Bajeti mwaka huu tayari Singida wanafungiwa *FM*; tena wanafungiwa Redio FM na *television*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, amezungumzia *TBC1*, *TBC* Taifa inapatikana kwa *dish* tu, tutakapoweka hizi FM zaidi na tutakapopata fedha zaidi, tutaongeza mikoa yote iweze kupata. Mheshimiwa Beatrice Shelukindo amesema kuna usikivu hafifu Kilindi; ni kweli na tunaendelea kuboresha.

Mheshimiwa Kabaka amesema, baadhi ya matangazo ya kuelimisha UKIMWI, yanakiuka maadili. Kufuatia ukubwa wa athari za UKIMWI na athari zake kwa Taifa, *TBC* hupokea matangazo kutoka kwa wadau mbalimbali, walio katika vita dhidi ya UKIMWI, baadhi yake huenda yasiwafurahishe watazamaji wote, lakini kwa kiasi kikubwa, *TBC* itahakikisha maadili yanazingatiwa ili tuweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya mtoa hoja; Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa George Mkuchika.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kushukuru kwa kunipa tena nafasi ya kuja kuzungumzia tena hoja yangu. Tulikubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri, ye ye azungumzie sekta zote na kutaja watu waliochangia, mimi nimesimama hapa kuelezea yale ya Kisera ambayo yametajwa katika mazungumzo yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kupokea shukrani za Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi nzuri inayofanywa na Vyombo vya Habari vya Serikali na vya Binafsi. Sisi katika Wizara, mmetutia moyo kwamba tupo pamoja, matatizo yetu mnayaelewa na mnaonyesha kwamba tupo pamoja.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi, kwa sababu ya muda wamekuwa ni wengi na wale waliochangia kwa kuzungumza pia ni wengi. Napenda nichukue nafasi hii, kutambua michango ya Wabunge wafuatao ambao walichangia kwa maandishi. Wabunge hao ni wafuatao:-

Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifani, Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Margaret A. Mkanga, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza.

Waheshimiwa Wabunge wafuatao walichangia kwa kuzungumza: Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Suzan J. A. Lyimo, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Martha M. Mlata na Mheshimiwa Joel N. Bendera, Naibu Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tunawashukuru wote waliochangia na kwamba, sasa nitazungumza machache yaliyobaki ya Kisera. Jambo la kwanza lililozungumzwa hapa ni uhuru wa vyombo vya habari. Imesisitizwa kwamba, Tanzania idumishe uhuru wa vyombo vya habari; sheria mpya isiwagandamize wanahabari. Nataka kusema, ushauri tumeupokea lakini pia nataka niliarifu Bunge lako Tukufu; katika Bara la Afrika nchi tatu zinazoongoza kwa kuwa na vyombo vingi vya habari ni pamoa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, sisi tunalizingatia hilo na yale tuliyoyasema kwamba sheria itatungwa ya kusimamia vyombo vya habari, wanahabari

wenyewe wameshirikishwa na hata lile suala la kutunga sheria ya uhuru wa habari, wanahabari wameshirikishwa na watashirikishwa. (*Makof*)

Kwa hiyo, nataka niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge, wanahabari na Watanzania wote. Tunaheshimu utawala bora katika nchi hii na kamwe hatutanga sheria ya kumkandamiza mtu kwa makusudi; isipokuwa tutatunga sheria ambayo itatakiwa iheshimiwe na kila mtu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunashukuru kwamba, *TBC* wamepongezwa. Ipo rai hapa kwamba, *TBC* tuwawezeshe kwa asilimia 100 washirikiane na wengine ili wasishindane na wengine kibiashara. Mimi nashukuru kuna Mbunge asubuhi wakati wa kuchangia ameeleza kwamba, hivi Habari, Utamaduni na Michezo shilingi 24 zinatosha? Jibu hazitoshi na ndiyo maana Serikali haiiachi *TBC* peke yake. Inaipa fedha kila mwaka ili waweze kuijendesha wenyewe mbele ya Safari.

Jambo moja la Kisera nataka kuliweka wazi; nchi yetu tumeamua kuchangia shughuli baina ya Serikali na wadau binafsi. Ninaposikia suala la Serikali kujiondoa kabisa katika vyombo vya habari, ninajitahidi kuelewa lakini sijaelewa. Tumeruhusu watu kujenga shule binafsi; zinafanya kazi, hatujazifunga nchi nzima. Shule za Serikali na za watu binafsi, zinashirikiana kuboresha elimu katika nchi hii. Hospitali za Binafsi na za Serikali, zinashirikiana kuboresha huduma katika nchi hii. Hakuna tunachogombana. Wale watu binafsi wataruhusiwa kuendelea na Serikali nayo itoe mchango wake. Yapo maeneo katika nchi hii, hakuna chombo cha habari hata kimoja cha mtu binafsi ambacho kipo huko au ambacho kimeonyesha nia ya kwenda huko; Serikali ikiacha nani atakwenda huko? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, upande wa michezo na sanaa za maonyesho, Naibu Waziri ameeleza Wizara yetu mpya imeanza mwaka juzi lakini tumekuwa tuna matatizo kwa sababu shughuli za utamaduni zinasimamiwa na Halmashauri za Wilaya. Halmashauri za Wilaya nyingi, zipo zingine hazina Maafisa Utamaduni wala Maafisa Michezo; zipo nyingine ambazo hazitengi hata senti moja kwa shughuli za utamaduni na michezo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, hasa Wabunge wenzangu wa Majimbo, sisi ni Madiwani tushirikiane kuona kwamba Halmashauri zetu zinatenga fedha na kuwawezesha Maafisa Utamaduni na Michezo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, hili jambo alizungumza vizuri sana Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, alimuunga mkono Mheshimiwa Ania Chaurembo. Tunakubaliana kwamba, lazima tufanye jitihada za makusudi, kuhakikisha Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo wanapatikana na wanawezeshwa. Namna ya kuwezeshwani kuwemo katika bajeti. Kama alivyosema Naibu Waziri, tunamshukuru Waziri Mkuu ametoa Waraka kwa Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya wote na Wakurungezi wa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, kuhakikisha wanatenga fedha za kuendesha shughuli za michezo na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa suala la kukatwa na kusachiwa Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mwanahalisi. Linakujaje Wizara ya Habari, nadhani ni kwa sababu yule ni Mwaandishi wa Habari? *Police Ordinance* inasema, Polisi wakishuka mahali fulani palipotendeka uhalifu, wanaruhusiwa kwenda ku-search mahali pale baada

ya kupata *search warrant*. Hii ni sheria ndani ya *Police Ordinance*. Katika hili, hakuna mtu aliye juu ya sheria; awe Mbunge, awe Mwaandishi wa Habari au mkulima; polisi wana mashaka na wewe ni ruhusa kuku-*search*. Taarifa tulizonazo bi kwamba, polisi walifuata taratibu zote. *Police Ordinance* inasema, mtu wakisham-*search* polisi wakiridhika kwamba hana makosa wanamwachilia. Sheria zilizopo sasa zinasema polisi wakishamwachilia, huna mamlaka tena ya kuhoji kwa nini mmem-*search* mkamwachilia.

Kwa hiyo, nilitaka hili nilieze kwamba polisi wamefanya kazi yao na Wizara ya Mambo ya Ndani mjadala unafuata. Kwa hiyo, ningeliomba nilieze tu kwamba, kwa utafiti tuliofanya katika Wizara, polisi wametekeleza wajibu wao. Anaweza kusachiwa dereva, anaweza kusachiwa mwaandishi wa habari au mfanyabiashara. (*Makofi*)

Mimi ndugu zangu katika hili nataka tuelewane, huyu kwa sababu masuala yake yameandikwa kwenye magazeti; hivi kweli kila siku hakuna mtu anayehojiwa ni huyu Kubenea, hakuna mwingine aliyehojiwa au aliyesachiwa katika nchi hii? Wenzetu wana kalamu lakini mimi katika Jimbo langu la Newala wapo watu wanasachiwa na polisi wakaachiwa, hawana kalamu hawajaandika. Kwa hiyo, hamna habari nazo. Kwa hiyo, nasema pale ambapo polisi wamefanya kazi yao, naomba suala hili tusilishushe na suala la ukandamizaji. (*Makofi*)

Wizara ya ni Waandishi wa Habari, ndugu yangu Mheshimiwa Zitto kasema hapa. Wizara ni Waandishi wa Habari wote, wala siyo Wizara ya vyombo binafsi. Nakubali, mimi ni Waziri wa Waandishi wote na wao wanajua na mimi najua kwamba ni Wizara yao kwa sababu vibali vya wao kuandika habari tunatoa sisi Wizarani kwetu katika Idara ya Habari. Kwa hiyo, tuko pamoja na waandishi na mimi najitambua na Wizara nzima inatambua kwamba, waandishi wa habari ni wadau wenzetu muhimu katika kupasha habari katika nchi yetu. (*Makofi*)

Nataka niseme lingine, ukiwa kiongozi lazima uwe mvumilivu, lazima uwalee, sheria iliyopo sasa ambayo haijafutwa, inampa kibali Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kulifuta gazeti endapo ameona limekwenda kinyume na maadili. Serikali haijalifuta gazeti hata moja. Mimi tangu nimekuwa Waziri, hatujafuta gazeti lolote. Tumefanya nini? Tunawalea, tunawaita kule *TCRA*; Tume ya Mawasiliano ipo; Kamati ya maudhui ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Bunge inateuliwa na Waziri anayehusika na mambo ya Habari. Tumewaita mara kadhaa, tumewaonya, tumewapa barua wajirekebishe na ndiyo hamjasikia. Mkitaka niseme nani kaonywa, alifanya kosa gani, niandikieni nitawaiteeni. Ninachotaka kusema sisi kama Serikali tunawavumilia Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine kwa nini kuna vurugu katika Uandishi wa Habari? Kuna vurugu kwa sababu taaluma hii imevamiwa na watu ambao siyo Waandishi wa Habari. Wale Waandishi wa Habari *proper*, waliokwenda shule kusomea habari, wanajua wanachokifanya na hatuna matatizo na wengi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini hili limetokea? Limetokea kwa sababu huko tulikotoka, chini ya mfumo wa Serikali ya Chama kimoja, Vyombo vy'a Habari vyote vilimilikiwa na Serikali na Chama Tawala. Kwa hiyo, Chama Tawala na Serikali, vilifundisha Waandishi wake wa Habari waliokidhi mahitaji yake. Tuliporuhusu kwamba sasa ruhusa mtu yejote kuanzisha Chombo cha Habari; hapa ndipo tatizo lilipoanzia, kwa sababu tukawa na Vyombo vy'a Habari vingi, vinahitaji wafanyakazi wengi, lakini waliopo ni wachache na ili kufanya kazi zake ili gazeti lisilale, wakaruhusu hata watu wasio na taaluma ya Uandishi wa Habari kuandika habari. Hilo ndilo tatizo letu na ndiyo maana katika Sheria tunayoitunga, tunazungumzia suala la kuinua taaluma ya Waandishi wa Habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwalimu kwa kusomea. Kwa kazi ya ualimu hata kama una *Ph.D*, ilimradi haukusomea ualimu, hujasomea *Educational Psychology*; ili uingie darasani kufundisha lazima upate leseni. Tunataka twende huko kwamba, mtu anayeandika habari awe na taaluma ya habari, utajiita wewe ni Mwaandishi wa Habari wakati huna taaluma ya habari! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wakunga wana Baraza lao wanasa jiliwa, Makandarasi wanasa jiliwa na Walimu wanasa jiliwa. Vurugu hii iliyopo ni kwa sababu Waandishi wa Habari wengine mnaowazungumza siyo Waandishi wa Habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ndugu zangu hapa hasa wa Zanzibar, wametuletea maoni ambayo wanaomba pawe na ushirikiano wa karibu kati ya Vyombo vy'a Michezo Tanzania Bara na Visiwani na hasa mpira wa miguu. Sisi tumelipokea, Waziri mwenzangu mwenye dhamana ya michezo Zanzibar, Mheshimiwa Shamhuna, tumewasiliana na tunashauriana katika shughulil za michezo.

Mheshimiwa Spika, niseme hili toka kauli ya watu si kauli ya Wazanzibari, maana alisema mtu alienda kwenye magazeti akasema kuanzia leo *ZFA* hatutashirikiana na *TFF*, hatutashirikiana Bara na Visiwani. Nadhani nilimjibu kwamba, katika nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna hata mtu mmoja mwenye madaraka ya kutangaza kwamba ushirikiano wa Tanzania Bara na Visiwani basi. Nashukuru kwamba, wenyewe wameliona hilo; *ZFA* na *TFF* kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, watakuwa wanakutana mara mbili kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme, wakati mwingine haya mambo yanatiwa chumvi. Mimi natosheka kwamba, ushirikiano uliopo kati ya *ZFA* na *TFF* ni wa hali ya juu na nitatoa mifano; moja, *TFF* ndiyo mwanachama wa *FIFA*, ili wewe uwe Kamisaa katika michezo sijui wapi na wapi, *TFF* ndiyo inayopeleka ile orodha. Ndani ya orodha ile, wamo Wazanzibari shahidi Ndugu Hafidh Ali Tahir yeye ni Kamisaa, juzi ametoka kuzunguka katika nchi tatu kuwa Kamisaa wa mpira kwenye Mechini za Kimataifa. *National Team* kocha msaidizi ni Mzanzibari, wachezaji watano ni Wazanzibari na Daktari wa timu ni Mzanzibari. Anasimama mtu leo anasema timu ile siyo ya Taifa ni ya Tanzania Bara peke yake; yupo sasa huyo? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *TFF* wameomba Copa Coca Cola iwasaidie kuwadhamini, wakakubaliwa kuendesha Kombe la Taifa vijana wenye umri wa miaka 17 kwenda chini. Mikoa yote 26 Tanzania Bara na Visiwani, wameshiriki katika hayo mashindano ya Copa Coca Cola. Kuna ushirikiano gani zaidi ya huo; tufanye nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mimi ndani ya Chama changu cha CCM, tunaamini kauli ile wala si kauli ya Wazanzibari na ndiyo maana mimi kama Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, wala sikukosa usingizi. Nililala usingizi maana ninajua kuna ushirikiano wa hali ya juu katika vyombo hivi viwili; *ZFA* na *TFF*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la misaada ya *FIFA* inawezekana ndiyo inayotugonganisha vichwa; kama nilivyosema, *TFF* ndiyo mwanachama wa *FIFA* ili Wazanzibari wanufaikie na misaada ya *FIFA*, lazima andiko la mradi liwahusise Wazanzibari tangu mwanzo. Huwezi ukaandika andiko la mradi wa kuukarabati Uwanja wa Karume fedha zikaja ukasema hapana hizi tunazimega; nusu ya fedha hizo ziende Zanzibar na nusu ya fedha hizo zikarabati Karume. Watakapokuja waliota fedha watalamu kwamba, mmetumia fedha kinyume na zilivyotolewa. Tumewashauri *TFF* na wamekubali watakapoandika andiko la mradi sasa *to pay special attention* kwa Zanzibar ili na wao wanufaikie na misaada ya *FIFA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Suzan Lyimo, alizungumzia kukatika kwa hotuba ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu. Mimi ninampa pole kwa mkasa uliompata, lakini maelezo yametolewa. Ndugu zangu, tazameni Vyombo vyetu; *TBC* siku zote tunatolewa *live* wote; awe Mbunge wa CCM au Chama gani? Imetokea balaa siku hiyo moja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, mitambo iligoma tufanye nini na asubuhi wakamfuata wakamwambia mzee yale uliyotaka kuyasema jana ambayo tuliyakosa sema leo; je, baada ya pale wangefanya nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka kusema kwamba ni jambo ambalo limetokea; *TBC* hawakupenda litokee na Wizara hatukupenda litokee. Dawa ni kuwapa nyenzo *TBC*, wafanye kazi kwa ufanisi mawasiliano yasikatike mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Vazi la Taifa nadhani limetolewa maelezo na tumelieleza kwenye hotuba kwamba, sasa limepelekwa kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri kufanyiwa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la *Ze Comedy* nadhani limekwishatolewa maelezo, wameenda Mahakamani, Sheria za Utawala Bora zinataka jambo lililopo Mahakamani lisizungumzwe.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie sasa kuhusu ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili. Kweli sisi Tanzania ndiyo Makao Makuu au chimbuko la Lugha ya Kiswahili na zamani sisi wakati tunasoma, tuliamiwi Kiswahili Sanifu kwa Afrika Mashariki nzima ni kile kinachozungumzwa Zanzibar pale Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wamesisitiza umuhimu wa kutumia Lugha Fasaha, tunaliunga mkono hilo. Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Charles Mlingwa wamezungumzia juu ya kuchanganya maneno, Waingereza katika *literature* wanaita *code switching*, hii leo unasema unajua nilimwona jana *in the afternoon*, yaani unachanganya sentensi moja ya Kiswahili na Kiingereza. Tuliona wenye matatizo ya kuchanganya maneno ni sisi Wasomi tunaojua Kiingereza. Wale ambao hawajui Kiingereza, anapozungumza Kiswahili anazungumza Kiswahili mwanzo mpaka mwisho.

Kwa hiyo, tufanye nini? Tujitahidi na mimi ninafurahi kwamba, jambo hili limetokea ndani ya Bunge hapa. Maana ndipo tunapochanganya hata mimi na wewe na wengine tunachanganya changanya. Ushauri umetolewa na sisi tumeupokea na umetoka kwenu Waheshimiwa Wabunge kwamba, tujitahidi tunapozungumza Kiswahili, tuzungumze Kiswahili mfululizo bila kuchanganya maneno.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kupoteza maana. Katika fasihi zipo lugha unaweza kuzzungumza mahali fulani, lakini mahali pengine huwezi kuzzungumza. Ma-pilot wana lugha kwa Kiingereza wanasesma, *International Language of the Air*. Maneno tunayotumia sisi wakati mwingine si wanavyoyatumia wao. Ukienda katika sanaa wataalam wana lugha yao, wana-introduce wimbo wanasesma nyimbo hii imetungwa na fulani, imetiwa muziki na fulani na leo itaimbwa na fulani. Ukiangalia katika *dictionary* ukiwa mmoja unaitwa wimbo, zikiwa nyingi ndiyo zinakuwa nyimbo. Sasa kwenye taarabu ukiyaleta katika kikao rasmi, ndiyo tunawachanganya wasikilizaji wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilitaka niliseme hilo kwamba, imetolewa rai hapa kwamba, tujitahidi kusema vizuri Kiswahili. Vilevile imetolewa rai hapa kwamba, sisi Watanzania tuwe makini katika kuwafundisha majirani zetu Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema muda muafaka wa Watanzania kuifanya kazi hiyo ni sasa na tuanzie ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu zamani walikuwa wanasesma Kiingereza, lakini sasa wameingia Wanachama wawili ambao wanazungumza Kifaransa. Lugha gani inaweza sisi nchi tano kutuunganisha pamoja ni Lugha ya Kiswahili. Tunayo orodha ya watu wanaotaka kwenda kufundisha Kiswahili nchi za nje, lakini kama vile ambavyo mchezaji akienda nje ni lazima sisi turidhike maslahi yake kule ataishi namna gani; ndivyo tulivyofanya. Wameandikiwa wale wote walioomba watueleze maslahi, ili tusiwapeleke watu kule halafu ikawa kama tumewatelekeza.

Mheshimiwa Spika, lingine la Kisera; kuna watu wamehoji kwa nini *TBC* inakopa *NSSF*, mimi ninauliza kwa nini watu binafsi kukopa *NSSF* si biashara? Ile ni biashara, *NSSF* nina ushahidi wa kutosha, inakopesha watu wa aina zote ilimradi ametekeleza masharti yanayotakiwa kukopa zile fedha. Sasa hapa mimi kidogo ninaona mgongano wa mawazo au mgongano wa mtazamo; tumeambiwa fedha wanazopata *TBC* ni kidogo

sana, sasa ili wafidie hilo pengo wameamua kukopa na mkopo wenyewe hawajaupata; tunawaambia wasikope, lakini wakati huo tunataka *radio* isikike nchi nzima, wafanye nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kusema hilo kwamba, *TBC* wale wanakopa kama biashara, kama watu binafsi ambavyo tunakopa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie lile la usikivu wa *TBC*. Tatizo lililotufikisha Redio ya Taifa isisikike nchi nzima ni chombo hiki cha utangazaji kutotengewa fedha za kutosha kila mwaka, si kwamba Serikali haitaki kuwatengea fedha; ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, nataka nilishukuru Bunge lako Tukufu, kupitia Kamati yetu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, tulipeleka kilio tumepata fedha mwaka huu. Mimi nina uhakika, mkitupa tena mwakani angalau shilingi bilioni sita, tukafunga mtambo wa *FM* kila Mkoa na zipo Wilaya nyingine kubwa, ipo Mikoa mingine mikubwa ambayo ukifunga *FM* Makao Makuu ya Mkoa bado Wilaya nyingine hazisikiki. Kwa jiografia yangu ya Tanzania, Mkoa unaoongoza kwa ukubwa sasa baada ya Arusha kugawanyika ni Mkoa wa Tabora halafu unafuata Mkoa wa Rukwa.

Sasa hatutegemei kufunga mitambo ya *FM* Tabora Mjini ikasikika mpaka kwa Mheshimiwa James Lembeli, sijui na kwa nani na nani. Tukipata fedha za kutosha, tutaondoka sasa pale Makao Makuu ya Mkoa kwenda Wilayani ili katika nchi hii watu wapate kuhabarishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mkakati tuliojiwekea, tumepunguza mwaka jana Mikoa karibu tisa, tumefunga mitambo na mwaka huu wa fedha tutafunga mitambo katika Mikoa mingine kumi kama Waheshimiwa Wabunge mtapitisha hoja iliyopo mbele yetu na mimi ninaomba muipitishe ili watu wapate kusikia *radio* na kuona *TV*.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Omar Kwaang' alichangia na pale nilipokuwa nataja majina nilimruka, kwa sababu shughuli imekuwa haraka haraka na Waziri mwenyewe anajifunza. Kwa hiyo, namwomba radhi kaka yangu kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida, ameleta karatasi jioni hii wakati tunafunga. Kwa hiyo, nadhani wamepishana na walikuwa wanaorodhesha. Mheshimiwa Godfrey Zambi nimemtaja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, wazungumzaji tungewataja mmoja mmoja walikuwa wengi sana. Ahadi ya Wizara yangu ni kwamba, zile hoja zote alizozijibu Mheshimiwa Naibu Waziri na nilizozijibu mimi, tutakwenda kuziweka katika kablasha maalumu tuwapelekee Waheshimiwa Wabunge wote ili wapate majibu sahihi kwa yale yote ambayo wamechangia wakiwa hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo nakushukuru sana kwa majibu hayo. Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni ya kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2008/2009, imetolewa na imeungwa mkono. Ila kwa utaratibu wa kanuni zetu, ipo hatua inayofuata ambayo tutaipitia kabla ya kufikia mwisho wa hoja hiyo. Katibu kwa hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 – *Administration and General Sh. 1,252,914,400*

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo katika ukurasa wa 20, napenda ninukuu inasema ifuatavyo:-

“Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM imesisitiza azma ya Serikali ya kuendeleza, kuenzi na kulinda historia, mila na desturi nzuri ya watu wetu na kuzitokomeza mila na desturi mbaya. Hivyo basi, Wizara yangu kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Utamaduni, ina wajibu wa kukuza na kuendeleza utamaduni.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya karibuni, yamezuka mashindano ya urembo tena kwa kasi kubwa sana na washindi wanazawadiwa zawadi nzito kama magari, fedha taslimu na vivutio kadha wa kadha. Nimejaribu kufanya utafiti kuona kama utamaduni huu unawasilisha labda kabilia fulani hapa Tanzania au Mkoa fulani, lakini sikupata jibu la hilo. Hili ninaloliona ni kwamba, utamaduni huu unawadhalilisha dada zetu hasa kwa vivazi vyao. (*Makofi*)

Napenda nipate ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri; je, utamaduni huu unatoa mafunzo gani kwa vizazi vyetu vya leo na kesho na kweli hii ndiyo azma hasa ya Ilani hii ya CCM iliyosomwa hivi sasa?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru ndugu yangu, kwa hoja yake. Kama nilivyosema, watu katika kuchangia hoja hiyo wameisema asubuhi, lakini pengine hatukupata muda wa kupitia vifungu vyote. Ahadi ya Wizara ni kwamba, tutahakikisha kwamba, yale yanayoonyeshwa katika mashindano, yanaendana na mila na desturi za Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulifanya hilo, Serikali itazingatia kwamba, nchi hii ni ya vijana na wazee. Wapo vijana ambao kama alivyosema Mheshimiwa pale

wanaweza wasimuelewe, kwa hiyo, ahadi ya Wizara ni kwamba, tutajitahidi tuwe katikati, tusiwaudhi vijana wala wazee. (*Makofî*)

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Fungu hilo hilo la 96. Nilitaka nipaye ufanuzi tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Hivi karibuni vyombo vya Habari hasa magazeti, yaliwaonyesha waandishi wa habari, wana habari maarufu kabisa wa siku za nyuma; ndugu yetu mmoja Godfrey Mwafongo, halafu na Mshindo Mkeyenge, walikuwa wanaonyesha kabisa kwamba, hali zao siyo nzuri na ilimaanisha kwa watu waliosoma yale magazeti kwamba wametelekezwa. Saa nilitaka nipaye ufanuzi; je, Wizara katika Sera ya Wizara ni kweli watu kama hao huwa wanatelekezwa na Wizara? Nashukuru.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyowakuta ndugu wawili aliowataja ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Sigonda, yanafanana na wastaa fu wote wa nchi hii si waandishi wa habari peke yake; na ndiyo maana imetolewa rai na Waheshimiwa Wabunge kwamba, endapo mtu anastaafu, mishahara ya Serikali ikipanda na wale waliostaafu nao watazamwe ili kiinua mgongo wanachopata kila mwezi kipate nyongeza. Tukilifanya hilo kwa watumishi wote wa umma waliostaafu, tutakuwa tumetatua tatizo hilo. (*Makofî*)

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nilikuwa nataka ufanuzi kidogo tu katika eneo la Idara ya Utamaduni, wakati Sekretarieti ya Mkoa ilipovunja Utamaduni katika Sekretarieti hii, Idara ya Utamaduni ilihamia katika Halmashauri za Wilaya, baada ya hapo ikawa inatambulika kama ni Idara; lakini hivi sasa inaonekana ni Idara ya Utamaduni kama Kitengo ndani ya Idara ya Elimu. Sasa mimi nataka kujua hali halisi; sasa hivi Idara ya Utamaduni ni Kitengo au ni Idara kama ilivyokuwa hapo awali? Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nimeulizia kuhusu suala la Kijiji cha Michezo katika Halmashauri ya Temeke. Kijiji hiki kilianza muda mrefu mimi nikiwa bado msichana, sasa hivi nimeshazeeka, lakini mpaka sasa hivi naona majengo yapo vile vile na hali bado ipo vile vile. Ningependa kujua, Wizara inatueleza nini kuhusu Kijiji cha Michezo ambacho kipo katika Wilaya ya Temeke? Ahsante. (*Kicheko*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitalijibu lile la kwanza, la pili atanisaidia Naibu Waziri. Ni kweli kwamba, kule Wilayani, Idara ya Utamaduni ipo pamoja na Idara ya Elimu kama vile ambavyo Afya na Maji wapo pamoja. Ule ni muundo tu. Kwa hiyo ni kweli unavyosema kwamba, Utamaduni ni Kitengo katika Kamati ile.

Tatizo sasa linalofanya ufanisi usiwepo kule Wilayani, siyo kuchanganywa na Idara ya Elimu, tatizo linakuwepo kwa sababu Idara ya Utamaduni haina Kasma ya kuendeshea shughuli zake na tumeahidi hapa na Waziri Mkuu ameagiza, Halmashauri zote kuhakikisha zinatenga fedha ili kuwawezesha Maafisa Utamaduni kufanya kazi zao vizuri. Ule muundo uliopo sasa ni wa kiutawala tu, hauna maana ya kwamba, Idara moja ni muhimu kuliko nyingine.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la pili la Mheshimiwa Mwanawetu.

Amezungumza kwamba, kuna Kijiji cha Michezo kimeanza muda mrefu pale Wilaya ya Temeke. Kijiji kile Serikali baada ya kupata ushauri wa wataalam ni kwamba, majengo yale mkandarasi yule hakujenga katika *standard* inayohitajika au kiwango kinachohitajika. Kwa hiyo, yale majengo sasa hivi hayastahili kuwepo na bahati nzuri katika huu mradi wa pili wa kujenga Kiwanja Changamano, *Phase Number II*, eneo lote lile yale majengo yote yanabomolewa. Kwa hiyo, Kijiji cha Michezo kipo pale pale, kitajengwa katika *phase* hii ya pili na kitakuwa na mahitaji yale ambayo yalikuwa yanahitajika. Bahati nzuri, pale sasa zaidi ya Kijiji cha Michezo, panajengwa pia na hoteli ya kisasa ambayo itachukua watu 750 ikiwa na *Five Star*, yaani nyota tano. Kwa hiyo, kijiji kipo kinaendelea, lakini majengo hayo Serikali imekataa kuwepo pale kwa kuwa hayafai.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani, tuligusia suala zima la ubadhifuru katika suala la michezo nchini, ambalo kwa sasa limekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vyombo vya michezo hapa nchini, pamoja na kusimamia michezo, vimekuwa vinajihuisha katika miradi mbalimbali ili kuongeza kipato katika vyama hivi vya michezo. Kadhalika kumekuwa na malalamiko makubwa kwamba, fedha inayopatikana katika Miradi ya Michezo, imekuwa inaliwa na wajanja wachache. Sasa je, Serikali ipo tayari kufanya ukaguzi maalum (*special audit*), kwa miradi hii ya vyama vya michezo na kuwachukulia hatua wale wote ambao wamehusika katika kutafuna pesa hizi ili kuondoa manung'uniko kwa wanamichezo? Naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kumjibu Mheshimiwa Jecha, swali lake la ubadhifuru kwenye vyama, pamoja na vilabu mbalimbali kama ifuatavyo:-

Anachokizungumzia ni kweli kwamba, kuna baadhi ya vyama na vilabu ambavyo vina matatizo ya uhifadhi wa fedha. Kama unavyofahamu, katika Sheria ya Baraza la Michezo, yupo Msajili wa Vyama ambaye ana jukumu la kukagua vilabu inapotokea matatizo. Suala hilo analolizungumzia limeshaanza na limeanza na *TFF*, nadhani sote ni mashahidi kwamba wamefanya *special auditing* kwa viongozi waliopita na ikigundulika kwamba wamehusika na ubadhifuru sheria itachukuliwa. Tunajaribu kukiimarisha Kitengo chetu cha Msajili ili suala hili lifanyike sasa ili kukomesha tabia hiyo ambayo inaendelea katika nchi yetu.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango, nilomba katika jitihada za kuboresha *TBC*, nipate maelezo kuhusu hali ya majengo pale Mikocheni, ambayo kwa muda mrefu sana yametelekezwa. Bahati mbaya sasa majengo haya yamepotea kwenye vitabu nya hotuba ya Wizara kwa muda mrefu. Kuna mambo mengi yanahusiana na majengo haya, ikiwemo wale waliojenga kule nyuma, hatujui ni nini kimeendelea. Tulitaka kupata maelezo nini kinaendelea na kwa kuwa gharama zinapanda kila siku na watumishi wetu pale *TBC* hawana Ofisi, wanafanya kazi kwenye mazingira magumu; je, kuna mkakati gani ambao unalenga kukamilisha yale majengo na wale waliohusika wamechukuliwa hatua gani?

Swali la pili, nilikuwa nimeuliza vilevile kwamba, nimepitia kwenye kitabu cha Waziri, katika kuangalia majukumu ya *TCRA* nikakuta kwamba, hayana uhusiano na mambo ya ujenzi wa barabara. Sasa nikawa nimeuliza, kuna taarifa kuhusu fedha zilizochukuliwa *TICRA* ambazo zimekwenda kwenye ujenzi wa barabara. Nikataka kwanza nipate uhakika kama taarifa hizo ni kweli; je, utaratibu wa fedha za Serikali unaruhusu na Serikali inasema nini kuhusu utaratibu huu kwa vile huko nyuma tuliruhusu mambo ya namna hii na mashirika yakafa; sasa Serikali inatoa kauli gani na kama ni kweli taratibu hazikufuatwa; je, zitarudishwa lini hizo fedha zilioenda barabarani kwenda kwa *TCRA*?

MWENYEKITI: Sijui hili la pili, Mheshimiwa Waziri maana yake Wizara inayoisimamia *TCRA* hasa ni Wizara ya Mawasiliano. Hebu anza na hili la kwanza, kama unaona inafaa.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilitaka nimjibu hivyo hivyo kwamba, mimi si Waziri wa Barabara wala ile *TCRA*, wapo Mawaziri wanaohusika pengine Mheshimiwa atanipatia nafasi siku yake. Kwa hiyo, naomba radhi kwamba, kwetu sisi mahusiano yaliyopo baina ya Wizara yangu na *TICRA* ni kwamba, ipo Kamati inayoitwa Kamati ya Maudhui (Kamati ya *Content*). Sheria inamruhusu Waziri wa Habari, kuteua Wajumbe wa kuketi katika Kamati ile ya Maudhui, wao ndiyo wanaskiliza malalamiko; tumeonyesha picha mbaya, sijui za kutisha, fulani amenitukana. Hayo tu ndiyo mahusiano ya Wizara yangu na *TICRA*. Kwa hiyo, nilitaka nijibu hilo.

Pili, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa kuonyesha kusikitishwa kwake na majengo ya Mikocheni yaliyokaa muda mrefu bila kukamilika. Nimeeleza pale tatizo ni kutotengewa fedha. Mwaka huu *TBC* wamepewa shilingi bilioni nne, kikubwa zaidi tumeona badala ya kuanza kushughulika na majengo kwanza, nchi nzima watu wasikie redio.

La tatu, tumefanya mazungumzo na chombo fulani cha fedha, yaliyosimamiwa na Kamati yetu ya Maendeleo ambayo yalihusisha Wizara ya Fedha, *NSSF*, *TBC* na Wizara. Malengo tupate mkopo kama wanavyokopa wengine, tukamilishe majengo yale, tukarabati yale yaliyoharibika ili majengo yawe katika hali nzuri kwa kiwango ambacho anakipenda ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Slaa. (*Makofii*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri kwa jitihada. Mimi naelewa ni tatizo la fedha, lakini nilitaka kujua ili fedha za Serikali zisipotee, haya majengo kuna waliosababisha yakafikia hapo. Sasa tulitaka kujua nini kinaendelea; je, walipelekwa Mahakamani, kwa sababu ilikuwa ni suala la mikataba lakini vile vile hata vifaa, sasa *TBC* inahangaika lakini tuna kitu? Inawezekana wamepelekwa Mahakamani, lakini kwa kuwa hatukupewa taarifa, Bunge hatujui. Kwa hiyo, tulitaka kujua ni kitu gani kinaendelea na tungependa kuyaona haya kwenye rekodi zetu ili tuweze kufuatilia kila wakati. Nashukuru Mwenyekiti.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Maelezo ya ziada Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba, kwa taarifa tulizozikuta Wizarani, muda mrefu Serikali haikutenga fedha za kuendeleza majengo yale. Kwa kutaka kuweka mambo yawe sahihi zaidi, namwomba ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Slaa, anipe muda niende Wizarani. Anataka kujua nini kilitokea, tutalifanya kazi tutamwandikia kwa maandishi.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwwenyekiti, nakushukuru. Nina suala moja tu linalohusiana na mjadala wa kuhusiana na jinsi gani ya kuweza kuendesha vyombo vya umma (*Financing Public Co-operations*).

Nataka kukubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba ni kweli kuwa taaluma ya waandishi wa habari imevamiwa na wasio waandishi, lakini kama ambavyo taaluma nyingine nyingi tu zilivyovamiwa, hata siasa imevamiwa na wasio wanasiaya.

Kwa hiyo, tusiwe wa kwanza kuwaonyeshea vidole waandishi wa habari na sisi wenyewe ni hivyo hivyo. Mimi nataka kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba ni kweli kuna shule za serikali na za binafsi. Kuna hospitali za serikali na za binafsi, lakini Wizara ya Elimu inazipa ruzuku shule zote za serikali na za binafsi. Hospitali binafsi zinapewa ruzuku na Wizara ya Afya kama KCMC hivi, lakini hakuna ruzuku inayotoka Wizara ya Habari kwenda chombo cha habari binafsi. (*Makofii*)

Ndiyo maana mwaka jana tukashauri na Waziri aliyejkuwa Waziri wa Habari, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatibm akakubali kuanzisha mjadala wa kuona ni jinsi ambavyo tutaweza ku-*finance public broadcasters* kwa sababu ni mambo mawili; *public broadcaster* ama achukue fedha asilimia 100 kutoka Serikalini au asijilingize katika biashara au afanye biashara asipate pesa za walipa kodi, kwa sababu ni suala la *principle* tu na lazima tu-*change attitude* kwa sababu tumeruhusu *private sector*. Kwa hiyo, nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri aniambie yuko tayari tuingie katika mjadala huu ili tuweze kuweka *fair play* ya uendeshaji wa vyombo vya habari vya binafsi na vya umma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru ndugu yangu, Mheshimiwa Zitto, kwa swali lake zuri. La kwanza, alikuwa ananifahamisha na mimi naomba nimfahamishe; hospitali zinazopata ruzuku ya Serikali ni zile zinazoitwa Hospitali Teule, kwa Kiingereza wanaziita *Designated Hospital*.

La pili, amezungumzia juu ya kuanzisha mjadala. Tumeeleza asubuhi, tunaandaa Muswada tutauleta hapa, hautapita bila Waheshimiwa Wabunge kujadili na kuweka mawazo yao mapya mle ndani. Kwa hiyo, namwomba ndugu yangu, Mheshimiwa Zitto, asubiri tutakapoleta Muswada. Nakiri kama alivyosema, kuendeleza mjadala muda wowote, bahati nzuri mimi na yeye tunazungumza vizuri; yeye Mbunge na mimi Mbunge, lakini tuna cheo cha ziada hapa ndani. Yeye kwake kule Naibu Katibu Mkuu wa Chama na mimi Naibu Katibu Mkuu wa Chama, hatuna tatizo la mawasiliano. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasiliana ili yale mazuri tuweze kuyaweka hapa.

Mwisho kabisa, haya masuala ya vyombo vyta utangazaji vya umma, inawezekana pengine tunayoambiwa sivyo yalivyo. Nilipelekwa Marekani kwenda kusoma, juzi juzi hapa tumeambiwa Sauti ya Amerika imewekwa pale na Serikali ya Marekani, kazi yake ni kutangaza mambo mazuri ya Marekani nchi za nje. Inalipiwa asilimia 100 na Serikali ya Marekani na yenewe ipo chini ya Wizara ya Nchi za Nje ya Marekani siyo Wizara ya Habari. Kwa hiyo, tunavyozungumza habari ya serikali kujitoa kabisa, hapana tutafika huko, lakini inawezekana ni mapema mno.

MWENYEKITI: Nadhani itabidi nifuate utaratibu ambao tumekwisha ukubali wa hoja ni mara moja tu, kwa sababu inatoa fursa pana na ninajua Mheshimiwa Zitto ni mwanademokrasia, bila shaka hatapenda kuweka ukiritimba katika muda wa kuchangia. Kwa hiyo, nahamia huku Mheshimiwa Godfrey Zambi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nina mambo mawili kwa ufupi sana. La kwanza, kwenye mchango wangu nilisema kwamba, kuna usikivu hafifu sana wa redio karibu Wilaya nzima ya Mbozi. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwenye taarifa yake anasema kwamba, imefungwa mitambo mipya ya redio pale Mbeya sehemu ya Iwambi, ambako kuna Kituo cha Redio Tanzania, mitambo ya FM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, bahati mbaya sana, nimezungumza kwenye mikutano kule vijijini na hususan Tarafa ya Igamba, pamoja na Kata ya Ihanda na baadhi ya Iyura na sehemu ya Kata ya Nyimbili; redio hii inasikika kwa uhafifu mkubwa sana na ndiyo chombo pekee ambacho wananchi wanakitegemea sana kupata habari muhimu za taifa, kwa mfano, habari za Bunge tunazozizungumza hapa ndani. Sasa pamoja na kufungwa hiyo mitambo, lakini kuna matatizo hayo. Hebu naomba Mheshimiwa Waziri, atufafanulie tatizo linaweza likawa nini na mtatusaidiaje kule Mbozi ili tuweze kusikiliza vizuri zaidi haya mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri hapa alipokuwa anazungumza ...

MWENYEKITI: Ni moja tu; tunakwenda na moja tu sasa. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru ndugu yangu, Mheshimiwa Zambi kwa swali lake zuri. Tumeeleza katika hotuba yetu ya bajeti na jioni hapa wakati nakamilisha mjadala kwamba, tunaanza kwanza kufunga mitambo kila Makao Makuu ya Mkoa na ile Mikoa mikubwa Mbeya ikiwemo, kuna uwezekano wa kufunga mitambo Mbeya isifike katika Wilaya zote kulingana na upatikanaji wa fedha, hatua itakayofuatia ni kufunga mitambo katika Wilaya zile ambako redio haisikiki. Lile alilolisema kama mitambo imefungwa na kama haifanyi kazi, basi hilo nimelichukua. Nitawatuma wataalam wangu waende Mbeya wakaangalie nini tatizo.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nina suala dogo tu la kutaka ufanuzi. Katika michango ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, yapo masuala yameelezwa sana kuhusiana na suala la upungufu wa viwanja vya michezo, ambalo linaleta shida na hasa kuweza kuifikia hii Sera ya Michezo nchini.

Nilikuwa nataka nizungumzie kitu kimoja, kutokana na uhaba uliopo huu wa viwanja, lakini zipo taasisi na hata vyama vya siasa vina viwanja vyake havijakamilika. Je, Wizara haioni kuna sababu sasa ikashirikiana na zile taasisi au vile vyama ambavyo vinamiliki viwanja, kwa mfano, Chama cha Mapinduzi Mkao wa Singida kina Kiwanja cha Kumbukumbu ya Namfua ambacho hakijakamilika na Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Iramba kina Kiwanja cha Lulumba ambacho hakijakamilika ili wakikamilishe tuweze kutimiza hiyo Sera ya Michezo nchini? Ahsante.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, tunavyo viwanja mikoani ambavyo vinamilikiwa na watu binafsi, mashirika na vyama vya siasa. Mimi kama Waziri wa Michezo, nianze kwa kuwapongeza hao wanaomiliki viwanja maana wamewezesha viwanja kuwepo. (*Makofi*)

La pili, wale wanaomiliki viwanja wanalo Baraza lao la Wadhamini au wana makampuni yanayomiliki vile viwanja. Ningetoa ushauri, endapo kuna Mkao wowote ambao unaona kwamba kiwanja chao kinahitaji kukamilika kama kule Singida kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Juma Killimbah, nashauri mkae na wamiliki wa vile viwanja, mtazame nini mkifanye katika Mkao wenu kuweza kuboresha kiwanja hicho kama ni kuingia ubia na wafanyabiashara au vipi, vinginevyo itakuwa vigumu sana kwa serikali kusema itaweza kukamilisha viwanja katika Mikoa yote.

MHE. MARTHA M. MLATA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi pia naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, wakati nachangia nilikuwa nimezungumzia suala la mikataba ya wasanii na nikahuisha *COSOTA* na Wizara yake, kwa maana ya kwamba, *COSOTA* ipo Viwanda na Biashara lakini bado wasanii wapo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati anajibu kuhusu *COSOTA*, alitoa wito kwamba wasanii waende wakajiunge kule. Bado sijaridhika na majibu hayo, kwa sababu wasanii

hawa tunaowazungumzia sio wasanii walioko Dar es Salaam ni wasanii wa Tanzania nzima na *COSOTA* ipo Dar es Salaam. Nataka kujua Wizara hii imejipanga vipi? Kwanza, ilitoa mapendekezo kwamba chombo kama *COSOTA* kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara bado kinahujumu hata Wizara yake pia kuweza kusimamia vizuri haki za wasanii hao. Sasa ukitangaza wasanii waende *COSOTA*; *COSOTA* ipo Dar es Salaam, mtu wa Kiomboi, Ndago kule hajui hata *COSOTA* ni kitu gani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufanuzi zaidi. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kumjibu Mheshimiwa Mlata, swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, *COSOTA* ipo Wizara ya Viwanda na Biashara. Ni utaratibu ambao Serikali iliuweka kwa sababu *COSOTA* imeingizwa kwenye makundi ya makampuni na ni kawaida makampuni yote yanjasajiliwa kule kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara. Si hilo tu, utaona hata hizi *NGOs* zote zimesajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini ni *SACCOS* zimesajiliwa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani badala ya Ushirika.

Kwa hiyo, ni utaratibu ambao Serikali imejiwekea. Cha msingi hapa ambacho nakubaliana naye ni kuiimarisha *COSOTA* ili ijitanue zaidi katika kwenda Mikooani mpaka Wilani ili wasanii walioko katika Wilaya nao waweze kufaidika. Kwa sasa hivi, ndio chombo pekee ambacho tunakitegemea na Sheria imeundwa, kwa hiyo, mpaka tuingie ndani ya Bunge humu tubadilishe tena ije kwenye Wizara yetu. Kwa sasa sheria ya *Copy Right Society of Tanzania* ipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara; ni kuipanua na kuipa fedha nyingi ili angalau iweze kusaidia wasanii Wilayani na Mikooani. (*Makofii*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi, niliishauri Serikali kuhusu timu mbalimbali za michezo zinapopata nafasi kwenda kutuwakilisha nchi za nje, ziwe zinaondoka zikiwa chini ya dhamana ya serikali. Nilisema hivyo kwa sababu kuna timu zinaondoka hapa za watu binafsi, unakuta mtu anatumia timu kufanya biashara zake. Kwa mfano, timu ya ndondi, juzi imeondoka yenye matokeo yake wamekuja kukamatwa na dawa za kulevya. Sasa hiyo inakuwa sio kashfa ya timu bali ni kashfa ya nchi. Kwa hiyo, ninaomba timu hizi zinapoondoka ziwe chini ya serikali na zifuate taratibu zote za Serikali ili kuepuka mambo haya yanayojitokeza. Naomba Mheshimiwa Waziri, anipe ufanuzi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ingawa tamaa ni tamaa tu, hawa wenye tamaa huwa hawajali chochote hata ukiwapa asilimia mia moja watatumia mbinu nyingine. Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu dada yangu, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli timu zote zinazokwenda kuwakilisha Taifa nchi za nje, zinapaswa kwenda chini ya usimamizi wa Serikali na ndivyo walivyokwenda wale. Najua anazungumzia watu wa Mauritius waliokamatwa na dawa kule. Serikali imewasaidia kuwaweka kambini, walikuwa na matatizo ya fedha, nikaitisha kikao ofisini kwangu tukakutana na watu wa *Tanzania Olympic Committee* na watu wenyewe wa ngumi, tukawatafutia fedha za kuwaweka kambini tukahakikisha wamesafiri, lakini kama ulivyosema, sisi tumesafirisha tukiamini hawa ni wachezaji wanakwenda kushiriki kumbe wameficha. Kama ni kweli, hata huyo mwenye mali tunaambiwa alibaki huku nyuma, hatutaki kuendelea zaidi kwa sababu nalo liko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, ni kweli watu wanaokwenda kutuwakilisha nchi za nje, wanakwenda kwa dhamana ya serikali na ndio maana panakuwa na shughuli maalum ya kuwakabidhi Bendera ya Taifa.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba ninukuu kifungu cha 4(3), ukurasa wa 15 wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba, masuala ya michezo si ya Muungano. Baada ya kunukuu kifungu hicho, ndio kinanipelekea kusema kwamba *TFF* na *ZFA* sio vyombo vya Muungano. Nilichotaka kulihakikishia Bunge hili ni kwamba, *TFF* na *ZFA* ni vyombo vyenye ushirikiano wa hali ya juu sana katika mpira wa miguu hapa Tanzania.

MWENYEKITU: Mheshimiwa Hafidh, hebu rudia hicho kifungu cha Katiba nikione.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 15.

MWENYEKITU: Ni Ibara, sio kifungu.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 4(3), mambo yasiyokuwa ya Muungano.

MWENYEKITU: Nimeona, endelea.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa hiyo, ndio kama ninavyosema kwamba, *TFF* na *ZFA* ni vyombo vyenye ushirikiano mkubwa. Nikubaliane na Mheshimiwa Waziri, katika maelezo aliyyoatoa hapa kwamba, hivi karibuni, yaani juzi tu, vyombo hivi vilikutana vikafanya mazungumzo. Katika mazungumzo haya, iliundwa Kamati ya watu wanane, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ni Mjumbe kutoka Zanzibar, anaitwa Hafidh Ali Tahir.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndio Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Ushirikiano baina ya *TFF* na *ZFA*. Ninachotaka kusema, katika mchango wangu nimewomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu mambo haya sio ya Muungano na *TFF* kuitia *FAT* ya zamani, hivi sasa imeshafanya kazi miaka 40, imeshaiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania miaka 40 bila ridhaa ya Zanzibar. Kwa hiyo, nilichokuwa ninamwomba ni

kwamba, tuunde Chombo cha Kitaifa cha Mpira wa Miguu Tanzania, kwa sababu mambo ya michezo Tanzania sio ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar wana Wizara yao ya Michezo na Muungano una Wizara yake ya Michezo. Sasa hapa tunapotaka kuunda kitu cha kitaifa, basi tuunde kitu kimoja ambacho kitasaidia katika kuendesha michezo na hii sio kwa mpira wa miguu tu, ni popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano huu umekuwa kwa muda mrefu, lakini ni nini kinachojitokeza? Kinachojitokeza pale, mmoja alipochukua hati miliki ya kufanya mambo peke yake hapo inaleta ugomvi na katika urafiki mzuri, unapokuwa na mwenzio mzuri mnasikilizana, unapofika mahali siku moja kaja nyumban ihuna viatu yeye kavaa buti, akikukanyaga kama humpendi huyo mwambie umenikanyaga. Kitu kilichofanyika sasa hivi, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa hili aunde chombo kitakachowenza kuendesha mpira wa miguu Tanzania. *TFF* wafanye shughuli zao Bara; Zanzibar wafanye shughuli zao Zanzibar, ili vitu hivi baadaye tuviweke katika hali ya kitaifa, tuwe na chombo ambacho kinatuongoza kwa pamoja.

MWENYEKITI: Dakika zako zimeisha na zimebaki dakika kumi sasa kufikia muda wa kuahirisha Bunge. Kwa hiyo, naitumia Kanuni ya 104(1) kuongeza muda usiozidi dakika 30 ili tuweze kuendelea. Kwa hili alilouliza Mheshimiwa Hafidh Ali, nalitolea *rulling*; haya ni moja ya matatizo ambayo nadhani kwa ushauri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi lipelekwe likajadiliwe na Wanasheria Wakuu, Waziri mmoja hawezikujibu kuhusu hili.

Tunaendelea, kwa sababu ni yale yale inawezekana kwamba, liliachwa na lilitakiwa liwe katika mambo ya Muungano, ndio haiwezi kuwa upande mmoja tu. Mheshimiwa Mohammed Rajab. (*Makofit*)

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimeshtushwa sana na Mheshimiwa Waziri, alipoeleza kwamba, wana mipango siku za mbele kukutana na Zanzibar, kwa ajili ya kuendeleza michezo. Hii inaonyesha dhahiri, walipoamua kupeleka mchanganuo wa kutengeneza viwanja vya michezo ndio maana wakaamua kutengeneza Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Karume bila kuujali uwanjwa ulipo Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii dhahiri na imenipa mashaka sana, kumsikia leo Mheshimiwa Waziri, ana mipango ya baadaye kupeleka michanganuo kwa kukaa pamoja. Kwa nini hapo mwanzo wasikae pamoja na inaeleweka dhahiri kabla ya uwanja huu mpya, uwanja ulio mzuri Tanzania ulikuwa ni Uwanja wa Amani. La kushangaza sana ni kwamba, haukufanyiwa ukarabati, ndio pengine utakuwepo katika mipango ya baadaye. Mheshimiwa Waziri, haoni hii ndio sababu inayosababisha hii migogoro midogo midogo ya ZFA na *TFF* au ndicho kilichomsukuma aweze kuweka mipango ya baadaye?

MWENYEKITI: Aah, sijui Mheshimiwa Waziri, maana yake unajua upande mmoja baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar, wanasema masuala ya michezo ni ya Zanzibar tu, halafu hapohapo inadaiwa kwamba yangepata fedha zote za msaada;

dola 200,000 utajenga *stadium* kweli tukigawana? Labda Waziri, una la ziada, kwa sababu tusipotatua tatizo la msingi hapa kwamba haya ni ya Muungano ama sio ya Muungano tunabaki pale pale. Nadhani tubaki kwenye *rulling* yangu ili tuendelee vizuri, yatazidi kutubabaisha tu, watu makini huwa wanatatua tatizo la msingi halafu haya mengine yote yanakuwa mepesi. Mheshimiwa Grace Kiwelu. (*Makofi*)

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala la Joseph Kaseba, kijana ambaye ameweza kuliletea heshima Taifa letu la Tanzania kwa kuweza kuleta mikanda miwili ya dunia katika nchi yetu. Kijana huyu katika mashindano haya ni yeze peke yake aliweza kuomba misaada na kuweza kushiriki mashindano hayo na mwezi ujao kijana huyu anatakiwa kwenda Japan. Je, Wizara inamsaidiaje kijana huyu?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Swali alilouliza Mheshimiwa Grace Kiwelu; mchana huu nimekutana na kijana wetu Joseph, amenieleza matatizo yake ya kutaka kwenda Japan, tumesema serikali itamsaidia kwenda. (*Makofi*)

MWENYEKIDI: Nadhani na kumtunza huko. Basi Mheshimiwa James Lembeli. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kupata ufanuzi juu ya uhusiano wa kiutendaji uliopo baina ya Kurugenzi ya Habari Ikulu, Ofisi ya Mwaandishi wa Habari wa Rais na Idara ya Maelezo; ni nani hasa kwa mujibu wa sheria ni msemaji wa Serikali na kama sheria hii kweli inafuatwa katika muundo huu? Ahsante.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwenye hotuba yangu nimelieleza, wala hakuna mgongano. Yule wa mwanzo anaitwa Mkurugenzi - Mawasiliano Ikulu, kazi yake ni kutangaza habari za Ofisi ya Rais na shughuli za Ikulu, yeze ndio Msemaji wa Ikulu. Idara ya Habari Maelezo, ndio msemaji wa Serikali, ndio maana watu wakileta maswali katika tovuti, yanaletwa kwetu katika Idara ya Habari na sisi tunayapeleka katika Wizara zinazohusika tunapata majibu tunawapelekea watu wanaohusika. Kwa hiyo, hakuna mgongano wowote wa utendaji kazi kati ya ofisi hizi mbili. (*Makofi*)

MWENYEKIDI: Mheshimiwa Lembeli, utaratibu mpya ni kwamba, ukishauliza basi. Kwa hiyo, niwie radhi, naendelea. Mheshimiwa Idd Azzan.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi, niliomba ufanuzi kuhusu Sheria Namba 12 ya Baraza la Michezo la Taifa, ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 1971. Katika Sheria hiyo, moja ya mambo ambayo Baraza la Michezo linatakiwa kusimamia kwa mujibu wa Sheria hiyo ni kuendeleza na kustawisha michezo ya ridhaa. Kwa hali halisi ilivyo hivi sasa, michezo hiyo ya ridhaa ambayo tunaizungumzia ambayo inasimamiwa na Baraza, imeshabadilika. Mingi imekuwa ni ya kulipwa, sijui Wizara ina mpango gani;

haioni kama Sheria hii inakingana na hali halisi ilivyo hisi sasa; kwa sababu mionganini mwa vilabu ambavyo vinacheza ligi kuu, wachezaji wake wanalipwa mishahara lakini hata wanaposajili huwa wanasa jiliwa kwa mikataba na kwa kulipwa? Wizara haioni kwamba, Sheria hii hivi sasa imepitwa na wakati na ipo haja ya kuifanyia marekebishi? Naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kumjibu Mheshimiwa Azzan kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza kwamba, Sheria hii ni ya siku nyingi; ni kweli ni ya toka mwaka 1971, Sheria Namba 12 ya Baraza la Michezo. Sasa hivi baada ya Serikali kuliona hilo, tumeshaanza mchakato kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata, Wilaya na Mkoa. Tumeshapata maoni ya kutosha, tunangojea sasa maoni katika hatua ya juu ya kitaifa ili tuweze kuiboresha Sheria ile iendane na wakati wa sasa. Nataka nimirambulisha kwamba, wanamichezo wetu wengi bado ni wa ridhaa. Vijijini na maeneo yote ni wachezaji wachache sana amba ni wakulipwa katika miji. Tatalizingatia hilo na bahati nzuri tutakapoitunga Sheria hiyo, italetwa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge, wanawenza kuchangia zaidi kuiboresha. (*Makofii*)

MWENYEKIDI: Ahsante, naomba nieleze tu kwamba, tulipoanza nilitoa fursa ya Waheshimiwa Wabunge, kuiliza ufanuzi wa nyongeza. Nilikuwa na matumaini kwamba, kwa kuwa ni 13 tu tungweza kumaliza, lakini imenibidi nirudi kwenye utaratibu unaoitwa *precedent* ili twende vizuri. Kwa hiyo, sio kwamba wale niliwapendelea ni kwamba, mambo yanakwenda kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa habari ni haki ya kila mwananchi; na kwa kuwa Wazungu wanasema *information is power*; na kwa kuwa Tanzania tuna wale mavu wale amba hawasikii, yaani viziwi kwa sababu nikisema wasiosikia maana yake ni watukutu, wale amba ni viziwi wako zaidi ya 1,500,000; na kwa kuwa watu hawa ni wengi na hivyo *Television* ya Taifa, hata zile nyingine, hazina wataalamu wa alama ili kuweza kuwasaidia waweze kujua ni nini kinachoendelea; sasa nilikuwa naomba kujua Wizara ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wanatoa wataalamu hao kwa sababu najua wapo, ili hawa wenzetu nao waweze kupata habari?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali alilouliza Mheshimiwa Susan Lyimo. Wiki mbili nyuma, nimekutana na Uongozi wa Chama cha Viziwi, wakanieleza tatizo la kwamba, vituo vingi vya *television* havina wakalimani wanaozungumza kwa ishara na kwa hiyo tunawanyima habari. Hatua ya kwanza niliyoichukua, nimeliagiza Shirika la Utangazaji (*TBC*), watafute mara moja mtu wa namna hiyo.

Hatua ya pili, tumewaandikia vyombo binafsi vya habari vinavyoonesha *television* kwamba na wao walizingatia hilo na mfano upo, wenzetu wa *ITV* walianza vizuri tu na

watu wakafurahia. Kama walifanya *ITV*, inawezekana pia kwa vyombo vingine vyote kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi ni kwamba, mafunzo kwa watu wa aina ile yalisimama kwa muda mrefu. Tukiwa hapa Dodoma, nimemwandikia barua Waziri Mwenzangu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili Chuo cha Ualimu cha Patandi kilichokuwa kinatoa mafunzo haya, kianze tena kuwafundisha watu hawa kwa sababu tuna uhaba sio tu wa watu kufanya kazi hapa, lakini pia wa kufanya kazi katika Mikutano ya Kimataifa.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nikubaliane na kauli ya Naibu Waziri aliposema kwamba, michezo ni viwanja. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilijaribu kueleza kwamba, Mheshimiwa Waziri kwanza ameipongeza mikoa yote ambayo ina viwanja na nina hakika walau vya kiwango fulani, lakini Mkoa wa Manyara hauna kiwanja chochote na ndio mkoa uliozaliwa mwisho. Tulipokuwa Arusha tulikuwa na uwanja, sasa hatuna uwanja na ni jukumu la serikali kusaidia inapogawa maeneo ya mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ufanuzi ninaoomba ni kwamba tu ingekuwa vizuri basi Serikali ingekuwa imeweka bajeti ya maendeleo walau mwaka hadi mwaka kusaidia ile mikoa ambayo haina viwanja kabisa kama Manyara.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufanuzi kwamba, baada ya kujenga Uwanja wa Taifa wa kisasa; je, Serikali sasa haiwezi kufikiria kujenga viwanja walau kwenye mikoa kama hii ya Manyara ambayo haina kabisa? Mheshimiwa Naibu Waziri alifika anafahamu na Mheshimiwa Waziri mwenyewe anajua kabisa amefanya kazi Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema hilo tu na sisi ni wapenzi wa michezo na vipaji vingi vinapatikana kwenye Mkao wa Manyara; kama riadha na hata mipira ya aina nyingine. Ahsante.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomjibu ndugu yangu, Mheshimiwa Juma Killimbah, kuhusu Singida kutaka kuboresha uwanja wake, maelezo yale yale wayatumie ndugu zangu wa Manyara.

Nilichoeleza ni kwamba, Serikali haina uwezo wa kujenga kiwanja kila Mkao na kila Wilaya. Masuala ya michezo yapo chini ya Halmashauri, kwa hiyo, ninashauri Halmashauri ambayo haina uwanja, waweke katika bajeti mpango wao kama wa miaka mine au mitano ili waweze kujenga uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa *DC* Mbulu, jirani zao. Tulipoona hatuna uwanja, tulikaa tukahamasisha wananchi tukamtafuta mtaalamu wa kuchora viwanja, akaja akatuchorea uwanja mzuri.

Leo Mbulu ni Wilaya, lakini wana uwanja unaofanana au unaozidi hadhi ya Mikoa mingine. Kwa hiyo, hilo linawezekana kama Halmshauri itaweka katika mipango yake.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* Sh. 347,257,500
Kif. 1003 – *Policy and Planning*... Sh. 281,756,000
Kif. 6001 – *Culture and National Languages* Sh. 1,872,659,100
Kif. 6004 – *Sports Development* Sh. 1,788,752,800
Kif. 7003 – *Information Services* Sh. 5,692,624,200

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)
MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 500,000,000
Kif. 6001 – *Culture and National Languages* Sh. 2,379,221,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 6004 – *Sports Development* Sh. 2,750,000,000

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika kifungu hicho, eneo la ujenzi wa viwanja, kuna *vote* mbili pale. Ninachotaka tu kufahamu ni kwamba, ...

MWENYEKITI: Kipi sasa?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 6385 ambayo ni masuala ya ujenzi wa viwanja. Waziri alipokuwa anajibu maswali na hoja za baadhi ya Wabunge hapa, amezungumzia suala zima la viwanja kumilikiwa na baadhi ya taasisi, vikiwemo vyama vyaya siasa na muda mfupi tu uliopita imeonekana kwamba, Mkoa wa Manyara hauna kiwanja.

Waziri anaweza akakishauri hicho chama cha siasa kinachomiliki hivyo viwanja vingine, kijenge Uwanja Manyara kama wataweza? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, kwanza, hicho kifungu wala hakihusiani, hiki ni cha ule uwaniwa mkubwa ulioko Dar es Salaam. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kif. 7003 – *Information Services* Sh. 4,300,000,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)
(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako tukufu lililokaa kama Kamati ya Matumizi, limepitia makadirio ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya mwaka 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja kwamba, makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Napenda niwashukuru nyote, kwa ushirikiano wenu kuanzia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wametoa hotuba na maelezo; Mwenyekiti wa Kamati na pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wametoa hoja nzuri tu na hatimaye michango ambayo imejaa hekima kama kawaida ya Bunge hili linaloendelea kukomaa na hatimaye tumeyapitisha makadirio haya, dakika kumi tu baada ya kile kipindi kinachohusika. Kwa hiyo, nina hakika Waheshimiwa Wabunge, mmechoka kidogo na mnahitaji kupumzika ili kesho tuanze ngwe ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 01.55 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 29 Julai, 2008 Saa 03.00 Asubuhi)*